Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 4 Agosti, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe.Anne S .Makinda ) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 327

**Chuo cha Mafunzo na Utafiti wa Kilimo Kilombero**

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA (K.n.y. MHE. CASTOR R. LIGALLAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Chuo cha *Kilombero Agricultural Training and Research Institute (KARTIN)* kilichopo nje kidogo ya mji wa Ifakara kilikuwa kiungo kikubwa kati ya wakulima na watafiti hasa kwa zao la mpunga na kwa kuwa, chuo hicho kwa sasa kinaonekana kutekelezwa kwa kupewa fedha kidogo na mazingira yake kutosafishwa:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kukipatia chuo hicho fedha za kutosha ili kimudu kufanya shughuli zake ipasavyo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa majukumu ya chuo hicho kwa sasa ni makubwa kuliko yalivyokuwa hapo awali?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

(a) Kituo cha KATRIN kinatambulika kuwa ni muhimu katika utafiti wa zao la mpunga na Serikali imekiteua kuwa Kituo – Kiongozi *(Lead Institute)* wa tafiti hizi.

Hivyo Kituo hiki bado ni kiungo muhimu kati ya wakulima, wagani na watafiti wa zao la mpunga katika ubunifu na usambazaji wa teknolojia bora. Mwaka 2007/2008, kituo cha KATRIN kilipata jumla ya shilingi 103,313,833 kwa ajili ya shughuli zote za utafiti ambazo ni sawa na asilimia 70% ya Bajeti yao. Hii imetokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali.

Pia kiasi cha shilingi 105,998,010 zilipelekwa kwa ajili ya kukarabati majengo ya chuo na chakula cha wanafunzi. Kituo hicho kwa mwaka huu wa fedha kimetengewa jumla ya shilingi 113,645,216 za utafiti na shilingi 116,597,811 za shughuli za mafunzo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mbunge kuwa majukumu ya sasa ya Kituo cha KATRIN ni makubwa kuliko yalivyokuwa hapo awali. Utekelezaji wa *Agricultural Sector Development Program (ASDP)* umevipa majukumu makubwa KATRIN na vituo vingine vya utafiti katika kuwashirikisha zaidi na kuwapatia teklojia bora wadau wa utafiti katika kanda. Kwa kuzingatia hilo ndio maana Wizara imejitahidi kuongeza kiasi cha fedha za utafiti na mafunzo mwaka huu ili kwa kiasi kikubwa ikidhi mahitaji ya kituo hicho.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyingeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa mafanikio ya Wizara ku-*recruit* au kuwapata wagani yamekuwa machache sana kwa sababu lengo lilikuwa ni kupata wagani 2500 na mpaka sasa wamepatikana kama 300 hivi. Je, Serikali haioni kama kuna umuhimu wa kuanzisha *short courses* (kozi fupi) katika vituo maalum badala kuwa miaka miwili pengine ikawa mwaka mmoja kama inavyofanyika kwenye programu za walimu kusudi kupata wagani wengi kwa mara moja?

Swali la Pili; kwa ujumla inavyoelekea vijana wengi ndiyo hakika wanapaswa wapewe kipaumbele katika suala la kuwahamisha washughulike katika masuala ya ugani kwa sababu wengi hawajihusishi au hawaelekei kupenda masuala ya kilimo.

Je, Wizara haioni wakati umefika kuunganisha vikundi mbalimbali vya vijana ambao wanaweza kupewa mafunzo ya ugani ili kusambaza fani hiyo katika vijiji na maeneo ya wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lyamba. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli htujapata idadi ya kutosha ya vijana wenye fani hii kama tulivyotarajia.

Lakini napenda kumhakikishia kwamba Serikali bado inaendelea katika kuwapa mafunzo vijana na wananchi wengine ambao tayari wameshajiorodhesha na kwamba muda si mrefu tutafikia lengo letu.

Kuhusu mafunzo ya muda mfupi ni wazo zuri tayari Wizara inalitafakari na hilo vilevile litafanyika. Kuhusu kuhamasisha vijana walioko chini. Nakubaliana na yeye kwamba ni vyema tukafanya hivyo na niseme tu kwamba wengi wanaoingia katika fani hii tayari ni vijana.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja ya nyongeza. Ni sifa gani za msingi zilizofanya Serikali kuchagua Kituo hicho kama ni Kituo Kiongozi kama alivyojibu katika majibu ya msingi; na kwa sifa hizo mnakipa kituo hicho upendeleo gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, sifa za kituo hiki kama nijuavyo mimi ni kwamba Kilombero ni walimaji wakubwa wa mpunga lakini vilevile kina sifa zingine ambazo zimepelekea kupewa hadhi ya kuwa kituo kiongozi katika utafiti wa mpunga.

Na**.** 328

**Kusaidia Maendeleo ya Mikoa ya Pembezoni**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa ni muda mrefu sasa tangu Serikali ilipoagiza kuwa kila Wizara ijitahidi kuona namna ya kusaidia Maendeleo ya Mkoa wa Rukwa na Mikoa mingine ya pembezoni kwa kuipa kipaumbele maalum ikizingatiwa kuwa Mikoa hiyo iko nyuma kimaendeleo.

(a) Je, mpaka sasa agizo hilo limetekelezwa vipi kwa sekta za kilimo, afya, elimu na maji kwa kipindi cha 2006/2007 na 2007/2008.

(b) Je, mpaka sasa ni asilimia gani ya mahitaji halisi ya pembejeo za kilimo imepelekwa Mkoani Rukwa kwa kipindi cha 2006/2007 na 2007/2008.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kuanzia mwaka 2006/2007 Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya kuendeleza sekta ya kilimo kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya *Kilimo (Agricultural Sector Development Programme (ASDP*).

Kupitia programu hii, Mkoa wa Rukwa ulipata jumla ya shilingi 647,644,983 mwaka 2006/2007, shilingi 2,670,571,306 mwaka 2007/2008 na shilingi 5,598,456,477 zimetengwa kwa mwaka 2008/2009.

Aidha *SGR* imekuwa ikinunua mahindi ya ziada Mkoani Rukwa kila mwaka. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita *SGR* imenunua jumla ya tani 26,565 za mahindi yenye thamani ya shilingi bilioni 5.14. Kwa utaratibu huu wakulima wa mahindi wa Mkoa wa Rukwa wanakuwa na uhakika wa soko.

(b)Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini ambayo inapewa kipaumbele maalum katika kugawa mbolea na mbegu bora za ruzuku. Katika mwaka 2006/2007, mkoa ulitengewa jumla ya tani 5,310 za aina mbalimbali za mbolea na tani 4,545 mwaka 2007/2008. Aidha kwa upande wa mbegu bora, mkoa wa Rukwa ulitengewa juma ya tani 139.8 mwaka 2006/2007 na tani 186.8 mwaka 2007/2008 za aina mbalimbali za mbegu bora ya mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maelezo na takwimu nilizonazo ni dhahiri kuwa, Serikali inatekeleza agizo lake la kusaidia maendeleo ya kilimo mkoani Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Paul Kimiti kwa kufuatilia kwa makini Maendeleo ya sekta zote katika Jimbo lake la Sumbawanga Mjini na Mkoa mzima wa Rukwa.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba mwongozo wako.

Kifungu cha 46 cha Kanuni zetu kinasema. Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa. Ukiangalia swali langu nililokuwa nimeuliza niliuliza hivi:-

**NAIBU SPIKA:** Naomba usome vizuri kifungu chenyewe, mimi sijakiona.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Kifungu 46 (1) kinasema hivi:- "*Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa isipokuwa kwamba kama jibu linalohusika ni refu na lina takwimu nyingi Waziri atampa Mbunge mwuliza swali nakala ya jibu mapema baada ya Kikao kuanza kabla ya muda wa kujibu swali hilo haujamalizika*."

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu lilikuwa *very clear*. Niliuliza hivi: *Kwa kuwa ni muda mrefu sasa tangu Serikali ilipoagiza kuwa kila Wizara ijitahidi kuona namna ya kusaidia Maendeleo ya Mkoa wa Rukwa na Mikoa mingine ya pembezoni kwa kuipa kipaumbele maalum ikizingatiwa kuwa Mikoa hiyo iko nyuma Kimaendeleo.*

*(a) Je, mpaka sasa agizo hilo limetekelezwa vipi kwa sekta za kilimo, afya, elimu na maji kwa kipindi cha 2006/2007 na 2007/2008?*

*(b) Je, mpaka sasa ni asilimia gani ya mahitaji halisi ya pembejeo za kilimo imepelekwa Mkoani Rukwa kwa kipindi cha 2006/2007 na 2007/2008?*

Sasa majibu niliyopewa ni ya upande mmoja. Naiomba Serikali hivi kwanini haikujibu swali la msingi la kwanza? Nataka maelezo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hilo sio swali la nyongeza. Huo ni Mwongozo kwa Spika. Kwa hiyo kufuatana na Kanuni ya 47 (3) inasema hivi: "*Iwapo Spika ataridhika kuwa swali la msingi au la nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika Kikao kingine cha Bunge.*"

Kwa hiyo, naagiza kabla ya Bunge hili jibu hili lijibiwe kwa ufasaha. (*Makofi*)

Na. 329

**Vyama Vya Kitaalam**

**MHE. DEVOTA MKUWA LIKOKOLA** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu ina vyama vingi vya wataalamu vinavyofanya kazi ya kuendeleza na kusaidia Watanzania kwa kujitolea mfano MEWATA, TAMWA na kadhalika.

(a) Je, kuna vyama vingapi vya wataalamu hapa nchini?

(b) Je, kuna chama chochote kilichowahi kufanya programu yoyote Ruvuma na nini matokeo ya kazi yao?

(c) Kwa kuwa, wananchi wa Ruvuma wana ari ya kuondoa umaskini. Je, Serikali ipo tayari kuwaunganisha wataalamu hao na wananchi wa Ruvuma ili kupanga na kutekeleza program kubwa ya kutokomeza umaskini?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Likokola (Viti Maalum) lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Msajili wa Vyama, kuna jumla ya vyama vya Kitaalamu 50 vilivyosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama. Aidha Vyama vinavyoweza kupata Cheti cha Ukubalifu chini ya Sheria ya NGOs ni vile tu ambavyo malengo yake ni kuhudumia jamii kwa ujumla na siyo wananchi wake tu.

Kwa msingi huo, si vyama vyote vya Kitaalamu vinavyosajiliwa na Wizara yangu. Hadi sasa kuna vyama vya kitaalamu 9 ambavyo vimesajiliwa na Wizara yangu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa kuna vyama vitatu ambavyo vimewahi kuendesha program katika mkoa wa Ruvuma. Vyama hivyo na program walizoziendesha ni kama ifuatavyo:-

(i) Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) mnamo mwaka 1998 kilitembelea Wilaya ya Songea, Mbinga na Tunduru, kwa lengo la kuhamasisha na kuelimisha jamii, pamoja na wadau wengine wa Maendeleo ikiwemo Serikali , *NGOs*, *CBOs* na Viongozi mbalimbali ili waweze kutambua sababu zinazochangia kurudisha nyuma Maendeleo ya Wanawake na watoto.*Program* hii ilitekelezwa kwa kushirikiana na vyombo tisa vya habari vinavyofanya kazi hapa nchini.

(ii) Chama cha Wanasheria wa Mazingira – *Lawyers Environmental Action Team (LEAT)*, kwa kushirikiana na *Tanzania Tobacco Control Forum* walitembelea Wilaya ya Namtumbo mwaka 2006/2007 kwa lengo la kujua athari za tumbaku katika kilimo, mazingira, afya za watu, haki za binadamu kwenye maeneo ya uzalishaji na athari za jumla katika maendeleo.

Matokeo ya utafiti huo yalitumiwa kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge kwenye semina ambayo iliambatana na kuwashawishi wakubaliane na Tamko la Shirika la Afya Duniani (*WHO*) juu ya athari za tumbaku *(WHO Frame work Conventional on Tobacco Control*) na hatimaye Tanzania iliridhia tamko hilo mnamo mwezi Aprili, 2007.

*(iii)Media Institute of Southern Africa* (MISA) kwa kushirikiana na Baraza la Habar Tanzania (*Tanzania Media Council*) waliendesha mafunzo ya uandishi wa habari za uchunguzi wa rushwa kwa nchi nzima mnamo mwaka 2007/2008. Mafunzo haya yalifanyika kwa Kanda na Mkoa wa Ruvuma ulinufaika kwa waandishi wake 30 kuhudhuria mafunzo hayo kupitia Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Mashirika haya hufanya kazi kwa dhana ya kujitolea na si rahisi kuwaamulia sehemu ya kufanya kazi. hata hivyo, katika utendaji wao wa kazi wanatakiwa kuwasilisha na uongozi wa Mkoa na Wilaya ili kupata maeneo ambayo yanahitaji huduma hiyo, kulingana na mpango wa kazi wa mkoa ili kuondoa mgongano wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ushirikiano anaoutoa kwa Wizara yangu hususani kwenye kuhamasisha Mashirika yasiyo ya Kiserikali kuja kujisajili. Yeye mwenyewe amefika mara nyingi katika Wizara yangu akiwa na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na kusajili Mashirika ikiwamo *Vikoba Apex* ya Songea. Napenda kuchukua nafasi hii kuyashukuru Mashirika na vyama vyote vya Kitaalam kwa mchango mkubwa wanaotoa katika kuchochea Maendeleo ya jamii nchini, hususan Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania MEWATA.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninaomba Mwongozo kufuatana Kanuni ya 46. Swali langu linahusu vyama vya

wataalam wa uchumi lakini katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hakuna mahali popote alipotamka vyama vya wataalam wa uchumi na badala yake ametamka vyama vya utaalam wa habari, afya na rushwa. Ninaomba mwongozo wako kama Wizara iko tayari kuchukua swali hili na kulijibu kiufasaha.

**NAIBU SPIKA**: Namtaka Mheshimiwa Waziri ajibu sasa.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri amelijibu vizuri. Lakini namwomba Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola kwamba swali hili kwa kweli tulivyolipata sisi na jinsi alivyoliweka naomba mwongozo wako ule ule uliotumika kwenye swali la Kilimo ili tukalifanyie kazi vizuri na kumjibu vizuri zaidi Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Huo sio mwongozo, ni ahadi yako kwamba hukujibu vizuri sasa unataka kujibu. Kwa hiyo, mtajibu kufuatana na ahadi uliyofanya Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, maswali ya nyongeza hamwezi kuuliza wakati majibu si sahihi. (*Makofi*)

Na. 330

**Tatizo la Maji Mpanda.**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

**MHE. GRACE S. KIWELU (K.n.y. MHE. SAID A. ARFI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Mpanda unakua kwa kasi na huduma ya maji haikidhi ongezeko na mahitaji ya wananchi:-

(a)Je, kwanini mpango wa huduma uliowasilishwa Wizarani kwa kuvutia kusafirisha matanki ya kuhifadhi na kusambaza maji toka chanzo cha Ikolongo, haijafikiriwa na kutengewa fedha?

(b)Je, Serikali itasaidia vipi juhudi za Mamlaka ya Maji Mpanda katika mpango wa kujenga njia za maji, maeneo yote ya majengo mapya, Kawajewae, Shamwe, Nsemlwa, Ilembo na Misunkumilo na kubadilisha mfumo chakavu katikati ya mji Kata ya Kashaulili.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo na kabla sijajibu haya maswali ndivyo yalivyoulizwa na Mheshimiwa Mbunge.

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya mpango wa huduma ya maji kutoka chanzo cha Ikolongo uliowasilishwa Wizarani umefanyiwa mapitio na kuonekena kuwa, mradi unahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina ili kuainisha gharama halisi ya mradi, uwezo wa chanzo wa kutoa maji, idadi ya wakazi wa mji wa Mpanda pamoja na watu wanaoishi kwenye vijiji ambavyo bomba litapita hadi Mpanda Mjini.

Ili mradi uweze kutengewa fedha za utekelezaji, inabidi kazi nilizozitaja hapo juu zifanyike kwanza. Hivyo katika mwaka wa fedha 2008/2009 mradi huu umeingizwa kwenye Bajeti chini ya Programu ya Sekta ya Maji kwa ajili ya kuanza uchunguzi.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusaidia juhudi za Mamlaka ya Maji Mjini Mpanda, Wizara yangu kupitia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji *(Water Sector Development Program)* ilitoa shilingi milioni 57 katika mwaka 2007/2008 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji Mjini Mpanda.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna wengine wanazungumza utafikiri tupo kwenye *Public Place.* Hamwezi kuzungumza kiti cha ng'ambo na cha pili. Haiwezekani. Tafadhali waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie hiyo sehemu. Katika kusaidia juhudi za Mamlaka ya Maji Mjini Mpanda, Wizara yangu kupitia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji *(Water Sector Development Program)* ilitoa shilingi milioni 57 mwaka 2007/2008 kwa ajili ya kuboresga huduma ya maji Mjini Mpanda.

Fedha hizo zimetumika kuagiza *submersible pump* (1) na viungo vyake. Pampu hiyo itafungwa kwenye kisima kilichopo eneo la Makanyagio. Vifaa vingine vilivyoagizwa ni pamoja na mabomba na viungio vyake kwa ajili ya kutoa maji kwenye chanzo cha chemichemi kilichopo Kijiji cha Manga kupeleka Mjini Mpanda na kupanua mtandao wa maji eneo la Nsemlwa.

Vifaa hivi pampu na mabomba viliwasili Mjini Mpanda mwezi Julai, 2008. Kazi ya kufunga pampu na mabomba inaendelea. Mpango wa kuboresha huduma ya maji utaendelea kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Katika utekelezaji wa Programu ya Sekta ya Maji, Halmashauri za Mji wa Mpanda na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, zimekidhi vigezo vya Benki ya Dunia kwa hiyo Halmashauri hizo zinatakiwa kuendelea kuzijulisha Kampuni zilizochaguliwa ili ziandae mapendekezo ya usanifu wa miradi ya maji.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya mheshimiwa Naibu Waziri, Mpanda kuna Bwawa la Milala ambalo kwa sasa hivi linaanza kupungukiwa uwezo kwa vile limekuwa dogo, lakini uwezekanao wa kulipanua lile bwawa na kulisafisha, na kama Serikali inaweza kutoa pesa inawezekana na bwaha

hilo linaweza kutosheleza maji kwa Mji wote wa Mpanda ebdapo litapanuliwa na kusafishwa.

Je, Serikali haioni badala ya kuhangaika na visima ikaliongeza bwawa hili ili kusudi maji ya bomba yaweze kupatikana kwa wingi na kwa vile lipo karibu na Mpanda na wala haliko mbali sana na Mji wa Mpanda?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimkumbushe kwamba tulishaleza Halmashauri na Mamlaka ya Mji ule yamekwisha fanya vizuri katika maandalizi ya mradi wao wa usambazaji maji.

Kwa hiyo hili analoliuliza naomba nilirudishe kwake kwamba mtaalam mwelekezi mshauri ambaye baada ya muda si mrefu ataanza kazi katika mji wa Mpanda na Wilaya ya Mpanda basi Mheshimiwa Nyami na Halmashauri ile imwonyeshe Bwawa hilo kwa sababu yeye ndiye atakayeitizamwa na kuingizwa katika uratibu wa usanifu halafu Serikali itatekeleza.

Na. 331

**Kuwaongezea Kipato Wastaafu**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. ERNEST GAKEYA MABINA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wastaafu ni akiba ya Taifa, lakini Serikali inaonyesha kutowathamini hasa wale waliostaafu kwenye miaka 1998 na kurudi nyuma ambapo wengi wao wanapata kiasi cha Sh. 21,000/=.

Je, Serikali itafikiria lini kuwaongezea kipato wastaafu hao ili waweze kumudu maisha yao ya kila siku?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Jimbo la Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mabina pamoja na na wabunge wote na wananchi kwa ujuml, kwa kuonyesha umuhimu wa kuwasaidia zaidi wastaafu wetu.

Hata hivyo, napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali inawathamini sana wastaafu wetu hasa kutokana na mchango wao mkubwa walioutoa katika kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 28/7/2008 wakati nikijibu swali Na. 295 la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Jimbo la Bumbuli, nililielezea Bunge lako Tukufu kuwa serikali imekwishaanza mchakato wa kuipitia Sheria ya Pensheni ili baadaye Bunge liweze kupitisha marekebisho ya Sheria hiyo ambayo yanalenga katika kuboresha maisha ya Wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mara nyingine tena, napenda kuwaomba Washeshimiwa Wabunge pamoja na Wastaafu kwa ujumla, wavute subira wakati Serikali inakamilisha suala hili na litakamilika katika mwaka huu wa fedha 2008/2009.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali na tukiwa tunasuburi hayo marekebisho yatakayoletwa hapo baadaye.

Je, Serikali sasa haiwezi kujipanga vizuri kuhakikisha wazee hawa wanahudumiwa katika hospitali bure. Japo Serikali huwa inasema kwamba wao wanatakiwa kuhudumiwa bure.

Lakini hilo halitendeki. Je, Serikali sasa iko tayari kuhakikisha kwamba wanahudumiwa bure hata katika tiba kwenye maeneo waliyoko?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msingi lilikuwa ni pensheni na hapa naulizwa kuhusu matibabu bure kwa wazee hawa.

Nataka niseme tu kwamba Serikali tayari imeishatoa mwongozo kwamba wazee hawa watibiwe bure katika hospitali zetu kutokana na hali zao. Na kama kuna hospitali haitekelezi, basi nadhani Halmashauri zisimamie hospitali hizo ili ziweze kutimiza lengo hili lililowekwa na Serikali.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa wale ambao walikuwa wanastahili kulipwa pensheni kati ya Januari na Julai, mwezi uliopita, hawajalipwa mpaka leo na hivyo kuwasababishia kusafiri kuja benki kuuliza na kurudi. Je, Serikali inaweza kutoa sababu ya tatizo hilo ni nini na lini watalipwa wastaafu hao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Pensheni kwa wastaafu tulikuwa tunalipa kwa kipindi cha miezi sita, sita na zilikuwa zinalipwa mapema *(advance)*. Wale ambao tuliokuwa tunawalipa kuanzia Januari – Juni, huwa zinalipwa Januari na ikifika Julai – Desemba, zinalipwa Julai.

Hakuna ambaye alikuwa hajalipwa kuanzia Januari – Juni, isipokuwa wazee wengi walifikiria kwamba zinalipwa mwisho. Pensheni za miezi sita sita zilikuwa zinatolewa mwanzo. Kwa hiyo, wazee wte wameishalipwa kuanzia Januari – Juni. Sasa hivi tuko katika mkakati wa kulipa mwezi hadi mwezi na wengi wao tumeishaweka katika akaunti zao fedha za mwezi wa Julai.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Nisingependa nikabishana na Mheshimiwa Waziri, lakini nina swali moja dogo. Mpaka hivi sasa, sasa hivi mimi nimetoka kuzungumza na baadhi ya wastaafu ambao wamepewa hela za kuanzia Julai mpaka Desemba ambazo walipata Januari mwaka huu. Hela za Januari mpaka Juni mpaka hivi sasa bado hawajapata! Sasa, mimi naomba, tunamwombe Mheshimiwa Waziri kwa ushauri kwamba ajaribu kwenda kupitia tu yale mafaili yake, nisingependa nikapishana naye. Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nadhani umepokea ushauri wake! Tunaendelea na swali lingine.

Na. 332

**Ajali za Barabarani**

**MHE. RAMADHANI A. MANENO** aliuliza:-

Kwa kuwa ajali za barabarani zimekuwa sugu hasa ajali za magari ya abiria yanapoteza sana maisha ya watu:-

(a) Je, Serikali ina uhakika kwamba magari yote yamekataliwa bima kubwa?

(b) Je, ni fidia ya shilingi ngapi wanazopewa ndugu wa mfiwa aliyefariki kwenye gari la abiria?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mbunge wa Jimbo la Chalinze, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria za Bima za Gari *[Motor Vehicle (Third Party Risks) Ordinance 1945 (Tanganyika) and Motor Vehicle (Third Party Risks) Decree 1953 (Zanzibar)]*, gari zote zinazoendeshwa barabarani zinapaswa kukatiwa bima dhidi ya maumivu ya mwili au kifo kwa wahanga wa ajali barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima inayotakiwa kukatwa na mwenye gari ni ile ijulikanayo kama *third party liability* na bima hivyo inatosha kutoa kinga inayotakiwa

kisheria. Bima mseto *(comprehensive insurance)* ni ya hiari na inaweza kukatwa iwapo mwenye gari ana uwezo kumudu ada inayotozwa na kampuni ya bima husika.

Hata hivyo, mmiliki wa gari lenye bima mseto anapata kinga kubwa zaidi ikiwa ni pamoja na kulipiwa fidia iwapo gari lake litapata uharibifu kutokana na ajali.

Kutokana na utaratibu uliopo hivi sasa wa ulipaji wa leseni ya barabara *(road licence)* gari lolote haliwezi kupewa leseni ya barabara bila kuwa na bima. Hivyo, Serikali inakuwa na uhakika kwamba gari zote zinakuwa zimekatiwa bima kisheria.

(b) Mheshimiwas Naibu Spika, mwathirika wa ajali analipwa fidia kutokana na kiwango alichoathirika. Uthibitisho wa kiwango husika hutolewa na:-

(i) Mahakama itakayothibitisha kwamba dereva wa gari alifanya uzembe wa uendeshaji wa gari barabarani na kusababisha ajali.

(ii) Taarifa za kitabibu zinazotolewa na hospitali ikiwa ni pamoja na hati ya kifo kama mwathirika amefariki dunia.

(iii) Umri na kipato alichokuwa nacho mwathirika.

(iv) Uamuzi wa mahakama katika kesi zilizotangulia ili kujua fidia zilizokwishalipwa katika ajali ya namna hiyo.

(v) Utegemezi wa ndugu wa marehemu au mwathirika kwa maisha yake yote yaliyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vigezo hivyo, ni jukumu la mwathirika au ndugu zake kujadiliana na kampuni ya bima ili kukubaliana kuhusu kiwango cha fidia au kwenda mahakamani wasiporidhika na kiwango hicho.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nipate kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa suala la malipo ya bima linawasumbua sana wananchi hasa kupitia mawakala pamoja na wamiliki wa magari inapotokea tatizo la malipo. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuondoa tatizo hili pamoja na kuhakikisha mtu mwenye basi au gari nyingine yeyote ya abiria au gari ya binafsi inakatiwa bima kubwa ili iweze kuondoa tatizo hili?

Swali la pili, kwa kuwa sheria ya bima ya magari ya mwaka 1945 imepitwa na wakati, Serikali haioni sasa kuifanyia marekebisho sheria hii ili iweze kuwasaidia watu wanaoathirika, wanaopata vifo au kupata majeraha katika ajali za barabarani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE) :** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka nieleze kwamba tayari Serikali iko katika mchakato wa kuipitia sheria hii ili kuweza kukidhi hali halisi ilivyo hivi sasa.

Lakini pia katika mchakato huo haya ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Maneno yataweza kuboreka na kuona kwamba inapotokea ajali basi hawa waathirika wanaweza kupata haki yao bila ya usumbufu wowote.

Namwomba Mheshimiwa Maneno avute subira, tuko katika kukamilisha mapitio ya sheria hiyo na tutaileta hapa katika kipindi cha mwaka huu.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipatia fursa niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wenye vyombo vya moto yaani wenye magari, wanapofika hatua ya kwenda bima hasa *National Insurance* kwenda kudai haki zao baada ya magari yao kupata ajali, kumekuwa na tatizo kubwa sana la kupata fedha.

Je, kuna tatizo gani katika Shirika letu hili. Linazo fedha au kuna mgogoro mkubwa mwingine unaoendelea katika Shirika hili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE) :** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani utakumbuka kuwa wiki mbili zilizopita Wizara yangu ilijibu swali hapa kuhusu habari ya Shirika letu la Bima. Tulieleza kwamba Shirika lina madeni mengi, tunakubali na tuko katika mchakato wa kuhakikisha kwamba madeni hayo yanalipwa. *(Makofi)*

Vile vile tuko katika mchakato wa kuli-*restructure* Shirika hili kwa sababu lina wafanya kazi wengi sana kiasi ambacho sasa hivi biashara ya Bima ni biashara ambayo ni ya ushindani. Kwa maana hiyo, tutakapokamilisha, nadhani hilo tatizo ambalo Mheshimiwa Mbunge analiona hivi sasa, litaweza kupungua au kumalizika kwa sehemu kubwa.

Na. 333

**_Armory_ – Kituo cha Polisi Mitundu**

**MHE. MGANA I. MSINDAI (K.n.y. MHE. JOHN P. LWANJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Kata ya Mgandu Wilayani Manyoni walijitolea kujenga Kituo cha Polisi Mitundu kwa ajili ya kupatiwa huduma za kiusalama, kulinda maisha na mali zao kutokana na wimbi la ujambazi ; na kwa kuwa baada ya kukamilisha ujenzi huo hadi sasa hakijafunguliwa kwa sababu ya kukosekana kwa chumba maalum cha kuhifadhia silaha *(Armory)*:-

(a) Je, ni lini Serikali itatimiza wajibu wake wa kujenga *Armory* kwa ajili ya kuhifadhia silaha?

(b) Je, Serikali haioni kwamba inawavunja moyo wananchi pale wanapojitolea kwa hali na mali kushirikiana na Serikali lakini baadaye wanaachwa kwa Serikali kutotimiza wajibu wake?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali Na. 333 kwa ruhusa yako, naomba nichukue fursa hii nimpe pole sana Mbunge mwenzangu kutoka Kagera, Mheshimiwa Savelina Mwijage, kwa msiba mkubwa na mzito uliomkuta. Namwombea Mwenyezi Mungu ampe subira katika yote yaliyomkuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John P. Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wananchi wa Kata ya Mgandu Wilayani Manyoni walijitolea kujenga nyumba kwa madhumuni ya kuwa Kituo Kidogo cha Polisi *(Out Post)* Mitundu kwa ajili ya kupatiwa huduma za kiusalama na kwa hili Serikali inawapongeza sana wananchi wa Kata ya Mgandu kwa jitihada yao. Jeshi la Polisi Mkoani Singida limeshindwa kupeleka askari katika kijiji hicho kwa sababu hakuna nyumba za kuishi askari na siyo kwa sababu ya kukosekana kwa chumba maalum cha kuhifadhia silaha *(Armory)*. Kwa mujibu wa taratibu za Jeshi la Polisi, Vituo Vidogo wa Polisi haviruhusiwi kuhifadhi silaha, hivyo havina *Armory*.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wananchi mara nyingi wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika shughuli mbali mbali za Maendeleo ikiwemo ujenzi wa Vituo vya Polisi.

Hata hivyo, pamoja na michango hiyo ya wananchi, ili Vituo vya Polisi viweze kutumika ipaswavyo ni muhimu sana ujenzi wa Vituo vya Polisi ukaendana na ujenzi wa nyumba za askari katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya haba wa Bajeti hivi sasa, Jeshi la Polisi linasita kupeleka askari katika Kituo hicho mpaka hapo uwezo utakaporuhusu na Serikali inafanya jitihada kuona kwamba uwezo uweze kupatikana. Jeshi la Polisi Wilaya ya Manyoni litaendelea kufanya doria, operesheni na misako kwa kuwashirikisha wananchi kupitia mpango wa Polisi Jamii.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa wananchi wa Mitundu wamejitolea kutoa nyumba kwa ajili ya Polisi kuishi kwa muda wakati wananchi hao wakisaidiana na Polisi kujenga nyumba za kudumu.

Je, Waziri atakuwa tayari kwenda Mitundu kuona nyumba iliyotolewa ili askari hao wakae na kuwasaidia wananchi wa eneo hilo?

La pili; kwa kuwa wakati Waziri anawasililisha Bajeti ya Mambo ya Ndani, pamoja na mambo mengine, alisema atasaidia kutatua matatizo yaliyopo kwenye vituo vingi vya Polisi vikiwepo Mitundu, Nduguti, Ibaga na Mwangeza. Je, wananchi wasubiri kwa hamu kutatuliwa matatizo yao kwa ajili ya usalama wao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza kwamba wananchi wa Mitundu wamejitolea na tayari wametengeneza nyumba ya askari kuishi na anauliza kama ningeweza kwenda nikatizama mwenyewe kushuhudia.

Jibu ni kwamba niko tayari na tutazungumza tuone utaratibu wa kwenda kutizama na kufanya ziara. Kwa hiyo, hilo naomba nimhakikishie Mbunge kwamba litafanyika. *(Makofi)*

Kuhusu suala la pili; kwa kweli tumezungumza katika Bajeti yetu ambayo nawashukuru sana Wahewshimiwa Wabunge kwa kuipitisha juma lililopita. Matatizo kweli yapo, lakini pia hata hapo katika maeneo aliyoyataja ya Mitundu, Nduguti na kadhalika.

Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba nitakuwa tayari mimi kufanya safari hiyo nitakayokwenda naweza nikaunganisha nikatizama hali halisi na tukatizama ni jinsi gani tunaweza kuwasaidia wananchi kwa sababu si azma ya Serikali kuwavunja moyo wananchi wake.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika swali la msingi hasa kipengele (a) kimezungumzia kuhusiana na ujenzi wa *Armory* huko Mitundu. Mimi nataka Mheshimiwa Naibu Waziri anieleze; kwa kuwa Kituo cha Polisi Shelui tayari tunayo Armory lakini bado silaha zinahifadhiwa Kiomboi, kilomita zipatazo karibu 40.

Je, sasa atakuwa yuko tayari kuishauri Polisi Kiomboi kuhifadhi silaha Kituo cha Shelui?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa sana kuzungumzia masuala ya Armory kwa sababu ni masuala ya usalama na ni masuala ambayo Serikali, Jeshi la Polisi linatizama wapi waweke na kwa sababu zipi na kwa vigezo vipi.

Lakini ningependa nimhakikishie kwamba hoja yake nimeipokea kuhusu kwamba kuna silaha ambazo zimewekwa Kiomboi, lakini angependa kuona kama wanaweza wakaweka baadhi katika Kituo cha Shelui. Mimi naomba hili nilizungumze na wataalam wa Polisi wao ndio wanajua zaidi.

Lakini kama uwezekano upo, sidhani kama kutakuwa na tatizo, lakini siyo kwamba naweka ahadi. Naomba Mheshimiwa Mbunge anipe fursa nitazungumza na yeye na nitazungumza na viongozi wa Jeshi la Polisi tuone nini linaweza likafanyika katika hilo.

Na. 334

**Kupandishwa Vyeo Askari Jasiri**

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD (K.n.y. MHE. HAFIDHI ALI TAHIR)** aliuliza:-

Kwa kuwa Tasnzania inajivunia kuwa na askari jasiri na wakakamavu; na kwa kuwa katika sherehe za elimu bila malipo zilizofanyika kwenye Viwanja vya Amani tarehe 22/1/2006 na Mgeni Rasmi akiwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Mlingoti wa Bendera uliokuwepo uwanjani hapo ulikaribia kuanguka kutokana na upepo mkali hali iliyosababisha askari kuzuia mlingoti huo kwa zaidi ya saa 2 ili usianguke chini; na kwa kuwa Kamishina wa Polisi wakati huo aliahidi kuwapandisha vyeo askari hao kutokana na ujasiri huo;-

(a) Je, ahadi hiyo imeishatekelezwa na kama imetekelezwa ni askari wangapi wameteuliwa?

(b) Kama bado, ni kwa sababu gani za kutotekelezwa kwa ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wakati wa maazimisho ya sherehe za elimu bila malipo zilizofanyika katika Uwanja wa Amani Mjini Unguja siku ya tarehe 22 Januari, 2006 ambapo Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar alikuwa mgeni Rasmi, Kamishna wa Polisi Zanzibar aliahidi kuwapandisha vyeo Askari watatu kutoka Komandi ya Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja ambao walifanya kitendo cha ushujaa na ujasiri mbele ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kudhibiti mlingoti wa bendera ya Rais wa Serikali ya Mapinduzi usiangushwe na upepo mkali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Inspekta Jenerali wa Polisi ameishatekeleza ahadi hiyo kama ifuatavyo:-

§ Askari Na. Z.2203 CPL Hafidh Ali Mgeni amepandishwa chao kutoka CPL na kuwa *Sgt.* Toka mwezi Januari, 2006.

- § Askari Na. Z.2337 CPL Ramadhani amepandishwa cheo kutoka CPL na kuwa *Sgt* toka mwezi Novemba, 2006.

- § Askari Na. Z.2298 *S/Sgt.* Rashid Zam ameteuliwa kuhuduria mafunzo ya Mkaguzi Msaidizi ili kuweza kumudu madaraka mapya mara atakapomaliza mafunzo hayo mwezi Agosti, 2008, yaani mwezi huu!

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kitendo walichokifanya Wizara hii kutekeleza ahadi walizoziahidi mara moja, ningeliomba sana na Wizara zingine ziwe na msimamo kama huu, ahsante! *(Makofi)*

Na. 355

**Ukosefu wa Masafa ya TVT na RTD Singida**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoani Singida hakuna masafa ya Redio Tanzania *(TBC* Taifa) wala Televisheni ya Taifa *(TBC1)* hali inayosababisha wananchi kuunganishwa *TBC1* na wafanyabiashara ambao wanatoza gharama kubwa; na kwa kuwa Serikali ilipojibu swali langu hapa Bungeni iliahidi kuwa katika mwaka wa fedha 2004/2005 ingeunganisha huduma hiyo, ahadi ambayo mpaka sasa haijatekelezwa: -

Je, ni lini Serikali itaupatia Mkoa wa Singida huduma za *TBC One* na *TBC* Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kirefu sasa, Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* limekuwa na mipango ya kuhakikisha kuwa matangazo yake ya Redio na Televisheni yanawafikia wananchi wote hapa nchini bila usumbufu wowote ikiwa ni pamoja na wasililizaji na watazamaji wengine kuingia kwenye gharama kwa kuwalipa wafanyabiashara ili kuweza kupata huduma hizo.

Katika jitihada hizo, hizi karibuni Shirika hili lilikamilisha ufungaji wa mitambo kumi (10) ya kuruhusu matangazo ya Redio kwa Mfumo wa *FM* katika Mikoa ya Kigoma, Tabora, Musoma, Mara, Dodoma, Arusha, Tanga, Bukoba (Kagera), Mwanza, Mbeya na Kisarawe kwa Mikoa ya Pwani na Dar es salaam. Mitambo hiyo ilizinduliwa rasmi na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Jijini Dar es salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma ya TBC Mkoani Singida , Serikali katika Bajeti ya mwaka huu wa 2008/2009 katika kitabu, ukurasa wa 153 kwa Bajeti ya

mwaka huu, imetenga fedha kwa ajili ya kununulia mtambo wa kurushia matangazo ya redio kwa mfumo wa *FM* kwa ajili ya Mkoa wa Singida.

Mchakato wa kupata mtambo huo unaendelea ili mara tu fedha hizo zitakapotolewa uweze kununuliwa na kuwekwa Singida. Na ni hivi karibuni tu Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Tido Mhando, tarehe 29Julai, 2008 alialikwa kwenye kikao cha *RCC* ili kuwahakikishia wananchi wa Singida kwamba mtambo huo utawekwa.

Kwa sasa, wananchi wa baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Singida wanaweza kupokea matangazo ya Redio kupitia mitambo ya *FM* iliyofungwa Mkoani Dodoma. Tayari baadhi yao wameanza kupata huduma hiyo na kushiriki mara kwa mara kwenye baadhi ya vipindi vya *TBC* Taifa na *TBC FM.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa idhini yako naomba uniruhusu nimshukuru Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Singida, kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilizia kuhakikisha kwamba Singida inapata usikivu wa Redio na kupata Televisheni. Hili ni swali lake la nne na limezaa matunda. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wazee wa Mkoa wa Singida waliweka nadhiri kwa Serikali yao ya CCM kwamba siku wakifungiwa Televisheni na Redio ya Serikali, wataizawadia Serikali ya CCM Mbuzi anayezaa mapacha, ikiwa ni shukrani yao kwa Serikali yao ya CCM. Je, kwa kuwa naamini Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba zoezi hili litafanyika haraka iwezekanvyo. Je, yuko tayari kuja kupokea mbuzi huyo anayezaa mapacha ikiwa ni shukrani yetu kwa Serikali ya CCM? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa inazawadiwa CCM au Waziri huyu au nani sasa? Eti siyo CCM, ni wewe utakayezawadiwa, kampokee mbuzi!

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba siku mitambo itakapokwenda kuzinduliwa, Wizara yangu kwa niaba ya Waziri iko tayari kumpokea mbuzi huyo anayezaa mapacha ili angalau tuweze na sisi kuendelea kufuga katika Wizara yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ili uwapelekee watoto yatima! Maana Wizara haiwezi kufuga mbuzi, inabidi uwapelekee watoto yatima. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 336

**Ubovu wa Ndege Ziendazo Kigoma**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa usafiri wa aina zote Kigoma ni wa matatizo kutokana na ubovu wa miundombinu au kutokuwa na y a kutosha:-

(a) Je, Serikali inatambua kuwa ndege ziendazo Kigoma nyingi ni mbovu na safari zake zimekuwa zikiahirishwa mara kwa mara kutokana na ubovu huo?

(b) Je, Serikali inatambua kuwa ubovu huo hutishia maisha ya Watanzania?

(c) Je, Serikali haiwezi kutafuta ufumbuzi wa matatizo hayo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiriwa Anga Tanzania *(Tanznia Civil Aviation Authority (TCAA)* huhakikisha kwamba ndege yoyote iliyoandikishwa hapa nchini huruka baada ya kuwa na cheti cha kuthibitisha ubora wa ndege hiyo, kuruka angani yaani *Certificate of Airworthiness*.

Kanuni za urushaji ndege zinaelekeza kwamba inapotokea hitilafu yoyote ya kiufundi, ndege husimamishwa hadi hapo hitilafu hiyo itakapotatuliwa kabisa. Kanuni hizo zinataka pia wahandisi wa ndege na marubani kujihakikishia kwamba ndege yoyote itakuwa imefanyiwa ukaguzi unaotakiwa kwa mujibu wa kanuni za uendeshaji ndege kabla ya kuanza safari.

Aidha, kanuni na taratibu za urushaji ndege zimempa rubani madaraka ya mwisho kuhusu usalama wa abiria na mali wakati wote wa safari. Hivyo, rubani ana wajibu wa kusitisha safari kama ataona kwamba hitilafu ndani ya ndege au hali ya hewa inatishia usalama wa abiria na mali zao au usalama wa ndege yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu hizi ambazo ni za Kimataifa na ambazo hapa nchini husimamiwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga zimewekwa kwa makusudi ili kuhakikisha kwamba usafiri wa anga unakuwa na usalama wa hali ya juu kwa kadri inavyowezekana. Hata hivyo pamoja na kuwepo kwa kanuni hizo, kuahirishwa kwa safari ya ndege huwa hakuepukiki.

Kuahirishwa kwa safari kunaweza kusababishwa na mambo mengi yakiwemo masuala ya kiufundi kama vile marekebisho kwenye ndege, masuala ya kiuendeshaji kama vile kuchelewa kwa ndege kwenye safari moja na hivyo kuathiri safari kwa ndege inayofuata au sababu zitokanazo na hali ya hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa usalama kwa abiria na kwa kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga itaendelea na jukumu lake la kuhakikisha

kuwepo kwa usalama wa usafiri za anga kwa kusimamia ipasavyo sheria na kanuni zote za usafiri wa anga.

Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga itaendelea kuyahimiza makampuni ya ndege kuhakikisha kwamba yanakuwa na mipango mizuri ili kupunguza kuvuruga ratiba zao.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu hayo ya ufafanuzi. Lakini kuna tabia mbaya ya kutotoa taarifa mapema ya uahirishwaji wa ndege hizo hali inayopelekea usumbufu kwa wasafiri kufika *Airport* na mara nyingine wanakaa muda mrefu bila kupewa taarifa kiasi kwamba wanaamua wafuatile wenyewe.

Je, hiyo ni sawa? Swali la pili; kwa Mkoa wa Kigoma tunategemea ndege ya Shirika moja tu ambapo inapoahirishwa kutokana na matatizo mbali mbali inakuwa ni usumbufu kwa wasafiri na kulikuwa na taarifa kwamba mwezi Aprili, *ATC* wataanza safari za kwenda Mkoa wa Kigoma. Je, ni lini zitaanza maana kuna *delay* ambayo hatuielewi wala hatujaelezwa ni sababu zipi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri kwamba ni usumbufu kupewa taarifa fupi ya kuahirisha ndege na hiyo tutaendelea kuyaelekeza makampuni husika ili yaweze kulirekebisha na kupunguza matatizo kwa wasafiri.

Upande wa swali la pili; ni kweli kuwa mashirika ya ndege yalikuwa na mpango wa kuanzisha safari zaidi Kigoma. Sasa hivi Kigoma inahudumiwa na *Precision Air* peke yake. Lakini kuanzia Mwezi Septemba 2008 Shirika letu la Ndege la Tanzania *(ATCL)* linatarajia kuanzisha safari za ndege kwenda Kigoma.

Lakini pia linatarajia kuanza safari kwenye mji wa Tabora, Dodoma, Songea na Shinyanga. Kwa maana hiyo ni kwamba tutegemee safari hizo. *ATCL* ilishatangaza kuanza safari hizo hapa Dodoma. *(Makofi)*

Bahati mbaya sana kwa matatizo ya kiutendaji na maandalizi ambayo naweza kusema kwamba hayakuwa ya kina. Safari ile ya kuja hapa Dodoma haikuweza kuanza mwezi Julai kama *ATCL* ilikuwa imepanga. Lakini sasa wamejiandaa vizuri kwa kuanzisha safari katika maeneo hayo.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa katika uwanja ule wa ndege Mkoani Kigoma ni kama kero, *VIP* tunapokuwa na mizigo huwa tunapekuliwa sana wakati mwingine unakuwa umeweka labda nguo zingine nyeti kwenye sanduku zinakuwa zinaangaliwa je, ni lini tutaletewa mashine ya kukaguliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge swali hilo ni lingine lakini basi Mheshimiwa Waziri, jibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kilio chake tumekisikia na tutakifanyia kazi ipasavyo. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwa kauli ya utangulizi ya swali inasema kwa kuwa usafiri wa aina zote Kigoma una matatizo hasa kutokana na ubovu wa miundombinu, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri atueleze pamoja na kwamba Shirika la Reli limeongeza treni moja, lakini bado abiria wanapata adha ya usafiria. Ni lini Wizara itafikiria kutatua na kuondoa kabisa adha ya usafiri wa treni kuelekea Kigoma na pengine Mpanda na Mwanza?

**NAIBU SPIKA:** Ninyi vipi mnauliza maswali gani hayo maana yake hili linahusu *Air Tanzania*, lakini Waziri jibu wanataka usafiri. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU**: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya juhudi kubwa sana kuhakikisha kwamba inaondoa tatizo la usafiri kwa wananchi wa Kigoma kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo na kwa haraka iwezekanavyo, hivi punde tu Serikali kupitia Shirika la Reli *(TRL)* limeongeza safari za kwenda Kigoma kutoka safari mbili hadi tatu na sasa hivi tuna safari tatu lakini pia Shirika la *TRL* linategemea kupokea mabehewa 23 mwezi huu wa Agosti, 2008 ambayo yatawezesha kuongeza safari za treni kufikia safari nne kwa wiki badala ya safari tatu kwa sasa na baadaye *TRL* itaendelea kwa nia ya kuwa na safari sita kwa wiki badala ya safari hizi ambazo tunazigemea hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande mwingine kazi ya ujenzi wa barabara ya Kigoma - Kidahwe imeanza kwa gharama ya Serikali lakini pia Kidawe - Uvinza ambayo inaufadhili wa *Saudi Fund* iko katika usanifu wa kina na Uvinza – Ilunge - Malagalasi ambayo iko katika ufadhili wa *Budhabi Fund* nayo pia iko katika hatua za mwisho za usanifu wa kina. Tunatarajia kwamba kwa juhudi hizo tutaiondoshea Kigoma matatizo ya usafiri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha Kigoma mmeahidiwa ndege na treni pia itaanza kufuatana na Waziri alivyosema, kwa hiyo, tunashukuru haya yafanyike.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wetu katika *public gallery* yetu, kwanza kabisa tunao wageni wa Mheshimiwa Saveline Mwijage hawa wametoka kwenye msiba kama mnavyofahamu uliowapata katika muda wa wiki chache zilizopita, wametoka kule ndiyo wamekuja hapa kwa lengo pia la kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge mlivyoshughulikia tatizo lile. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Ignatus R. Alibaliwo, yupo Hawa Rutu, Happiness Peter, Prudencia Mwijage, Gervas Mwijage huyu ni mmojawapo aliyenusurika kwenye ile ajali, mzazi wa mjukuu aliyefariki baadaye, maana baada ya ile ajali walifariki watu wawili na mtoto alipelekwa hospitali na bahati mbaya naye akaja akafariki mzazi wake ni

Servania Slyvanus. Tunawapeni pole tena haya ni mambo ambayo hatuwezi kuyakwepa na kila mmoja wetu ndiyo njia yake hiyo, mvute subira Mungu atawasaidieni.

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna wanachuo 40 na wakufunzi wawili kutoka Chuo cha Ualimu *Capital*, naomba wasimame pamoja na walimu kama wapo, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wanafunzi 42 kutoka shule ya sekondari ya Nkuhungu wasimame na walimu wao kama wapo, tuna mgeni wa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa ambaye ni ndugu Nasibu Bataani Masaguti ambaye ni Katibu wa CHADEMA tawi la Kwandene, Kata ya Balari, Wilaya ya Karatu, karibu sana Katibu. Mgeni wa Mheshimiwa Yahya Kassim Isaa ni Joseph Mwambole Said karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo mengine, tangazo la kwanza kabisa, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib atakuwa anakaimu nafasi ya ukuu wa Shughuli za Serikali Bungeni alianza tarehe 2 hadi 6 Agosti, 2008 kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko nje ya Dodoma kwa hiyo, hatuna shaka tutashirikiana vizuri. *(Makofi)*

Matangazo mengine ya kazi ni kwamba Mheshimiwa Spika kama mnavyofahamu yupo nchini Malyasia kwenye Mkutano Mkuu wa *CPA* duniani na anatoa salaam zake na kuwatakieni kikao chema pamoja naye amefuatana na Waheshimiwa wafuatao ambao ni Dr. Raphael Chegeni na mnajua yeye ni Mwenyekiti wa *branch* yetu hapa, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ni Makamu Mwenyekiti wa *branch* yetu ya hapa, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Mussa Zungu na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa wapo Malyasia na kikao kitaisha tarehe tisa, Mheshimiwa Spika wetu ni Makamu wa Mkutano huo akirudi kutoka huko atakuwa ndiye Rais wa *CPA* kwa sababu mwaka kesho sisi ni wenyeji wa Mkutano wa *CPA*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ofisi inaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri amefiwa na mama yake mzazi jana tarehe 3 Agosti, 2008 Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuitangazia pia Kamati ya Uongozi pamoja na Tume ya Huduma za Bunge kwamba baada ya kuahirisha kikao saa saba kutakuwa na kikao, Wajumbe wa Tume ya Uongozi na ile ya Uongozi wa Serikali, Wenyeviti wa Kamati mbalimbali tutakuwa na kikao saa saba mchana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli za leo, tunategemea wale wachangiaji waliopo watapewa nafasi halafu mchana tunamwachia Mheshimiwa Waziri aweze kujibu hoja. Mheshimiwa Kingunge Ngombale Mwiru yeye hajachangia hata mara moja, Mheshimiwa Maria Hewa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Msafiri hao kwanza halafu tutaendela na wengine. *(Makofi)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 – Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. KINGUNGE NGOMBALE-MWIRU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ningependa kwanza nitoe rambirambi kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Tarime Mheshimiwa Chacha Wangwe, kifo chake cha ghafla kimetustua wengi na kimetusikisha sana, mimi binafsi nilimheshimu sana ndugu Wangwe kwa sababu nilimwona kuwa ni mtu ambaye alikuwa na mambo anayoyaamini na alikuwa tayari kuyatetea bila wasiwasi, alikuwa mkweli na mtetezi wa watu wake ambao alikuwa akiwawakilisha, tumempoteza Mtanzania shujaa kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nimpongeze Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uamuzi wake wa kuunda Wizara hii mpya kwa kuunganisha shughuli za ufugaji na uvuvi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli hizi zimekuwa kwa muda mrefu hazipewi nafasi yake inayostahili, matumaini yetu ni kwamba kwa kuundiwa Wizara zitapata nafasi za kushughulikiwa kwa kulingana na umuhimu wake, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa hotuba yake nzuri na kuwapongeza pia Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara, Wizara hii ina umri ambao haujafikia miezi minne lakini tumeshaanza kuona matokeo ya kazi nzuri ambayo wameanza kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya uchanguzi ya CCM kuna maelekezo ya msingi, kwanza ilani inasema uchumi wetu uko nyuma na tegemezi, na ili kukabiliana na hali hiyo ilani inatuelekeza kwamba majukumu yetu makubwa ni mawili katika kipindi hiki, kwanza ni kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea yaani kufanya *modernisation* ya uchumi, kujenga uchumi wa kisasa, *modernisation* maana yake ni usasa. *(Makofi)*

Mhehimiwa Naibu Spika, pili ni kutekeleza sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwamba ili ubadili uchumi uwe wa kisasa ni lazima uwe na sera ya kuwawezesha wananchi kushiriki katika kuleta mabadiliko hayo kwa hiyo, kujenga msingi wa uchumi wa kisasa lakini njia kubwa ni ya kuwawezesha wananchi waweze kushiriki katika kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ilani inapanga vipaumbele katika kufanya kazi, kipaumbele cha kwanza ni elimu, lakini cha pili ni sekta kubwa ya kilimo na ufugaji na uvuvi. Kwa hiyo, hapa tunazungumzia sekta ambayo ni ya umuhimu wa pili katika kubadilisha uchumi wetu, zipo sababu zinazofanya sekta hii kubwa ya kilimo, ufugaji na uvuvi ikapewa kipaumbele cha nafasi hiyo muhimu kwa sababu kwanza sekta hii ndiyo

inayotoa chakula kwa binadamu, pili sekta hii kubwa ndiyo inayoajiri zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania, tatu sekta hii ndiyo inayoweza kutoa malighafi kwa ajili viwanda ili kutengeneza mahitaji mengine ya kimaendeleo na zipo sababu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sekta hii imekuwa na udhaifu mkubwa, mimi nilitaka nitoe mapendekezo, kwanza udhaifu mkubwa tulionao, tuna mifugo mingi tunaambiwa sisi ni wa tatu katika Afrika, ukichanganya ng'ombe, mbuzi, kondoo na wanyama wengine, wako karibu milioni 40 kwa hiyo mifugo mingi lakini kwa bahati mbaya haisadii wenye mifugo hiyo kuondokana na umaskini kwa sababu ufugaji wetu ni wa jadi, tunachunga badala ya kufuga, wananchi wetu wenye mifugo wanaishi kwa kukimbizana na wanyama na wanyama wanachoshwa wanashindwa kutoa maziwa na nyama wanazotoa ni kidogo sana ukilinganisha na wanyama wa aina hiyo hiyo katika nchi zilizoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za hali hii tunazijua, maoni yangu ni kwamba mpaka sasa hatujaweka mpango wa kushughulikia sababu zinazofanya ufugaji wetu ukawa ni wa nyuma kabisa na tusiweze kufaidi wingi wa mifugo tuliyonayo badala yake ikawa zaidi mifugo hiyo mingi inakuwa ni tatizo zaidi kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Wizara yetu mpya ushauri wangu ni kwamba ungetazama mambo gani ya kufanya ili tuweze kutoka hapa tulipo, tupige vita kwanza tuwe na mikakati ya kuondokana na wenye mifugo kuhamahama na kukimbizana na wanyama nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu tunazijua ambazo ni kwamba mifugo inatafuta maji, malisho, kwa hiyo, tuwe na mipango thabiti ya mabwawa na malambo katika maeneo yale yote ambayo yana mifugo mingi, pili mifugo inahitaji matibabu, majosho yetu hata yale yaliyokuwepo hayafanyi kazi, kwa hiyo, tuwe na mkakati na mpango wa kukarabati yaliyoharibika na kujenga mapya pamoja na vituo vya afya vya wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili tunahitaji ng'ombe wetu watoe maziwa siyo ng'ombe anatoa maziwa chupa moja kwa siku kwa sababu ya kumkimbiza kimbiza lakini vile vile kwa sababu ya aina yenyewe ya ng'ombe. Kwa hiyo, tuwe na mpango wa kueneza mbegu bora za maziwa katika nchi yetu, mpango kabambe ng'ombe wapo tufanye *cross breeding*, tueneze madume ya kisasa kwa ajili ya mbegu bora ya maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tueneze madume ya ng'ombe kwa ajili ya kueneza na kupata ng'ombe wenye nyama nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho tunataka kuingia kwenye ufugaji wa kisasa, mimi nadhani changamoto kubwa moja ni kuwatumia vijana wetu tuliowasomesha utalaamu wa ufugaji katika vyuo mbalimbali pamoja na vyuo vikuu, tuanzishe mfuko wa kuwawezesha hawa kuingia katika sekta ya ufugaji wa kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu Julius Nyerere wakati fulani alizungumza pale *SUA* na kuwapa changamoto wasomi waingie kwenye ufugaji na kilimo cha kisasa, mimi nadhani Serikali yake inge-*take up* hili suala ili tuwape changamoto vijana wetu tutaweza kuunda sekta mpya ya ufugaji wa kisasa ambao vijana wa Kitanzania wasomi wataweza kuishughulikia kama ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na ushauri huo naomba kuunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwanza kwa kupata nafasi hii nyeti ambayo kwa kweli wala hata sikuitegemea na sikuitegemea kwa sababu sikuwepo na pili niombe tu labda naweza nikawa wa kurudia rudia hoja za wenzangu, hii ni kwa sababu sikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutokuwepo kwa muda huu lakini bado nikarudi nikiwa salama na nimeungana na wezangu katika hoja hii ya kuichangia hotuba ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msemo wa kabila moja huwa wanasema mnisamehe lakini kwa wale ambao litawagusa kwamba neno la mtu mfupi husikika jioni.

**NAIBU SPIKA:** Wafupi wote ndiyo wameguswa?

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hata huyo binadamu anayezungumzwa mfupi ni kwa nini asikilizwe jioni ni makosa, tunapaswa wote kuwa sawa katika kusikilizwa kwamba huyu ni mrefu, maana ya usemi huo katika kabila hilo ni kwamba mtu akitoa hoja au atakayeanza kujibu pamoja na kuwemo hawa wafupi yule aliyesema ile hoja atabaki kuangalia wale warefu kwa sababu ni warefu, kumbe hawa wafupi sasa wapo kwapani na chini chini huku kumbe na wao wanahoja sawa na wale warefu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hii Wizara ni sawa sawa na Wizara zingine, tuifikirie sawa na Wizara zingine kwa sababu ni Wizara mpya tusije tukaiweka katika upya wake hapana, tuilinganishe vizuri sambamba na Wizara zingine katika Bajeti

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashindwa kuelewa tunaposema Tanzania haina wafugaji bali ina wachungaji, ukiulizwa Tanzania inajishughulisha na shughuli gani za kiuchumi, tunasema ni ya wakulima na wafugaji na wafanyakazi lakini hakuna mahala pameandikwa ni ya wakulima na wachungaji na wafanyakazi, hebu tukubaliane sasa tunarudije katika mfumo wa ufugaji tuendane na tamko letu, tunafuga vipi ili tutoke huko ambako wanasema Tanzania hatufugi bali tunachunga, mchungaji ni wa dini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wafugaji wana sababu kwa nini wanahama, hakuna mtu anayependa kuacha mji wake, wanahama kwa sababu ya kukosa huduma,

huduma yao ni maji, malisho na soko, wafugaji tukikubali tuwaweke sehemu moja hakuna anayekubali kuhama nyumbani kwakwe, akihama ana sababu aidha, anabanwa na njaa au anabanwa na tatizo lingine lakini kwa mfugaji kwanza mara nyingi huwa anahitaji msaada, ng'ombe wakimzidi hata mwishowe huwa anashawishika kuoa mke zaidi ya mmoja kwa sababu anataka mifugo yake iwe na amani, lakini kama pana maji, malisho, dawa zipo na yenye ruzuku sidhani kama atahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara hii pamoja na ufinyu, nilimwona juzi Waziri Mheshimiwa John Magufuli akisema kwamba kidogo nilichonacho nitajitahidi kukitumia, basi ajitahidi kweli kukitumia katika mahitaji hayo, wafugaji hawawezi wakaenda Njombe kwa kina Makwetta huko ambako wanafukuzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba tuweze kuwafikiria hawa kwa sababu wanapohama wanawaacha wake zao katika hali ipi, mwishowe hata janga hili la UKIMWI litahamia kwa wafugaji, naomba Serikali pamoja na huo ufinyu ili tuweze kuwaweka wafugaji mahala. Mfano mzuri ni marafiki zangu hawa Wamasai mbona wamepelekewa neno la Mungu wamelitii, tunaona kwenye vyombo vya habari kwamba sasa badala ya kufanya matambiko yao ya namna fulani umefika wakati sasa wamepelekewa neno la Mungu wametulia na wanasikiliza vizuri. *(Makofi)*

Sasa leo neno la ufugaji watalikataa kweli. Naomba jamani Serikali tufike mahali tukubali kwamba sisi tuko tayari kama wafugaji tutatulia, la maana kwamba tunapoweka Bajeti tuweke mazingira ambayo yatawatuliza wafugaji waweze kukaa katika sehemu moja na familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sawa mimi sijakataa maandalizi ambayo yanawekwa na Wizara hii ya kuweka viwanda, ya kuweka na mambo mengine. Lakini niombe katika Bajeti hizi tunazoziweka katika Wizara hasa hasa Wizara hii inayozungumziwa. Elimu tu, ukimuelimisha mfugaji kwamba kata ng'ombe 100 peleka mahali fulani kwa maana ya kwamba tayari umemwandalia soko. Kata tu ng'ombe 100 wauze ili baadaye hela hii utakayoipata unaweza ukaifanyia mambo kadha wa kadha. Tufike mahali hata kama ni semina hizi ziteremke kwa wafugaji hawa kabisa. Narudia msemo niliousema kama watu wa dini wameweza kueleweka kwa nini sisi Serikali tusieleweke? *(Makofi)*

Naomba kabisa hizi semina ziteremko huko, tuitoe elimu ya ufugaji bora. Wamehama jamani Wasukuma wangu, Wamasai, Wanyaturu na Wagogo mnisamehe labda ninyi huwa mnajisifu kwamba huwa mnabaki. Lakini wale wote waliohama nadhani ni kwa kukosa tu elimu. Mtu anapoteza ng'ombe 1000 mpaka 3000 maana yake nini Tanzania hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu niwaambie kitu kimoja, katika ufugaji huwa tunasema ng'ombe hapotezi kitu chochote katika mwili wake bali sauti yake. Hata sauti nayo inauzwa mbona kwenye simu zenu kuna watoto wanalia wanafanya nini, wekeni milio ya ng'ombe ili kusudi kila kitu kitumike kwenye ng'ombe hapo ndipo mtajua faida ya kuthamini mifugo maana yake nini, kila kitu kinatumika. Tutakuja kumsikiliza mtu mfupi huu muda umeshapita. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba kabisa, Wizara hii mimi ninamwamini sana Waziri Magufuli, kila sehemu alipopita huwa ni vyema tu yeye. Sasa kapewa Naibu Waziri wake naye ametoka kwenye kundi la wafugaji ni Mkurya. Sasa leo Wizara hii idumae, itadumaa kwa vipi, tuwaungeni mkono hawa ni watu shupavu kabisa watatufikisha mahali mimi ninaamini hii Wizara itakwenda tu hawa wanatoka katika maeneo ya ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende haraka haraka sasa kwa wavuvi. Pamoja na makelele yangu haya nimesikia kengele. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Wavivu.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi, siyo wavivu wewe hutoki huko kwenye eneo la wavuvi. Ninachotaka kuzungumza na wenyewe pia wanahitaji hivyo hivyo suala zima la kuelimishwa, mimi nasema kuelimishwa kwa sababu hivi hizi nyavu wanazitoa wapi kama siyo madukani, wenye maduka wanazitoa wapi kama siyo vibali vya Serikali? Wanavitoa mahali ambapo Serikali inajua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba tu kwa haraka haraka kwamba kama tunawabana hawa tubanane wote, kuanzia Serikali unapochoma nyavu za mvuvi lazima pia uangalie hivi kazitoa wapi um-*trace* huyu mahali alipozitoa ili wote tuingie katika adhabu hii. Kwa nini tuangalie mwisho tu. *Okay*, labda wakati mwingine wanazipata hata kwa magendo inabidi haya magendo si Serikali inapaswa kudhibiti?

Kwa mfano, ukimchukulia Mkerewe Kanda ya Ziwa siwezi kuongelea Pwani, mimi sijaishi huko. Niongelee Ziwa Victoria, samaki wanaishi, tunasema hivyo, watakapoisha Mkerewe aliyezaliwa tangu mwanzo hajui jembe, anajua tu kuvua leo uje umwambie hapana kuvua Ziwa Victoria hatujaunda kundi fulani la ajabu la kushinda njaa ili Serikali hii iwalishe. Niombe katika hili hata tunapozungumza samaki wanaisha sasa ndiyo tupambane, Bajeti zetu zinazungumzia katika suala zima la kuisha samaki, tunaangalia tu wazito wanajenga majengo yao wanaweke vyombo vyao katika fukwe katika maeneo ya mazalio ya samaki, tupo tu tunaangalia. Tunayajua maeneo lakini vibali vinatoka kwetu Serikalini tukubali hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo kwa mfano kama Mwanza kule maeneo ya Ukanda wa Magu watu wanajenga tu kwa nini tusiwe na nguvu ya ziada kufuatilia sasa maeneo ambayo mazalio ya samaki yanavurugwa na samaki kwa maana ya mayai wanatoa mayai mengi kiasi kwamba tukidhibiti kwa muda fulani samaki watakuwa wengi Ziwani. Naomba kabisa tuwe *serious* yaani tuwe makini kweli na kudhibiti maeneo ya mazalia ya samaki tutafika. Lakini kumkataza Mkerewe asivue jamani ni kumuua kwa sababu tangu aanze hajui jembe, yeye kukicha ni Ziwani, sasa leo utamwambia kaa na huyu mkubwa je, tuna neno gani la kumwambia kaa twende wote pamoja hao ndiyo wanatuvurugia maeneo na kulipua bomu wapi na wapi Mkerewe analijua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wote pamoja kama tunambana mdogo na mkubwa tumbane na wenyewe waone. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, jamani katika hili basi tuweke na vyombo vinavyozunguka majini. Mimi nilipozama na wenzangu nilidhani nitaokolewa walau na chombo cha Serikali badala yake niliokolewa na Wakerewe kwenye mitumbwi. Sasa naomba basi viweko na vyombo vya doria vya kupita hata tunapozungumza sasa kwamba tunadhibiti hapa, hayo maeneo basi yalindwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, lakini ninasisitiza chombo cho doria. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nikupe shukrani kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa lengo la kutaka kuiunga hoja hii mkono. Hata hivyo yapo mambo kadhaa ambayo nitapenda Serikali inipe majibu ama ya sasa hivi ama inipe majibu kwa ajili ya ufuatiliaji wa baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme kwamba mimi ni Mjumbe wa Bodi ya *TAFIRI* lakini katika bodi yetu hii tumekuwa tukiomba sana Serikali isaidie. Napenda nishukuru kipindi ambapo tumeweze kujengewa ofisi lakini tuliahidiwa kupata maabara ambayo bado hatujaipata. Tuliomba wafanyakazi waangaliwe mishahara yao hasa watalaam naomba kushukuru kwamba haya yamefanyika. *(Makofi)*

Ninachopenda kusema ni kwamba uvuvi bila utafiti maana yake ni uvuvi wa kijadi na uvuvi ambao siyo wa kisayansi. Hatuwezi kupiga hatua kama tutasema zama tulizonazo hizi bado ni zama za kuacha tuendelee kuwa na uvuvi usio wa kisayansi. Lakini huwezi kuunda kitu kinaitwa *TAFIRI* taasisi ya utafiti Tanzania kuhusu samaki halafu wale watalaam wake tuliowapandishia mishahara ukawajengea ofisi, ukishindwa kuwapa mahali pa kufanyia utafiti ambao ni maabara wachunguze lakini ukashindwa kuwapa fedha za kufanyia utafiti huo halafu ukasema kwamba utafanikiwa ipasavyo katika uvuvi wa samaki katika Ziwa, katika mito na hata katika bahari. Naomba suala hili liangaliwe na *TAFIRI* ipate maabara na vile vile wale watafiti wapate fedha za kufanyia utafiti. *(Makofi)*

Uvuvi katika Ziwa Victoria ambalo pia mimi ni mdau kwa sababu nikiwa Mbunge wa Muleba Kaskazini kata zangu 10 ziko katika nchi kavu, kata zangu mbili ziko katika Ziwa Victoria zenye jumla ya vijiji nane. Mimi niruhusu nisome hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 86, napenda nimpongeze kwa sababu Wizara imepata mradi wa kusimamia uvuvi katika Ziwa Victoria ambao unahusisha nchi tatu, Tanzania, Kenya na Uganda na mfadhili mkubwa katika mradi huu ni Umoja wa Nchi za Ulaya. Kitu ambacho mimi sijui kama kiko sahihi katika mstari wa mwisho anapoelezea ibara 127 anasema katika mwaka 2007/2008 kazi zifuatazo zimetekelezwa, naomba nisome ile ya namba moja anasema, kuandaa mwongozo wa Kikanda na Kitaifa wa kuanzisha na kusimamia vikundi vya ulinzi wa rasilimali ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vikundi anavyovizungumza na huu ulinzi anaouzungumza unaosimamia rasilimali ya uvuvi katika Ziwa Victoria, mimi napenda nipate pengine maelezo au nieleze mimi kwa jinsi ninavyofahamu kuhusu hivi vijiji vyangu nane ambavyo viko ndani ya Ziwa Victoria ambavyo kazi kubwa inayowaingizia kipato na kuendeleza maisha ni uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba wananchi ambao wamekuwa wanashughulika na kazi ya uvuvi wana taabu ya hali ya juu sana kuhusu ulinzi. *BMU* imeanzishwa mimi napongeza sana. Lakini *BMUs*, katika maeneo mengine zimegeuka kuwa ni za faraja. Lakini katika baadhi ya maeneo zimegeuka kuwa ni za matatizo kwa sababu hazina namna ya kuziendesha ila wanaendesha kwa kujitegemea. Sasa pale ambapo vijiji havina uhusiano mzuri na *BMUs* uongozi wa Serikali za vijiji imekuwa sasa wanaokandamizwa kutaka kugharimia hizi *BMUs* ni wasafiri katika mitumbwi. *(Makofi)*

Suala hili linakuwa ni la kero kwa sababu tulikwishamaliza kero ya wasafiri katika vyombo walikuwa wanatozwa fedha mara wanaposhusha mizigo yao ama wanapokwenda kuingia katika boti zinazokwenda katika hivi visiwa. Sasa suala hili tena limerejea mfano mwalo wa Kyamkiki unalalamikiwa sana kwamba unatoza kila anayeingia na kifaa chake ndani ya boti. Lakini eneo lingine visiwani linalalamikiwa sana ninapozungumza hivi nimefanya ziara kabla sijaja hapa katika hili Bunge lako ambayo nilimaliza tarehe 1 Juni, 2008. Kwa hiyo, ninazungumza kitu ambacho nina uhakika nacho. *(Makofi)*

Lakini ninapenda niseme mwezi Aprili, 2008 tulipokuwa hapa Bungeni wavuvi wa Kisiwa cha Kinagi walivamiwa na majambazi yalikuwa mengi yalikuja na boti karibu nne wamevamiwa tangu saa nne za usiku mpaka saa nne asubuhi kumekucha kweupe majambazi yanaringa, yanatamba ndani ya Ziwa Victoria karibu na hiki kisiwa. Kilikuwa ni kilio cha kutisha sana simu zimepigwa lakini hakuna majibu yaliyoweza kupatikana. Mwisho wamekuja kupata walinzi ambao ni askari wetu polisi saa kumi za jioni. Wananchi waliwafukuza kwa sababu waliona hawana manufaa yoyote. Lakini mimi naitetea polisi. Kwa nini naitetea polisi, polisi haina chombo cha kufanyia doria chenye uhakika ndani ya Ziwa. Polisi hawana mafuta, mimi ninapokwenda katika hili Ziwa huwa naondoka si chini ya lita 600 sasa unapompa askari polisi lita 20 ukimpa lita 50 sijui, katika kifungu cha dharura ambacho hakieleweki ili aende katika Ziwa hawezi kusaidia kazi yoyote. *(Makofi)*

Mimi naomba litengwe fungu maalum kwa ajili ya kuweka ulinzi katika visiwa. Serikali iangalie katika fungu la dharura inunue chombo cha kufanya doria katika Ziwa Victoria kuwanusuru wavuvi maisha yao, kunusuru vyombo vyao na mali lakini kuwapa imani na Serikali yao kwamba na wenyewe wanaangaliwa. Kwa hiyo, Wizara hii imeundwa pia kuona kwamba sekta ya uvuvi inapewa nguvu na wavuvi wenyewe pia wanaangaliwa na zana zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba suala hili liangaliwe kwa makini na naomba Serikali ilichukulie kwa uzito wa pekee ili wananchi waache kuendelea kuwa wanalalamikia na wanapoteza mali nyingi sana kwa sababu tu hakuna ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma pia katika kitabu hiki naona inajengwa mialo sita katika nchi kavu ya Ziwa Victoria (kwenye Bara). Lakini nikawa najaribu kutazama kwa sababu na mimi kama alivyokuwa Mheshimiwa Maria Hewa, sikupata nafasi ijumaa sikuwepo lakini nilikuwa najaribu kuangalia kitabu mialo hii kwa nini haijajengwa ndani ya visiwa? Wilaya ya Muleba moja ya mapato yake makubwa inayoyapata yanaendesha Wilaya ya Muleba yanatoka katika Kisiwa kinaitwa Kelebe kingine kinaitwa Goziba. Visiwa hivi havijawahi kufikiriwa kwa nini? Kwa sababu usipoipa mialo uendelee kujua kwamba ile namna yake ya vyombo kugoa pale ni ngumu, kuingia na kutoka kwake ni kugumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Serikali iangalie uwezekano wa kujenga mialo katika visiwa vilivyo ndani ya Ziwa lenyewe. Mimi napendekeza kisiwa cha Mahaiga, makao yake makuu ya Kata kipate mwalo mzuri. Mimi napendekeza Kitua, Kijiji ndani ya Kata ya Bumbile kipate mwalo na pia napendekeza Kijiji Kelebe makao makuu ya Kata ya Goziba na wenyewe wapate mwalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hizo hoja zangu mbili naomba niende hoja ya tatu. Naomba niseme moja kwa moja kwamba wakati Bunge linafikia maamuzi ya kubinafsisha *ranch* za *NARCO* mimi nilikuwa Mbunge ndani ya Bunge lililopita. Kwa hiyo, katika maamuzi hayo nilikuwepo. Kwa hiyo, ninaposimama hapa kuzungumza sizungumzi kutaka kupinga uendelezaji wa ufugaji katika *ranch* hata kidogo. Naunga mkono nchi yetu isimame na ihakikishe kwamba inaendeleza ufugaji endelevu ambao utaweza kupatia nchi yetu tija wa kitalaam mzuri. Lakini napenda niseme tulipokuwa tunafanya maamuzi hayo hatukuyafanya kwa lengo kwamba wananchi ambao kwa namna moja au nyingine wakijua ama hawakujua walikuwa wanaishi tayari ndani ya zile *ranch* kwamba watapewa shida sivyo tulivyozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyosema hivyo ninayo barua iliyoandikwa mwaka 2006 na Waziri mwenye dhamana yenye kumbukumbu namba GN.317/544/01 ilikuwa ni tarehe 11 Agosti, 2006 barua hii iliandikwa kwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera ikiwa inafuatilia, ufuatiliaji wa ziara aliyoifanya Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati ule Mheshimiwa Edward Lowassa, katika Mkoa wa Kagera ikiwa moja ilikuwa ni kufuatilia hili suala zima la utekelezaji wa ugawaji wa *ranch* ndogo ndogo lakini bila kuwa wameachiwa wananchi ambao wanaishi katika hayo maeneo. Barua hii kimsingi ilikuwa inasema kama ifuatavyo; naomba machache haya niyanukuu, inasema; "Kwa vijiji ambavyo vimepimwa na vimo ndani ya *ranch* na vinayo miundombinu kama shule na kadhalika na mimi naongeza kama makanisa, misikiti litazingatiwa kwa makini…" Lakini barua ikaendelea katika kipengele kilichokuwa kinafuata kwamba mapendekezo mengine yatazingatiwa ili hatimaye wananchi wetu waishi kwa amani na usalama, nina-*underline* na waweze kujilitea maendeleo bila usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sivyo ilivyo katika *ranch* yangu za Kagoma. *Ranch* ya Kagoma ni *ranch* iliyo ndani ya Jimbo la Muleba Kaskazini ndani ya Wilaya ya Muleba. Ndani ya ile *ranch* kuna vijiji vitatu ambavyo ni Ngenge, Rutoro na Kishuro. Hivi vijiji vimesajiliwa kwa namba 577, 205 na 202.

Kwa hiyo, vijiji hivi vilikuwa vipo ndani ya *ranch* lakini hakuna aliyejua. Nadhani hata *ranch* hawakujua, mimi sikujua hata wananchi hawakujua. Lakini utaratibu wa Serikali ilikuwa kwamba wananchi waitwe washirikishe maamuzi yanapotaka kufanyika, hili halikufanyika. Nilipofuatilia nikaambiwa kwamba siku moja ambayo haijulikani lini uliitwa mkutano niseme lilivamiwa gulio langu ninalo gulio moja ambalo wanajikusanya wauzaji wa mifugo katika Wilaya ya Muleba huwa kawaida unafanyika siku ya Ijumaa. Ndani ya hilo gulio eti ndiyo wananchi wakatangaziwa kwamba wanabinafsishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninapokuwa naomba kura siwezi kwenda kuomba kura katika hiyo kadamnasi, kwanza haikusanyi wananchi wa maeneo hayo tu, pili ni ya kuuza ng’ombe, tatu ni mahali pa starehe. Hivi Serikali imefika wapi huko inafanyakazi zake katika mahali pa vinyweo na gulio ni lini? Sasa matokeo yake wakastuka wananchi wanakuja kuambiwa haya tupeleke viongozi tukawapimie mipaka hawa wanashangaa mimi wananipigia simu mimi nashaangaa, lakini baada ya pale nilikwenda kuonana na Waziri anayehusika Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, napenda nimshukuru alilishughulikia vizuri sana, alinipa nilipeleke kwa Mkuu wa Mkoa, sasa kwa Mkuu wa Mkoa ndipo suala hili lilipoanzia kukwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda haukupita mabadiliko ya Wizara nayo yakaja nikalipeleka kwa Waziri aliyekuwa anahusika wakati huo Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa bahati mbaya Mheshimiwa Diallo alikuwa *busy* sana hakuweza kunipa nafasi ya kuweza kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilipata nafasi ya kumwona Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati huo alikuwa Mheshimiwa Edward Lowassa nikamweleza juu ya suala hili, naye akaniambia kwamba nirudishe suala hili kwa Waziri mhusika na Waziri mhusika akanirudisha kwa *RC. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonisikitika hivi ninavyozungumza bado hili jambo halijapatiwa ufumbuzi, lakini shukrani yangu kwa Mheshimiwa John Magufuli na Naibu Waziri wake wamenipa nafasi ya kunisikiliza. Mimi napenda niwaombe baada ya kunisikiliza na baada ya kuzungumza leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba yafuatayo, kwanza Wizara ijipange upya irudi ikazungumze na wananchi wa vijiji nilivyovitaja. Lakini naomba hili lizingatiwe nimesema hatupingi *ranch*, kwa hiyo, ninachokiomba naomba zisiachwe shule pekee, ikaachwa misikiti na makanisa pekee bila kuwapa wananchi ardhi ya kutosha. Wananchi wa vijijini siyo mjini ni lazima walime, ni lazima wafuge au wachunge na ni lazima waweke miundombinu. Hivi leo kizazi ambacho unakikatia juu ya nyumba na juu ya

shule unageuza hivi tu unawanyang’anya wananchi wote   ardhi hawawezi kuishi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, habari kwamba hili eneo limekaliwa na Wanyarwanda ni la uzushi, linazushwa na wale ambao hawataki hao wananchi wapate ardhi. Mimi ninasema kama kuna Wanyarwanda ambao wamekaa ndani ya ardhi ya Tanzania si kwao waondolewe. Lakini mwananchi wenye haki yake ambaye ni raia wa Tanzania apewe haki yake.

Mimi kwa heshima na unyenyekevu mkubwa naiomba na ninaisihi Serikali kwamba irudi iwasikilize wananchi hao na ikubali kuwapa eneo ili  waweze kupata mahali pa kuishi, kufugia na hizo shule zilizopo waweze kupata mahali pa kukaa na watoto wao waende shule, lakini wawe na amani. *(Makofi)*

Mwisho, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* naiomba Serikali itoe tamko, naomba wale waliopewa hilo eneo waache kuwapiga wananchi, waache kuwashikia bunduki, waache kuweka *fence*, tulikubaliana kwamba wasubiri Serikali itatoa kauli kwamba wananchi wakae wapi na wao wakae wapi?  Lakini tuliomba amani na utulivu uwepo. Sasa hao wabinafsishaji wanaokwenda kuharibu amani hiyo hao ni raia wa wapi labda kweli ni Wanyarwanda, waondolewe.  Lakini kama kweli ni Watanzania wasiotaka kuisikia kauli ya kiongozi wao kule kwenye eneo mimi ndiye ninayekwenda sana kama Mbunge wao waliyenichagua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninawaheshimu na mimi ninaomba waniheshimu na hao waliokuja kuwekeza kwenye eneo langu wapo chini yangu lazima na wenyewe waniheshimu.  Kwa hiyo, naomba Serikali itoe kauli ya usalama na amani katika eneo hilo iwepo wakati Serikali itakapokuwa inaendelea kulishughulikia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda nikushukuru na ninarudia kusema kwamba nitahitaji majibu na hoja niko pamoja nayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:**  Mheshimiwa Mbunge wanasema ili wakujibu vizuri hawajui mwalo ni kitu gani? Mwalo ni nini?

**MHE RUTH B. MSAFIRI:**  Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kitabu hiki imeandika mialo sita itaendelezwa, nitaitafuta kwenye ukurasa alipoiandika, mialo 12 inajengwa. Ujenzi wa mialo sita itajengwa. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:**  Tueleze wenzio tunataka kujua.

**MHE. RUTH  B. MSAFIRI:**  Ni ukurasa wa 86 Ibara 127. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge hebu nisikilize, sisi wengine hatujui mialo, sisi hatujui. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kiswahili ni fukwe na kwa Kihaya neno lililozoeleka mpaka kwa Serikali ninaona ni mialo, sasa maana yake limeandikwa. Kwa hiyo, naomba mlichukulie ni Kiswahili kilichokopwa na limekwisha kukubalika na Kihaya sasa kimekuwa Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Kicheko)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi nichangie Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tunasikitika tu hii Wizara ni mpya na ni Wizara muhimu sana hapa nchini lakini imetengewa fedha kidogo sana. Mimi nina imani Serikali itaangalia upya ili mwaka ujao wa fedha hii Wizara iongezewe fedha za kutosha ili ifanye kazi karibu na wananchi wengi ambao ni wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kwanza kwa kuangalia *cover* ya kitabu hiki wameweka vizuri sana ng'ombe bora, samaki, kuku wa kisasa, nguruwe, lakini wamesahau kuku wa kienyeji. Mkoa wangu wa Singida ndiyo unasifika sana kwa kwa ufugaji wa kuku wa kienyeji na sasa hivi tunafanya mapinduzi ili tufuge kuku wengi zaidi baada ya barabara zetu kutengenezwa. Sasa hivi soko kubwa la kuku wetu ni Dar es Salaam na sasa hivi Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hao kuku tunawafuga kienyeji kweli kweli. Tunaiomba Serikali itusaidie, tunataka kufuga kisasa na tufuge kuku wengi zaidi ili watu wafaidi zaidi. Ni kuku ambao kwa kweli wanakula chakula cha asili hakuna dawa za ajabu ajabu zinazoongezwa na mayai yake, wanakutana jike na dume ndiyo linatoka, siyo hao kuku wa kisasa yai linatoka bila jogoo kufanya kazi yake. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri atilie mkazo ufugaji wa kuku wa kienyeji hasa katika Mkoa wa Singida na Mikoa ya jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo la dawa, tuna tatizo la uwezo wa kuweza kufuga kuku wengi, wasaidieni wananchi wetu wapate mikopo, wafuge na ikiwezekana mimi huwa nasikia maafisa mifugo tu, lakini maafisa kuku sijawasikia huko kwenye Wilaya zetu. Kwa hiyo, naomba hao maafisa kuku watafutwe, wakasaidie wananchi wetu. Ni zao ambalo kwa kweli tukiliangalia kwa makini linainua sana uchumi wa nchi yetu na linawapa wananchi wetu kipato cha kutosha sana. Kwa hiyo, mimi ninamwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake na watendaji wake watembelee Singida na siyo waishie Singida Mjini wafike vijijini wakaone jinsi ambavyo wananchi wetu wanaofuga ili waweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija upande wa mifugo. Wenzangu wamekwishasema inasikitisha sana kuona Serikali bado haijaamua kuwasaidia wafugaji, kuwasaidia wapate ng'ombe bora wa maziwa na nyama na kwa kuwasaidia wapate maeneo ya malisho ya mifugo yao, kuwasaidia wapate maji ya kutosha kwa ajili ya mifugo. Sasa hivi fedha zinazopelekwa Wilayani kwa uchimbaji wa malambo ni fedha

kidogo sana, shilingi milioni 10 haziwezi kutosha kuchimba bwawa la kutosha kwa mifugo ya eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wafugaji wengi hawahami, wamesema wenzangu wanalazimishwa tu kwa sababu hakuna maji, na kama wakipatiwa maji ugomvi kati ya wakulima na wafugaji utakwisha. Kwa hiyo, mimi ninaomba sana Serikali iliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji, nirudie kusema, sisi wa Mikoa kame, Mikoa hii ya Morogoro, Dodoma, Singida, Arusha, Manyara, Shinyanga na Tabora, sehemu ya Mwanza na Mara tuliambiwa kabisa kwamba kuna mradi ambao utakuja maalum kwa ajili ya kuchimba mabwawa makubwa kwa ajili ya mifugo yetu, kama siyo kuchimba mabwawa kuzuia haya makorongo yaliyoko kwenye maeneo yetu ambayo wakati wa mvua huwa yana maji mengi sana, tunaomba mtusaidie kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kwenda mbele kila mwaka tutakuwa tunasema tunapanga mipango, hii mipango itakuja kukamilika lini? Sasa hivi ni utekelezaji. Maji mengi sana yanahitajika kwa ajili ya wanyama wetu, kwa ajili ya kufuga samaki, haya makorongo yakizuiwa, tutapata samaki, ng’ombe wetu watapata maji, wakulima watalima bustani na kadhalika. Kwa hiyo, naomba sana suala hili tulizingatie. Ng’ombe tunawaofuga sisi hawana faida, kwanza nyama haina kiwango kile kinachotakiwa. Sasa mimi nawaomba ili tuweze kupata faida, wananchi wetu wapate faida, Serikali yetu ipate faida, tuanze kutumia madume bora na siyo lazima tupate madume bora, madume bora yako, ukienda kule Usa-Naiki kuna madume ambayo kazi yao ni kutoa mbegu tu, hawana kazi nyingine. Wanalishwa vizuri na kutoa mbegu kwa aliji ya ng’ombe wa nyama na ng’ombe wa maziwa. Sasa sisi tunaiomba Serikali kupitia Halmashauri zake, hili liwe jambo la lazima na hii itasaidia kuwapa faida wananchi wetu badala ya kuswaga mchana kutwa, jioni anawarudisha. Anafuga ng’ombe wachache wenye ubora na kwenye eneo dogo lakini mpaka leo Serikali haitilii mkazo. Sisi tunaomba sana iwe lazima na Serikali itoe pesa bila hivyo tutaendelea kuwasikia wenzetu Botswana, Botswana, wenzetu wanafanya hiyo kazi, lakini kwa nini Serikali yetu imeshindwa? Kwa nini Serikali imeshindwa kutenga pesa kwa ajili ya kuboresha mifugo yetu. Kwa nini haitengi fedha kwa ajili ya madawa ya mifugo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia kwenye kitabu ukurasa wa 114 na 115, majosho yalipangwa kukarabatiwa mwaka 2007/2008. Ukienda Mkoa wa Singida, iko Halmashauri ya Wilaya ya Singida na Manyoni. Ukienda ukurasa wa 115, majosho yaliyopangwa kujengwa 2007/2008 iko Manispaa Manyoni na Singida. Hivi Waziri hujui kwamba Iramba kuna wafugaji wengi kuliko hata maeneo haya mliyoyataja? Kwa nini haikupewa mpango wa kujenga majosho mapya na kukarabati ya zamani? Nitapenda nipate majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wanahangaika huko, lakini Serikali haitusaidii. Kwa hiyo, naomba sana nipate majibu na naomba mfahamu kwamba Iramba iko ndani ya Mkoa wa Singida, mnapopanga mipango, msije mkatusahau. Sisi hatujahamia Manyara, wala Shinyanga wala wapi, tuko Mkoa wa Singida. Wakulima

wetu na wafugaji wetu wanataka wapate msaada. Ukienda maeneo Nyahaa, Endasiku, Mwangeza, Dominiki, kuna wafugaji wengi ambao hata hawasumbui kwa kuhamahama lakini tunataka msaada wenu, wapate maji ya kutosha na madawa ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Ugani mliosema, bado hawajafika kwenye vijiji vyetu vyote Tanzania. Tunaomba mfundishe watu wengi zaidi na tunawaomba Maafisa Mifugo wasiwe 'Mamangimeza', waende kutembelea vijiji vya wafugaji, waende kutembelea vijiji vya wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu nina Mto Sibiti, unatusaidia sana kutupatia samaki wengi sana na ndiyo tegemeo letu na Ziwa Kitangiri lakini Maafisa wa Uvuvi hawatoshi. Kwanza kama huku Mto Sibiti, Iramba Mashariki hatuna Afisa Uvuvi kabisa. Kwa hiyo, naomba sana mjitihadi kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu niliyokuwa nayo ni hayo tu. Nakushukuru, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa atafuata Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, yuko Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, yuko Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, yuko Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, yuko Mheshimiwa Jacob Shibiliti, yuko Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko na yuko Mheshimiwa Riziki Lulida. Naomba hawa wawe karibu.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika Wizara hii muhimu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo maarufu inajulikana kama Wizara ya Kitoweo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze rafiki yangu Mheshimiwa Magufuli, Waziri wa Mifugo, Naibu Waziri na Watendaji wake wote, kwa jambo moja tu kwamba wanajiamini, hata hivyo wametupa matumaini Watanzania kwamba wanaweza. Kwa hivyo, tunategemea kwa sababu wamejiamini na nasema wanaweza, yatokee mabadiliko katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimpe pole na kweli nimshangae kidogo Mheshimiwa Magufuli kwa jinsi anavyojiamini. Anajiamini vipi kwa Wizara hii ambayo ni mpya na bajeti imepunguzwa kwa bilioni 6 kutoka bilioni 47.9 ya mwaka jana ingawa mwaka jana haikuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi lakini ukijumlisha unapata bilioni 47.9 na mwaka huu bilioni 41.8, bilioni 6 zimepungua, atafafanyaje kazi? Atatumia miujiza gani? Kwa hiyo, nampa pole kidogo kwa hili pamoja na ujasiri wake lakini kule Pemba kuna usemi wanasema kwamba ngoma ipigwavyo ndivyo ichezwavyo. Hii ni ngoma nzito Mheshimiwa Magufuli lakini tunakuamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni mpya toka 2006 mpaka leo bado ni mpya, 2006/2007 ilikuwa mpya kwa sababu ilitoka katika mikono ya Wizara ya Kilimo, ikaanza kutengeneza Sera, Sera za Kitaifa za Mifugo ambayo nadhani ilimazika mwezi uliopita tu hapa. Lakini kabla haijakaa sawa, wameongezewa uvuvi mwaka jana na sasa

hivi wameanza mchakato wa kukarabati Sera ya Taifa ya Uvuvi. Mabadiliko haya ya mara kwa mara katika Wizara zetu yanadhoofisha Wizara. Kwa kweli, unaupa wakati mgumu watendaji wetu na wataalam wetu katika kazi hizi. Wizara hii kama ilivyo Wizara ya Kilimo kwa sababu Wizara nne ikiwemo Wizara ya Mifugo na Uvuvi zinafanya Wizara ya Sekta ya Kilimo. Sekta ya Kilimo nayo hivyo hivyo, imepata matatizo hayo hayo. Imeondolewa Wizara ya Umwagiliaji imepelekwa katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Nilikuwa namwona hapa rafiki yangu Mheshimiwa Wasira wakati anafanya majumuisho ya michango ya Waheshimiwa Wabunge anapata tabu, anazungumzia kilimo, anataka kuzungumzia maji anashindwa kwa sababu anajua maji iko Wizara nyingine. Sasa kwa kweli kilimo cha wakati huu cha kisayansi utazungumziaje kilimo bila ya maji? Hatukatai mabadiliko, lakini sasa mabadiliko haya yakifanywa mara kwa mara kwa kweli yanaleta matatizo. Hata mabadiliko ya Mawaziri ya mara kwa mara kuna Mawaziri wamebadilishwa mara kama nne hivi katika kipindi hiki. Kipindi hiki cha miaka mitano wamekanyaga Wizara nne. Sasa nafikiri ufanisi wenyewe sijui kama wanaweza kupimika vizuri kwa hali kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nijikite katika uvuvi. Mimi naishi Visiwani na kazi yetu kubwa kule ni uvuvi. Nataka nizungumzie kuhusu uvuvi wa baharini. Utafiti uliofanywa na Shirika la Chakula Duniani *(FAO)* mwaka 2002 imeonyesha kwamba Tanzania ni tajiri mno kwa samaki na imeiweka Tanzania ni ya kumi bora (*Top Ten)* katika Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti mwingine ambao umefanywa ni kwamba Tanzania wanaweza au tunaweza kuvua kiasi cha tani 730,000 kwa mwaka. Wameorodhesha Wilaya kama 13 ambazo zinafanya ukanda wa baharini Tanzania, ikiwemo Muheza, Tanga, Pangani, Bagamoyo, Kinondoni, Ilala, Temeke, Mkuranga, Rufiji, Mafia, Kilwa na Mtwara. Maeneo haya wakati huo walikuwa kama wavuvi au watu kiasi cha milioni 20 lakini katika taarifa hii ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba wavuvi wadogo wadogo ni kwamba makisio yao ni tani 43,418 tu. Sasa utakuta ukilinganisha na yale makisio ambayo yamefanywa na vyombo vya kimataifa ni kama tunavua asilimia 5.9 tu. Kwa kweli huu ni msiba, ni hasara, watu wengi kama hao na samaki tunao wengi kiasi hicho lakini tunavua asilimia 5.9 tu! Kweli jambo hili linafaa liangaliwe vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini takwimu hizi nafikiri ni kwa sababu ni takwimu za wavuvi wale wa biashara hazipatikani na meli zipo, lakini idadi ya kinachovuliwa hakijulikani. Mheshimiwa Waziri anasema kwamba kuna meli 69 ambazo zina leseni na kuna meli 140 hazina leseni lakini kinachovuliwa hakijulikani. Hii ni hasara lakini tunajua nchi ambazo zinavua hapa, sasa kama hatuwezi kuwazuia wasivue kwa nini basi leo tusiwaambie msituibie samaki wetu? Wanakuja hapa wanavua wanavyotaka wanaondoka lakini hatuwazui kwa sababu pengine hatuna uwezo lakini vile vile kuwaambia kidiplomasia jamani mbona mnatuibia samaki, sisi ni wanyonge! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna dalili za ufisadi ndani yake. Itakuwaje sasa tuwaachie rasilimali zetu hizi zinachukuliwa bure, sisi tumekaa kimya tu jamani. Japo

hatuna uwezo lakini hatuna mdomo wa kusema? Inawezekana hapa kuna ubadhirifu na kuna *element* za ufisadi ndani yake. Kwa hiyo, hili jambo nafikiri tuliangalie vizuri ili tuhakikishe kwamba tunapata rasilimali yetu na kuitumia vizuri kwa sababu ni yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi, kwa mtazamo wa watu wengi, unapozungumzia uvuvi, unakuta ni mtu ambaye ni wa hali ya chini, dhoofu, hana *future*. Huo ndiyo mtazamo wetu. Lakini ni kweli, mvuvi ni sawa sawa na mkulima. Lakini uvuvi kwa wenzetu kwa mfano kama Japan, ni mtu muhimu na ana heshima. Lakini uvuvi kwa wenzetu kwa mfano Japan, ni mtu muhimu, ana heshima kama injinia. Lakini uvuvi tumeudharau, hata Serikali imedharau uvuvi, bajeti hii ndogo haina nia ya kuuendeleza uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mfano mmoja ambao naweza kutoa hapa. Kwa mfano kule Zanzibar walianzisha shule za michepuo ya Kilimo, ya Uvuvi. Wale wanafunzi ambao wamefaulu katika shule hizi za Sekondari za michepuo ya uvuvi walikuwa wanajisikia vibaya sana, kama ni watu wanaodharaulika dharaulika hivi. Kwa hiyo, ili tuupe heshima uvuvi kama wanavyoupa heshima watu wa Mataifa mengine, lazima tumfanye mvuvi kuwa ni mtu anayezalisha na anayefaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tufanye nini katika hili? Kwa sababu mambo siyo mazuri, mimi nazungumzia uvuvi wa bahari lakini kuna uvuvi wa ziwa na mito na kadhalika, huku baharini tu tunavua asilimia 5.9, wakati mnao uwezo wa kuvua samaki wengi sana. Sasa nini tufanye, labda tuiulize Ilani ya CCM inasemaje. Ilani ya CCM ukurasa wa 32 inasema, Serikali itawasaidia wavuvi kutumia maarifa ya kisasa ya uvuvi ili kuongeza ufanisi na mapato yao. Hivi ndivyo Ilani inavyotuambia. Je, hali ndiyo iko hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wetu hawatumii maarifa yoyote ya kisasa. Wavuvi ni kama wakulima. Wakulima hawatumii elimu ya kilimo cha kitaalam, wavuvi ndiyo hivyo hivyo. Wakulima dhana zao ni duni, wavuvi ndivyo hivyo hivyo wanatumia vyombo duni kabisa. Sasa hapo ndipo tulipofika sasa hivi. Ilani inasema hivi lakini hali halisi ndiyo hiyo! Sasa tunafanyaje? Ni lazima tuwapatie wavuvi wetu zana za kisasa za kuvulia. Zana ambazo zitatuambia kwamba pale pana kiasi gani cha samaki ili avue halafu awe na vyombo vya kuhifadhi samaki wake, awe na majokofu ya kutosha, halafu anapokwenda kwenye *landing site* ambazo tunazo nyingi tu kama 232 waweze ku-*store* samaki wao vizuri wakati wanasubiri soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kilimo, kuna utaratibu wa stakabadhi ya mazao ghalani, kwa nini tusifanye kwenye uvuvi? Wavuvi kwa kweli wanapovua wakati mwingine hawajui waweke wapi samaki wao. Safari moja nilikuwa Lindi kule, walikuwepo wafanyabiashara kutoka Dar es Salaam, wananunua samaki, wana ma-*freezer* lakini baada ya kuondoka tu pale basi hawana pa kuhifadhia samaki, wanauza samaki watano kwa shilingi 200, kweli mvuvi hapo anafaidika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli uvuvi wa kisasa uwe na zana za kisasa. Tuangalie kidogo mchango wa uvuvi katika pato la Taifa. Kwanza, uvuvi unashuka

badala ya kupanda. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri kasema kwamba uvuvi unakua kwa asilimia 4.5 kutoka asilimia 5, sasa huko si kukua ni kushuka. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi wetu umeshuka kutoka asilimia 5 mwaka 2007/2008 hadi asilimia 4.5. Lakini vile vile uvuvi katika pato la taifa umekuwa vile vile *stagnant* kwa muda wa miaka mitatu ni 1.6%. Hii ndiyo hali halisi. Sasa mambo haya hayajaja kwa bahati mbaya. Ni kwa sababu Serikali haijajipanga vizuri kwa sababu miundombinu yetu ni mibovu. Wakati mwingine mvuvi anaona bora apeleke samaki wake nchi jirani kuliko kuleta hapa Dar es Salaam kwa mfano kwa sababu haiwezekani. Kwa hiyo, miundombinu yetu siyo mizuri ya kumfanya mvuvi avue samaki wake na auze anakotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu tunazo leseni ambazo zimepitwa na wakati. Meli zinazovua 140, 69 hazina leseni lakini na pengine hawa-*renew* wanatumia leseni ambazo zimepitwa na wakati. Haya ni mambo ambayo yanapunguza mapato yetu. Halafu kuna vitendo vya rushwa. Kuna kesi ile iliyotokea Lake Victoria, nafikiri mwaka 2003, tani 36,000 zilipelekwa Kenya bila kulipiwa ushuru, Serikali ikapoteza kiasi cha dola milioni 36. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo yanachangia uvuvi wetu kuonekana kwamba hauna tija kwa sababu hatujajipanga vizuri. Mheshimiwa Magufuli, kazi kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuangalie kidogo mfano wa nchi ambazo zimepiga hatua kwenye uvuvi. Mheshimiwa Magufuli anafahamu Namibia, alikuwepo kule hivi karibuni. Namibia ilipata uhuru mwaka 1990 lakini miaka minane tu baada ya uhuru uvuvi umechangia kwa asilimia 10.1 lakini miaka 10 baadaye yaani kufikia leo 2008 inachangia kwa asilimia 23.1. Lakini mambo haya hayakuja bure ni kutokana na Serikali imejipanga vizuri, wametumia teknolojia ya kisasa, miundombinu mizuri, wavuvi wamewezeshwa na kwa hivyo wamevua vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi kama New Zealand mpaka mwaka 1970 waliingizia nchi yao chini ya dola milioni 20 lakini leo hii wanaiingizia nchi yao karibu dola trilioni 1.3 zaidi ya mara hamsini. Lakini kilichofanya waendelee hivi ni kwa sababu wamekubali kuwawezesha akina mama, miundombinu yao na mizuri na kwa kweli wanatumia teknolojia nzuri, wanavua katika kina chochote kile. Kwa hiyo, uvuvi wetu unaweza kukua kama Serikali itakuwa *serious*, bajeti itakuwa nzuri na itajipanga vizuri ili kuzuia eneo lote la ubadhirifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu mradi wa usimamizi wa mazingira wa ukanda wa Pwani. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba mwaka jana alipeleka Zanzibar shilingi bilioni 10 katika bilioni 19 na hapa Tanzania Bara akaacha bilioni 9.
*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Killimbah na Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga na Mheshimiwa Manyinyi wajiandae.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami awali ya yote, nichukue nafasi hii, kwanza nimpongeze Waziri, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kwa kazi nzuri anayofanya katika Wizara hii. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi kwa maandalizi mazuri ya bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi hizo, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, hasa kwa kuuona umuhimu wa kutenganisha hizi shughuli za wafugaji, kuziweka pamoja na wavuvi kulingana na hali ya unyeti wake ulivyo. Kwa hili, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii, kama nilivyoeleza, ni nyeti kama tunavyozungumzia kilimo. Kilimo kinakwenda pamoja na ufugaji. Unapomzungumzia mkulima, utakuwa pia unamzungumzia mfugaji kwa namna moja ama nyingine, kwa maana ya kwamba tunaposema zile asilimia 80 za wakulima nchini, basi katika hizo asilimia 80 lazima zitakuwa zinajumuisha wafugaji. Tunaamini kabisa wakulima wetu bado ni wakulima ambao wanatumia zana duni na majembe ya kukokota ambayo yanaendeshwa na wanyamakazi, kwa hiyo, ili uwe mkulima mzuri, lazima uwe mfugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie juu ya fedha zilivyotengwa kwa Wizara hii, shilingi bilioni 4. Kulingana na unyeti na jinsi kazi yenyewe ilivyo hasa hii ya ufugaji, naamini hizi fedha ni kidogo sana kwa Wizara kiuendeshaji kwa kipindi cha mwaka mzima. Kwa hiyo, kipindi kinachokuja ili kuimarisha Wizara kiutendaji, upo umuhimu wa kutenga fedha za kutosha ili sasa Wizara iweze kufanya kazi yake barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Wizara hii inahusika na mambo ambayo yanamgusa mfugaji na kwa namna moja au nyingine tunaposema mfugaji anaguswa pia mkulima anaguswa. Naona yako matatizo mengi yanayowagusa wafugaji sasa hivi ambayo yanahitaji kutatuliwa ili tumfanye mfugaji awe wa kisasa afuge mifugo yenye tija, yenye kutoa maziwa mengi, yenye kutoa nyama nyingi na mifugo ambayo haitaleta bughudha kwa suala zima la ardhi, malisho na kadhalika. Kwa hiyo, upo uhaba ambao tunauona, hizi fedha zingeongezwa ili kuifanya Wizara hii iweze kufanya shughuli zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tumezungumza wazi kwa katika kipindi cha mwaka 2005/2010 namna ya kumboresha mfugaji wa Kitanzania kwa maana ya kutoka ule ufugaji wa kizamani na kuja ufugaji wa kisasa. Kwa maana ya mfugaji kupata malisho yaliyo bora, kuondoa uhaba wa maji, hizi *water point* lazima ziwekwe, kuwa na malambo kwa maana hiyo, madawa ya mifugo, majosho na kadhalika. Yote hayo ni katika kuendeleza sekta hii ya ufugaji. Sasa unapotenga pesa kiasi hicho cha bilioni 4, naamini kabisa bado hatuwezi tukawa tumekidhi haja ya kujenga miundombinu

katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, nyenzo bado ziko duni. Lakini pia hatuwezi tukasema kwa nadharia tu kwamba tunataka wafugaji wabadilike wawe wafugaji wa kisasa. Hawa wafugaji wanahitaji wapewe elimu, waelimishwe kwamba wanabadilikaje kutoka ufugaji waliouzoea na kwenda ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida, ni Mkoa wa wafugaji na hasa Jimbo langu la Iramba Magharibi, ni Jimbo ambalo tunafuga sana. Sasa vitu hivi nilivyovieleza uhaba wa malambo, malisho duni, madawa ya mifugo hamna, majosho, nimeangalia katika hii bajeti tunayosema bilioni 4 na nimekuja kuangalia mwisho kabisa huku kwenye majedwali namna ya vitu vilivyogawanywa, hii miundombinu ilivyogawanywa na Wizara katika mwaka huu wa fedha, inasikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo eneo kubwa la wafugaji, eneo kama la Msombi, Madalawa, Mayanzani, Mlandala, Ujungu na Msansao. Hili eneo lote ni eneo la wafugaji na wana ng'ombe wengi kweli kweli. Lakini hakuna josho hata moja katika eneo hilo ambalo tumetengewa, tukaambiwa kwamba litajengwa josho ili basi hawa wafugaji waweze kufanya mageuzi katika ufugaji na waende katika ufugaji pengine kwa kuhudumia mifugo yao iwe mifugo bora. Bado wafugaji wa maeneo haya niliyoyataja, tunafuga ule ufugaji wa kizamani. Maeneo haya niliyayotaja yalikuwa ni maeneo ya wahamiaji wamehamia kufuata malisho, sasa wamekaa pale na wamejenga pale, wameingizwa imekuwa ni Serikali sasa na kijiji kipo, lakini ili tuweze kukaa nao hawa watu na Serikali iwajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kwamba pamoja na mambo yote najua na ufinyu wa bajeti jinsi ulivyo na fedha zilivyokuwa ndogo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Magufuli atakapofika mwisho, aniambie juu ya umuhimu kwa hawa wafugaji wangu wa maeneo haya, basi na wao waweze kupata hata lambo moja tu ili mifugo yao badala ya kutoka umbali huo ninaousema maana ukitoka Mayanzani maji wanakuja kuyapata huku maeneo ya Ujungu ambako ni mbali sana. Kwa hiyo, naomba atakapofikia mwisho, aone umuhimu wa kuweza kuwapa chochote kama itawezekana hata tupate josho moja katika maeneo hayo na vile vile tupate lambo katika maeneo hayo, naamini maeneo hayo manne niliyoyataja wote wanaweza ku-*share* na ikawa mambo siyo mabaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia ufugaji wa kisasa, tunahitaji wataalam kwa maana ya Maafisa Ugani ambao wanaweza wakatoa elimu kwa hawa wafugaji na wakatoka katika ufugaji waliouzoea na wakaenda katika ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili, kwa Wilaya ya Iramba, mbali ya hawa tulionao, tunawatumia Maafisa Kilimo, ndio hao wanaotumika hata kwa mifugo, naomba sana tupate hawa Maafisa Mifugo ambao wamesoma, wenye vyeti vya kueleweka, vya masuala ya mifugo ili waweze kukaa katika maeneo haya ya wafugaji. Najua kunaweza kukawa na uhaba lakini hata tukipata wawili, watatu basi watagawanyika katika maeneo hayo ili kuweza kufanya kazi hiyo na kukidhi haja kwa maeneo ambayo yatakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende haraka haraka kwa sababu naona kengele ya kwanza imeshagonga, nizungumzie suala la kuboresha minada, minada ambayo ndio hawa wafugaji kwa namna moja ama nyingine wanaweza wakaenda wakauza mifugo yao. Mimi katika Jimbo langu la uchaguzi, ninayo minada ambayo inakaribia saba au nane. Upo mnada wa Mgongo, Malendi, Mtekente, Usule, Kaselya, Kiele, Kiomboi na Kigaa, ambao upo Luono. Hii minada yote toka wakati ule niseme kwamba haijawahi kukarabatiwa, sasa naiomba sana Wizara ione umuhimu wa kuweza kukarabati hii minada na pia ili iweze kufanya kazi iendane na hali ya kisasa kuliko sasa hivi ambavyo wafugaji wakipeleka mifugo yao wanapata taabu sana kuuzia sehemu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nizungumzie kituo cha Madume ya Mbegu ambacho kipo katika kijiji cha Mkulu. Ni muda mrefu hiki kituo kimejengwa na pale tunalo banda limejengwa lakini hatujaletewa hayo madume ambao sasa wanaweza wakaja wakawa ndio mbegu kwa ajili ya kuweza kupata ng'ombe wa kisasa. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri, atakapofikia mwisho basi aone umuhimu wa kwamba sasa kile kituo cha Mkulu, ambacho kimejengwa na Serikali yenyewe, badala ya kukaa bure basi wamalizie kwa kuleta hayo madume na kiweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie zao la kuku. Mkoa wa Singida ni Mkoa ambao una kuku wa nyama wengi sana. Kwa hali ya sasa, bei ya kuku iko juu sana. Lakini ufugaji wa kuku ambao wanafuga wenyeji wa Singida bado ni wa kienyeji sana. Namwomba Waziri, atupe utaalamu ili sasa wale kuku wa kienyeji wabadilike, liwe zao la biashara. Ninaamini sasa hivi kuku mmoja anakwenda takribani Sh.7,000/= mpaka Sh.8,000/=. Kwa hiyo, ikiwa mfugaji wa kawaida kwenye kaya moja akiwa na kuku 100, anauhakika akiwauza vizuri kwa Sh.5,000 tu atapata Sh.500,000/=. Kwa hiyo, itasaidia hawa watu kuweza kuondokana na hali ya umaskini. Naomba sana utaalamu kuhusiana na suala hili muhimu la kuweza kuwabadilisha wafugaji wa Singida ili kuwa wafanyabiashara badala ya kufuga wale kuku kwa ajili ya matumizi yao ya kawaida basi ili wawatumie katika matumizi ambayo ni ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii, nikushukuru sana na niseme kwamba ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima siku hii ya leo, nami nikiwa hapa mbele yako kuchangia hoja ya Wizara hii. Pili napenda kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufikisha kwa Mheshimiwa Waziri, ujumbe wa wavuvi wa mwalo, Bwiru Mnarani. Wapiga kura wa Bwiru Mnarani au wavuvi wa Bwiru Mnarani, wanaomba Mheshimiwa Waziri, utoe sauti yako kwani sauti yako inasikika zaidi ili waweze kupata mwalo ambao uko mbali na makazi ya watu. Mwalo wanaoutumia sasa hivi uko katika makazi ya watu na suala hili wameshalipigia kelele muda mrefu bila mafanikio yoyote. Kwa hiyo, katika ombi hili, nitamuomba Mheshimiwa Waziri, atekeleze ombi hili kwa kutoa sauti yake kwani sauti yake inakwenda mbali zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kuongelea manyanyaso ya wavuvi hasa katika Ziwa Victoria, ambayo ninayafahamu vizuri. Kumekuwa na manyanyaso katika Ziwa Victoria hasa kwa hawa watu wanaoitwa Bwana Samaki au Bibi Samaki, sijui kwa jina lingine wanaitwa vipi. Watu hawa wamekuwa wakionekana kwa nyakati fulani tu na nyakati hizo wakionekana katika mialo kama Kabangaja, Igombe, Kayenze, inakuwa ni tafrani yaani wavuvi wanaanza kutafutana, wanajua hapa kilichokuja leo ni kimbunga au wenzetu wanaita *Tsunami* ambayo imeingia katika mwalo huo. Hukamata nyavu zao na wakadai kwamba wanakwenda kuziteketeza, lakini watu hawa huzunguka kwa nyuma wakachukua nyavu zilezile wakawauzia watu wengine tena kwa bei nafuu kidogo. Kwa hiyo, hili halifurahishi na wala halipendezi, kama unasema unakamata kitu kuteketeza, kiteketeze mbele ya watu waone na ili wajue kitu hicho kimeteketezwa. Lakini pale unapoondoka nacho na hugeuka ukaenda upande wa pili ukaenda ukamuuzia mtu mwingine, huu tunaweza tukauita ni wizi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, tunaomba ukae chonjo sana na watu hawa, wapo wengi na majina tunayo lakini tunawahifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuongelea suala moja. Hivi karibuni tumesikia kwamba Ziwa Victoria limefungwa, wavuvi wanaovua kwa nyavu wasivue, wavue wavuvi wa ndoana. Hii imepelekea dhahama kubwa sana hasa kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ya ziwa au kandokando mwa ziwa, mboga kwao imekuwa shida. Tangu zamani baada ya kuwa na viwanda vingi kwao mboga ilikuwa shida lakini cha ajabu viwanda vya samaki katika jiji hili la Mwanza, vinafanya kazi kama kawaida. Tunajiuliza hili ziwa limefungwa kwa hawa watu wanaotafuta mboga au umefungwa kwa watu wote pamoja na wa viwanda? Kwa sababu watu wa viwanda ndio wanaovua samaki wengi zaidi au wanaonunua samaki wengi zaidi kuliko mvuvi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uvuvi huo sijui kama Mheshimiwa Waziri, analifahamu hili, hawa watu wa viwanda, wanaovua samaki na wanadai kwamba samaki hawa wao wanawapata, kwa mfano kama samaki wa sangara, samaki wa sangara anapoingia kiwandani kila kitu ni mali sasa hivi hakuna kitu kinachotupwa. Mabondo ya sangara ni mali kuliko mnofu wa sangara, ngozi ya sangara pia ni mali, panki, anapokatwa sangara nyama, anabakia na kichwa na ngozi, nayo pia ni mali, mayai ya sangara ni mali, vipande vya sangara pia ni mali na kuna kitu wanaita samaki wale *reject* ambao wanakuwa na matatizo kidogo ambao hawawezi kuchanwa kwa ajili ya kupelekwa nchi za nje ambao wanakula Watanzania pia ni mali. Lakini tunashangaa watu wanaofanya kazi hizi ni vijana wetu, wanafanya kazi hizi kwa mshahara mdogo, lakini sijui kama Serikali inaelewa kwamba tofauti na chipsi hizo au tofauti na minofu ya sangara hao wawekezaji kuna kitu wanakipata zaidi ya hicho? Kwa hiyo, tunaomba suala moja, kama wawekezaji na viwanda wanaruhusiwa kuvua na wavuvi wa kawaida waruhusiwe kuvua kwa sababu viwanda ndivyo vinavyomaliza samaki ndani ya ziwa Victoria na sio wavuvi wadogowadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo hawa wenzetu wanaohusika na masuala ya samaki wanatumia vibaya nafasi zao. Wanakwenda kwenye mialo, wanawanyanyasa wavuvi katika mialo kwa kuwawekea kiwango fulani angalau kwa mwezi ili wasije kusumbuliwa na zile nyavu, watimize kiwango Fulani na mfano wa

mwalo mmoja uliowekewa kiwango ni mwalo wa Besi. Umewekewa kiwango kwamba kama mnataka tusiwasumbue, mfanye hili na hili lakini mwisho wa mwezi sisi chetu tukikute, hii si uadilifu. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri, watu hawa awafuatilie katika mialo ya Besi ili aweze kuwafukuza kazi mara moja kwa sababu hawawatendei haki wavuvi, wanawanyonya kwa mlango wa nyuma wakati wao wana mishahara yao waliyopangiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia kuna muungano wa Ziwa Victoria wa Afrika Mashariki. Mimi napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, hivi na wenzetu huwanyang'anya nyavu wavuvi wao na wakawachomea au huwapa nyavu mbadala wanapowanyang'anya nyavu zile? Au katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni kipi ambacho wamekaa wakakiongea, ni jinsi gani wataweza kuwasaidia wavuvi kulikoni kuwataabisha wavuvi kwa sababu kama walivyoongea wasemaji waliopita, nyavu hizi wanazinunua madukani na nyavu hizi zinaingia madukani tayari zikiwa zimelipiwa kodi ya Serikali. Kwa hiyo namuomba Mheshimiwa Waziri, wakati anajumuisha anipe angalau takwimu za Afrika Mashariki kuhusiana na nyavu, wanatumia mtindo gani? Kwa sababu kuna maneno ya chini chini tunasikia wenzetu wanachukua nyavu zisizofaa wanawapa nyavu zinazofaa, je, hili ni kweli au limekaa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mkoa wa Mwanza una wafugaji. Tatizo la sekta ya mifugo, wafugaji ni masikini sana na wafugaji si masikini wa ng'ombe, wafugaji unaweza kukuta ni masikini kwa sababu mtu ana mifugo mingi lakini anapoishi kwa kweli panakuwa tofauti kabisa na mifugo aliyonayo. Kwa hiyo, binafsi ninamuomba Mheshimiwa Waziri, wafugaji hao wapate elimu ya kutosha. Wafugaji hawa tunapowaambia wapunguze mifugo tuwafundishe ni jinsi gani ya kupunguza mifugo sio mtu umwambie tu punguza mifugo, punguza mifugo, lakini mtiririko wa jinsi ya kupunguza mifugo humpatii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba wafugaji hawa wapewe taaluma ya kutosha, watakapoelimishwa wanaweza wakapunguza mifugo. Ni kwa jinsi gani watapunguza ni kama watakavyoelekezwa na kupewa mafunzo ya kupunguza mifugo hiyo. Kwani hapa tumeambiwa watu wanakula nyama sana, kwa ajili ya mifugo na kama hii mifugo ni mingi basi watu hawa wasaidiwe ni jinsi gani watapata soko la kuuza mifugo yao, kupata soko ndani ya nchi na nje ya nchi kwa ajili ya kuuza mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake ameongelea kwamba Sheria ya Nyama ilipitishwa mwaka 2006 na mimi nakubali japo yeye mwenyewe ndio kaliongea. Lakini tangu mwaka 2006 mpaka hii leo haijaundwa Bodi ya Nyama na ninapenda nimuulize Mheshimiwa Waziri, atakapofanya majumuisho anieleze hii Bodi ya Nyama itaundwa lini? Ili wafugaji waweze kuneemeka na mifugo yao, waweze kupata utaalamu wa kusindika nyama zao na waweze kupata masoko nje ya nchi kwa kuweza kuuza nyama hizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, wakati wa majumuisho nitaomba uniambie Bodi hii itaundwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninapenda kuongelea kitu kimoja kuhusiana na uchache wa Maafisa Ugani. Maafisa Ugani, kwanza ni wachache, halafu Maafisa Ugani

wanatumiwa kwa taaluma mbalimbali. Afisa Ugani huyohuyo atatumiwa kwa uvuvi, atatumiwa kwa kilimo na kadhalika. Sasa unaweza kuja kukuta Afisa Ugani ambaye amepelekwa kwenye mifugo hana taaluma ya mifugo, hivi kweli atawasaidia wafugaji hawa? Ni kwa nini Maafisa Ugani hawa wasiteuliwe kwa nafasi zao au kwa elimu yao? Kwanza kabisa Maafisa Ugani hawa wana matatizo mengi, hawana usafiri, nyumba za kuishi na hata wenye nyumba, nyumba ni duni, mishahara yao ni midogo, sasa ni lini Maafisa Ugani hawa watajaaliwa ili waweze kufanya kazi zao kulingana na matakwa yanavyotakiwa? Hii ndio inayopelekea Afisa Ugani wa Kilimo anapelekwa kwenye mifugo, ni kweli ataelewa huyu ng'ombe anaumwa, anahitaji *cc* ngapi za dawa ili kumtibu inavyotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri, yeye ni mfugaji, wote pamoja na Naibu wake ni mfugaji, wajaribu kukaa na wafugaji na waache kuongea na watu wakubwa walioko maofisini, washuke chini wakaogee na wafugaji wenyewe, waelewe matatizo ya wafugaji kwa sababu watakapofika maofisini watapewa takwimu nyingine ambazo si sahihi na wenyewe watatuletea takwimu ambazo si sahihi, au wataambiwa huku kuko shwari wakati hakuna ushwari wowote. Wakija watatuambia punguzeni mifugo, punguzeni mifugo lakini wale wanaokaa maofisini hawawaelimishi wananchi wapungeze mifugo kwa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwangu yalikuwa machache kwa sababu mengi yamekwishaongelewa, nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ni machache hayo kweli? *(Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na Mheshimiwa Shibiliti na Mheshimiwa Nsanzugwanko pia wjiandae.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Awali ya yote, nami naungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, ndugu yetu, Mheshimiwa Magufuli pamoja na wasaidizi wake akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri Wanyancha, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo, Mkurugenzi wa Uvuvi pamoja na watendaji wengine kwa kazi yao nzuri ambayo mmeifanya katika Wizara hii mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu, lengo la bajeti hii ni kuhakikisha kwamba wafugaji wanapata maisha bora, wanafuga kisasa, wanafuga kwa tija hali kadhalika wavuvi wanafaidika na uvuvi unaoendelea lakini Serikali nayo iendelee kupata mapato kutokana na uvuvi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia mifugo pamoja na uvuvi lazima kwanza uzungumzie matatizo ambayo ni imani yangu kwamba hili ndilo lengo la Wizara hii kuwepo kwa ajili ya kupunguza matatizo haya. Ndugu zetu wafugaji wanayo matatizo

ya aina nyingi na makubwa, mojawapo ya matatizo ni migongano iliyopo katika ya wafugaji na wakulima. Wakulima wanalalamika kwamba wafugaji wanalisha kwenye mashamba yao, haya ni baadhi ya matatizo ambayo yanapaswa kupunguzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ufugaji tulionao, wote tunakubaliana kwamba hauleti tija, kwa hiyo, tunahitaji ufugaji wenye kuleta tija. Lakini liko tatizo kubwa la madawa, mifugo mingi inazaliwa lakini mingi inakufa kwa sababu ya ukosefu wa madawa. Hali kadhalika tuna matatizo makubwa ya soko, kwamba watu tunao ng'ombe, tunao mbuzi, tunao kondoo, lakini namna gani tuweze kuuza ili tuweze kupata fedha nyingi au fedha za kutosha, linakuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa uvuvi yako matatizo kama ya uvuvi haramu ambayo yanaelekea sasa kusababisha hata samaki wote waweze kuisha ziwani na baharini. Kuna matatizo ambayo wavuvi kila leo wanalalamika kwamba hawafaidiki na ule uvuvi wanaovua kule kwa sababu hawana vitendea kazi vizuri, lakini liko tatizo kubwa la wavuvi wanalalamika kwamba wananyang'anywa zile nyavu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya yote ni matatizo ambayo ni imani yangu kwamba kwa kadiri tunavyowafahamu hasa hao walioshikilia Wizara hii, Waziri Magufuli pamoja na wenzake, kwamba katika bajeti ijayo haya ni baadhi ya matatizo makubwa ambayo yangepata majibu na wananchi wetu waweze kufaidika na uvuvi ambao wanao hali kadhalika na ufugaji unaoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Wizara hii imepewa fedha kidogo lakini na mimi ninakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba bado unaweza ukapata fedha kidogo ukafanya kazi nzuri na bado unaweza kuwa na fedha nyingi na usiweze kufanya chochote. Kwa hiyo, changamoto tuliyonayo ni kuangalia kwa kiasi gani Wizara imepata fedha kidogo na hizi fedha chache zilizopatikana hebu ziweze kuleta *impact* kwa wafugaji wetu pamoja na wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda tu Mheshimiwa Waziri anisaidie kufahamu hili kutokana na rasilimali tulizonazo. Katika nchi yetu tunazo ranchi nyingi, kwa mfano tuna ranchi ya Kongwa, nakumbuka kule Mwanza tuna ranchi ya Mwabuki, nakumbuka kule Pwani tunayo ranchi ya Ruvu pamoja na ranchi nyinginezo zilizoko Kagera na kwingineko. Hebu anisaidie kwanza kufahamu, hivi hizi ranchi kwa namna zinavyofanya kazi, hivi katika uzalishaji zinafanya kazi katika *capacity* yake ile inayopaswa kuwa au bado zinafanya kazi lakini uzalishaji wake uko chini?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, hizi ranchi tulizonazo zikiachiwa bila kuweka mkono wa Serikali kwa kutoa ruzuku, bila Serikali kuwalipa watumishi mishahara, hivi hizi ranchi zinaweza kujiendesha? Maana hili tunalisema kwa sababu watu wengine ufugaji ni biashara, kama ufugaji ni biashara maana yake mtu ana ranchi peke yake hiyohiyo anapata fedha za kuendesha ranchi lakini vile vile anapata faida yake. Kwa hiyo, tunapenda tujue hivi hali ikoje katika hizi ranchi zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi leo ninapenda kujikita katika ushauri kwamba pamoja na mawazo mengi na mazuri ambayo Serikali mnayo, ni vizuri mkaongezea yafuatayo kama kutakuwa na upungufu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapozungumzia habari ya ufugaji bora na ufugaji wa kisasa, ufugaji wenye tija, lazima tuhakikishe kwamba baadhi ya ng’ombe wetu tulionao ni sharti tuwabadili. Maeneo mengi hasa Kanda ya Ziwa ukiwemo Mkoa wetu wa Mara, ng’ombe wengi tulionao ni wale wa aina ya *Zeb*. Aina hii ya *Zeb*, kama tulivyosoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa ili aweze kukua mpaka aweze kupata uzito wa kilo 400 ng’ombe huyo ni lazima umfuge kati ya miaka minane mpaka 10. Lakini ukimchukua huyo ng’ombe ukam-*cross* na Bolan au hawa wengine, tafsiri yake ni kwamba ng’ombe huyo utamfuga ndani ya miaka miwili na nusu mpaka miaka mitatu uweze kupata kilo hizo 400 unazozihitaji. Sasa kama tunajua kabisa na tunakubaliana kwamba hilo linawezekana na tumekubali kwamba tunazo ranchi za kutosha, mimi ni imani yangu kwamba hizi ranchi zote zingeweza kuangaliwa ziweze kuzalisha mpaka ile *capacity* yake ya mwisho, *to the maximum,* ili tuweze kupata madume ya kutosha na tuweze kupata mitamba ya kutosha. Tutakapopata mitamba ya kutosha na kwa kuwa sasa tunahitaji mitamba hii ienee nchini kote, mitamba isiuzwe kwa bei inayouzwa, maana mtamba ukienda katika hizi ranchi zetu bei ya chini ni 250,000/=. Hebu tujiulize hivi ni wafugaji wetu wa kienyeji wangapi ambao tunataka wabadilike anaweza kununua mtamba huyo kwa shilingi 250,000/= wakati yeye akienda kuuza mtamba wake anamuuza kwa 120,000/=.

Kwa hiyo, nadhani aidha Wizara ingeishawishi Serikali, kwamba kama ranchi zile haziwezi kupunguza wale mitamba zikawauza kwa bei nafuu basi Serikali iwe tayari kutoa ruzuku kama inavyotoa ruzuku kwenye kilimo kwamba gharama ya mtamba ni 250,000/= Serikali iweke pale 100,000/= ili yule mkulima anunue kwa 150,000/=. Tunadhani kwa kufanya hivyo, wafugaji wengi zaidi wataweza kununua wale mitamba na matokeo yake sasa ile *speed* ya kuwageuza wale ng’ombe tulionao itakuwa kubwa, huko ndiko kutakako tusaidia kuelekea kwenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumeona hapa wakati napitia hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anasema Mpwapwa wanategemea kugawa madume 90, sasa ukiangalia kweli ndugu zangu katika hizi hifadhi zote au ranchi tulizonazo, leo tukisema tunagawa madume 90 manaa yake madume hayo tunaweza kuyagawa sana katika Kata moja, hivi haya mapinduzi ya ufugaji bora yatapatikanaje? Kwa hiyo, badala ya hizi ranchi zetu kuwa zinafika mahala zinauza wale madume waliopo basi ni vizuri zingekuwa na kazi moja tu ya kuzalisha madume na hao madume wangekuwa wanatumika kama mbegu na hii ingetusaidia zaidi katika kuhakikisha kwamba haya mapinduzi ya mifugo mingi na ambayo ni bora ingeweza kupatikana kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ushauri mwingine ni haya madawa ambayo watu wengi tunalalamika kwamba hayaonekani na hatujui wale waliopewa uwakala. Ni ushauri wangu kwamba hebu tuhamasishe Wilaya na Mikoa, waunde ushirika wao na ushirika huo uweze kupewa jukumu la kununua yale madawa pamoja na kuyasambaza kwa ajili ya wafugaji wetu na kwa kufanya hivyo basi tunaamini kwamba zoezi hilo

litaenda vizuri na ndugu zetu watafaidika zaidi na watajua kwamba hayo madawa ya majosho pamoja na madawa ya mifugo yanaweza kupatikana wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sula la uvuvi tumekuwa tukilalamika zaidi sana kwamba kuna uvuvi haramu ambao kusema kweli unamaliza samaki walioko ziwani, walioko mitoni na walioko baharini na sababu kubwa ni kwa sababu ya uvuvi haramu anaoendelea. Pamoja na juhudi ambazo Serikali imeziweka kwa kuanzisha hivi vikundi vya *Beach Management Unit* lakini bado tatizo linaelekea kuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa hapo, hebu Serikali iangalie, Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha yale mafunzo ya ufugaji wa samaki. Ukienda katika zile nchi za wenzetu, ukienda Thailand ukaenda kule China, watu wanafuga samaki kwa ufugaji kwa kutumia teknolojia ambayo ni rahisi ambayo mimi naamini kama wale watu wetu wangefundishwa basi wangeweza kufuga ufugaji huo wa samaki ambao ungeepusha ile athari ambayo tunaipata ya uvuvi haramu unaoendelea kule ziwani. Ni imani yangu kwamba ule uvuvi wala hauhitaji fedha nyingi na kama Wizara itaamua leo, uvuvi huo utatusaidia sana kuhakikisha kwamba watu tunakuwa na uvuvi ambao ni uvuvi endelevu ambao utaweza kusaidia watu wetu kuliko hivi sasa na kwa hali ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile katika kuboresha suala zima la uvuvi na ufugaji, watu wengi pale wanapoona ndipo wanapoamini na ndipo wanapojifunza. Hebu wale wataalamu wetu walioko kule, hao wa uvuvi na ufugaji, nao ni vizuri, ninashauri kwamba hata Serikali ingejaribu kuwapa uwezo kama yeye ni mtaalamu wa mifugo naye akawa na ng’ombe wake pale anafuga ili tukiona pale basi inatusaidia zaidi kuamini. Kama huyo ni mtaalamu wa uvuvi basi naye awe pale na uvuvi mdogo anafuga, anafuga samaki na kwa kuona hivyo watu wengi zaidi tutaweza kujifunza kuliko ilivyo sasa kwamba wale wote ambao ni wataalamu kule hakuna anayefuga na wala hakuna anayevua. Kwa hiyo, kwa wakati mwingine inatuwia vigumu sana kwa ile lugha wanayoihubiri ya ufugaji bora wakati yeye mwenyewe wala si mfugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hayo ndiyo yalikuwa maombi yangu ambayo ninapenda kama Wizara iyaweke maanani kwa sababu na yenyewe yangeweza kutusaidia katika kuhakikisha kwamba ufugaji mzuri unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ni la masoko. Suala la masoko unapozungumza hasa katika mifugo yetu maana samaki kiasi fulani wanayo masoko ya kutosha, yapo masoko mengi na yapo masoko ambayo wala si ya shida sana. Lakini kitu kinachotakiwa ni namna ya unenepeshaji wa mifugo yetu ili iweze ku-*meet standard* za yale masoko, maana nchi yetu ni nchi ya tatu nadhani ukiacha Ethiopia na Sudan kwa uwingi wa mifugo. Lakini mifugo yetu kwa kuwa hatujainenepesha vizuri ndiyo maana suala la masoko linatusumbua. Lakini hata ukingalia tu masoko ya Afrika yenyewe tunayo masoko mengi na mimi kwa kweli ni mdau mmojawapo wa wale ambao wanafaidika na masoko haya. Sasa ninaiomba tu Wizara ingeangalia namna bora ya kuendelea kuwaelimisha wafugaji wetu ili nao waweze kufaidika na masoko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamuita Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti na Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko ajiandae na Mheshimiwa Riziki Lulida umo kwenye orodha.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika bajeti hii ya Waziri wa Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watumishi wengine wote kwa jinsi walivyoweza kutoa ufafanuzi mzuri katika hotuba yao. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pole kwa kazi ngumu aliyonayo Mheshimiwa Waziri, pesa alizopewa ni kidogo sana yeye mwenyewe ameeleza kwamba atajitahidi lakini sisi tunasema kwamba atafanya kazi katika mazingira magumu, pesa ni kidogo na tunatoa wito kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha aangalie sana katika bajeti ijayo zitengwe pesa za kutosha ili aweze kufanya kazi aliyoikusudia ili aweze kufanikisha majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze wachangiaji wote ambao wameweza kuchangia vizuri tu na Wizara yetu kwa sababu imechanganywa na uvuvi wote kwa kweli tumechangia vizuri tu, waliochangia upande wa uvuvi wameeleza vizuri na waliochangia upande wa mifugo kwa maana ya ng’ombe na vitu vingine wamechangia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Rais ameunda Wizara hii na kutuunganisha pamoja si kwa maana ya kuvutana, tuendelee kuchangia kwa maana ya kila mtu anapochangia anachangia jinsi anavyoelewa, anayeelewa samaki achangie hivyo hivyo na afafanue vizuri na sisi tunaofahamu mifugo kwa maana ya ng’ombe basi tujikite katika masuala yetu haya bila kuvutana upande na upande, nia ya Mheshimiwa Rais ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielezee tu uonevu wa wafugaji nchini mwao. Kumekuwa na matatizo makubwa sana, wafugaji wamekuwa wakionewa, kila mara wanapokwenda wanasukumwasukumwa, wanaonewa kweli na mfano halisi ni huu wa juzijuzi. Mheshimiwa Missanga aliuliza swali hapa kuhusu jinsi ya ng’ombe wa Mzee Mahola zilizokuwa zimepotea zikapatikana kwenye Kata yake, zikapelekwa mpaka Kituo cha Polisi, zikapelekwa mpaka Wilayani kwa *OCD*, baadaye zimeuzwa pale. Yaani hii ni picha tosha kwamba wafugaji wanaonewa, mali zao zinakwenda hivihivi na mimi nasema tu kwamba kwa sababu Mheshimiwa Waziri aliahidi hapa tunaomba kabisa baada ya majibu ya uhakika Mzee huyu apate ng’ombe zake na nimpongeze sana Mheshimiwa Missanga kwa jinsi ambavyo aliliweka vizuri na Wabunge wote wa Singida

nawapongeza sana, hiyo ni picha ambayo inaonyesha kwamba wafugaji bado wanaonewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwa wafugaji ambao walihamia Rukwa, walikwenda kufanya nini? Tatizo lao kubwa lilikuwa ni maji na malisho. Lakini hapa nijikite kwa kusema ukweli kwa sababu kuna baadhi ya wafugaji wametoka sehemu za Misungwi, Magu, Kwimba na sehemu nyingine kama Shinyanga, niwe muwazi, kwa Mheshimiwa Mizengo K. Pinda wamejaa sana kwenye Jimbo lake na Mheshimiwa Dr. Christopher M. Mzindakaya pamoja na Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, wanakiri kwamba wamepokelewa vizuri sana na hawana kero katika maeneo hayo. Wamepokelewa vizuri wanasaidiwa, wanashauriana na wanachangia shughuli za maendeleo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo chini ya Waziri Mkuu hongereni sana mnafanya kazi nzuri na mnawapokea vizuri na endeleeni kukaa nao na wataendelea kuchangia maendeleo kadri wanavyoweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirejee Mbarali. Mbarali walikuwa wanaishi vizuri lakini katika zoezi la kuhamishwa waliyoyapata, wanalalamika ni kwa nini walikwenda huko. Mfugaji aliyekuwa na ng’ombe 6,000 amebakiwa na ng’ombe 20 yaani ni unyanyasaji wa hali ya juu. Hili sitaki niingie kwa kina kwa sababu ipo Tume iliyoundwa tunasubiri ripoti yake ije hapa, tuijadili kwa sababu na bahati nzuri sasa hivi kuna hawa PINGOS nao wamejitolea wamekwenda kuangalia jinsi mambo yalivyokwenda. Wamekuja hapa kwetu Wabunge wamejaribu kutuelezea yaliyotokea kule ni ya matatizo kweli, wameonewa, zimechangishwa pesa zisizo na utaratibu. Sasa mimi sioni hata sababu hawa PINGOS kuja kwetu hapa kwa sababu tunasubiri ripoti ya Mheshimiwa Rais. Sisi walivyokuja hapa tuliona hii kitu sawa tunaipokea lakini hatuwezi tukaijadili sana kwa sababu na ninyi mmefanya kazi, ni nzuri lakini tunasubiri zaidi ile ripoti ya Mheshimiwa Rais itakapokuwa imekuja hapa na tunaiomba iletwe hapa tuje tuijadili angalau tuweze kuona kwamba kuna nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wao wanatajataja mambo kwamba kuna risiti za Halmashauri, kwenye makusanyo yale kulitumika risiti za Halmashauri, Serikali Kuu, Sekondari, Kodi za Maendeleo yaani zimekusanywa tu pesa na zilizofika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbarali ni pesa kidogo sana nyingine zimeyeyuka. Wamekuwa wakitajataja mtu, wanamtaja Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya kwa jinsi alivyokuwa anafanya shughuli hiyo. Sasa mtu kutajwatajwa kwenye taarifa hizi wakati tunasubiri taarifa nyingine muhimu si vema, ni vema ripoti ije hapa tuone kama tuwasafishe au tuwasafirishe kwa sababu haya mambo yaliyotendeka hapa si ya kuoneana huruma haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninaomba tu uzidi kusisitiza kwamba ripoti ije hapa, tuje tuione, ni ripoti yetu, Tume tuidai vinginevyo nadhani Mheshimiwa Lucas L. Selelii alisema kwamba atatoa hoja binafsi, tutamuunga mkono na baadaye tutahitaji Kamati ya Bunge sasa ifanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Misungwi. Wizara yetu ya Mifugo imekuwa ni Wizara ya kuhamishwahamishwa mara iunganishwe kwenye Kilimo mara

ipelekwe kwingine. Iliwahi kuunganishwa na Kilimo na ilipounganishwa, kwa Wilaya yangu ya Misungwi, watumishi wengi wa mifugo walikaa Ukiriguru, tunaye Dr. Kaganda yeye ni Daktari Bingwa wa Mifugo, sasa hivi anapaswa ahamie Mabuki na tayari ameshahamia hapo Mabuki ana *staff* wake kama 15 hivi lakini wako wanne tu waliofika Mabuki. Nimuulize tu Mheshimiwa Waziri kwamba sijui amejipangaje kuhusu hicho kituo chetu cha Mabuki hana Ofisi, nyumba amepata atakarabati. Ni kiasi gani cha pesa ametengewa ili angalau huyu Daktari pamoja na wengine waliobaki Ukiriguru warudi kwenye Kituo chao waweze kufanya kazi nzuri zaidi ambayo watasaidia wafugaji wetu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapohapo nizungumzie hawa Nyatimaji. Nyatimaji nadhani kwa Tanzania wanapatikana Mabuki tu, ni wanyama ambao wanaweza wakafanya kazi nzuri sana. Kule Kilimanjaro kwenye umwagiliaji wanafahamu jinsi ambavyo kazi inafanyika lakini hawa wanyama sasa wanazidi kudhoofika yaani kile kimo walichokuwa nacho sasa hivi kinazidi kudhoofu nadhani kuna tatizo la madume. Kuna wakati fulani Mheshimiwa Edward N. Lowassa alikuwa anafuatilia ili aweze ku-*import* madume au mbegu kwa ajili ya kuhamilisha tuweze kupata mbegu bora za hawa Nyatimaji. Sasa tuombe tu katika bajeti hii hebu wajaribu kuangalia hiyo ni zawadi ambayo alipewa Mheshimiwa Baba wa Taifa kutoka Misri, sasa kuiachia hivi tu iteketee itakuwa si jambo la busara. Nina imani Mheshimiwa Waziri atalifuatilia suala hilo ili angalau basi hao Nyatimaji waendelee kutusaidia katika maeneo hayo na nchini kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee tu kumpongeza Mheshimiwa Waziri katika mpango mzima wa *DADPs*, tunajaribu kuelekeza mambo mbalimbali katika sekta ya mifugo. Kuna malambo, tutachimba kwenye eneo letu la Misungwi lakini tumetenga tuseme kwamba ile bajeti kwa sababu ni ndogo tunatumia kama milioni 10 kwa lambo, haitoshi! Lambo linahitaji karibu milioni 300 na kuendelea. Kwa hiyo, tukirejea kwenye bajeti unaona kwamba bajeti kwa kweli ni ndogo tunahitaji tuongezwe pesa ili angalau tuweze kuchimba malambo ambayo ni makubwa ya kutosha. Nimeshaleta maombi yangu kwako kuhusu tupate lambo kubwa pale kwenye Kata ya Mwaniko. Jaribu kuliangalia kwenye bajeti ijayo ili watu wa mwaniko basi na wao waweze kuondokana na tatizo ambalo linawa-*face* kwa wakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa majosho nikiri kwamba bajeti inatosha na tumejipanga vizuri, pesa tulizonazo zitatosha kukamilisha majasho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga wakati anachangia amejaribu kuelezea faida za samaki sangara. Nimempongeza sana yule Mama amejikita kwa yule samaki ana faida nyingi, nijielekeze kwenye ng’ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu ng’ombe ana faida nyingi mimi kwa sababu ya harakaharaka nina faida kama 18 hivi lakini baadaye Mheshimiwa Waziri kwa sababu wewe ni mtaalamu wa takwimu utazipata. Sisi kwetu Wasukuma faida ya kwanza ni kuolea, lazima utoe mahari ambayo kwa kweli inaridhisha ili yule mtoto wa watu unamleta kwako sasa aonekane kwamba ana heshima hiyo. Faida ya pili ni benki.

Unaweka benki kwa ajili ya kesi na kadhalika, kuna kesi inaitwa Njigu mtu anapokuwa amepata matatizo hayo basi tunalipa hizo ng'ombe. Kulima na kuvuta tera ni faifa ya tatu. Maziwa kama chakula ni faida ya nne. Faida ya tano, Maziwa kama dawa, mtu kama amekunywa sumu hebu mpe maziwa tu mara moja atatapika hiyo sumu na atabaki hai. Faida ya sita, maziwa kama dawa kwa mtu aliyeungua moto au *either* kumwagikiwa maji au uji, mmwagie maziwa. Hiyo ni faida ya huyo mnyama. Ngozi inafahamika kwa maana ya viatu, mkanda na masanduku. Mafuta kwa kula ni samli safi ambayo kwa kweli wakati mwingine hata kama akijitokeza nyoka mmwagie hayo atakufa hapohapo. Samadi, kwenye suala la mashamba yetu ukishaweka samadi ni miaka mitatu huhangaiki tena na mbolea nyingine. Kwa hiyo, ni kitu ambacho ni cha msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati mwingine sisi tunatumie kama kikome kwa hiyo unapokoka ule moto siyo kwa ajili ya kuota ni kwa ajili ya mkutano wa kila jioni kwa ajili ya kupanga mipango ya kazi ya kesho. Kwa hiyo, sisi kikome tunakiheshimu sana mtu ambaye amekulia kwenye kikome hata maadili yake yamenyooka. Kwato ni gundi, hiyo faida ya kumi na moja. Pembe ni vufungo, vifungo nilivyonavyo hapa hivi ni vya pembe vimekaa vizuri. Faida ya ng'ombe hiyo. Mkia ni leso unaweza ukajifuta na mambo yakaenda vizuri tu. Mifupa, ni chokaa au chakula cha mifugo, mambo yanakwenda vizuri tu. Lakini wakati mwingine huwa tunamtumia huyo ng'ombe kama burudani, wakati anachoma kichugu namna hii anaburudisha tu na unajisikia raha. Huyu ng'ombe ana faida nyingi lakini ng'ombe wakati anatolewa kama tunu au zawadi, mambo kama hayo yanahitajika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida zipo nyingi sana na sasa nijikite kwenye eneo moja la kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo ameweza kulichukulia maanani suala la mnada wetu wa Upili uliopo pale Nyamatara Misungwi kwamba ataukamilisha. Ninakupongeza sana kwa kweli hebu ukamilishe huu mnada ili wananchi waweze kuutumia, eneo ni la kutosha na niwakaribishe sana wananchi kutoka Mikoa ya Kagera, Singida, Geita na sehemu nyingine mbalimbali watumie kivuko kizuri kilichopo pale MV Misungwi, unavuka ukishafika Usagara ni kilomita kama 15 kuja Nyamatara pale kuelekea Shinyanga, ukiwa Ukiriguru ni kama kilomita 7, ni mnada ambao kwa kweli tutakuwa tunapima kwa kilo. Kwa hiyo, tunawakaribisha Watanzania kwamba badala ya kuuza mifugo yenu kwa kuangalia sasa tutatumia kilo, karibuni sana Misungwi, ni Wilaya ambayo imejipanga vizuri kuwakaribisha wageni, soko litakuwa ni zuri, unyanyaswaji hautakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maeleo hayo, niendelee kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri John P. Magufuli kwa asilimia mia moja na ninampongeza sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamuita Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko na msemaji wetu katika orodha yangu wa mwisho ni Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili nichangie Wizara hii muhimu sana katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona Mheshimiwa Mbunge wa Misungwi amezunguza faida za mifugo lakini hakutueleza hasara za mifugo, lakini hata hivyo hayo ni mazungumzo mengine baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kwa dhati kabisa nitoe salamu za rambirambi kwa kifo cha mwenzetu Mheshimiwa Chacha Wangwe. Nilimfahamu sana na mimi nilifanya naye kazi nikiwa Kambi ya Upinzani miaka ile, ni mtu niliyemfahamu sana na kwa kweli tunaomba familia na wale wote wenye uchungu wa dhati, kwa kweli tunaomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira katika kuomboleza kifo hiki muhimu sana cha Mheshimiwa Chacha Wangwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa John P. Magufuli, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu kwa kweli na timu yote ya Watalaamu katika Wizara hii, maana Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ina historia kwamba watu wote ni wasomi wazuri katika sekta hii na wala hawababahatishi na wewe Mheshimiwa John Magufuli tunakufahamu kwa umahiri wako wa kufuatilia mambo lakini kubwa zaidi kwa umahiri wako wa kuwa mtu wa matokeo na ni matarajio yetu kwamba Wizara hii sasa utaipa sura mpya kabisa kwa kadri tunavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia na mimi nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuanzisha Wizara hii kwa kweli ni Wizara muhimu sana. Kwa mfano, kule Kigoma utakuta Ziwa Tanganyika limekaa tu *impact* katika uchumi ni kidogo lakini sasa nafikiri wenzetu katika Wizara hii, ni mahali pazuri na ninafikiri Mheshimiwa Rais aliliona hili na kwamba sasa anzeni kufanya kazi bila kuchoka na mjielekeze katika maziwa yote kama ya Tanganyika, Nyasa, Victoria na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niipongeze sana Ofisi ya Waziri Mkuu. Kule Jimboni kwangu, wakati Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Edward Lowassa akiwa Waziri Mkuu, aliombwa na wanakijiji wa kijiji cha Nyenge kule Kasulu kuhusu kituo chao cha mifugo na Kilimo ambacho *Go-down* ilikuwa imeezuliwa na upepo na kwa juhudi zake alitoa maagizo na sasa yametekelezwa. Naomba kwa dhati kabisa, niishukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu Mstaafu na huyu aliyepo kwa kazi nzuri. Sasa tuna kituo kizuri cha mifugo na kilimo cha kijiji cha Nyenge ambacho ni kijiji muhimu sana na chenye watu wengi katika Jimbo la Kasulu Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya pongezi hizo, naomba nifanye mapitio tu kidogo kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hasa nijikite katika eneo la utafiti na hasa taasisi hii ya TAFIRI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri unakumbuka kwamba pale Kigoma kuna Kituo cha TAFIRI, ni kituo cha muda mrefu sana. Lakini naona katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri huonyeshi kama hicho kituo kipo na ni muhimu sana, amekitaja tu *by passing* bila kueleza mambo hasahasa ambayo yatafanyika katika eneo

lile. Niseme tu kwamba ni kituo muhimu sana Mheshimiwa Waziri na kipeni nyenzo ya kazi ili wafanye kazi ya utafiti katika mwambao wote wa Ziwa Tanganyika kutoka Kaskazini hadi Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikizungumza habari ya TAFIRI niliunganishe moja kwa moja na mradi wetu mkubwa wa bonde la Ziwa Tanganyika. Kule Kigoma na wenzangu wa Rukwa, tuna mradi mkubwa sana wa *Lake Tanganyika Basin* ambao utakuwa na mabilioni mengi ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilikuwa nataka nitoe angalizo kwamba mradi huu mkubwa wa Bonde la Ziwa Tanganyika ambao ndiyo unaanza kutekelezwa katika nchi zetu nne za Congo, Tanzania, Burundi na Zambia, kwa upande wa Tanzania utahusisha Mikoa hii miwili. Lakini kuna mambo sana mtambuka katika mradi huu, nitoe tu kama angalizo Mheshimiwa Waziri kwamba mradi huu mkubwa utahusisha Wizara karibu nne, Wizara ya Uvuvi na Mifugo, Wizara ya Maji kwa maana ya maji ya Lake Tanganyika na mito yake ya Malagalasi, lakini wenye mradi wenyewe ni Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na Wizara ya nne ni TAMISEMI kwa maana ya kushirikisha *Local Authorities* katika ushirikishwaji wa wananchi kupitia Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika,  ninaomba sana kupitia kwako na sasa Waziri nadhani kuwe na *harmonisation* ambayo itafanya mradi huu uweze kutekelezeka vizuri bila vikwazo vya kitaaluma, kisheria na kadhalika, maana yake ikija maji ni Wizara ya Maji, ikija Uvuvi ni Wizara ya Uvuvi na Mifugo, *Community Participation,* TAMISEMI na ukija wenye mradi wenyewe ni Ofisi ya Makamu wa Rais. Sasa ninaomba sana Wizara hizi nne waweke vichwa vyao pamoja ili mradi huu utekelezeke vizuri kwa Mikoa ya Rukwa na Mkoa wa Kigoma vinginevyo najaribu kuona kwamba kuna hatari ya kupata matatizo ya utekelezaji, kwamba linaanza hiki unakuta pengine Sheria hii inagongana na nyingine. Sasa naomba sana Mheshimiwa John Magufuli, hili jambo kwa kweli kuwe na aina fulani ya *cooperation*, *harmonisation* na ku-*share resources in terms of man power* na vitu vingine na hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sisi tuna huu mradi wa Lake Tanganyika zaidi ya bilioni 40 halafu kuna mradi wa *Beach Management Unity* kutoka kwenye Wizara yako takribani bilioni 26. Sasa unakuta wote mtakuwa katika eneo lile lile, nafikiri ni vizuri rasilimali ziunganishwe kwa pamoja ili ziweze kuwa na tija iliyokusudiwa. Ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa John Magufuli hili jambo utalizingatia wewe na wenzako na nikuombe basi uwe ni dereva katika jambo hili ili liweze kutekelezeka kwa umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni hili suala la wafugaji. Siku ya Ijumaa kulionekana kama kulikuwa na mechi kati ya wafugaji na wavuvi, kati ya wavuvi na wakulima na wafugaji juu yake. Mimi ninataka niseme tu kwamba jamani hakuna ugomvi hapa, lazima tuishi pamoja yaani wavuvi, wakulima na wafugaji na kuishi pamoja huku maana yake ni kuishi kwa kuheshimiana na kufuata taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri naomba hii u-*note* kabisa kwamba Mkoa wa Kigoma sasa hivi ni Mkoa wa wafugaji wale waliotoroka Ihefu, wale waliokimbia Ihefu na wengine wakakimbia Bonde la Mto Rukwa, sasa wamevamia Mkoa wa Kigoma na hasa Jimbo langu la Kigoma Mashariki, nina wafugaji wengi sana katika Vijiji vya Titye, Rungwe Mpya, Ahsante Nyerere, Sogeeni na hata Kagera Nkanda, kote huko wamejaa wafugaji na wanatembea na ng'ombe wengi kweli ndiyo maana Ndugu yangu Jacob D. Shibiliti nilikuwa namuuliza mbona hakusema hasara za wafugaji hawa? Hawa watu wanazunguka na ng'ombe wengi sana na kusema kweli Mheshimiwa Waziri wanahatarisha ardhioevu ya Mto Malagarasi. Sasa hoja yangu ya msingi hapa ni kwamba kwanza Mheshimiwa Waziri utambue hili kwamba sasa sisi tumekuwa na wafugaji wengi sana na kwa bahati nzuri au mbaya wafugaji hawa wote ni Wasukuma, wote! Nini hatima ya kuzunguka na mifugo kila mahali?

**WABUNGE FULANI:** Wana nyama!

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Aah! Wana nyama kweli kama anavyosema ndugu yangu Jacob D. Shibiliti, wanatupa maziwa kweli lakini wanatukera kwelikweli maana wanaharibu mito hawa na haiwezekani, Mheshimiwa Waziri wafugaji wazurure tu nchi nzima, inawezekana kweli jamani eeeeh!

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu yangu Kaika Telele, nilimsikia anasema kwa huzuni kabisa mpaka anakumbuka enzi za wakoloni. Haiwezekani wafugaji hawa wazurure na mifugo kila mahali, haiwezekani! Hawa wameharibu Mbarali, leo wako Kasulu na wanakata miti hawa sijawahi kuona mimi.Lazima hatua zichukuliwe haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi tumewapokea vizuri pale kwenye vijiji vyangu na tumejadili kwenye vikao vyetu vya Halmashauri, tumezungumza kwenye *RCC* jambo hili, sisi tunataka Co-*existance* na wafugaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumza na Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, juzi akaniambia anatofautisha juu ya kupunguza mifugo na kuvuna mifugo, haiwezekani wafugaji hawa wazurure nchi nzima tu, wanazurura kila mahali, wanaharibu ardhi yetu na vyanzo vya maji. Basi wavune hiyo mifugo ili adha ya uharibifu wa mazingira ipungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa John Magufuli pamoja na kwamba hawa ni ndugu zako, sisi kule Kasulu tumewapokea vizuri lakini tunataka *co-existance,* niletee fedha tufanye elimu kwa wafugaji na wakulima, niletee pesa na mimi mwenyewe nitasimamia jambo hilo na Halmashauri yangu tuweze ku-*co-exist* na hawa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ndugu zangu Wasukuma ndugu zangu wafugaji, haiwezekani ng'ombe wazurure kila mahali, haiwezekani! Itakuwa nchi ya ajabu sana hii. Wameharibu Lake Rukwa, wanakuja kuvuruga bonde na ardhioevu ya Malagarasi!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yako Mheshimiwa Waziri ardhioevu ya Mto Malagarasi wala si mali yetu peke yetu ni ardhioevu ya hifadhi ya Kimataifa. Sasa

nafikiri ni jambo muhimu sana kuweza kulizingatia na alete pesa tuweze kuwaelimisha wafugaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninapenda kulizungumzia ni suala la ranchi ya Uvinza iliyouzwa yaani Ranchi ya *NARCO*. Pale Uvinza kulikuwa na ranchi kubwa sana ranchi ile imeuzwa na kweli imekuwa msitu, wale waliouziwa ranchi ya *NARCO* hawaiendelezi nadhani ni wachache tu, wameiendeleza ranchi ile. Mimi ninakushauri tu Mheshimiwa Waziri ile Ranchi ya *NARCO* wale walioshindwa ardhi ile irudisheni *NARCO*, limeni majani ya mifugo ili hawa jamaa wanaozungukazunguka na ng'ombe basi wawe wananunua majani kutoka katika maeneo kama vile ya Uvinza. Mbona duniani inafanyika hii? Duniani inafanyika kote Ethiopia, inafanyika kule wakulima wanalima majani na wafugaji wananunua majani kwa ajili ya mifugo yao kuliko kukimbia kila mahali tu wanazagaa nchi nzima na wanatuharibia kweli mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninakuomba Mheshimiwa Waziri kwanza unieleze *status* ya ile ranchi ya Uvinza iliyouzwa na wale waliouziwa kwa kweli tufike mahali sasa aha, basi bwana! Ile ardhi irejeshwe *NARCO* na pengine itumiwe vizuri zaidi au kwa wawekezaji wengine zaidi ambao watatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa niseme wakati muda unakimbia, ni ufugaji wa samaki katika mabwawa. Nafikiri Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wangejikita pia katika ufugaji wa samaki katika mabwawa ya asili.

Kuna mabwawa ya asili kwa mfano kule Jimboni kwangu nina bwawa kubwa sana ambalo ni kama ziwa, (*mean Lake)*, bwawa la Kaguruka, lina samaki wengi sana, kwa sasa tumeingiliwa sana na viboko. Sasa nasema haya nayo yawe na *strategy* maalum. Wizara washirikiane na Halmashauri kuangalia tunavyoweza kulinda rasilimali zetu katika mabwawa ya asili ambazo ni *min Lakes* ambako kunakuwa na samaki wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwashikisha adabu wavuvi wa makampuni makubwa. Yeye mwenyewe anasema ni shamba la bibi na nakubaliana kabisa kwamba nchi yetu isifanywe shamba la bibi, *now you have instrument* Mr. Magufuli, kama hawatulipi kodi wasivue, kama hawalipi *percent*, wasivue. Wale samaki baharini watakaa tu, hawataoza na kwa kweli Mheshimiwa Magufuli katika hili tunamwomba sana akaze kamba na Dr. Wanyancha amsaidie kukaza kamba, katika bahari na maziwa. Hawa ni watu ambao hawafuati sheria, hawatulipi kodi yetu, wasiruhusiwe kuvua katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ni eneo la *EEZ*, mwambao wa kilomita mia mbili kutoka mpaka wa kwetu kwenye *High Seas* kule. Kumekuwa na *process* wanafanya wenzetu wa Nishati na Madini kupitia *TPDC* ili kuomba kibali kwa Umoja wa Mataifa ili kumiliki eneo lile la kilomita 200 za baharini. Najua hili suala pia lipo kwa wenzetu wa ardhi wanalishughulikia. Nakumbuka mwaka jana Serikali ilitoa shilingi bilioni moja ikawa bado inadaiwa shilingi bilioni moja ili kukamilisha ili

hatimaye tuombe kumiliki kilomita 200 *off shore* za bahari ili wenzetu wa Kenya, *Seychelles* na *Comoro* wasije wakatupiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara yake na Wizara ya Nishati wakae pamoja tuone kama tunaweza kupata hiyo *EEZ* ya kilomita 200 kwenye *off shore* na taarifa ni kwamba *deadline* ni tarehe 1 Mei, 2009. Tukichelewa wenzetu wa Kenya, *Seychelles* au *Comoro* wanaweza kutupiku na tutakuwa tumepoteza hiyo *opportunity*, maana tukishachelewa ndiyo tumechelewa. Lakini Mheshimiwa Waziri analifahamu kwa sababu najua lipo kwake kwa sababu hata kwenye Kamati yetu tumelizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Kasulu Mashariki. Kero ya hawa ng'ombe wa Kisukuma tunahangaika nayo na tutapata majibu yake kadri tunavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Magufuli - Waziri kwa kuteuliwa kwake katika Wizara hii muhimu sana ya Mifugo na Uvuvi maarufu kitoweo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Wanyancha kwa kupata nafasi katika Wizara hii. Sitakuwa na mengi ya kuongea, ninayo machache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa, leo hii Mkoa wa Lindi ni wadau katika sekta ya mifugo na uvuvi. Tumeletewa wafugaji kutoka Mbarali, wameingia katika Mkoa wa Lindi. Lakini kuna mazuri na ndani yake kuna mapungufu ambayo inabidi yarekebishwe. Kwa mfano, Wabunge wa Mkoa wa Lindi kama wadau hawakushirikishwa katika mikutano yoyote ambayo ilifanyika kuhusu mifugo katika Mikoa yetu. Hii haina pingamizi na wala hakuna mjadala ndani yake, maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutushirikisha sisi kungesaidia tuwe na ufahamu na uelewa katika sekta hii ya mifugo iliyoletwa Lindi. Sasa matokeo yake kila mara kuna kulumbana. Hali hii haivutii, inaleta mushkeli kidogo. Leo hii tunaangalia *page* 114 na 115, kule Lindi tumepelekewa mifugo mingi na ya kutosha, lakini humu ndani ya majedwali hatukuwekewa fungu lolote la kujengewa majosho na malambo.

Sasa je, hamwoni mtatuletea mgongano kati ya wafugaji na wakulima? Kwa sababu hawatakuwa na majosho wala malambo ili mifugo yao kupata maji, itabidi waende katika mito ambayo itatuletea uharibifu wa mazingira. Hili tusiwalaumu

wafugaji wala wakulima, tuilaumu Serikali kwa kutofanya utafiti wa kutosha na kuweka mazingira ya kutosha ili kuondoa usumbufu wa aina hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tuna sehemu nyeti ambazo tunategemea kuwa ni nzuri kwa kilimo kama Makangaga, Mto Mbwemkuru, Mavuji, hizo *area* hata mtu ukienda kuziangalia utasema kweli hizi ni nyeti kwa ajili ya kilimo endelevu. Lakini kwa vile wafugaji hawakuwekewa mazingira mazuri na miundombinu wamekwenda katika sehemu hizo. Walitengewa maeneo, wakajiona wako porini, wakasema hatuwezi kukaa porini, tunahitaji kukaa na wenzetu, hivyo wamevamia sehemu za wakulima wamekaa pale. Matokeo yake wakulima wakiamka asubuhi mahindi yao yameliwa na ng'ombe, ukiwauliza, wanasema hatukuwekewa mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili na alitafutie ufumbuzi ili mgongano usijitokeze. Kwa kuwa tayari wafugaji wameshafika kule, kinachohitajika sasa hivi ni kuhakikisha kwamba, mazingira mazuri na miundombinu bora vinawekwa ili kuondoa utata ambao unajitokeza. Wakikaa wenzetu wafugaji, ohoo tunaonewa, tunanyanyaswa: Je, mkulima anayetegemea mahindi yake, yakiliwa na mifugo anyamaze kwa vile mfugaji amepelekwa kule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kurekebisha hii hali, naomba Mheshimiwa Waziri asilichukulie suala hili kuwa ni dogo, alifanyie kazi, akae na wadau wote wa Mikoa ya wafugaji na kule walikopelekwa wafugaji hawa ili waone tatizo liko wapi, muafaka upatikane. La sivyo kila siku itakuwa, sisi tunaonewa, tunanyanyaswa, tumepelekwa kule, lakini ukiangalia kila mmoja anatetea haki yake na hii haki itapatikana baada ya kukaa kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wanasema tumeweka mkutano Arusha, lakini katika Mikoa iliyoalikwa, hakuna Mkoa wa Lindi wala Mkoa wa Pwani au Kigoma kwenda huko kuangalia mazingira yako vipi. Je, ufumbuzi utapatikana vipi katika masuala kama haya? Pili, naona kuna Wizara kama nne ambazo inabidi zishirikishwe, Wizara ya Mazingira, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, zikae kwa pamoja zione tathmini ya athari ya wafugaji na mazingira yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mabonde ya Rufiji kulikuwa na miti ya kutosha, lakini sasa hivi pale wanakata mkaa tu, baada ya miaka michache, tutakuwa na ukame wa kutosha na msitu utaharibika. Je, tutamlaumu nani? tutajilaumu sisi wenyewe kwa kuwa hatukufanya utafiti wa kutosha na wala hatukuweka mipango ya kutosha ili kuona hili suala linakwendaje. Sawa, tulifanya makosa, lakini tunao uwezo wa kurekebisha makosa haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri namwamini sana, leo hii Lindi tuna raha sana kutokana na barabara ya kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam na hili analiweza. Naomba tukimaliza Bunge hili twende na Mheshimiwa Waziri akaone hali halisi, yeye na Mheshimiwa Wanyancha wakatembelee Mikoa hiyo ambayo watu wanalalamika, wataona ukweli wa mambo kuliko kukaa hapa, yatakuwepo malumbano ambayo hayana muafaka halafu sio vizuri, tumekuja hapa kuwatetea wananchi, hatukuja hapa kulumbana, lakini tukienda pamoja huko nafikiri na hawa watani zetu watakuwa

wameridhika. Lakini tukikaa hivi hivi itakuwa kila siku Msukuma anamlaumu Chinga na Chinga anamlaumu Mmasai, ugomvi huu utaisha lini? Naomba Mheshimiwa Waziri alitatue tatizo hili ili tuwe ndugu moja tukiwatetea wananchi wa Tanzania hii. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi, Mtwara, Tanga na Mkoa wa Pwani tunategemea sana uvuvi, lakini wananchi wetu ni maskini. Naona mabilioni kila siku yanatengwa, lakini ukienda katika vijiji ukaviangalia wanavyoishi, unauliza ni nini hiki? Tumeletewa hapa *MACEMP* mpaka sasa hivi nilikuwa katika Kamati ya Mazingira, *MACEMP* hawajawa tayari kuwaendeleza na kuwakomboa wavuvi. Fedha zote zinakwenda kwenye *workshop*, *seminar* basi, lakini ukiangalia tathmini ya wananchi wanafaidika vipi na huu mradi, bado wako nyuma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi semina zimetosha, makongamano yametosha, tuwasaidie wavuvi hawa kuwaondoa katika umaskini, sio kuwawekea waraka ambao unawabana, matokeo yake wataendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wameshaanzisha vikundi, Mchinga yote kuna vikundi, ukienda Mikindani kuna vikundi, ukienda Pangani kuna vikundi, lakini wananchi au wavuvi hawajanufaika na huo mradi. Sasa hivi waachane na masuala ya *workshop*, waende kuwaangalia wanavikundi, wawatengenezee maboti na wawaelimishe kuhusu nyavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hujanielimisha kuhusu nyavu, nataka nikavue dagaa au duvi, nitajua kama duvi inachukua nyavu ya inchi tatu, maana yake tuangalie kuna samaki wengine wana kimo fulani, udogo wa kiasi fulani, leo unawaambia ukionekana umechukua nyavu ndogo ndogo utachukuliwa hatua za kisheria. Je, ulimwelimisha? Kama hujamwelimisha atafanya nini? Ataishije? Ina maana aendelee kuwa maskini, wakati anategemea kwenda baharini na kupata maslahi yake kupitia bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tulipata mitambo ya barafu katika Wilaya ya Lindi, Kilwa Kivinje, Mtwara yale majokofu wamepewa wajanja wanayatumia, hayamfaidishi mvuvi na maana ya kuleta ule msaada uwasaidie wavuvi wapate angalau barafu ziwasaidie katika masuala yao wanapokwenda kuvua ndiyo waweze kuzitumia, lakini anapewa mtu mmoja azimiliki barafu zote na hata ushuru hatoi na wala hakuna faida yoyote inayopatikana kwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ile mitambo ya barafu ambayo ipo Lindi, Mtwara na Kilwa itafufuliwaje? Je, yule anayetumia, Serikali inanufaika na nini? Maana yake anapata faida kubwa kwa bidhaa za baharini, lakini mimi mwenyewe nilikuwa katika Halmashauri nikakuta analipa Sh.140,000/= kwa mwezi. Je, tumemkomboa Mtanzania katika njia hiyo? Mvuvi mdogo anachajiwa hela kubwa, mfanyabiashara mkubwa ambaye anakwenda kule kununua samaki wote analipa Sh.140,000/= tu kwa mwezi. Kwa kweli imefikia mahali tunataka tupate jibu, kwa nini hatoi kodi? Kwa nini anaachiwa atumie rasilimali zetu kwa pesa ndogo kiasi hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi, nilikuwa nataka nichangie machache tu katika upande wa uvuvi. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Ziwa Nyasa halina samaki wengi *(naturally)*, kuwezesha wananchi wa Ludewa waishio mwambao wa ziwa hilo ambao hawana fursa nyingine za maendeleo yao zaidi ya uvuvi, Wizara itawasaidiaje wananchi hawa kuwa na uvuvi wenye tija endelevu ili nao wawe na haki sawa na wananchi wengine kiuchumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine la wananchi wa mwambao wa Ziwa Nyasa – Ludewa, ni ukosefu wa barabara za kusafirisha samaki na mazao mengine kutoka mwambao hadi kwenye masoko yanayopatikana mashariki ya milima ya Livingstone, je, Wizara hii inaweza kuchangia kwa namna gani katika kuwezesha usafirishaji wa mazao hayo ya ziwa kwenda kwenye masoko?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile uwekezaji katika sekta ya madini hususani chuma pale Liganga – Ludewa, unatarajiwa kuanza mwaka huu 2008 na kwa vile uwekezaji huo utavutia watu wengi sana katika maeneo yanayozunguka migodi hiyo ambao utahitaji mazao mengi ya mifugo, Wizara hii itaisaidiaje Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kuwa na mipango mizuri ya matumizi ya ardhi pamoja na matumizi ya ufugaji ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na ufugaji wenye tija na endelevu?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa 74 (Kifungu 106), kuna boti mbili kwa ajili ya kuimarisha uvuvi katika Ziwa Nyasa, je, hizi ndizo boti zilizoahidiwa wananchi wa Wilaya ya Ludewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Ziwa Nyasa, lina kina kirefu sana na mazingira magumu kwa uvuvi na kuhitaji teknolojia maalumu na zana madhubuti ili uvuvi katika ziwa hilo uwe na tija na endelevu, Serikali inawasaidiaje wananchi hasa wa Ludewa kupata teknolojia hiyo na zana zinazotakiwa ili kuwa na uvuvi wenye tija na endelevu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile usimamizi na uimarishaji wa uvuvi katika maziwa ya Victoria na Tanganyika, unashirikisha nchi jirani zinazozunguka maziwa hayo, kwa nini hakuna utaratibu kama huo katika Ziwa Nyasa kwa kushirikiana na wenzetu wa Malawi na Mozambique?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa samaki aina ya Mbasa, Mbelele na dagaa, ndiyo aina muhimu sana katika Ziwa Nyasa na ukiondoa dagaa, Mbasa na Mbelele wanaelekea kupotea, Serikali ina mkakati gani maalum wa kuhifadhi na kuongeza upatikanaji wa samaki hawa katika Ziwa Nyasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Nyasa, unafanyika kupitia kituo kimoja tu cha Kasumulo (Kyela), kilichoko kwenye ncha ya ziwa hilo na kufanya kazi hiyo iwe ngumu na kutowezekana kutokana na umbali

kutoka mpakani na Mozambique, kwa kuzingatia kuwa karibu nusu nzima ya mwaka, ziwa hilo huwa na dhoruba sana na kutopitika kirahisi. Kwa nini kusiwe na kituo kingine upande wa kusini pale Manda, Wilaya ya Ludewa ili kusaidiana na kile cha Kyela?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini miradi yote ya Sekta ya Uvuvi inalenga maziwa ya Victoria na Tanyanyika na hakuna mradi wowote katika Ziwa Nyasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 87, Kifungu 130, Wizara inazungumzia uhamasishaji wa hifadhi ya mazingira kwa kuhimiza matumizi bora ya ardhi ya malisho na nishati mbadala ya *biogas*: Jje, uhamasishaji huu unahusisha mambo gani *practically*?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mikakati gani wa kusimamia uvunaji na uhifadhi wa samaki wa mapambo katika Ziwa Nyasa na Tanganyika?

**MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wakazi wa Wilaya ya Lushoto, tumebaini kwamba kwa Jiografia yetu ya milima, ufunyu wa ardhi na wakazi laki tano, hatuwezi kuchunga. Tunamuomba Waziri atusaidie ushauri na uwezeshaji tupate ng'ombe wa maziwa wenye uwezo wa kutoa lita 20 – 40 za maziwa, mbuzi wa maziwa pamoja na mabwawa ya samaki ili kuinua lishe na kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wasaidizi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa faida ya wananchi wetu. Kwa kipindi kifupi walichokaa, tumeona mabadiliko makubwa sana upande wa uvuvi na mifugo, nawaomba muendelee na kasi hii hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wafugaji hasa tunaotoka Mikoa mikame, tunategemea sana malisho, maji na madawa kwa ajili ya mifugo yetu, naomba sana nipate msaada wa kuchimba mabwawa makubwa matatu maeneo ya Dominiki, Kinampanda na Matongo. Maeneo haya yana wafugaji wengi na wao huwa hawahami, kwa hiyo, ni busara kuwaondolea kero kubwa ya maji walionayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, wataalamu wa uvuvi, watembelee na kuwatambua wavuvi wanaovua mto Sibiti, aweze kufahamu matatizo yao ya nyavu na vitendea kazi vingine, aweze kutoa msaada kwao. Pia kuwapatia elimu ya uvuvi ili wasiende kinyume na Sheria ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba sana wafugaji wakumbukwe kwa madawa, majosho na pia elimu itolewe zaidi ili waanze kufuga mifugo yao kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu zaidi itolewe na Halmashauri zote zitakiwe kutoa elimu ya uzalishaji wa chupa na zitenge fedha za kutosha kwa ajili ya kununua mbegu toka Arusha, kitovu cha uzalishaji wa chupa kwa ajili ya kupata ng'ombe bora wa nyama na maziwa. Halmashauri zote ziende na Madiwani wao na watendaji wajifunze kama wenzao wa Iramba walivyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza Waziri, Mheshimiwa John Magufuli, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Wanyancha, Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara hii mpya ya Mifugo na Uvuvi. Sina hakika kama mifugo na sekta ya uvuvi vinaenda pamoja labda tu kwa sababu sekta zote hizo ni watumiaji wakubwa wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie sekta ya uvuvi. Miaka ya hivi karibuni, sekta ya uvuvi, imekua sana hasa katika uvuvi wa sangara katika Ziwa Victoria na pia ukuaji wa soko la Kamba katika ukanda wa Pwani. Nashukuru kwamba sekta hii inafahamika sio tu Tanzania bali ulimwenguni kote kutokana na bidhaa za uvuvi za Tanzania kuuzwa katika masoko mengi ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado katika ukanda wa Pwani, kuna uharibifu mkubwa kutokana na uvuvi haramu pia wizi wa maliasili unaofanywa na nchi nyingi za kigeni zinazokuja kuiba malihai hiyo. Nashauri Wizara iandae kikosi maalum kwa kushirikiana na vikosi vya usalama na ulinzi nchini ili kulinda maliasili zetu dhidi ya uvuvi haramu na wizi unaofanywa na meli za nje. Waunde kikosi kama cha *TANAPA* ambacho kimeweza kupunguza sana masuala ya ujangili kwa wanyama na nyara za Serikali. Ni kweli zinahitajika fedha nyingi kuanzisha kikosi cha namna hii, lakini sekta yenyewe kwa jinsi inavyoleta mapato mengi nchini, inawezekana kabisa ikagharamia haya yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *MACEMP*, uangaliwe vizuri, una fedha nyingi sana toka nje ambazo kama zingetumiwa zaidi katika ujenzi wa maboti na viwanda vya nyavu, shida kubwa ya sekta hii ni vifaa vya kisasa vya uvuvi. Tukiwa na vifaa vya kutosha, uvuvi haramu utatoweka na hata Wizara itaweza ku-*control* matumizi ya nyavu zinazofaa na kadhalika. Nashauri fedha za mradi huu zitumiwe vizuri zaidi kwa ununuzi wa vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba niongelee haya machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa mifugo nchini, naomba ieleweke wazi kuwa mifugo hapa nchini inayo uwezo wa kuchangia pato la Taifa ikifuatia Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu/matatizo, viwanda vya kusindika nyam. Tanzania inayo ng’ombe zaidi ya milioni kumi na nane kwa sensa ya 1990s, naamini sasa hivi wameongezeka. Kwa bahati mbaya, nchi yetu haina viwanda vya kusindika nyama ili tuweze kuuza mazao ya nyama nje ya nchi yetu kwa ajili ya kuongeza kipato cha ufugaji na pato la taifa. Nimependekeza viwanda vya nyama vijengwe maeneo yenye ng’ombe wengi ikiwemo Mikoa ya Arusha, Manyara, Mwanza, Shinyanga, Mara na Kagera. Mkoa wa Kagera na hasa Wilaya za Misenyi, Karagwe, Muleba, Ngara na Biharamulo zina mifugo mingi inayojumuisha ng’ombe, mbuzi, kondoo, kuku na nguruwe. Tunaomba kiwanda cha kusindika nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya ngozi, naomba vijengwe viwanda vya ngozi maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko ya mifugo, Tanzania inazo ng’ombe milioni 18, inauza nje ya nchi 0.2 ya mifugo yetu. Botswana inazo ng’ombe milioni mbili lakini inauza nje asilimia 80% ya ng’ombe wao. Kwa nini sisi tushindwe kuuza nje ng’ombe wetu japo kwa 50%. Tunaomba masoko nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Serikali iwapatie wafugaji mbegu bora ya ng’ombe inayokubalika ki–mataifa. Mfano Botswana wanayo mbegu bora sana aina ya Semento, ina nyama tamu inayokubalika nje ya nchi. Je, kwa nini wananchi/wafugaji wasipewe mbegu hizo hata kama ni kwa kununua?

Mheshimiwa Naibu Spika, upandishaji mbegu kwa chupa na njia nyingine za kisasa, tabia ya kuzalisha ng’ombe kwa madume haina tija na imepitwa na wakati. Kwani ni gharama kubwa kununua madume bora pia siyo rahisi kupanga ng’ombe atazaa lini kwani huwezi kumlazimisha dume kumpanda jike, ni lazima apende yeye mwenyewe tena kwa kupanda jike mmoja mmoja pengine kwa siku kadhaa au wiki kadhaa. Napendekeza ziletwe mbegu bora kwa njia ya chupa na ile ya kurutubisha yai ili kupata *identical* ndama watakaozaliwa na kukua kwa pamoja. Idara ya *production*, ni lazima iwezeshwe na ifanye kazi hii kwa haraka ili wafugaji wetu waweze kushindana na dunia nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za chanjo za mifugo, ni kubwa mno mfano chanjo ya *FMD* imetolewa Wilayani Karagwe kwa Sh. 2,000/= kwa ng’ombe mmoja. Wafugaji zaidi ya 50% walishindwa kumudu hizi gharama na kwa wale waliochanja walifanya hivyo kwa njia ya kulazimishwa. Lakini pia kwa kuwa kuna ambao hawakuchanjwa hivyo zoezi zima limekuwa ni kazi bure kwani wale ambao hawakuchanjwa wataambukiza waliochanjwa. Hiyo yote ni kutokana na gharama za chanjo kuwa ghali mno. Nashauri Serikali iimarishe Kitengo cha Utafiti ili kiweze kutengeneza chanjo ya *FMD* badala ya kuagiza toka nje. Kwa kufanya hivyo, gharama itapungua angalau iwe Sh.100 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, alama kwa mifugo yote nchini. Mifugo ya Tanzania yote haina alama ya kuitambulisha. Hii ni hatari kwani mifugo yetu inapoibiwa ni vigumu kuitambua. Pia alama zitadhibiti uingizaji wa mifugo haramu toka nje ya nchi hasa Mikoa ya mpakani mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa za ruzuku. Dawa za ruzuku haziwafikii wafugaji ambao ni walengwa. Wilayani Karagwe hizo dawa hazipo na kama zinafika wanafaidi wachache. Zoezi hili halijafaninkwa na nina wasiwasi zinahujumiwa, hivyo, Serikali iangalie upya utaratibu huu ambao utawanufaisha walengwa. Wauzaji wengine wanauza bei ya mtaani ambayo siyo ya ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya ufugaji yaliyokuwa ya Kitengule ranchi. Maeneo ya ranchi ya Kitengule, walipewa baadhi ya wafugaji kama *sub-lease* na tayari walishalipia gharama zote zilizotakiwa lakini hawajapewa *agreement* yoyote na baadhi yao tayari wameshaanza kuendeleza mashamba yao. Ni vema wapewe *sub-lease agreement* ili kuhalalisha uwepo wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia eneo la Kitengule ranchi sehemu kubwa amepewa mwekezaji wa *Kagera Sugar* ambaye hafugi ng'ombe wala mifugo yoyote. Inaelekea eneo kubwa la ranchi ya Kitengule karibu nusu amepewa *Kagera Sugar* na hivyo kuwafanya wafugaji walio wengi kukosa nafasi ya kufuga, badala yake wameingia katika hali ya kuzurura na mifugo yao. Kesi nyingi zimeibuka kutokana na mifugo kuingia katika mashamba ya wafugaji. Ni kwa nini *Kagera Sugar* wamehodhi ardhi na ranchi ya Kitengule wakati hawafugi? Naomba Serikali iangalie jambo hilo kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia baadhi ya wafugaji waliopewa *plots (blocks)* zinazopakana na vijiji vya Katanda, Kibwera na Mushabiguru, wamekuwa kero kwa raia kutokana na kuwazuia wananchi wa vijijini kuokota kuni, kukata nyasi na kukosa maeneo ya kulishia mbuzi wao na wengine kutishiwa maisha yao. Nashauri Mheshimiwa Waziri afike Wilaya ya Karagwe ili asaidie kutatua tatizo hilo haraka ili kuzuia uvunjifu wa amani na utulivu unaoelekea kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Nyama na *Meat Council*. Sheria ya Nyama ifanye kazi yake vizuri pamoja na *Meat Council* ili kuboresha sekta ya nyama nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya maziwa, naomba Serikali ijenge kiwanda cha maziwa Wilayani Karagwe ili kiweze kununua maziwa ya wafugaji wote wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wafugaji wanaoibiwa mifugo yao, Maafisa Mifugo hawana magari, pikipiki na mafuta ya kwenda vijijini kwa wafugaji na wakati mwingine wafugaji hutakiwa kulipia mafuta wao wenyewe. Maafisa mifugo wakae vijijini kwa wafugaji na kwa kuwa ni wachache sana, nashauri waajiriwe wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kwa kuwasilisha hotuba yake kwa umahiri mkubwa. Naomba pia nichukue fursa hii, kumshukuru Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na taasisi zilizo chini ya Wizara hii na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuleta ufanisi wa Wizara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejaliwa kuwa na mifugo mingi kwenye ardhi yake na samaki kwenye maziwa, mito na baraharini. Hii yote ni kudra ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za makusudi za kuhakikisha wafugaji na wavuvi wanafaidika kiuchumi na kimaendeleo kwa ujumla kutokana na mifugo na samaki wetu, zinahitaji kufanywa ili kuwatoa kwenye lindi la umaskini wa kipato ambapo wengi wa wafugaji/wachungaji na wavuvi wetu wamo. Kufanikishwa kwa suala hili, kutaiwezesha pia Serikali kujiongezea maduhuli yake kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanikisha hilo, mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa.

(1) Kuwapa elimu juu ya ufugaji bora na uvuvi bora na salama wavuvi wetu;

(2) Kufunza na kuwasambaza kwenye maeneo mbalimbali wataalam wa mifugo na samaki;

(3) Kujenga majosho ya kutosha kwenye maeneo ya ufugaji;

(4) Kueneza elimu ya ufugaji wa kisasa wa samaki;

(5) Kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa kuwa na maeneo maalum ya ufugaji ili kuepusha mgogoro kati ya wafugaji na wakulima;

(6) Kuhakikisha dawa za kinga na tiba ya mifugo zinasambazwa kwenye maeneo ya wafugaji;

(7) Kuongeza vituo vya kuzalisha mitamba kwa ajili ya kupata aina bora ya mifugo wakiwemo ng’ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika; na

(8) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kusindika vyama na samaki nchini ili tuuze mazao yaliyochakatwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa, maeneo yote niliyoorodhesha hapo juu, hayajafanyiwa kazi vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie mambo machache yafuatayo:-

Kwanza, migongano ya wafugaji na wakulima Wilaya ya Mbozi, katika Jimbo la Mbozi Magharibi hususan kwenye Kata za Myunga, Ivuna, Chilulumo na Kamsamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujio wa wafugaji wenye maelfu ya makundi ya mifugo kutoka Mikoa mingine hususani Mwanza, Shinyanga, Manyara na Arusha kwenye Bonde la Rukwa na maeneo mengine Jimboni kwangu, kumeleta uharibifu wa mazao ya wakulima na mazingira, kiasi cha kusababisha mtafaruku mkubwa ulisosababisha mapigano mara kwa mara. Kuna haja kubwa ya Wizara yako, kuwapa msisitizo Maafisa Mifugo wanaotoa vibali vya kusafirisha wanyama kufuata maelekezo ya Wizara yako badala ya kutoa vibali kiholela kama wanavyofanya hivi sasa.

Pili, uvuvi wa kutumia Kokoro ziwa Rukwa. Ziwa Rukwa linavamiwa na wavuvi wanaotumia nyavu za matundu madogo, maarufu kwa jila la kokoro. Kutokana na hali hiyo, kuna uwezekano wa samaki kutoweka kabisa kutoka ziwa hilo katika kipindi kifupi kijacho kutokana na nyavu hizo kukokota samaki na mayai yao. Ombi la wananchi wa Mbozi Magharibi, ni kuzipatia Halmashauri za Wilaya ya Mbozi, Chunya na Sumbawanga boti za doria ili kupambana na uhalifu huu.

Tatu, kuwe na vituo maalum vya mafunzo ya ufugaji bora wa wanyama na samaki katika Jimbo la Mbozi Magharibi ambalo nusu yake ni bonde la ufa lenye uwanda mzuri kwa mifugo na mito na Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa kuuza nyama bora nje ya nchi, bado hatujaupa nafasi kubwa, kwani Tanzania ina idadi kubwa ya mifugo kulinganisha na nchi ya Garbon, lakini nchi ya Garbon inakuza uchumi wake kupitia sekta ya mifugo kwa kuuza nyama yenye kiwango nje ya nchi, hivyo kupiga hatua kubwa katika kuboresha wafugaji wake na pato la nchi ya Garbon, lakini sisi Tanzania bado hatujaelekeza nguvu hizo kuboresha mifugo ya kuuza nyama nje ya nchi. Hivyo, ninashauri Serikali kuandaa mkakati maalum ili kuboresha mifugo kwa wafugaji na kuanza kuuza nyama nje ya nchi lili tuweze kufikia dhana ya MKUKUTA kwa wafugaji wetu na kuongeza pato la taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, machinjio ya mifugo mengi tuliyonayo nchini, ni ya kienyeji tena mengine yako katika mazingira yasiyoridhisha hasa wakati wa mvua kama vile machinjio ya mbuzi kule Vingunguti Dar es Salaam, hivyo ninaishauri Serikali kujenga machinjio ya kisasa ya mbuzi vingunguti.

Mheshimiwa Naibu Spika, wizi wa mifugo hasa Mikoa ya mipakani ni tatizo kama ilivyoripotiwa miezi michache iliyopita kule Rorya ambapo mifugo toka Tanzania,

iliibiwa na kupelekwa Kenya.  Hivyo ninashauri Serikali kutoa kauli kwamba ng'ombe walioibiwa Rorya wamepatikana au la, kama la, ni juhudi gani Serikali imeichukua?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la migogoro kati ya wafugaji na wakulima, bado linaendelea kuwepo katika maeneo kadhaa Tanzania, hivyo ninashauri Serikali Kuu kupitia Serikali za Mitaa, vijiji hadi vitongoji kutoa elimu kwa maeneo husika, maeneo yapi ni ya wafugaji na maeneo yapi ambayo ni ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba ya malisho ya mifugo bado hatujatoa umuhimu mkubwa kama vile VIKUGE, kwani wafugaji wetu wengi wanategemea kutafuta malisho kwa kuhamahama na kupelekea migogoro kadhaa katika jamii. Hivyo, ninashauri Serikali kuongeza mashamba ya malisho, hasa Mikoa yenye upungufu mkubwa kwa mfano Dodoma na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la wavuvi wetu kuporwa na majambazi kwenye maziwa. Wavuvi wetu kwenye Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na hata Ziwa Victoria, wananyanyaswa na majambazi na kuchukua vitendea kazi vyao na kuwapora fedha na wakati mwingine kupigwa, hivyo, ninaishauri Serikali kutafuta namna ya kuwalinda wavuvi wetu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wetu wengi kwenye bahari ya Hindi na hata kwenye maziwa, wanapoteza maisha pale vyombo vyao vinapozama na hii imekuja kwa sababu ya vyombo vya uvuvi havina makoti ya kuokolea maisha. Hivyo, ninashauri Serikali kuwakopesha wavuvi wetu makoti ya kuokolea maisha na waweze kulipa kidogokidogo ili tuweze kuwakinga, kuwalinda na vifo hasa wakati wa dhoruba baharini na maziwani.  Ni vema tukawalinda wavuvi kwani na wao wanachangia kiasi kikubwa katika dhana nzima ya MKUKUTA na kukuza pato la taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naomba kuwasilisha.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Magufuli na Naibu wake kwa kazi  nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Nyasa, ni ziwa lililosahauliwa kwa muda mrefu katika kuwaendeleza wavuvi ukilinganisha na maziwa ya Victoria na Tanganyika. Wavuvi wa Ziwa Nyasa ni duni, masikini na wana zana duni na hafifu. Bado wavuvi wale wanatumia mitumbwi ya miti ya miembe katika kavua jambo ambalo haliwaongezei tija. Ziwa Nyasa, ni kati ya maziwa yenye mawimbi makubwa hivyo kuhitaji vyombo vya kisasa na vyenye usalama wa hali ya juu ili kunusuru maisha ya wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Ruhulu, ni mto pekee ambao ndiyo mazalia makubwa ya samaki aina ya Mbelele, Mbasa, Ngumbu na kadhalika lakini wachimbaji madini wadogo wadogo huharibu vyanzo vya mto huo kwa kutia udongo wa zebaki kwenye vyanzo vya mto huo hivyo kuharibu mazalia ya samaki na kusababisha mto kukauka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi yafuatayo:-

- Wavuvi wapatiwe zana za kisasa za uvuvi hasa maboti ya injini ili kuongeza tija;

- Elimu ya uvuvi bora kama semina na kozi mbalimbali ziendeshwe ikiwahusisha wataalam wa Wizara;

- Aliyekuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zabein Mhita, aliahidi kuwaletea Wavuvi wa Ziwa Nyasa boti la ulinzi ili kuzuia uvuvi haramu. Naomba sasa boti hilo liletwe;

- Mikopo rahisi kwa wavuvi ili waweze kununua nyavu na maboti; na

- Wachimbaji wadogo wadogo waache kuchimba kandokando ya mto Ruhulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo ni kati ya rasilimali zilizoko nchini lakini hali halisi inaonekana sekta hii haipewi umuhimu unaotakiwa vivyo hivyo katika sekta ya uvuvi – imeachwa kujiendesha yenyewe hasa kwenye maziwa madogo kama vile Ziwa Rukwa na kadhalika, Ifuatayo ni hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma kwa sekta ya mifugo Vijijini, hakuna uhakika kwa mifugo iliyoko vijijini hasa ile iliyoko bonde la Ziwa Rukwa, Wilayani Chunya. Huduma hizo ni kama vile ukosefu wa majosho, malambo na tiba. Wafugaji hujitafutia mbinu za kuhudumia mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa Watendaji (Wagani), katika Jimbo la Songwe lenye ukubwa wa kilomita za mraba 29,000 na ambako mifugo imeenea hakuna ugani wowote unaotolewa, ufugaji unafanyika kienyeji tu. Matokeo yake mifugo inayofugwa huko ni ya daraja la chini sana. Nashauri utaratibu ufanyike kwa kuwapeleka wagani kwenye Jimbo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro kati ya Wafugaji na Wakulima, je, Wizara inashughulikiaje migogoro hiyo ambayo hivi sasa inaonekana kama ni hali ya kawaida? Wafugaji ndio chanzo cha migogoro kwa kuingiza na kufugia kwenye mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, usindikaji wa mazao ya mifugo, je, Kituo cha *Tanganyika Packers* cha Mbeya kitarejeshwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi Ziwa Rukwa, ni rasilimali ambayo ni kama imetelekezwa. Maana uvuvi unaofanyika huko hasa kusini mwa ziwa hilo, Wilaya ya Chunya na Mbozi, ni wa kiholela isingekuwa vema Wizara ikasimamia uvuvi huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu wa mazingira, ni mikakati ipi Wizara ya Mifugo inafanya kuzuia uharibifu wa mazingira unaofanywa na mifugo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, hata hivyo, ninayo machache ya kusisitiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Mkoa wa Kigoma na hasa Wilaya ya Kasulu, ilivamiwa na wafugaji wa ng'ombe waliofukuzwa katika bonde la Ihefu huko Mbarali Mbeya. Aidha, wengine ni wale waliondolewa katika Bonde la Ziwa Rukwa. Wafugaji hawa wamevamia katika vijiji vya Titye, Rungwe Mpya, Asante Nyerere, Sogeeni na Kagera Nkanda, vyote vipo Wilaya ya Kasulu tena Jimbo langu la Kasulu Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo, wafugaji hawa wanaharibu sana mazingira na vyanzo vya maji, wamevamia eneo tengefu la mto Malangarasi na Mto Ruchugi hivyo kusababisha kupungua kwa kasi ya uoto na maji katika maeneo hayo, kwa sababu ya uholela huo, idadi ya ng'ombe haujulikani na maradhi ya mifugo yameongezeka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini Kifanyike? Wizara ya Mifugo ikisaidiana na Halmashauri ya Kasulu, fanyeni sensa ya mifugo katika vijiji nilivyovitaja Wizara yako iongeze vijia *(take lead).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo, iitambue Wilaya ya Kasulu kwamba sasa ni Wilaya yenye mifugo mingi, hivyo uwekezaji kwa ngazi ya Taifa katika Sekta hii uitizame Wilaya hii kwa jicho la kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo fedha ili kufanya utafiti wa jinsi wafugaji hawa wanavyoharibu mazingira na itoe ushauri endelevu ambao pia utashirikisha wananchi na Serikali za Vijiji katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iingie kikamilifu kuhamasisha kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, matumizi bora ya bidhaa za mifugo kama vile ngozi, kwato, kusindika nyama na hata biashara ya mifugo kwa nchi jirani za DRC na Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara isimamie shughuli za uvuvi katika mabwawa asilia ya Kapuruka na mashamba ya samaki *(fish ponds).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itenge fedha kwa ajili ya maeneo haya mapya ya mifugo na hasa Wilaya ya Kasulu ili kukuza kipato cha watu na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, uvuvi katika Ziwa Tanganyika. Kwa kuwa mradi wa Bonde la Ziwa Tanganyika unaanza kutekelezwa 2008/2009, niombe na kusisitiza kwamba Wizara ya Mifugo na Wizara ya Mazingira, ofisi ya Makamu wa Rais, zishirikiane kwa karibu ili mradi huu uwe na tija na faida endelevu. Kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya Kuzingatia ni kuanzisha Viwanda vidogo vidogo vya kusindika dagaa na samaki (migebuka) mjini Kigoma na mwambao wa ziwa Kusini na Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe na kikao cha pamoja kati ya Wabunge wa Mkoa wa Kigoma na Rukwa ili tuzungumze juu ya Sekta hii ya uvuvi katika ziwa Tanganyika. Wizara yako isaidie kuandaa kikao hiki katika Bunge hili hili kabla ya tarehe 20/8/2008. Kikao hiki kitatupa fursa ya kubadilishana mawazo na kupashana habari juu ya sekta hii muhimu ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inisaidie kutoa habari/taarifa za biashara na masoko ili sekta binafsi ihamasishwe kuwekeza katika sekta hii. *The Ministry must steer the wheel.* Aidha, viongozi wa Wizara hii karibuni Kigoma ili tupate fursa ya kubadilishana mawazo katika sekta hii.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza jirani yangu kwa ujasiri na uchacharikaji katika kuiletea maendeleo nchi hii na Jimbo lake la Chato. Nampongeza pia Mheshimiwa Dr. Wanyancha kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Geita hususani Jimbo la Busanda, linakabiliwa sana na uhaba wa maeneo ya kuchungia mifugo. Hali hii imesababishwa na kilimo, pamoja na kazi za uchimbaji madini. Naomba kwa kuwa eneo hili linazungukwa na misitu ambayo haina wanyamapori, wafugaji waruhusiwe kuchungia mifugo yao katika mapori hayo. Wapewe masharti ya kutolima na wala kukata miti. Itapendeza kwani Wamasai wameruhusiwa kuishi katika mbuga za wanyama. Wafugaji hawa watapewa masharti ya kutunza maeneo na wako tayari. Hivi sasa wanachungia humo kwa kuiba na kutoa rushwa kwa Askari, wanadhulumiwa sana na Mabwana Misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mabwawa yaliyokuwa yakitumiwa na ng’ombe yafufuliwe. Kwa mfano Jimbo la Chikobe, Nyarugusu, Kamena na Buzanaki. Wafugaji wanakabiliwa na uhaba wa maji kutokana na mabwawa haya kutofanyiwa mkarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kianzishwe kiwanda cha kusindika zao la mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wapewe semina juu ya haki zao kwani wanaonewa na wanadhulumiwa kwa kuwa wengi wao wanakuwa hawajui haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wanaibiwa sana na majambazi. Wengi wanazamishwa na kuuawa. Naomba boti ya kuangalia patrol katika ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MIZENGO K.P. PINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kuwa tatizo la Ziwa Rukwa, sasa ni *slitting*. Ziwa Rukwa halina mito inayotoa maji. Mito yote kabla ya kuingia ziwani, inapita katika maeneo yenye mifugo mingi Wilayani Chunya, Mbozi, Sumbawanga na Mpanda, wakati wa msimu wa mvua, udongo wote uliokanyagwa na mifugo huwa vumbi, huchukuliwa na mito hadi ziwa Rukwa, hivi sasa ziwa limejaa tope jingi sana. Hivyo, uhai wa ziwa uko mashakani. Hivyo, suala la kuwa na mkakati maalumu wa hifadhi ya mazingira kwa ajili ya ziwa hili ni muhimu sana.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, walioandaa hotuba hii na kusomwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake, kutokana na kujitosheleza hutoba hii ina mchango mdogo tu unaohusu kuku. Kuku ni miongoni mwa mfugo unaopendwa sana vijijini na kusaidia wananchi katika kukuza kipato chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuku ni kiumbe dhalili asiyependa taabu na hastahili vishindo ukilinganisha na viumbe vingine vinavyofugwa pia kuku ni kiumbe kinachofugwa na hata watu wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kiumbe hiki hufugwa na mtu yeyote, kumejitokeza tabia ya baadhi ya wafugaji na wanunuzi wanapopeleka bidhaa hii sokoni huchukua kuku na kuwaning'iniza vichwa chini miguu juu. Hali hii huwasababishia kuku maumivu na wengine hufa. Kitendo hiki nakiona ni cha kikatili na inapaswa kupigwa vita. Uchukuzi huu wa kuku na badala yake wawekwe kwenye matenga au masusu yanayoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tatizo hili, ninamwomba Mheshimwa Waziri (Serikali), alitolee kauli suala hili ili lisiendelee pamoja na kuweka adhabu kali kwa atakayeendeleza ukatili huo unaofanyiwa kuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wenu kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwenye sekta hii ni kukuomba Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wako kusimamia kwa karibu na kuratibu

shuguli za uvuvi wa bahari kuu. Uvuvi huu kama utasimamiwa vizuri, bila shaka utasaidia sana kuinua kipato cha wananchi na hatimaye Serikali nayo itafaidika.

Usimamizi wa karibu unatakiwa hasa kwenye nchi za nje ambazo usimamizi wake utahitaji vyombo na zana za kisasa ili kuweza kuwa na uwezo wa kukabiliana nao pindi wakitaka kufanya hadaa. Kwa bahati nzuri, tunayo *Radar* ya kisasa pale Kigamboni au eneo la kuvuka kuelekea Kigamboni. *Radar* hii basi na iwe ndio macho ya Serikali kumjua nani ameingia na nani anatoka katika eneo la bahari linalomilikiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kusimamia hili basi jeshi la *KMKM* la Zanzibar litumike ili ku- *enforce* eneo hilo la bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu, mchango huu mdogo utasaidia katika kuona Wizara inaimarika na hatimaye sekta hii iungane na sekta nyingine kama vile za madini na utalii katika kuimarisha uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuombeeni mafanikio katika kupitisha bajeti hii na katika utendaji wenu kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nachukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na uwezo wa kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uvuvi nchini, uuvi ni sekta moja muhimu katika nchi yoyote duniani yenye bahari na au maziwa. Ni sekta ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa pato la nchi hasa kama sekta hii itaendelezwa kwa mikakati mahsusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejaliwa sana kuwa na bahari na maziwa ambayo ndani yake wako samaki wa kila aina. Sasa linalohitajika ni mikakati thabiti ya uvuvi ili wananchi wa nchi hii hasa wale wavuvi wapate kunufaika na rasilimali ya samaki waliomo baharini na kwenye maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wadogo wadogo, wananchi wengi wanaoishi visiwani kama vile Mafia, Unguja, Pemba, Ukerewe na kadhalika, wanategemea uvuvi katika kujipatia mahitaji yao ya maendeleo. Hatua ya Serikali ya kupiga marufuku baadhi ya vifaa vya uvuvi ambayo ni rahisi wananchi hao kuvipata na kuvitumia, kwa kweli haikuwatendea haki wavuvi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali ingefanya juhudi ya makusudi ya kuwaelimisha wavuvi nini maana ya MAZINGIRA na jinsi yanavyoharibiwa. Lakini tendo la kupiga marufuku bila kutoa taaluma halikuwa la kiungwana hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii wavuvi wangapi wamekosa kazi, hivyo kukosa mapato na kwa maana hiyo watapata wapi pesa za kuwasomeshea watoto, pesa za matibabu na hata pesa ya kununua chakula?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaitaka Serikali ilegeze msimamo wao huo ili kuwapa fursa Watanzania wengi ambao wamejiajiri katika sekta hii ya uvuvi kufanya shughuli zao.  Ni kweli kuna haja ya kulinda uharibifu wa mazingira na uvuvi haramu, ni muhimu sana, lakini elimu itolewe kwa wadau katika hili ili mambo yote haya mawili yaende sambamba yaani wavuvi waruhusiwe kuvua na hifadhi ya mazingira pamoja na uvuvi haramu yatiliwe mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, halitakuwa jambo la busara, meli za nje zinazovua bahari kuu na ambazo mara nyingi faida tunayopata ni kidogo sana, zinaruhusiwa kuvua lakini wavuvi wadogo wadogo na ambao wanatoa kodi kwa maendeleo ya nchi wawekewe vikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hali itaendelea kama ilivyo ya wavuvi kuwekewa vikwazo, je, Serikali inao mpango gani mbadala wa kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo wa nchi hii kupatiwa mitaji na vifaa vya kisasa vya uvuvi?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inajua kwamba wavuvi wadogo wadogo wanafanyiwa vitendo vya unyanyasaji na Maafisa wa Idara ya Uvuvi kwa visingizio vya kudhibiti uvuvi haramu?  Kama inajua, ina mpango gani wakulikomesha tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kudhibiti uvuvi haramu, ni muhimu sana na Maafisa wetu waendelee kufanya hivyo lakini wazingatie sana kanuni bora za utendaji kazi pamoja na ubinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi katika maziwa hasa Ziwa Tanganyika, bado wanapata mashambulizi makubwa na hata kunyang’anywa vifaa vya uvuvi kama vile maboti, mashine na nyavu kutoka kwa maharamia wa nchi jirani.  Hivi Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na vitendo hivyo vya uharamia ambavyo vinawagharimu sana wavuvi hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, tungependa kujua wakati Waziri anapofanya majumuisho ni maharamia wangapi wametiwa mbaroni kwa kipindi cha Juni 2005 – Juni 2008? Ni hasara gani, kwa maana ya kiasi cha fedha na vifaa, wavuvi wetu wameipata kwa kipindi hicho cha miaka mitatu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuunga mkono hoja.

Aidha, napenda kuwapongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, pia Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii kwa utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu sana maana inashughulika na chakula aina ya kitoweo.  Bila kitoweo, ni vigumu kidogo kukamilisha chakula kwani si

rahisi chakula kikaliwa bila ya kitoweo. Kwa ajili hiyo, ni vema yafuatayo yakazingatiwa:-

Kwanza, ni lazima utafiti wa Taasisi za Mifugo na Uvuvi ziimarishwe. Vile vile zipewe wataalamu, vifaa na mafuta ya kutosha. Tukifanya mchezo, magonjwa na athari za mifugo zitaendelea kuathiri sana afya za Watanzania.

Pili, Wizara irudishe mara moja Chuo cha Utafiti wa Mifugo Liti – Temeke ambacho kimefungwa. Chuo hiki ni muhimu sana kwa kuzalisha Watafiti wa Mifugo. Kuendelea kutotoa wataalam wa maabara, ni wazi kuwa wataalam wa utafiti hawatakuwepo na hivyo utambuzi wa uthibiti wa magonjwa hautakuwepo, hii ni hatari.

Tatu, Wizara ya Mifugo iimarishe suala la uendelezaji wa majosho. Majosho ni muhimu sana kwa mifugo na hasa kwa kuwa hapa nchini ndigana baridi, ndigana kali ambazo chanzo ni kupe huchuka nafasi. Ni vema basi majosho yakaimarishwa.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Mara, napenda kutoa shukrani zetu kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa ushirikiano na upendo mlioonyesha kwetu kutokana na kifo cha mpendwa wetu, marehemu Chacha Wangwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuwakumbuka wafugaji na wavuvi wa Taifa letu hususan wa Wilaya ya Rorya kwa kuwateua viongozi wa ngazi ya juu kuiongoza na kusimamia Wizara hii, viongozi ambao wanatoka katika Mikoa, Wilaya na vijiji vya wafugaji na wavuvi. Mheshimiwa Magufuli – Chato, Mheshimiwa Wanyancha – Serengeti na Katibu Mkuu, Nyamurunda – Rorya. Wizara sasa imepata wafugaji na wavuvi, wananchi wana imani na uongozi wao. Wananchi wa Rorya wanawategemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maombi na maoni ya wananchi wa Wilaya ya Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uvuvi. Wilaya ya Rorya, ina vikundi 34 vya ulinzi wa rasilimali ya uvuvi *(BMUS)*. Vikundi hivi vinajitahidi sana kulinda rasilimali yetu kwa zana duni na maslahi duni ikilinganishwa na nchi jirani. Naomba Kituo cha Sota kipewe boti kwa ajili ya doria hii ni pamoja na mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani kwa aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dialo ambaye aliingiza Sota katika orodha ya Mialo ya kisasa kwa msaada wa wafadhili. Nampongeza Mheshimiwa Magufuli na timu yake kwa kutekeleza ahadi ya Serikali ya CCM kwani Sota itakuwa miongoni mwa mialo ya kisasa. Wananchi wanaomba wafikishiwe huduma za umeme. Maombi yapo Tanesco. Wizara isaidie kusukuma barabara toka Ruka – Utegi – Sota, iwe inapitika wakati wote. Namshukuru Mheshimiwa Magufuli ambaye ndiye aliwezesha barabara hii kutengenezwa kuanzia mwaka 2002, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Rorya ndiyo inapakana na nchi jirani ya Kenya, imeathiriwa sana na uvuvi haramu, utoroshaji wa samaki kwenda Kenya, asilimia 75% ya samaki wanaovuliwa huenda nchi jirani kwa njia ya magendo. Wavuvi wadogo wanavamiwa, wavuvi wanatumia boti na meli ndogo, hawana uwezo kwa kujitetea. Naomba ujenzi wa mialo ya kisasa katika maeneo ya Nyang'ombe – Kata ya Namagoro, yenye wavuvi wengi lakini hawana awezo wa kuhifadhi samaki, hawana zana za kisasa, Masonga, Busanga na Kabuji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya mifugo. Tangu mwaka 2003, nilileta ombi Wizarani ili kuwawezesha wafugaji wa Wilaya ya Rorya ukarabati wa majosho 11 wilayani. Kwa kuwa Naibu Waziri aliyekuwa katika Wizara hii, Mheshimiwa Dr. Mkinga, aliniahidi atakwenda mwenyewe kukagua majosho hayo, naomba Mheshimiwa Waziri amtume Naibu wake/wataalam wake kwenda Rorya kusaidia wafugaji kuhusu, majosho ambayo hayafanyi kazi. Natambua kuwa suala hili linaanzia Halmashauri lakini pamoja na Halmashauri ya Wilaya kuwa ndiyo inajukumu hilo, Wizara inajukumu la kutoa ushauri na namna ya kupata fedha katika vyanzo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya ng'ombe Mkoa wa Mara inakadiriwa kuwa ni milioni 1,216,466. Wilaya ya Rorya inakadiriwa kuwa na ng'ombe zaidi ya 400,000. Pamoja na idadi kubwa, wezi wamekithiri. Kuanzia mwaka 2006 – 2008 ng'ombe wapatao 3,000 waliporwa kutoka kwa wananchi na wengi wanatoroshwa kwenda nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba minada katika mipaka ya Wilaya ya Tarime na Wilaya ya Rorya ambayo ndiyo vyanzo vya wizi huu, wafanyabiashara kutoka Kenya ndiyo wanunuzi wa ng'ombe katika mnada wa Randa, Nyamagiku, Ochuna na kadhalika, mpango ufanywe na Wizara kwa kuwatangazia wafugaji wetu kujiandaa kwa biashara ya mifugo, mazao yake (ngozi), katika nchi za nje kwa mfano UAR, Oman, Kuwait, Comoro, Italy, Hongkong, India na Uturuki badala ya Kenya na Uganda ambao wanatuibia. Mheshimiwa Waziri uwatangazie wananchi wa Rorya utakapohitimisha hotuba yako kwa kuijibu hoja hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wa Mkoa wa Mara hususan Wilaya ya Rorya, wanaomba Serikali iwapatie wawekezaji wa Kiwanda cha Usindikaji wa Nyama na Kiwanda cha ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, anijibu si kwa sababu unaniheshimu bali kwa kuwa maombi haya ni kutoka kwa wafugaji na wavuvi. Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu ni watoto wa wafugaji na wavuvi, wananchi wanapenda kusikia sauti yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naomba majibu.

**MHE. CASTRO R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa hotuba nzuri yenye *data* nyingi.

Mchango wangu utajikita katika maeneo mawili. Kwanza ni uvuvi katika *"minor waters"* kama Mito ya Wilaya ya Kilombero. Wilaya ya Kilombero ina mtando wa mito mikubwa na midogo ambayo yote inaingia katika Mto Kilombero na Kilombero kuingia mto wa *Great Ruaha* na kisha kuingia mto Rufiji kuelekea baharini. Mito hiyo ni pamoja na Mto Mpanga, Mto Mnyera, Mto Kihansi, Mto Mngeta, Mto Ruipa, Mto Lumemo na mingine mingi.

Uvuvi mwingi katika mito hii hufanyika katika mto mkubwa wa Kilombero na kama nilivyowahi kusema katika Kamati ya Kilimo, mifugo na maji kwa uvuvi huo huwa unafanyika na wavuvi kuishi kwenye makambi ya muda. Kisheria sehemu hizo zilikuwa haziruhusu maisha ya kudumu ya wananchi au wavuvi hao. Hii ilisaidia kuhakikisha kuwa hawa wavuvi kwa wakati fulani wanarudi kijijini na kuungana na familia zao.

Ilivyo sasa hivi, hali haikuwa hivi. Wapo wavuvi ambao wanakaa kwenye makambi hayo kwa muda wa mwaka mzima bila kurudi nyumbani, jambo ambalo linasababisha tatizo la kijamii kwani wake zao hubaki na majukumu yote ya familia kama elimu, matibabu na michango mbalimbali.

Katika swali langu katika moja ya mikutano ya Bunge, niliwahi kulielezea tatizo hilo na kujibiwa kuwa sheria iko mbioni na kuhakikisha wavuvi hao wanapata leseni kwa kuvua kwa miezi mitatu tu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hili sikuliona na napenda nimwombe Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake atueleze ni lini sheria hii itaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la makambi haya, yako mbali na vijiji ambavyo ni makazi ya watu au wananchi. Ni vigumu maeneo hayo kupata Watendaji wa Serikali ambao wanaishi huko.

Kwa hiyo, katika hali hii, hao wavuvi hutumia hata zana za uvuvi ambazo ni haramu yakiwemo makokoro yanayokwangua hata mazalia ya samaki hasa jamii ya *cichlidae* ambao hutaga mayai kwenye viota chini ya mito. Aidha, baadhi ya aina za samaki kwenye mito hii ambayo hapo zamani zilikuwa nyingi, zimeanza kutoweka kabisa, kwa mfano, njuju na Mbala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa samaki *(Fish Culture).* Nimesoma hotuba ya Waziri na kuona katika eneo hili, mkazo wa ufugaji wa samaki katika Kituo cha Kingolwira pale Morogoro ni kuongeza vifaranga vya perege na Kambale.

Lakini nilishaeleza mara nyingi, perege sio *species* nzuri ya kufuga kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Kama mfugaji hatawavua kwa kuwatenganisha kwa jinsia *(mono sex),* perege wana desturi ya *prolific breeders*. Kwa muda mfupi wanaweza wakajazana, kwenye bwawa na kisha wakawa wamevia kutokana na kunyang'anyana chakula.

(ii) Kama utafuga madume peke yake na majike peke yake, perege huwa wanakuwa vizuri.

(iii) Kituo cha Kingolwira kinatakiwa kiende mbali na usambazaji wa vifaranga vya perege bali wafanyatafiti za kuingiza mbegu mpya za samaki wafugwao kama ifuatavyo:-

(1) Kuchanganya ufugaji wa samaki na ufagaji wa bata aina ya *peking ducks* kama wafanyavyo pale Bwawani. Bata wale waliingizwa na Idara ya Uvuvi miaka ya 1980 lakini wakapewa Magereza baada ya Idara kushindwa kuwahudumia bata hao.

(2) Kutafuta *species* nyingine kama *common carp (cyprinus coarpio sp) grass carp, silve, carp* ambazo uzito wake kwa samaki mmoja unaweza kumpa mfugaji faida kubwa kuliko perege.

(iv) Wataalam waende kwenye nchi jirani kujifunza kutoka kwa wenzetu (Uganda, Kenya).

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi wa majongoo, Mheshimiwa Waziri naomba atueleze kwa nini wavuvi wadogo wadogo wazuiliwe kutovua majongoo? Ukweli hakuna sababu wavuvi wadogo kuzuiliwa uvuvi huo ukiangalia wananchi wanaoishi sehemu ya bahari ya Hindi ndio wanaoweza kusomesha na kujikimu kimaisha.

Kuzuiliwa kuvuna *Shells* – kama Mapasi, Madondo na *Shells* ambazo Serikali imezuia. Ukweli ni kwamba kwa kufuata taratibu za baadhi ya nchi wafadhili, vitu hivyo kuzuiliwa sio jambo la msingi. Sisi wengine ndio vitu vilivyotusomesha na tumekulia kwenye mazingira ya uvuvi wa *Shells* pamoja na samaki. Kuzuiliwa kutumia uvuvi wa Kioo pamoja na viatu, yaani *Killper,* naomba Mheshimwia Waziri anieleze kuvaa vifaa hivyo tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ndogo za kuwazuia wavuvi wadogo wadogo na kuwapa uwezo wa kutumia bahari yetu Watanzania, kuwapa fursa wageni au wavuvi wa bahari kuu hamwafanyii haki wavuvi wadogo wa Kitanzania. Namwomba Mheshimiwa Waziri sheria nyingine ziangaliwe kwa uyakinifu kwa sababu Watanzania ndio wanaoathirika. Sheria za nyavu ziangaliwe upya. Kwa sababu nyavu inategemea ukubwa wa macho ya nyavu. Ukweli sheria hizi zinawaumiza wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN DAMIAN KOMBA NA MHE. STELLA MARTIN MANYAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunapenda kumpongeza Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Awali ya yote tunapenda kumpongeza kwa kazi nzuri anayoifanya. Ni kwa muda mfupi tu tunashuhudia juhudi zao pamoja na Wizara kwa ujumla jinsi wanavyoshughulikia masuala mbalimbali na matatizo

yanayoikabili Wizara hususan katika suala zima la uvuvi. Tunampongeza sana pia Naibu Waziri wake - Mheshimiwa James Wanyancha na Katibu Mkuu wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge tunaowakilisha eneo la Ziwa Nyasa tunashuhudia matatizo makubwa wanayoyapata wavuvi wetu katika Ziwa Nyasa na hivyo kusababisha umaskini uliokithiri wa kipato na maisha kwa ujumla.

Ziwa Nyasa kwa asili, lina mawimbi makali na hivyo kusababisha vifo hasa wakati wa dhoruba. Lakini katika ziwa hilo, Mungu ametoa neema kubwa ya dagaa na samaki ambao tuna imani amewahi kula na kushuhudia utamu wake. Kutokana na kuzuiliwa kuvua kwa makokoro na maji ya kina kifupi, wavuvi hulazimika kwenda kwenye kina kirefu kwa kutumia mitumbwi hafifu iliyochongwa kwa miti ya miembe michanga, kwani hata upatikanaji wa miti mikubwa asilia kwa sasa ni mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri chonde chonde tupo chini ya miguu yake tuonaomba atuwezeshe kupata maboti mawili, katika vituo vyetu vya Kihagara na Liuli ikizingatiwa kuwa toka asili Kihagara inaongoza kwa uvuvi wa dagaa ikifuatiliwa na Liuli jambo ambalo Tanzania itaweza kuwe na usambazaji wa dagaa kutoka Ziwa Nyasa, hivyo kuongeza kupato cha wananchi hao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali tunaomba Mheshimiwa Waziri aseme asikike, ili wananchi wa kando ya Ziwa Nyasa nao wasikie ni wadau wa bajeti hii na kwa heshima kuwa kitoweo kimempata mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwategemea na tunawapenda sana.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa dhati mtoa hoja Mheshimiwa John Magufuli, akisaidiwa na Naibu wake Dr. James Wanyancha, Katibu Mkuu Dr. Charles Nyamurunda na watumishi wote kwa jinsi walivyoandaa hoja hii vizuri na kwa kina. Nimefurahishwa sana na mpangilio wote wa hoja hii. Naiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Magufuli kwa jinsi anavyokuja Mkoani kuzindua sherehe ya siku ya kunywa maziwa, Mkoani Rukwa kwa niaba ya Taifa. Sisi tuliona ni heshima kubwa na kwa kweli wana Rukwa walihamasika sana kwa kuona umuhimu wa kunywa maziwa.

Katika kutekeleza maagizo uliyotuachia wananchi wanaomba kuanzia mwaka huu wafikiriwe kuhusu maeneo yafuatayo:-

(1) Kuimarisha mpango wa kupa ng’ombe lipa ng’ombe, mpango huu ndio ukombozi wa kudumu wa mfugaji mdogo Mkoani Rukwa.

(2) Pamoja na jitihada za Mkoa katika matumizi ya wanyama kazi kwa viwango vya juu, lakini kuna upungufu mkubwa wa vituo vya kueneza matumizi ya zana

mbalimbali za kilimo zinazokokotwa na wanyamakazi. Kuna kila sababu ya kuimarisha utalaam kwa wakulima wenyewe na Maafisa wa Ugani. Tuomba tujengewe vituo vya kutosha angalau kwa kila Tarafa au Kata.

(3) Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la magonjwa ya kuambikiza kwa mifugo ni tishio kubwa sana kwa usalama wa mifugo yetu. Wafugaji wanaendelea kuiomba Serikali kwa kutoa ruzuku wa dawa mbalimbali za mifugo. Majosho mengi hutumika kidogo sana na wakati mwingine wafugaji hupata tatizo la ukosefu wa maji. Hivyo, wanaomba *"sprayers"* nazo zinapoingizwa nchini zisiwe na kodi kubwa.

(4) Mpango maalumu uendee kutolewa kwa wafugaji kwa kuwapa kozi fupi fupi ili wapate utaalamu wa jinsi ya kutibu mifugo katika maeneo yao na ninashauri vijana waliomaliza *Form IV* na wanaoishi humo humo vijijini, wapewe mafunzo hayo na wabaki kama *Livestock Attendants* chini ya Serikali zao za Kata/Vijiji. Tuimarishe vyuo vyetu ili vifanye kazi za ziada za kuandaa vijana hawa.

(5) Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba pia Serikali kwa kushirikisha Wizara husika iandae kwa haraka *Land Use Plan* ili matumizi ya kila eneo yajulikane kwa uwazi ili kupunguza mapigano ya mara kwa mara kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna umuhimu wa kuimarisha *"stock routes"* hapa nchini. Hali ya sasa inaonyesha hatujaweka maandalizi ya kutosha, katika eneo hili. Hakuna mahali pa kupumzikia mifugo au sehemu ya kunyweshea maji mifugo hiyo inaposafirishwa. Hali hii inasababisha uharibifu wa mazingira, barabara na hata kingo nyingi za mito yetu kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho namwomba Mheshimiwa Waziri aone namna ya kunusuru upungufu mkubwa wa samaki katika Ziwa Rukwa, baadhi ya sababu hizo ni uvuvi kwa kutumia makokoro. Pia, wingi wa mamba katika ziwa hili ni tishio kwa samaki wachache waliomo ndani ya ziwa hilo. Nashauri Mheshimiwa Waziri Magufuli awasiliane na Mheshimiwa Waziri Mwangunga wa Maliasili na Utalii ili wakubaliane jinsi ya kuvuna mamba hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii pia kwa ajili ya Waziri, amewapa heshima Mawaziri wenzake waliomtangulia. Tujenge tabia kama hiyo kwa kila Wizara.

**MHE: FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kusema kuwa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalamu wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenye kuonyesha mwelekeo wa Wizara hii, ni matumini yangu kwamba kwa kuwapatia uwezo wa bajeti inayoombwa, Wizara hii itaweza kufikia malengo. Kwa mantiki hii ninaunga mkono hotuba ya Waziri kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu, napenda kuunga mkono kwa kuchangia kwenye vipengele vifuatavyo:-

(1) Wapo wafugaji wapatao 3,000 ambao walikuwa wakifugia mifugo yao katika eneo la Kunkanda. Serikali iliwajengea shule na Kituo cha Afya kuanzia miaka 30 iliyopita ili kuwawezesha kuendelea na Sekta hiyo ya mifugo ipatayo ng'ombe 12,000. Watu hawa hawana madhara kwa ujangiri, lakini wamefukuzwa katika eneo hilo bila kujali wanapelekwa wapi. Wananchi hao wanahangaika na mifugo yao kiasi kwamba sasa ng'ombe wanakufa kila siku kutokana na kutokuzoea majani.

Ninaomba Serikali ingilie kati kuhakikisha hawa wananchi wanahangaika na mifugo yao ili waweze kuendeleza Sekta hiyo ya mifugo. Naomba hii izungumzwe wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha.

(2) Wilaya ya Kibondo inao wafugaji wengi na kwa hakika wapo ng'ombe wengi ingawa idadi yake nimechelewa kuipata. Ninaomba wafugaji wa Wilaya ya Kibondo kama wafugaji wengine, wapewe majosho ya kutosha pamoja na huduma ya tiba kwa kuepusha athari za magonjwa toka nchi jirani kama vile Burundi na Rwanda.

(3) Ninaomba ule mpango wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe chini ya *Heifer Project* chini ya Serikali, iwafikie wananchi hao wa Kibondo ili wajikwamue na umaskini. Miradi hii ya maendeleo kwa wananchi ilisahaulika kufikishwa kwa wananchi wa Kigoma na husan wale wa Wilaya ya Kibondo na ndiyo maana Mkoa mzima uko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ya kutosha kuhusu vipengele hivyo vitatu.

**MHE: USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa bajeti nzuri na yenye kutia matumaini kwa Watanzania, lakini pia ni bajeti ambayo inatekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ya uvuvi ni sekta moja muhimu sana kwa wananchi katika kukua kwa pato la Taifa kama sekta hii ingepewa umuhimu. Lakini kwa kutopewa umuhimu sekta hii ni kwa kiasi kidogo tu ndio wananchi wanafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii karibu sehemu kubwa ya eneo lake limezungukwa na bahari ambayo ndani yake kuna raslimali nyingi hasa ile ya samaki. Lakini jambo la kushangaza, raslimali hizi nyingi huwa zinachukuliwa na meli za kigeni ambao huwa zinavua katika eneo letu na kuvuna samaki wengi na kuwasarifisha nchi za nje.

Mhesimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kutafuta meli za uvuvi pamoja na vifaa vya kisasa ili tuweze kutumia kwenye bahari kuu kuvuna raslimali hizo kwa

manufaa ya nchi nii na hata kukuza pato la Taifa, kuimarisha doria ili kudhibiti uvuvi haramu, pamoja na kuimarisha kikosi cha doria kwa kukipatia vifaa.

**MHE: MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti katika Tarafa ya Kigamboni wavuvi wetu wamekuwa wakipewa maelekezo ya kuvua mchana, kutotumia vioo vya kuzamia baharini/viatu vya kuogelea na kutumia bunduki za kuvulia samaki. Haya yote kwa sisi wengine tuliokulia sehemu za bahari yanatushangaza sana, hivyo watu wote wa mwambao na wavuvi wa maji bahari hawalielewi vyema hili.

Nashauri litolewe ufafanuzi wa kutosha juu ya madhara yaliyopelekea kuzuiwa kutumia vifaa hivyo na wavuvi. Kwa maoni yangu, vyote hivyo havina madhara, lakini kwa kuwa ni maamuzi, lifanywe zoezi maalumu la kuelimisha wavuvi. Wavuvi wengi nchini wamekuwa wakilalamika juu ya uwepo wa lazima wa kila mvuvi kuwa na leseni tofauti za uvuvi kutegemea aina ya uvuvi.

Ni vyema sasa wavuvi wakafikiriwa kuwa na leseni moja ya uvuvi badala ya kuwa na leseni nyingi tofauti. Kwa mfano, leseni ya uvuvi wa kamba, leseni ya uvuvi wa pweza, leseni yake binafsi ya uvuvi, leseni ya chombo cha uvuvi na kadhalika.

Nashauri leseni iwe moja (ziunganishwe) mvuvi ni sawa na mwindaji, hatakiwi kuwa na leseni tofauti. Kwa nini? Kwa vile uwindaji wa nyati, uwindaji wa swala, leseni ya uwindaji wa pale pale na kadhalika. Serikali haina budi kuliweka sawa suala hili la leseni kwa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti nitasimama kwenye vifungu pindi hautatolewa ufafanuzi.

**MHE: MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii mpya kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa kipindi kifupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wetu walio wengi bado ni maskini wa kutupwa pamoja na kwamba wana mifugo mingi kwa idadi, umaskini huu unatokana na kutokuwa na elimu au mwanga wa kuwaonyesha vipi wangeweza kufaidika na ufugaji wao. Kuna makabila ambayo hufuga ng’ombe wengi kwa malengo ya ushindani wa nani ana ng’ombe wengi bila kuangalia wanawanufaisha vipi ng’ombe hao. Nyumba zao ni duni na hata maisha yao hayalingani kabisa na mali walizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya kuendelea tena kwa kasi kuwapa elimu wafugaji wetu ili waweze kufaidika na mifugo hiyo. Utozaji wa ada ya mifugo kwa kila mfugaji sio suluhu ya kumfanya mfugaji apunguze mifugo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la malambo na majosho kwenye maeneo mengi ya wafugaji ukizingatia kuwa mifugo mingi inastawi kwenye maeneo kame na matokeo yake mifugo mingi hufa kutokana na ukame/ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kuwa, Wizara ya miundombinu kwa kushirikiana na Wizara hii iweke utaratibu kwenye mikataba ya miradi ya ujenzi wa barabara kwenye maeneo husika, kuyafanya maeneo ya machimbo ya changarawe kuwa malambo mara kazi ya ujenzi wa barabara unapokamilika badala ya kufukiwa kama ilivyo utaratibu wa sasa. Hii itawezesha wafugaji wengi kupata malambo ambayo yatakidhi mahitaji ya mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, majosho bado hayatoshi, ni vyema Wizara ikaongeza ujenzi wa majosho ya mifugo ili kupunguza maradhi ya mifugo. Baadhi ya majosho machache yaliyopo yamekuwa hayafanyiwi matengenezo na matokeo yake yamegeuka kuwa nyumba za mijusi. Ni vyema Serikali ikayafufua majosho haya ili yatumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio kikubwa kwa wafugaji ni bei na upatikanaji wa madawa ya chanjo ya mifugo yao, bei ya juu sana wanashindwa kumudu. Ni vyema Serikali ikatoa ruzuku kama ilivyofanya kwa madawa ya wakulima ili wafugaji wamudu dawa hizo na hivyo kupunguza mfumuko wa magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matukio mengi ya uvuvi haramu kwa wavuvi wanaotaka utajiri wa mkupuo, pamoja na juhudi inazozichukua Serikali ya kupambana na uvuvi haramu huo, bado kuna tatizo kwa Maafisa Uvuvi kukosa nyenzo/vifaa vya ufuatilaji kwenye maeneo husika. Serikali iwapatie Maafisa hao vitendea kazi zikiwemo boti na silaha za kufanyia doria kwenye maeneo hasa ya maziwa na bahari ili waweze kuwabaini na kuwakamata wahalifu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Wizara ijikite zaidi kuelekeza kwenye uvuvi wa bahari kuu *(deep sea)* ili kukuza pato la Taifa. Uvuvi huo kwa sasa unanufaisha wavuvi haramu kutoka nchi za nje ambazo huvua kwa meli maalumu za kuvulia bila ya Serikali kubaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukisikia kuwa Serikali ina rada ya kuweza kuona meli zikiwemo zile za uvuvi haramu ndani ya mipaka yetu baharini. Nini ukweli huu? Je, ni mali ngapi za uvuvi haramu zilikamatwa kwa kipindi cha mwaka 2007/2008?

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya samaki ni kubwa sana kwa walaji katika nchi yetu pamoja na kwamba tumezungukwa na bahari, maziwa na mito tunayo kwa wingi. Serikali itoe hamasa kwa wavuvi wetu ikiwa pamoja na kuwapa mikopo kwa ajili ya kununulia vifaa vya uvuvi pamoja na boti za kisasa ili kuongeza idadi ya samaki watakaovuliwa na hivyo bei zitapungua na wananchi watapa vitoweo na afya njema ukiachilia kuongezeka kwa pato la nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE: JACOB DALAI SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kutenga muda wa kutosha tutoe maoni yetu. Nianze kwa kumpongeza Wazri, Naibu

Waziri na Katibu Mkuu kwa ushirikiano wao katika kazi za Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta hii ni muhimu sana, hivyo tunaishauri Serikali itoe kipaumbele katika bajeti ijayo ili mkulima afaidi mazao ya mifugo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuanza kuiona Sekta ya mifugo kuwa inaweza kuchangia zaidi katika pato la Taifa kuhakikisha ruzuku ya madawa ya mifugo inaongezwa na utaratibu mzima wa kuwafikishia walengwa madawa hayo au bidhaa hiyo ili lengo lifikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Serikali kwa ujumla wake hasa baada ya kuona umuhimu wa kukamilisha mnada wa upili mnada wa nyamataka (misungwi) sisi wananchi wa Misungwi tunaahidi ushirikiano ili wafugaji waweze kuuza mavuno ya mifugo yao baada ya kunenepesha na baadaye wajiletee maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri katika ziara zao watembelee Misungwi na kujionea ujenzi wa majosho na malambo. Hii itasaidia kupunguza maswali Bungeni na kubaki ushauri tu kwa wadau. Picha imeonyesha juhudi tulizofanya za kuwashirikisha wadau vijijini na kuibua miradi inayowahusu tunaomba tuungwe mkono sehemu ambayo inahitaji msaada wa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Misungwi imeguswa na Ziwa Victoria na bahati nzuri eneo lote hilo ni mazalia ya samaki hivyo uvuvi ni wa muda mrefu sana na hata miradi inapopatikana, Wilaya yetu husahaulika. Hivyo, Serikali tunaiomba sana miradi inayopatikana na hasa uboreshaji wa mazalia ya samaki, ni vyema Wilaya ipewe miradi hii itawafanya wananchi walinde maliasili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vitendo vilivyofanyika wakati wa *operation* ya wafugaji huko Ihefu kuna uonevu mkubwa sana Serikali itoe ripoti ya Tume ili tubaini ni kwa nini uongozi wa Serikali uliwatendea hivyo na kuwafanya kuwa masikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi tena kumtakia kila la heri Waziri kwa kazi nzuri waliyonayo juu ya ufufuaji wa kampuni ya ranchi za tarifa. Naomba uendelee na moyo huo. Naunga mkono hoja.

**MHE: EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa John P. Magufuli, Naibu wake Mheshimiwa Wanyancha, Katibu Mkuu na watumshi wengine wa Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya bajeti hii. Kipekee sana, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Magufuli kwa kuwasilisha bajeti hii kwa ufasaha na umahiri mkubwa. Katika kuunga mkono bajeti hii, napendekeza mambo yafuatayo yapewe kipaumbele:-

(1) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni tatizo la malisho. Katika kuboresha ufugaji, naishauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Ardhi, Wizara ya Kilimo pamoja na TAMISEMI kutambua kuwa ufugaji ni shughuli inayotambulika na hivyo ardhi maalum itengwe kwa ajili hiyo kila kijiji. Kwa sasa na kuhamasisha ufugaji, hakuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji. Sehemu zote ambazo wafugaji wapo, wamekuwa wakifukuzwa na wenzao wakulima. Katika Wilaya ya Kahama kwa mfano, maeneo mengi yaliyokuwepo kwa ajili malisho hivi sasa yamechukuliwa na wahamiaji wakulima kutoka wilaya jirani. Hali hii imesababisha wafugaji kuhama kutafuta maeneo mengine yenye malisho. Watanzania waliotimuliwa Ihefu, wengi wao ni kutoka Mkoa wa Shinyanga. Naomba sana jambo hili lifanyike kwa dharura na haraka kwani sasa limeanza kutishia usalama. Kwenye Jimbo la Msalala naomba meneo ya wafugaji Kata ya Bulige, Ngaya, Chela na kadhalika yalindwe.

(2) Katika kuboresha ufugaji, tunaiomba Wizara isaidie kuboresha miundombinu na huduma kwenye maeneo ya wafugaji. Wafugaji wapatiwe malambo, majosho na pembejeo (madawa ya mifugo) kwenye maeneo yao. Ninaomba Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI (hasa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama) iboreshe majosho yaliyokuwepo toka zamani, majosho ya Chela, Ngaya, Busangi na sehemu nyingine ambazo kuna wafugaji.

(3) Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isaidie kuanzisha mpango wa kuhamilisha (kuipandisha ng’ombe kwa chupa) ng’ombe. Ni kwa njia hii pekee ndipo mazao ya mifugo yataongezeka na hivyo hoja ya kupunguza mifugo kwa wafugaji itaeleweka. Tunaomba vianzishwe vituo vya mafunzo ya kuhamilisha ng’ombe walau maeneo matatu ya Kahama, Isaka Bulige na Lunguya.

(4) Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Wizara pia isaidie kuhama tupate machinjio ya kisasa. Soko la nyama lipo kubwa, kuna migodi, kilimo na wasafiri na biashara za nchi jirani.

(5) Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isaidie upatikanaji wa mikopo kwa wafugaji wadogo wadogo wa kuku. Kahama kuna soko kubwa sana la kuku migodini. Kwa kuwa tayari kuna wafugaji wadogo wadogo wa kuku sehemu za Bugarama, Kakola, Buyange na hata Segese, naiomba Wizara isaidie upatikanaji wa mikopo. Watu hawa wanahangaika na kusaidiwa na *NGOs* na mgodi wa Bulanhulu bila msaada wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, naomba kusisitiza Wizara itoe majibu kwa hoja zangu zote. Kwa kuwa siwezi kuchangia wala kusimamia kwenye vifungu, naiomba Wizara inijibu angalau kwa maandishi (sio lazima leo, lakini) nipate majibu nitakayoenda (ambayo, kwa msingi wa *collective responsibility*, nitawajibika kwenda) kuwaeleza/kuwajibu wananchi wangu, ambao ndio hasa wanaoyahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Asante.

**MHE: JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi kwa kutujalia uzima na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongezaa wewe, Naibu Spika, Wenyeviti, Viongozi wa Upinzani kwa kutuongoza vizuri. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kutokana na bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya mifugo ni muhimu sana kwa wananchi wenye kipato cha chini, cha kawaida, pamoja na kipato kikubwa. Pia Sekta hii inasaidia kuongeza pato kwa wafugaji, pato la Taifa na kukuza uchumi wa nchi na hivyo kusaidia kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wapatiwe maeneo ya ufugaji yakiwa na uhakika wa upatikanaji wa maji kwa kuwajengea malambo na mabwawa. Pia wapatiwe maeneo yenye uhakika wa malisho ya mifugo yao pamoja na majosho na madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhamishwa kwa wafugaji kutoka Ihefu na maeneo mengine kwenda sehemu mbalimbali kulisababisha migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Je, sasa hali ikoje? Je, kuna mafanikio kiasi gani katika suluhisho la migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania tuna mifugo mingi wakiwemo ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, bata n.k. Usindikaji wa mazao yataokanayo na mifugo muhimu sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali itilie mkazo suala la viwanda kwa ajili ya usindikaji wa mazao ya mifugo. Hii itasaidia kuongeza kipato kwa wafugaji pamoja na uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika nchi yetu kuna samaki wengi katika bahari na maziwa viwanda vya kuzindika samaki ni muhimu kujengwa. Hivi vitasaidia kuongeza ajira kwa vijana na wananchi mbalimbali na hivyo kuongeza pato kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu itolewe kwa wavuvi kuhusu uvuvi bora usioharibu mazingira pamoja na mazalio ya samaki na viumbe vingine vya bahari. Pia, elimu itolewe kwa kubadilishana mawazo baina ya wavuvi na Wizara ni kwa namna gani vyombo vilivyopigwa marufuku vinaweza kuharibu mazingira au kinyume chake. Hii itasaidia kuondoa mfarakano baina ya Wizara na wavuvi hasa ikizingatiwa kwamba maisha ya wavuvi yanategemea uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa wa Bonde la Ufa ulipoteza mifugo mingi na hivyo kupunguza kipato kwa wafugaji pamoja na pato la Taifa. Je, kuna ukuaji kiasi gani katika Sekta ya mifugo tangu kumalizika kwa ugonjwa wa Bonde la Ufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu itolewe kwa wenye mifugo mingi ili wawe wafugaji badala ya wachungaji. Hii itasaidia kuboresha maisha yao pamoja na kipato chao.

**MHE: FUYA GODWIN KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Hai, ninawapongeza sana nikianza na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wengine wote hapo Wizarani kwa Utendaji wenu ikiwa ni pamoja na kutuletea hotuba yenye takwimu. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza mambo machache yafuatayo ambayo ni pamoja na mengine, ninatumaini yatatusaidia katika Sekta yetu ya mifugo.

(i) Ubora wa mifugo. Ninashauri tuongeze juhudi za kusambaza mbegu za wanyama i.e *artificialinsermination* ili tuweze kuongeza idadi ya mifugo yetu kwa maana ya kupata nyama kwa wingi pamoja na maziwa.

(ii) Ninapendekeza kwenye minada yetu tuwawekee mizani ili tuachane na huu utaratibu wa kuuza mifugo yetu kwa kutizama kwa macho kwani wakulima wetu wanapunjwa sana.

(iii) Tuongeze idadi ya viwanda vya meat processing na vya maziwa, kwa mfano pale wilayani Hai tunahitaji sana kiwanda cha maziwa kwa kuwa tuna maziwa mengi sana.

(iv) Ninapendekeza tuwe na mfuko wa ufugaji kama tulivyo na mfuko wa uvuvi.

(v) Tunaomba ruzuku kwenye madawa ya mifugo pamoja na virutubisho vingine.

(vi) Ili kuondoa hizi kelele nyingi sana kutoka kwa wenzetu ambao sio wafugaji ninapendekeza tujenge majosho na mabwawa ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE: JUMA H. KILIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa John Pombe Magufuli - Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha - Naibu Waziri wa Mifugo na uvuvi. Pia nawapongeza Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya maandalizi ya bajeti hii ya 2008/2009.

Pamoja na pongezi hizi, nachukua fursa hii kutoa maoni ya ushauri kwa maeneo kadhaa ili kuboresha bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2008/2009. Ufugaji wa kisasa bado sijaona juhudi za Wizara katika kumbadilisha mfugaji kutoka ufugaji wa kienyeji na kuwa na ufugaji wa kisasa, kwa maana kuwa na mazao mifugo yenye tija na maslahi kwa mfugaji, bidhaa mifugo kama ng’ombe, mbuzi, kondoo kuku na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi bado wanafuga kwa mbinu za kizamani, bado wafugaji wanayo mifugo aina hiyo ile ya kienyeji ambayo mara nyingi hutegemea malisho huria yale yasiyoidhinishwa, Madawa ya mifugo ya kukabiliana na

matatizo mbalimbali ya magonjwa hayapo na hivyo kusababisha vifo vingi mara magonjwa yanapojitokeza. Hii ni pamoja na uhaba wa majosho, malambo kwa ajili ya maji ya mifugo bado haba na hivyo kutekeleza mifugo hasa ng'ombe, mbuzi na kondoo kwenda umbali mrefu kusaka maji na malisho, ng'ombe wa kisasa kuwa na mitamba kwa maeneo mbalimbali ya wafugaji ili kueneza mbegu na kuwa ng'ombe wa kisasa kwa kuwa na kilo za kutosha za nyama, maziwa mengi na mengineyo. Mengi ambayo yote yana faida kubwa kwa mfugaji ambaye ni mkulima pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo kubwa la Maafisa Ugani tunahitaji Maafisa Ugani wa kutosha kwa dhamira ya kutoa elimu kwa wafugaji na kuwa na ufugaji endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo kama kuku hasa wa kienyeji ambao upatikanaji wake ni kwa wingi Mkoani Singida, kuku hawa ni watamu sana hasa kwa nyama (mboga). Elimu itolewe kwa wafugaji wa kuku (kwa maana katika mazingira ya vijijini kila kaya lazima iwe na kuku) kwa maeneo hiyo wananchi wahimizwe kufuga kuku na madawa yapatikane hasa yale ya chanjo kwa magonjwa kama kideli na mdondo. Wananchi wa kada ya chini wakifuga kuku wa kutosha kimsingi watakuwa wanapiga vita umaskini kwa maana bei ya kuku mmoja wa kienyeji ni Sh. 7,000/= mpaka Sh. 10,000/= hivyo mwananchi wa kawaida akiwana na kuku 100 mpaka 200 anao uhakika wa kuwa na Sh. 700,000/= hadi Sh. 1,400,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvuvi, Jimbo la Iramba Magharibi tunaloziwa Kitangiri, ziwa hili ni hodari kwa samaki aina ya perege, kamongo na kambale katika hali ya kawaida mavuno ya samaki kwa ziwa Kitangiri ni ya mfululizo mwaka mzima. Samaki wengi wanaovuliwa Kitangili husambazwa kwa soko la Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kusema mvuvi wa Kitangiri ambaye ni mwananchi wa chini, mazingira wanayofanyia kazi yanasikitisha sana, zana za uvuvi ni duni sana kutokana na hali ya ziwa lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi hawana mitaji ya kutosha, pamoja na kuanzisha *SACCOS* ya wavuvi sehemu za Shauritanga bado wavuvi hawa hawathaminiwi na hata wakiomba mikopo hawapewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itoe boti la doria ili kuwalinda wavuvi kwani wavuvi haramu wale wanaotumia makokolo na baruti kuvulia. Maeneo ya Usiulize mpakani mwa Meatu, yatazamwe kwa upana hasa kiulinzi kwa kuwa wavuvi haramu wengi hutokea huko. Pia Wizara itoe Afisa Uvuvi mwenye taaluma ambayo atakuwa Afisa Uvuvi wa Wilaya ili ashirikiane na wavuvi wa Kitangiri kwa masuala mbalimbali ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Wilaya ya Iramba inayo mifugo mingi kama nilivyoitaja naomba Wizara itoe vifaa, kama gari na pikipiki kuimarisha shughuli za ufugaji Wilayani. Kituo cha Maksai Mkulu, Jimbo la Iramba Magharibi kwa nini kituo hicho hakifanyi kazi hadi sasa tatizo lake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa wizara na mashirika yote yaliyoko chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kutoa pole za dhati kwa wananchi wa Kata ya Mazinga, Jimbo la Muleba Kusini kufuatia janga la moto lilitokea wakati bunge hili linaendelea na mkutano wa bajeti. Watu wamekufa na nyumba nyingi kuteketea na mali za wananchi wa kata hiyo ya Mazinga. Naomba Wizara hii iangalie namna ya kuwasaidia wavuvi hawa ambao sasa wamerejeshwa kwenye lindi la umaskini kutokana na ajali ya moto. Wavuvi wote katika Jimbo langu la Muleba Kusini wanahitaji na wanastahili kuwezeshwa na Serikali ili uvuvi wao uwe endelevu kwa kuhifadhi mazingira ya *Ziwa Victoria* na Ziwa Burigi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali isimamie kikamilifu uvunaji wa samaki katika maziwa na bahari. Utajiri huu raslimali hii yenye thamani kubwa katika soko la dunia, kuachia watu wa nje wanaotumia migongo ya watu maskini wa ndani sio jambo jema. Watoto wetu na wajukuu wao watatulaumu. Serikali ijenge viwanda vya kusindika samaki, iwezeshe wavuvi wetu kuvua na kuwapa soko la uhakika. Hatimaye hisa za viwanda hivyo wauziwe wananchi kama tulivyofanya kwenye viwanda vya sementi na mabenki. Hii ndio njia sahihi ya kumilikisha wananchi wengi uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa mkakati madhubuti wa kuendeleza mifugo na kuivuna kwa njia za kisasa, ikiwemo kuanzisha viwanda vya nyama. Utajiri wa mifugo ukitumiwa vizuri ni mkombozi kwa Taifa letu.

Serikali inayo nafasi kubwa katika hili, kwa sababu mifugo mingi inamilikiwa na maskini. Tukiachia sekta binafsi kwa wakati huu, itakuwa ni kusaliti wananchi wetu ambao bado wanahitaji elimu kumudu mazingira na maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naishauri Serikali ichukue tahadhari ya kutosha katika kugawa ardhi kwa ajili ya ufugaji wa kisasa. Wajanja wachache kwa majina tofauti, inadaiwa wanamilikishwa ardhi kubwa sana. Tunawatengenezea watoto wetu na wao bomu la hatari kwa kugawa au kuachia ardhi yetu ovyo ovyo. Urithi wa thamani kwa watoto wetu ni elimu na ardhi. Ubinafsishaji usiozingatia ukweli huu ni potofu. Nashauri kwa dhati Serikali isijivue wajibu wake wa kulinda na kuhifadhi raslimali za Taifa letu kwa maslahi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni nyongeza kwa mchango wangu wa maandishi uliotangulia. Baada ya kusikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge wafugaji na wavuvi, kwa heshima namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu amshauri Mheshimiwa Rais, atenganishe Wizara hii, mifugo iwe Wizara peke yake na Uvuvi iwe ni Wizara peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga Mkono hoja tena, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi ya kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mingi sekta ya mifugo imekuwa inahudumiwa kama sekta ndogo na hivyo kutotengewa fedha ya kutosha kuboresha/kuendeleza sekta hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi sana wanatumia mifugo kuendesha maisha yao ya kila siku. Cha kusikitisha Serikali haijatambua hilo na hivyo kuipa sekta hii uwezo wa kutosha kwa mantiki ya kuondoa umaskini kwa wafugaji hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kutueleza hapa kuwa tuna ng'ombe milioni 18.8, Mbuzi milioni 13.5, kandoo milioni 3.3, nguruwe milioni 1.4, kuku milioni 50 hapa Bungeni imetupa picha halisi kuwa tuna mifugo mingi sana lakini ni kwa nini bado hatujaweza kutumia mifugo hiyo kuinua kipato cha Mtanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wengi wamekuwa wakihangaika huku na kule kutafuta malisho na mara nyingi hili limesababisha migongano ya matumizi ya ardhi. Hili limesababishwa na Serikali kutotenga maeneo maalum ya wafugaji na ya kutosha kwa ajili ya kuendeleza mifugo. Nashauri sasa Serikali iainishe maeneo yote muhimu kwa ufugaji na kuyatenga kwa ajili ya wafugaji. Mpango wa matumizi ya ardhi ufanyike na wapatiwe hatimilki za maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo na migogoro mingi inayotokea kila leo Wilaya ya Urambo Mkoa wa Tabora. Wafugaji wamekuwa wanakamatwa mara kwa mara kwa kupigwa faini eti wamechungia kwenye eneo la hifadhi. Kuna mapori ya *Ugalla Game Reserve*, Mpanga Kapengele na *Myonzi Game Reserve.* Mipaka ya hifadhi hii haieleweki hivyo askari wanakaa mbali na kuwategea wafugaji. Mifugo ikiingia tu wanawakamata na kuanza kuwapiga faini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wizi wa wazi unaofanywa kwa wafugaji wanaozunguka mapori haya na kwa habari nilizopata hata viongozi/watendaji wa Serikali wanahusika. Askari wa mgambo wanaotumwa na viongozi wa Wilaya kwenda kutoa faini kwa mifugo inayoingia kwenye hifadhi wanafanya biashara ya ajabu. Kwanza wanakwenda na wanunuzi wa ng'ombe huko porini, wakishakamata mifugo wanamlazimisha mwenye mifugo auze baadhi ya mifugo pale pale kwa bei kati ya shilingi 50,000/= hadi shilingi 30,000/= kwa ng'ombe mkubwa ili wapate faini yao. Mfugaji analazimika kufanya hivyo na akikataa anapata kipigo hadi anasaliti amri. Ng'ombe wa shilingi 200,000/= hadi shilingi 300,000/= anauzwa shilingi 50,000/=, huu ni wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa Watanzania kwa sehemu kubwa ni wa kienyeji. Wengi wanaangalia wingi wa mifugo na siyo ubora wa mifugo. Ni juhudi gani za Wizara kuhakikisha wanabadili mifumo tuliyonayo na kwenda kwenye ufugaji wa kisasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa na mifugo hiyo bado hakuna mipango madhubuti ya kupata masoko mazuri kwa mazao ya mifugo. Kwa sasa tunazalisha maziwa kwa wingi lakini mengi yanaharibika kwa sababu hayasindikwi na kuweza kuuzwa kwa muda mrefu hata nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali kuwekeza kwenye sekta hii ya mifugo kikamilifu ili iweze kusaidia kuinua uchumi wa Watanzania walio wengi wanaotegemea kufuga na maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ile ile ambapo Serikali imeanua kutenga Kanda mbalimbali kwa ajili ya kilimo cha mazao mbalimbali na kuwapa pembejeo. Basi Serikali sasa iainishe maeneo ya wafugaji na kuwapatia huduma zote muhimu ikiwepo, masoko, dawa, wataalam, majosho na malisho mengine yote muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji viwanda vya kusindika maziwa, nyama na mazao mengine ya mifugo. Wakati Waziri ana *wind up* naomba atufafanulie miaka ya nyuma tulikuwa na kiwanda cha kusindika nyama na maziwa *Tanganyika Packers,* Kawe, Dar es Salaam. Kiwanda hiki kilisaidia sana kutoa soko kwa mazao ya mifugo. Leo kile kiwanda hakifanyi kazi na pale pamejengwa ukuta kwa miaka mingi hakuna chochote kinachofanyika pale. Ni kwa nini Serikali isifufue kiwanda hiki ili kifanye kazi ya kusindika nyama na maziwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kufufua kiwanda hiki nashauri viwanda vingine vijengwe kwenye mikoa ya wafugaji. Suala la kuacha ujenzi wa viwanda kwa watu binafsi na kusubiri wawekezaji halisaidii sana Watanzania wafugaji. Maeneo haya muhimu yanatakiwa kupewa uangalizi mkubwa na Serikali yenyewe ili kuendeleza sekta hii ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia iandae utaratibu wa kuwaelimisha wananchi matumizi ya maziwa. Watanzania wanaokunywa maziwa ni wachache sana wengine hawatumii kabisa na hawajui wanakosa nini kwa kutokunywa maziwa. Hii ndiyo maana watoto wanapata utapiamlo na *Marasmus* wakati wanaishi maeneo ambayo kuna maziwa ya ng’ombe, mbuzi na mayai ya kuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya kutosha itolewe, kwani hili litaongeza soko. Ahsante sana.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI**: Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi na Mtwara baada ya *operation* ya uvuvi haramu, tuliahidiwa kupatiwa boti ya doria ili wale wavuvi haramu wasirudie tena, lakini hadi leo bado kupatiwa. Tunaomba boti ya doria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wavuvi walionyang'anywa nyavu na pia kuacha kabisa uvuvi haramu, waliahidiwa kusaidiwa zana halali mbadala za uvuvi, lakini, hadi leo vile vikundi vimeundwa havijasaidiwa. Tuliotegemea kutusaidia *MACEMP* hawajatusaidia wanachukua muda mrefu sasa, hawajaanza *MACEMP*, tunaowaona ni *WWF* ambao wapo Kilwa tu. Tunaomba sana wavuvi wa Lindi, Kilwa, Mtwara, Sudi, Mikindani wasaidiwe. Wavuvu wale wote wa mwambao wa Lindi na Mtwara wasaidiwe.

**MHE. HEMED MOHAMOUD HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu alieniwezesha kuishika kalamu hali nikiwa mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake iliyo na nia ya kukuza uchumi wa nchi yetu kupitia Wizara yake na kumgombea Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa naomba nielekee kutoa mchango wangu katika Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo muhimu la kuweza kukuza uchumi wa nchi yetu ni eneo hili. Pili ni eneo la ajira binafsi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumejitokeza vitendo haramu kutumia mabomu. Uvuvi huu unateketeza samaki pia mazalia yao. Uharamia huu unaongezeka siku hadi siku kutokana na Serikali kutokujipanga kuilinda bahari yetu. Pia kuna baadhi ya wavuvi kutoka nje ya nchi yetu kuingia na meli zao kuvua samaki katika bahari yetu bila ya malipo. Kitendo hiki kinafanywa kila leo na kulikosesha Taifa letu mapato. Hivyo kweli Serikali inailinda bahari yetu? Pia kuna Maziwa mengi ndani ya nchi yetu ambayo yanazalisha samaki wengi, lakini hali ni hiyo hiyo wanaofaidika ni wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mifugo, ieleweke kuna mgogoro mkubwa kati ya mkulima na mfugaji. Watu hawa kama Serikali haikuwa macho kunaweza kuzaa balaa kwa Watanzania wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasoro zilizopo juu ya mifugo yetu ni kukosekana kwa elimu, pia kuwa waongo katika kutenda. Serikali katika Bajeti yake inasema imetenga maeneo mahususi kwa kilimo na ufugaji, hii sio kweli. Mifugo inahitaji mambo muhimu kama vile, majani, maji, majosho, masoko pia madaktari wa wanyama. Je, Serikali imefanikisha yote hayo huko vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumzunguze ng'ombe kwa ufupi ng'ombe mwili wake hakuna kisicho na faida. Lakini hakuna umuhimu wa mifugo yetu ya ng'ombe. Wafugaji hatuwajali. Wanyama walipopata ugonjwa wa homa ya bonde la ufa, uliathiri uzalishaji wa nyama ya ng'ombe, mbuzi, nguruwe, kondoo na kuku. Kuathirika kwa mifugo yetu, imebaki ni historia tu na sio maandalizi ya wakati mwingine yakitokea kama hili

lililotokea je, Serikali imefanikisha lipi huko vijijini kuhakikisha mifugo yetu iko salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masoko juu ya wafugaji wetu bado yako duni. Ni vyema Serikali iwasaidie wafugaji kuwapatia masoko ya uhakika ili nao waweze kujua umuhimu wa kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, inafahamika umuhimu wa Maziwa kwa mwanadamu, yapaswa Serikali ihakikishe kuwapatia wafugaji ng'ombe bora walio na uwezo wa kutoa Maziwa mengi pia na nyama bora. Tukiweza kufanikisha hili kutasaidia mfugaji kuachana na kuwa na mifugo mingi, kutatuwezesha sisi sote kupata maziwa na nyama ili tuwe miongoni mwa watu wanaopata chakula bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa nisema nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kumpa mategemeo makubwa mfugaji. Nasema ahsante.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuunga mkono hoja hii iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja katika utekelezaji wa Bajeti yake, hii inatokana na hali halisi ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii kwa sasa ina jukumu kubwa la kuinua sekta ya uvuvi na mifugo hapa nchini. Ni vizuri Wizara ikajikita zaidi na sekta hizo katika kuinua mapato ya wavuvi na wakulima na hatimaye uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru sana Serikali kupitia miradi yake ya *MACEMP* na *RUMAKI*. Miradi hii ina lengo la kutoa elimu na hatimaye kuwapatia wana vikundi vifaa vya kufanyia kazi kama *grant.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mradi wa *RUMAKI,* kwa kweli umeweza kuwaandaa wananchi kuweza kujitegemea kwa kuanzisha vikundi vidogo vidogo vya kuweka akiba *(VICOBA).* Katika vikundi hivyo hadi sasa baadhi ya vikundi vina akiba ya zaidi ya shilingi 10,000,000/= kinachosikitisha ni kuwa vikundi hivyo kwa sasa vinaanza kufa kutokana na kutokuwa na fursa ya kukopa. Tatizo hili tayari nililifikisha katika Wizara ili waone namna ya kuviboresha toka *VICOBA* hadi *SACCOS.* Mpaka sasa majibu hayajapatikana!

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni mradi wa *MACEMP.* Mradi huu ulianzia katika wilaya za Rufiji, Mafia, Kilwa kama *pilot study.* Naishukuru Serikali kwa kuweza kuvipatia vikundi *grant* ya fedha za kununua vifaa mbalimbali ya uvuvi na ujasiriamali. Jumla ya shilingi 320,000,000/= zimetumika kwa shughuli hiyo katika kukamilisha zoezi hilo fedha zilizotolewa ni kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya vikundi hivyo. Maombi ya fedha za kukamilisha miradi hii, tayari imepelekwa makao makuu ya *MACEMP* Dar es Salaam. Lakini tangu yalipopelekwa hadi sasa hakuna

majibu yoyote. Naiomba Serikali itoe maelezo ni lini fedha hizo zitatolewa ili vikundi hivyo vianze kazi ya uzalishaji mali.

Jambo lingine ni kuhusiana na vijiji vilivyo ndani ya mradi wa *MACEMP*, kutokuwa na mradi hata mmoja. Baadhi ya vijiji hivyo ni Kiongoromi, Mbuchi, Mbwera, Kiomboni, Mchinga na vingine ambavyo sijavitaja. Naiomba *MACEMP* iende katika vijiji hivyo ili nao waweze kufaidika na mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie ahadi za *MACEMP* ya kujenga *Community Centre* pamoja na *Fish Landing Site* pale Nyamisati hadi sasa hakuna na wala hatujui ujenzi huu utaanza lini, namwomba Waziri aeleze sababu zilizocheleweshsa ujenzi wa majengo hayo. Pamoja na hayo Waziri pia aeleze ni lini atapeleka gari Wilaya ya Rufiji kama *MACEMP* ilivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine iliyojitokeza ni kuhusu aina ya nyavu zinazotakiwa kutumika katika uvuvi. Hivi sasa kuna tatizo kubwa la askari waliotumwa na Wizara wameenda Rufiji na kuwalazimisha wavuvi kutovulia nyavu za robo tatu inchi. Namuomba Waziri aelewe kuwa nyavu hizi zinatumika kwa kuvulia kamba *(prawns)* na si vinginevyo. Nyavu hizi hutumika katika maeneo ya mitoni *(delta)* kamwe kamba hawavuliwi kwa nyavu za inchi tatu. Naiomba Serikali iweze kueleza wazi ni kwa nini wananchi hao hawasikilizwi kilio chao wakati wanaeleza taratibu na aina ya nyavu zinazotumika katika uvuvi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu wa *MACEMP* una kasoro moja kubwa ya kuwa fedha zote zimekuwa *centralized* pale makao makuu ya Wizara, hili ni tatizo. Naishauri *MACEMP* kwa kuwa kuna ofisi chini ya wakurugenzi watendaji wa halmashauri ya wilaya na vizuri mara baada ya mchakato wa Bbajeti katika halmashauri kumalizika na *MACEMP* wakubali basi fedha hizo zitumwe wilayani ili zianze kutumika katika vikundi au miradi iliyokusudiwa. Naomba tuaminiane kwani watumishi hao ni wa Serikali na wanafuata tararibu zote za matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wao wote wa Wizara hii kwa hotuba yao nzuri ya Bajeti iliyopangika na yenye mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kwa upande wa ufugaji bado kunahitajika kutolewe elimu ya kutosha kwa wafugaji wenyewe, kwani utakuta mtu ana ng’ombe zaidi ya 100 anakua hana shughuli yoyote, kazi yake kuangalia ng’ombe tu hawakogi, wala hawajui kuvaa, wala hawajui watoto nyumbani wanakula nini wao wapo kwenye ng’ombe tu, huyo akipatiwa elimu ya namna ya kuwatunza hao ng’ombe, ili waweze kuwapunguza kwa kuwauza, ili wapate fedha za kuwasaidia kwa mahitaji maalum, kama kujenga nyumba bora, kuwasomesha watoto na kadhalika na kujiwekea fedha benki, kuliko kuwa na ng’ombe wengi wengine wabovu, wagonjwa, wameshazeeka, kwa hiyo, wakipatiwa elimu, natumaini wao watafaidika na nchi pia itapata faida, pato la uchumi

litaongezeka ikiwezekana wapelekwe wataalamu makusudi ili kuwakagua ng'ombe, pia kwa hali hii ardhi ya wafugaji itakua haina shida na kazi ya kuhama hama itapungua, pia kuweko na majosho ya kutosha, madawa na kadhalika.

Kwa upande wa uvuvi, uvuvi nao ni tegemeo kubwa la kipato kwa wananchi pia na Taifa, hivyo wangeelimishwa wavuvi wadogo wadogo, ili waunde vikundi na Serikali iwawezeshe kuwapatia vifaa vya uvuvi vya kisasa vikiwemo boti, *engine* na kadhalika.

Japo kwa njia ya mikopo, kwa njia hii itawasaidia kuinua kipato chao kwa kiuchumi na kimaisha badala ya kuwazuia wasivue kwa hivyo vifaa visivyotakiwa kwa kuharibu mazingira vile vile nchi za uvuvi zinazokuja kuvua kutoka nje au za kigeni zinaua kweli uchumi wetu wa nchi, kwani Serikali inakua hata haijui wala haina habari na wananchi wanalalamika hawajui wamwambie nani wala waripoti wapi na hasa sehemu za mwambao wa bahari zetu, pia kwenye Maziwa na Mito Serikali iweke mikakati na ichukue hatua kwa jambo hili kwani kuna faida kubwa sana kutokana na mito yetu, Maziwa na bahari kwa shughuli za uvuvi na sijui Serikali inalitizamaje suala hili baadhi ya mazao mengine yanayopatikana kutoka baharini kama vile majongooo, mwani, kombe na vinginevyo, kwani navyo vinasaidia uchumi wa nchi, naomba Waziri anijibu, kwenye majumuisho yake suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika,mwisho naitakia Wizara utekelezaji mwema wa kazi zake.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yangu binafsi na wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini, tunaipongeza Wizara hii kwa ujumla pamoja na watendaji wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri ya Bajeti ambayo ameiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima ninaomba kuchangia maeneo machache ya Wizara hii.

Kwanza ni kuhusu uvuvi. Sekta ya uvuvi ndio moja ya mgodi mkuu ambao utaweza kutuwekea uchumi mkubwa katika Taifa hili. Tanzania ina bahati kubwa miongoni mwa dunia yetu. Tanzania ina eneo kubwa la Bahari ya Hindi, aidha ina eneo kubwa katika nchi za maziwa. Naishauri Serikali tuwekeze kwa nguvu kubwa kwenye uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uvuvi wa bahari kuu *(Deep Sea)* lazima tupate meli za uvuvi *(Fishers Ships)* ambazo zina uwezo mkubwa wa uvuvi wa bahari kuu ambapo tutapata au kuvuna samaki wakubwa na wengi. Aidha, ziwe na uwezo wa kuwatunza kwenye vyumba vya baridi. Kwa uvuvi wa mwambao mwa bahari na maziwa yetu, lazima tuwekeze kwa wavuvi wa mwambao kwa kuwapatia vyombo vidogo na vya wastani ili waweze kufuatilia maeneo yenye samaki wengi aidha, wavuvi wetu wapatiwe zana za uvuvi wa kisasa. Zaidi ya hayo wapatiwe elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mifugo yetu, Tanzania ina ng'ombe wengi, mbuzi, kondoo na kadhalika, lakini bado tuna tatizo kubwa la kuhangaika na mifugo yetu hasa kwenye malisho ya ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati sasa tuwe na ufugaji wa kisasa na wa kitaalam sana, paandaliwe mahala maalum kwa mifugo yetu hasa kwa malisho, malambo, majosho na madawa ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuwe na ufugaji wa kitaalam kabisa tuondokane na ufugaji huu wa kiduni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuwe na soko au minada, magulio mazuri kwa uuzaji wa mifugo yetu kwa uzuri au uendane na masoko ya ufugaji wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja kubwa ya kuimarisha machinjio ya wanyama wetu, lazima yawe ya kisasa yaendane na machinjio ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu ambao ni mchache sana, sasa kwa heshima kubwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara isaidiane na wafugaji kutenga maeneo ya mifugo ili kukwepa migogoro na matumizi mengine ya ardhi. Pia msisitizo wa kuheshimu maeneo ya ufugaji yasivamiwe na wakulima wala idara/hifadhi za wanyama pori. Dawa za ruzuku zisimamiwe vizuri ili ziwafikie wafugaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkazo wa *training* ya *para-vets* ili kuziba upungufu wa wataalam wa mifugo vijijini. Naomba mtaalam wa dawa kwa ajili ya *Amei vet centre* iliyoko Kiteto ili kituo kihudumie wafugaji wa Kata zilizopo tarafa ya Kijungu.

Pia Wizara ipange na kuendesha wiki ya wafugaji Tanzania ili kuhamasisha umma wa Watanzania juu ya nafasi ya ufugaji katika utekelezaji wa MKUKUTA Tanzania. Wiki ya wafugaji *(Pastoralists Week)* pia ingetumika kuwahamasisha wadau wa ufugaji kubadilishana *experience* na kujifunza fursa zilizopo nchini za kuboresha mifugo na mazao ya mifugo, kuboresha *access to markets* na kuongeza mchango wa ufugaji katika *YDP*.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri Mheshimiwa John Magufuli, Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote kwa ujumla kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la maofisa ugani katika jimbo langu hasa vijijini. Nashauri vijiji vilivyo mbali na makao makuu ya wilaya wapewe *priority* ya kupata maofisa ugani. Mheshimiwa Rais ametenganisha Wizara hii na ya kilimo hivyo narudia kusisitiza maofisa kilimo na mifugo nao watenganishwe. Nashauri wawepo na

ofisa mifugo kushughulikia mifugo pekee wakati maofisa kilimo nao washughulikie kilimo pekee. Sio maofisa wote wanaweza kujua fani zote yaani kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Singida tunafuga sana kuku wa kienyeji na kulisha Dar es Salaam, Dodoma, Tabora, Morogoro na kadhalika. Ombi langu ni kuwapa elimu wafugaji hawa wafuge kisasa na dawa za maradhi ya kuku nazo zitolewe ruzuku. Maofisa ugani wa mifugo wapo mbali na wafugaji kuku. Nashauri Serikali itusaidie sisi wa Singida kutupatia wawekezaji wa viwanda vya kuchinja kuku na kuwatengeneza kitaalamu ili waweze kusafirishwa nje ya mkoa wetu na hata nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali itoe ruzuku katika dawa za mifugo mbali mbali sio tu za kuogesha mifugo bali na maradhi mengine yanayoathiri mifugo yetu. Huo ndio utakuwa msaada wa kutosha kuliko hali ya sasa. Mheshimiwa Waziri, naomba sana rafiki yangu unipe msaada wa kunipatia mabwawa na malambo kwani kuna upungufu mkubwa jimboni kwangu. Nitampatia Mheshimiwa Waziri mahitaji yangu ya mabwawa na malambo ili anisaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nianze kwa kuwapa pole familia ya aliyekuwa Mbunge wa Mara aliyekufa kwa ajali ya gari na Mungu ailaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimpongeze Waziri na Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara hiyo kwa kutuletea hoja yao hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Ziwa Tanganyika ina kina kirefu, samaki walioko wakubwa sana ambao wanalingana na watu wako ziwa hilo na vile vile vyombo vya kuweza kuwavua samaki hao hakuna, zamani mwaka 1970 kulikuwa na chombo ambacho kilikuwa kinaitwa *Yorogwe* kilikuwa kinavua samaki wakubwa sana ambao ni wakubwa kama mtu. Baada ya chombo hicho kuharibika sasa samaki tunaowapata ni kidogo na wale wadogo wadogo mno, na kwa kuwa Ziwa hilo lina samaki hao ningeomba Serikali iweze kuleta mwekezaji wa kuweza samaki hao pamoja na kujenga kiwanda cha kusindika samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mkoa wa Kigoma na sisi tuna ng’ombe ambao wanafugwa na wananchi, mpaka sasa hivi sisi hatuna majosho ya kuogeshea ng’ombe tulionao kwa hiyo, naiomba Serikali itujengee josho za kuogeshea ng’ombe hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nami nichangie kuhusu Wizara hii. Ningependa kusema kuwa mikopo ya uvuvi haifiki kwa wavuvi wadogo wadogo, hilo ni tatizo kubwa sana na halikidhi kabisa matakwa ya uvuvi wa kisasa.

Pili naomba kujua hivi kiwanda cha ngozi cha Mwanza kiliuzwa kwa ajili ya kukiendeleza au kukifanya stoo na kama dhamira haikuwa kukifanya stoo, basi Serikali inachukua hatua gani kwa mnunuzi huyo? Pia pale katika kiwanda cha ngozi palikuwa na chuo cha ngozi je, chuo hicho kipo mpaka leo na mmiliki ni nani? Naomba jibu la kutosheleza sasa basi kama kunahitajika ajira, ni kukifufua kiwanda cha ngozi ili wafugaji waweze uza ngozi zao ili waweze kujikimu katika maisha ambayo ni magumu sana, na kama tunavyojua ajira ni muhimu sana tena sana, hatuwezi uza kiwanda na kukifanya stoo. Kwa hali hii tutaua ajira kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti nzuri yenye lengo la kuboresha Wizara hii na kuinua uchumi wa nchi yetu kupitia mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutamka rasmi kabla sijaanza kutoa mchango wangu kuwa naunga mkono Bajeti hii kwa kutambua mchango mkubwa wa Mheshimiwa John Magufuli kama ilivyoada yake kuchapa kazi akisaidiwa na Naibu wake Mheshimiwa Dr. james Wanyancha ambaye ni babu yangu watafanyakazi nzuri, Mwenyezi Mungu awatangulie ili azma yao iweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi na kuunga mkono sasa ninaanza kuchangia kama ifuatavyo. Kuhusu ufugaji wa mifugo wa kienyeji, ni ukweli usiojificha kuwa nchi yetu ya Tanzania ina mifugo mingi sana ukiwemo mkoa wa Singida. Tatizo ambalo linafanya ufugaji huu usiwe na tija ni ufugaji usio na taaluma. Mfano wafugaji wanafuga ng’ombe wengi sana wakati malisho yanakuwa kidogo sana, vile vile dawa za mifugo kidogo sana na maji yanapatikana kwa taabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa wafugaji ili kupunguza mifugo kwa kuwauliza ili wafugaji wabaki na idadi ambayo wataweza kuitunza vizuri.

Kuhusu ujenzi wa majosho mapya kila kijiji, natambua kuwa Serikali inawajali sana wafugaji ikiwa ni pamoja na kuwajengea majosho wafugaji wake. Kwa kuwa kasi ya ujenzi wa majosho ya kuogeshea mifugo ni duni sana, naishauri Serikali kujenga majosho kila kijiji na kama kijiji kina mifugo mingi yajengwa majosho mawili. Hii itasaidia tiba ya mifugo ili isipate maradhi ama kuumwa na wadudu mfano kupe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkoa wa Singida na Wilaya zake bado unakabiliwa na upungufu wa majosho ama majosho mengine yamekufa. Sasa yafufuliwe na yajengwe mengine mapya.

Kuhusu malambo ya kunyweshea mifugo, ni ukweli usiojificha kuwa maji ni muhimu sana kwa ajili ya mifugo yetu. Vile vile ninawapongeza wananchi

wanavyoshirikiana vizuri na halmashauri na Serikali katika kujenga malambo. Naiomba Serikali kufuatilia ujenzi huu pale inapotolewa tenda kwani wengi wanaopata tenda hawachimbi na kujengea vizuri na kusababisha malambo haya kutokutunza maji ya kutosha mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hifadhi ya malisho ya mifugo, napenda kuikumbusha Serikali kuwa ufugaji wa mifugo bado sio wa kitaalam kwani hata maeneo ya kuchungia huwa hayatengwi, wafugaji huchungia eneo lolote hata kwenye mashamba ya kilimo na kufanya ardhi za mashamba kuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa Serikali kutunga sera yenye kutenga maeneo ya malisho ya mifugo kila kijiji ili tusiathiri mazingira yetu. Hii itasaidia mimea kutokuliwa na mifugo na maji yaliyotengwa kwa ajili ya binadamu yasitumiwe na mifugo.

Kuhusu maombi ya machinjio ya kisasa mkoani Singida, naomba kutumia nafasi hii kuitaarifu Serikali kuwa kati ya mikoa yenye mifugo mingi ni pamoja na mkoa wa Singida. Hivyo basi naiomba sana Serikali kujenga machinjio ya kisasa mkoani Singida, ili kusaidia wafugaji wa mkoa wa Singida kuboresha ufugaji wao kuwa wa kitaalam zaidi na kupunguza mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ranchi ya Kongwa, napenda kutumia nafasi hii kuitambua ranchi ya Kongwa ingawa uzalishaji wake bado una tija ndogo sana. Ninapenda kuishauri Serikali Ranchi ya Kongwa isiwe ya kufuga ng’ombe bali iwe ya kusindika nyama na kusafirisha nchi za nje. Mradi ambao naamini utaleta faida sana badala ya kufuga ng’ombe. Hii niliona kwenye mahesabu yao mbele ya kamati ya *POC* hawana faida.

Suala la kupandisha ng’ombe kupata chotara, napenda kuieleza Serikali kuwa ili kupandisha soko la ng’ombe ni vyema sasa tuwasaidie wafugaji kupanda madume ya kisasa ili waweze kupandisha ng’ombe wetu wa kawaida ili kupata chotara ambao watakuwa na ubora mkubwa na kupata soko kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia halmashauri zake kununua madume na kukodisha kwa wafugaji ili wapate machotara yatakayotoa maziwa mengi, nyama zitaongezeka na ubora wa mifugo utaongezeka. Napenda kupata majibu mpango huu utaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, samaki katika Ziwa Kitangiri na uvuvi wake, namshukuru Mungu kwani Singida nayo inalo Ziwa ambalo linatupatia samaki ambao ni wazuri kwa afya ya wananchi. Hivyo basi kwa kuwa samaki katika Ziwa hilo ni wachache na ni aina chache tu yaani kambare au perege. Naiomba Serikali kutuletea maafisa uvuvi ambao watatusaidia kupanda samaki wengine ambao wanaweza kuishi humo ili kukuza uvuvi kwa kukuza uchumi pia kutoa elimu ya njia bora ya uvuvi kuacha njia mbaya ambazo zinaua samaki wachanga. Nategemea Waziri atatoa jibu juu ya kutuletea maafisa uvuvi huko Kitangiri.

Kuhusu ugugaji wa kuku Singida, natumai Mheshimiwa John Magufuli ataungana nami kuwa Singida inaongoza kwa ufugaji wa kuku na tunalisha eneo kubwa la Tanzania. Naomba Serikali kutambua ufugaji huu. Vile vile kusaidia ufugaji huu sasa uwe wa kisasa ili kuinua vipato vya wafugaji hawa na mkoa mzima wa Singida. Naomba tupatiwe maafisa wenye fani ya kuku pia ili kupambana na kideri na kadhalika yanayoathiri kuku na kuleta dawa za kutosha.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Kwanza kabisa kuhusu ufugaji, kwa sasa ndio suluhisho la mfugaji na mkulima, na itaondosha tatizo la kuzurura ovyo kwa wachungaji na kumletea tija mwananchi ikiwa mkulima/mfugaji. Wafugaji waelimishwe kuweza kutumia mifugo yao kwa kutatua matatizo yao. Mfano, mfugaji ana kundi la ng’ombe si chini ya 800, kwa nini asiweze kuuza ng’ombe hata 300 ili aweze kutengeneza bwawa lake la maji na shamba la akiba la malisho ili ajitosheleze kwa huduma hiyo. Hamasa zaidi iwafikie wafugaji kuweza kuongeza ufugaji wa mbuzi wa maziwa. Kwani maziwa yake yana bei kubwa kwa sasa lita inafikia shilingi 1000/= hadi 1500/=. Lakini pia maziwa ya mbuzi ni tiba ya maradhi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji waelimishwe kuunda vikundi ili wawe na nguvu, sauti, malengo na mipango ya pamoja ambayo ni rahisi kusikika na kuweza kuzitumia fursa zilizopo za ndani na nje ya nchi. Tanzania tumebarikiwa kuwa na maziwa na bahari kuu ambavyo ndivyo vyanzo vyetu vya samaki. Vyanzo hivi kama tutavitumia vizuri basi wananchi wetu walio katika maeneo hayo wataondokana na umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwe na mpango mkakati wa muda mfupi, wa kati na muda mrefu kuwawezesha wavuvi kukopa na kununua vifaa vya kisasa na vyenye ubora ili kuweza kuvua katika kina kirefu cha maji na hili likiwezekana litapunguza kwa kiasi kikubwa, uharibifu wa mazingira na kuua mazalio ya samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuunga mkono tena hoja.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo ya Uvuvi, pia nikushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii. Kabla sijaendelea naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mifugo mimi naona hivi sasa wafugaji wa wanyama hapa nchini wanapata shida sana kwa kuhangaika kila sehemu kwa kutafuta malisho pamoja na maji. Pia hivi sasa hata majosho ya wanyama hakuna kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuombe Waziri, wafugaji hawa wapatiwe sehemu za majosho kwa wanyama wao pia kuhusu malisho Serikali isimamie ili wafugaji wetu wasizurure ovyo.

Kuhusu uvuvi, wavuvi wawezeshwe kwa vifaa vya kisasa ili waweze kuwa na uvuvi wa kisasa na waondokane na ule uvuvi wa kuvua samaki wadogo na kuwatupa ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada hayo nazidi kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Waziri baada ya Bajeti atembelee jimbo la Mtwara Vijijini ili aweze kusaidia kuzungumza na wavuvi wa eneo langu ili aone jinsi ya kusaidia jimbo hilo.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza sana Waziri yeye binafsi, Naibu Waziri wake pamoja na Wizara nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya kuiongoza Wizara yao. Aidha, nampongeza sana Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuiunga mkono Bajeti hii namuomba Mheshimiwa Waziri asaidie jimbo la Sengerema kwa kutupunguzia kero kuhusu ubovu wa majosho yafuatayo kwa kuyatengea kasma Nyamasala shilingi 10,040,360/=, Kahumulo shilingi 13,488,035/=, Lwenge shilingi 1,113,960/=, Nyamizeze shilingi 13,469,835/=, Lubungo shilingi 1,113,000/=, Ngoma shilingi 13,085,000/= na Sima shilingi 10,630,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILBROD PETER SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:

Kwanza, kwa kuwa miaka miwili iliyopita, serikali iliunda Tume ya Jaji Chande, kuchunguza jinsi wafugaji walivyoondolewa Ihefu; kwa kuwa Tume hiyo ilitumia fedha za wananchi; na kwa kuwa ni muda mrefu sasa tangu taarifa hiyo ilipowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais:-

(a) Je, Tume hiyo ilitumia fedha kiasi gani kufanya kazi hiyo?

(b) Je, mambo au maeneo gani kati ya mapendekezo ya Tume yametekelezwa na serikali?

(c) Kwa nini serikali inaendelea kuwa na kigugumizi kuweka hadharani taarifa kamili ya Tume hiyo ili Watanzania waifahamu?

(d) Kama imekuwa vigumu kuiweka hadharani; serikali ipo tayari kuigawa kwa Wabunge wote ili angalau Wabunge waipitie kwa niaba ya wananchi hasa walioathirika na utaratibu uliotumika katika kuwahamisha toka Ihefu?

Pili, kwa kuwa wakati wa ziara yake Tanga hivi karibuni, Mheshimiwa Rais baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wavuvi wadogo; alitoa kauli ya kusitisha Waraka wa Mkurugenzi wa Uvuvi uliopelekwa kwa Halmashauri kuzuia kilichoitwa uvuvi haramu wa *Ringnet* na njia mbalimbali zinazotumika na wavuvi wadogo:-

(a) Wizara itatekeleza lini kauli hiyo ya Mheshimiwa Rais ili kulinda maslahi ya wavuvi wadogo wadogo?

(b) Kwa kuwa katika kutekeleza Agizo la Wizara, polisi walivamia wavuvi na kuchana chana nyavu zao Tanga; jambo lililoleta uharibifu wa zaidi ya shilingi milioni 17 na nyaraka mbalimbali. Taarifa kuhusu uharibifu huo zimewasilishwa kwa Waziri na hata Waziri Mkuu. Serikali inatoa kauli gani ya uharibifu wa mali za wananchi; hata kama wangelikuwa na makosa kwa nini mali zao ziliharibiwa badala ya sheria kuchukua mkondo wake?

(c) Wakati wavuvi wadogo wadogo wanazuiliwa kuvua kwa nyenzo zilizo ndani ya uwezo wao, serikali inatoa kauli gani kwa meli kubwa zinazovua na kuleta uharibifu mkubwa zaidi katika bahari zetu; wakati wananchi wanyonge wanaojitafutia chakula chao na fedha za kusaidia familia wanabughudhiwa ndani ya nchi yao? Hii haina maana serikali isilinde sheria zilizoko wala kuisimamia, lakini suala la msingi ni kwa nini kuna ubaguzi huu; jambo hili linaashiria nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuupongeza uongozi mzima wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuanzia kwa Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote.

Pili, napenda kufahamu Wizara inafanya nini; ikiwa ni pamoja na sheria za kuhakikisha kuwa migogoro inatatuliwa kwa kuweka matumizi bora ya ardhi katika wilaya zote? Maeneo mengi ya wafugaji yamechukuliwa na wakulima kwa sababu mfugaji anaweza kuacha alama; mifugo inaposwagwa endapo mkulima anavamiwa; je, maeneo ya malisho hayawezi kuwa *gazetted* ili yasivamiwe ovyo?

Tatu, mifugo huhamahama kwa ajili ya kutafuta malisho, maji na huduma za tiba na chanjo; je, serikali inasemaje katika kuhakikisha miundombinu yetu inayohitajika inakuwemo katika maeneo ya wafugaji ikiwemo maji, majosho na vituo vya *veterinary.*

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani zangu.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Wizara kwa mikakati mizuri ya kukuza na kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, Sekta hii imekuwa ikikua kwa asilimia ndogo sana, ikilinganishwa na Sekta nyinginezo licha ya kwamba, asilimia kubwa ya wananchi hujishughulisha na ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango iliyobainishwa ni mizuri na itaweza kabisa kuiendeleza Sekta hii; japo swali la kujiuliza ni je kwa, *budget* iliyopangwa tutaweza kweli kufikia malengo yetu na yale ya MKUKUTA; kwani Wizara hii imekuwa ikitengewa fedha kidogo sana mwaka hadi mwaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni la muhimu katika Sekta ya Mifugo ambalo Wizara haikulizungumzia ni suala zima la sensa ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana kuwa na sensa inayoendana na wakati, kwani sensa iliyopo ya mifugo ni ya muda mrefu tangu mwaka 1984. Sasa ni dhahiri kabisa, idadi ya mifugo itakuwa aidha imeongezeka au imepungua na ile mikoa inayoongoza kwa uwingi wa mifugo pengine kwa sasa ndiyo inayoongoza kwa uchache wa mifugo!

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inaweza kupotosha kabisa Mikakati Maalumu ya Serikali dhidi ya sekta hii; mfano, kwa sasa Serikali inajipanga kujenga viwanda vya kusindika nyama na vile vya maziwa katika baadhi ya mikoa, lakini cha kusikitisha ni kuwa mipango hii imezingatia sensa hiyo ya 1984 ambayo ni ya muda mrefu sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Waziri atueleze ni sababu zipi zinapelekea kutokufanyika kwa sensa itakayokidhi mipango hii maalumu ya serikali? Pamoja na ufinyu wa bajeti; Wizara haioni umuhimu wa kufanya sensa ya mifugo nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naomba kuwasilisha.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu, wake kwa mwanzo mzuri wa Wizara hii mpya. Ninawaombea Mwenyezi Mungu awaongoze vyema. Sina wasiwasi nao; ni mahodari na makini. Kama alivyokwishasema Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere; *"It can be done, play your party."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiutaratibu kama Waingereza husema; *"Charity starts at home."* Kwa misingi hiyo, naomba malambo na majosho kwenye Jimbo langu la Bukene. Kusema kweli malambo au majosho yaliyopo yanahitaji ukarabati; ni malambo au majosho yaliyochimbwa enzi za Machifu wa Ukoloni. Naomba ukarabati wa hali ya juu kwa malambo au majosho yaliyoko Mahene, Buhondo, Nawa - Kata ya Mwamala, Igusule, Ikindwa, Karitu na Isagenhe na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo bila maji au dawa ni shida kubwa na mifugo hufa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo ni mali na inaweza kututoa katika dimbwi la umaskini hasa ukizingatia kwenye mifugo mfano, ng'ombe kuna ngozi ambayo ni mali, maziwa ni mali, samli ni mali, nyama ndio basi. Hivyo, kwa misingi hiyo tunaomba majosho na dawa ikiwezekana kwa ruzuku, kama pembejeo kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ukarabati basi wa malambo au majosho niliyoyataja hapo juu. Kuna bwawa pale Itobo ambalo Hayati Dr. Mwaisela alipatwa umauti wake hapo wakati akiwinda bata. Hayati Dr. Mwaisela ni mmoja wa madaktari wa kwanza Waafrika wa nchi hii. Nilishalielezea kwenye Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati *World Vision* walitoa Mradi wa Uvuvi na sisi hatuna historia ya uvuvi wa kitoweo cha samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, walichukue ombi langu hili kujenga bwawa la kufuga samaki na kupata ajira kwa vijana na akina mama kwa biashara yote ya samaki tangu uvuvi hadi uuzaji. Namwomba Mheshimiwa Waziri, alichukulie suala hili kwa uzito wa hali ya juu. Nasema *"It can be done, play your party"*. Vijana, wanawake na wananchi, wapo tayari kuupokea Mradi huu na hivyo kupata kitoweo cha samaki ambacho ni *protein*. Naomba na nina imani kubwa tutapata Mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nielekeze mchango wangu kwa Chuo cha Uvuvi Mbegani Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo kinakufa bila sababu na tunakihitaji sana. Naomba wapewe fedha za kutosha ili wakifufue Chuo hicho, kwani ni muhimu sana. Chuo kina meli mbovu ambazo zinahitaji matengenezo. Meli hizi katika dunia ya ushindani, zinaweza kuvua samaki *(Deep Sea Fishing)* na hivyo kukipatia chuo mapato na kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima itoe fedha ili ipate fedha. Naomba basi wafufue meli na mashine zile za umeme ili wataalamu waweze kufundisha vizuri. Kwa kifupi, wapewe nyenzo na motisha. Walimu hapa wanafundisha mabaharia hata wa nchi za nje, wakitoka pale wanapata mishahara minono na wengine wamehama kufuata *green pastures*. Kwa misingi hiyo, naomba waliobaki hapo wapandishwe vyeo, mishahara ua posho ilimradi motisha ili tusiwapoteze na tuongeze nguvu. Tukifufue chuo hiki, kinajulikana nchi za nje kuliko ndani. Hivyo, tukitangaze lakini tukipandishe *status* yake pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ila si kwa umuhimu, wale wataalamu wa ufugaji wa kuku wa kienyeji, wasambazwe nchi nzima hadi kwenye *grassroots* vijijini. Naomba waje jimboni kwangu wanifundishie ufugaji wa kuku wa mayai ya kienyeji kwa kisasa ili wananchi wangu au taifa waondokane na umaskini na wapate lishe pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA**: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukame Jimbo la Nyang'hwale Shinyanga Vijijini ambayo ni kame; mMifugo hupata matatizo ya maji miezi ya kiangazi ambapo hubidi kuhamia maeneo ya maji (Lubaga).

Naomba yafufuliwe malambo yaliyochimbwa na wakoloni yajulikanayo kama "Malambo ya Wazungu" ya Nyang'hwale kwa Kujenga tuta lililobomoka, kusafisha lambo au kuchimba; Lambo la Ibolelo/Busolwa kwa kujenga ukuta wa lambo na kuchimba tope; kuchimba lambo Kata ya Nyugwa; na kuchimba lambo Kata ya Mwingiro.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

Sekta ya Mifugo: Kulipozuka ugonjwa wa *(rift valley)*, pamoja na kuwa na maabara ya mifugo (Temeke), lakini bado sampuli za damu zilikuwa zinapelewa Nairobi kwa uchunguzi. Je, kwa sasa hivi maabara hii imeshapata vipimo hivyo ili kila kitu kifanyiwe uchunguzi hapa hapa nchini badala ya kupeleka sampuli nje ya nchi?

Kampuni ya Ranchi ya Taifa *(NARCO)*: Pamoja na kampuni hii kunenepesha na kuzalisha mifugo, bado haifanyi kazi kwa kasi ipasavyo katika sekta hii. Tunaweza kuliingizia taifa fedha nyingi sana za kigeni kwa kuuza maziwa na nyama nje ya nchi kama nchi za Uarabuni ambako huwa wananunua nyama nyingi sana kutoka nje ya nchi hata Mabara ya Ulaya.

Nashauri wafugaji wazidi kupewa elimu ili wafanye ufugaji wa kisasa. Wawepo madaktari wa mifugo wa kutosha mpaka kule vijijini na gharama za dawa za mifugo ziwe za bei nafuu. Wizara iwawezeshe waweze kutoa hata vipeperushi vya kutosha vinavyohusu ufugaji bora.

Pamoja na serikali kuhimiza unywaji wa maziwa, lakini maziwa haya lazima yawe safi na salama kiafya. Kama tujuavyo, maziwa yasipochemshwa vizuri yanaweza kuleta magonjwa kama TB; kuna haja ya kuhamasisha sekta binafsi ili wajenge viwanda vya kusindika maziwa safi na salama yaweze hata kuuzwa nje, siyo tu kutafuta wawekezaji wa kuja kuchimba madini yetu ambayo faida wanayopata wahusika ni ndogo sana.

Kwa kuwa kuna mikoa iliyopangwa kuwapokea wafugaji kutoka Ihefu, lazima ikumbukwe kuwa wafugaji hawa ni wanadamu; hivyo lazima miundombinu iandaliwe kama vituo vya afya endapo wataugua, mashule kwa watoto wao, makazi ya kuishi, maji safi na salama ya kunywa na kupikia, ikiwa ni pamoja na majosho na malambo. Je, mpaka sasa hivi serikali inafanya maandalizi gani kwa wafugaji hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba jibu.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla ya kutoa mchango wangu, niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara, kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba serikali sasa ifike mahali na kutafakari kwa kina, kilio cha kila siku cha wafugaji. Licha ya mazao ya mifugo kuchangia kwa kiasi kikubwa Pato la Taifa na kwa kiasi kikubwa chakula cha Watanzania, bado sekta hii haijapewa *priority* inayostahili kama inayopewa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linaloikabili sekta hii ni suala zima la miundombinu. Hakuna malisho ya uhakika, maji ya kutosheleza, majosho ya kisasa, mabwawa na kadhalika. Mbaya zaidi, ukame unapokumba maeneo ya wafugaji, serikali haiipi uzito unaostahili ili kuwasaidia wafugaji ili nao wajione ni Watanzania sawasawa na wakulima. Badala yake, wanapohama kutafuta kunusuru mifugo yao, serikali inaungana na wasio wadau kuwashutumu na kuwaongezea *frustration.*

Mheshimiwa Naibu Spika, laiti ingeeleweka huzuni na kilio kinachowakumba wafugaji wanapofikia hatua ya kuamka na kuhama na mifugo yao, usiku wa kuamkia siku ya kuhama, jamii hii ina huzuni kubwa kwa kuwa kuhama huko kunaambatana na mifugo kufa njiani; mifugo kuliwa na wanyama njiani; watoto kuliwa na simba, fisi na wanyama wakali njiani; kunyang’anywa mifugo yao; wanawake kuachwa wenyewe kwenye maboma na hivyo kungoja kuvamiwa na huko hakuna waandishi wa habari wa kuripoti matukio haya.

Kwa hiyo, kuhama ni huzuni kubwa si kuwa wanapenda bali inabidi iwe hivyo na kwa kuwa mifugo wanalia usiku kucha kutwa wanapokosa maji na malisho; hata wewe usingevumilia ungehama. Mimi ni Mbarbaig/Datoga *pure*, naelewa uchungu huo.

Naiomba serikali itenge fedha za kutosha kuimarisha miundombinu kwa ajili ya wafugaji na mifugo yao ili wasiendelee kuhamahama, waboreshe afya zao na wapate maendeleo kama wenzao wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ninalotaka kuchangia ni la muundo wa Wizara. Mimi naomba serikali iridhie muundo wa Wizara ya Mifugo kuwekwa pamoja na Uvuvi. Hizi kwa mtizamo wangu, zina *priorities* tofauti kabisa.

Wavuvi hawana shida na ukame, hawana tatizo la majosho wala malisho, wana mila na desturi tofauti kabisa na wafugaji.

Wafugaji wengi hawapendi hata kula samaki, hawajawahi hata kuelewa matatizo ya wavuvi na kadhalika. Kwa hiyo, wadau wa sekta zote mbili wanapokaa pamoja ndani ya Wizara hawana *common problems,* hawana *common understanding* za idara zao na kadhalika. Naomba serikali iangalie hili, ili wadau washirikiane kuendeleza sekta zao *smoothly.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, chonde chonde, naomba serikali iingilie kati suala la wananchi wa Vilima Vitatu Wilayani Babati, Manyara ili hawa Wabarbaig nao wajione ni Watanzania wanaoheshimika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri asome hii *paper* yangu kwa makini kama mfugaji na aliwekee uzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Mheshimiwa Waziri alitaje jina langu wakati ana-*wind up* ili Wabarbaig wa Vilima Vitatu Babati wasikie kwani wananipigia simu kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, natunguliza shukrani.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa maandishi Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inasimamia mambo muhimu ya rasilimali za nchi. Ningependa kutoa maoni yangu juu ya masuala ya uvuvi; kitendo kinachoendelea sasa cha kuwazuia wavuvi wasivue baadhi ya maeneo uangaliwe upya ili kuondoa malalamiko ambayo wavuvi wadogo nao wananufaika na rasilimali hii katika bahari, mito na maziwa na kuinua hali zao za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna mifano hai; mfano hivi karibuni (Wilaya ya Bagamoyo), kuna boti ya TAWAQAL ilikamatwa ikiwa na nyavu nchi 1, 2, 3 na kuambiwa hazifai na jambo hili huwachanganya sana wavuvi maana hawajui hasa ni nyavu za inchi ngapi hazitakiwi. Serikali itoe tangazo kwa ajili ya ufafanuzi.

Vilevile ningependa kuisisitiza serikali hizi meli kubwa za uvuvi zilizopo baharini huwa zinavua mavuno zaidi lakini mapato yanayolipwa ni madogo, sasa ni wakati muafaka serikali kufuatilia suala hilo ili nchi ipate mapato zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam ni Jiji la Biashara kama serikali ilivyotueleza katika Jiji hili, lakini jambo la ajabu na la kukera; baadhi ya wakazi huwa wanafuga ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku. Ufugaji huu ni kero kwa wakazi wa Jiji kama Osterbay, badala ya kutengeneza bustani nzuri katika maeneo hayo utakuta ng'ombe na mifugo mingine na maeneo mengine ya jiji hali ndio hiyo; kero kubwa. Naomba serikali ipige marufuku kufuga mijini, kutasaidia kuharibu mazingira na kuondoa harufu mbaya ya kinyesi cha mifugo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu haya naunga mkono hoja.

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *MACEMP* ni mzuri na lengo lake kuu ni kulinda na kuboresha mazingira ya bahari ambayo yameathirika sana. Jambo ambalo linafurahisha kwa wananchi wetu ni kuwa, wameonyesha kuelimika kwa kiasi kikubwa juu ya umuhimu wa kulinda mazingira ya baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ambayo yanaharibu mazingira ya baharini ni mengi lakini yafuatayo ndio makini: Utumiaji wa nyavu za macho madogo katika bahari ya maji kidogo; utumiaji wa wavuvi wa kutumia mabomu na aina nyingine za sumu; na uharibifu wa matumbawe na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na lengo na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Mradi huu lakini zipo sehemu ziimarishwe zaidi. Tanzania kwa ujumla, haina viwanda vya vifaa vya uvuvi kama vile nyavu na mashine. Aidha, Tanzania haina viwanda vya kuhifadhia samaki na hatimaye kuuza samaki wengi nje ya nchi.

Nashauri Tanzania ifikirie kuwa na viwanda vya kuhifadhia samaki. Tanzania iwe na viwanda vya vifaa vya uvuvi. Vilevile iitumie bahari kwa kupata zao la samaki kuwa ni zao la biashara kwa kuliingizia taifa fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ichukue tahadhari za mara kwa mara kukabiliana na ugonjwa wa kichaa cha mbwa ambao ni hatari sana.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Nampongeza Waziri, Mheshimiwa Magufuli, Naibu Waziri, Mheshimiwa Wanyancha, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa maandalizi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Hali duni ya sekta ya mifugo imekuwa duni kwa miaka mingi kutokana na ufinyu wa fedha zinazopewa katika bajeti mwaka hadi mwaka. Hali hii imepelekea sekta hii kukosa miundombinu ya msingi kama vile malambo, majosho, mabwawa na miundombinu muhimu ya maji katika maeneo ya jamii za wafugaji. Hali hii imepelekea sekta hii kukua kwa kiwango cha chini cha kati ya asilimia nne na tano kwa mwaka na mchango wake katika Pato la Taifa ni asilimia nne pointi saba, ambazo ni ndogo kuliko mchango wa sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri serikali itoe kipaumbele kinachostahili kwa kuongeza bajeti ya Wizara hii ili nayo itoe mchango mzuri katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa huduma za maji kwa maana ya malambo na mabwawa, kumesababisha wafugaji wetu kuwa wachungaji wa asili, wanaozagaa kila mahali nchini wakifuata malisho na huduma za maji kwa mifugo yao. Kuzagaa kwa mifugo bila mpangilio maalumu, kumepelekea mifugo kuharibu vianzo vingi vya maji na uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ukosefu wa miundombinu ya maji, jamii hii ya wafugaji inakosa huduma za afya na elimu zikiwa mojawapo. Katika hili ni vyema serikali ikatenga sehemu za malisho ya mifugo na sehemu za kilimo kama ulivyonuia siku zote. Kama hili litatekelezwa, basi serikali itaweza kutafuta jinsi ya kuwapa huduma za kijamii ikiwemo maji, elimu na afya kwa jamii za wafugaji. Kwa njia hii, wafugaji hawa hawatakuwa na sababu ya kuhama na mifugo yao na kuzagaa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine katika sekta hii ni la mbegu bora ya mifugo. Kwa kuwa ufugaji wetu ni wa asili kwa kiwango kikubwa, sasa wakati umefika wakati wa kubadili mifugo yetu ili iwe bora kwa kutoa maziwa mengi na nyama nyingi ambayo itaboresha mapato ya mfugaji na ubora wa nyama.

Eneo lingine ambalo ningependa kulielezea ni la upatikanaji wa dawa za mifugo. Serikali inatoa ruzuku kwa wakulima na tunaipongeza serikali katika hili, lakini ruzuku hii kwa asilimia kubwa inakwenda kwa wakulima kama mbolea, zana za kilimo na dawa za mazao. Wafugaji, hasa hawa wanaohama hama, hawapati dawa hizi za ruzuku. Ninaishauri serikali ione jinsi ya kuwapa wafugaji hawa fursa ya kupata dawa hizi za mifugo kwa kiasi kinachoridhisha kwa ubora na mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza serikali kwa hatua nzuri ya kuandaa mazingira mazuri ya kuanzisha viwanda vya usindikaji wa nyama. Huu ni ukombozi mkubwa kwa wafugaji kwa kuwa mazao ya mifugo hasa nyama itakuwa na soko lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie suala zima na adha waliyopata wafugaji waliohamishwa kutoka Bonde la Usangu kwenda Mikoa ya Lindi, Pwani (Rufiji) na Rukwa.

Pamoja na nia njema ya serikali kuondoa mifugo katika Bonde la Usangu ili kuokoa vianzo vya maji na mazingira, zoezi hili limegubikwa na matatizo makubwa ya utekelezaji, matatizo ambayo yamesababisha hasara kubwa kwa wafugaji husika.

Kwa kuwa kuna Kamati iliyoteuliwa kushughulikia suala hilo, tunaomba taarifa ya Kamati hiyo Teule, iletwe Bungeni katika kikao hiki cha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nazipongeza asasi mbalimbali zilizofuatilia matatizo ya wafugaji. Asasi hizo ni pamoja na Pingos Forum, Haki Elimu, Legal and Human Rights Centre, HIMWA, PAICODEO na wafugaji wa Mikoa ya Arusha, Manyara na Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi zote za serikali za kuendeleza wavuvi, bado wavuvi hao wapo katika umaskini mkubwa. Wengi wa wavuvi wadogo wadogo kwenda kwao kuvuwa ndio njia inayowapatia chakula cha kila siku, bila ya kuwa na akiba inayoweza kuwasaidia siku ya pili yake kupata chakula ni umaskini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, ipo haja serikali kuwawezesha wavuvi hao kwa nguvu zaidi ikiwemo kuondoa ushuru katika zana zile za mvuvi kwa mfano, mashine za boti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Ukanda wa Pwani wa Tanzania Bara na Visiwa vya Zanzibar vipo katika Mradi wa *MACEMP*. Mradi huu utachukua miaka sita. Bila shaka mategemeo ya Mradi huu ni kunyanyua maisha ya wavuvi wa Ukanda huo wa Bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina kawaida ya kuitekeleza Miradi iliyo chini ya wafadhili vizuri, lakini ufadhili unapomalizika Miradi hiyo hufa. Je, huu Mradi wa *MACEMP* utakapomaliza muda wa ufadhili utaendelea? Je, serikali imejiandaa vipi kuhakikisha Mradi huu utaendelea baada ya kwisha ufadhili?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ijiandae vya kutosha kudhibiti uvuvi wa Bahari Kuu unaofanywa na meli za kigeni. Wizara ione kuwa mapato makubwa yatatokana na uvuvi huu badala ya kuwabana wavuvi wadogo wadogo. Ahsante.

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amenipa uhai na afya njema na nikaweza kutoa maoni yangu kwenye hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake. Vilevile namshukuru Waziri, Naibu wake, pamoja na timu yake yote kwa jinsi walivyoandaa hotuba na kuiwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, hakuna kijiji au wanakijiji wanaokataa wafugaji, sote tunafahamu umuhimu wa sekta hii ya ufugaji kwa sababu inatupatia mambo mengi muhimu kwa afya zetu na kutusaidia kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri atakubaliana na mimi kuwa, maeneo mengi yamevamiwa na wafuagaji kwa mfano, kama kule Morogoro Vijijini kuna Vijiji vya Ngelengele, Tununguu, Magogoni na Kata zake, maeneo yote yanatumiwa na wafugaji waliohamia hivi karibuni kwani kuna nafasi kubwa hazitumiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenyeji wa vijiji hivyo waliwapokea vizuri sana wafugaji hao, kwa kuona washirikiane na kuuziana na kubadilishana bidhaa kwa bei nafuu.

Kama unavyofahamu, wanavijiji huwa wanategemea sana maji ya mito kwa matumizi yote muhimu. Cha kusikitisha, wafugaji hawa wanaharibu maji haya, baada ya kutenga maeneo kwa ajili ya kunyweshea mifugo yao na kusababisha adha na kero kubwa kwa wanavjiji hao, kiasi kwamba, watu wanajengeana chuki. Je, Waziri atakubaliana na mimi kuwa, kuna kila haja ya kutolewa elimu ya kutosha kwa wafugaji hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wizara haitachukua juhudi za makusudi, basi kuna hatari kwa vijiji nilivyovitaja kupata maradhi ya mlipuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linalowakera wanavijiji ni wakulima na wafugaji wanaotia mifugo yao ndani ya mashamba ya watu kwa makusudi na kusababisha madhara makubwa ya uharibifu wa mazao. Namwomba Waziri avitembelee vijiji vilivyopelekewa wafugaji ili Wizara ichukue jitihada za makusudi kutoa elimu ili kuepusha mifarakano baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri lile toleo lililotolewa na Mkurugenzi linalowakandamiza wavuvi lifutwe mara moja, kwa sababu limewafanya wavuvi wadogo wadogo kushindwa kazi zao na kusababisha samaki kupatikana kidogo na kupunguza mapato yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli kwa sheria hizi za kukurupuka, tunayo nia ya kuwaondoshea wananchi wetu umaskini? Naiomba serikali ilizingatie sana jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ahsante.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja.

Tanzania tuna ng'ombe wengi sana kuzidi Kenya, lakini Tanzania tuna kiwanda kimoja tu cha mazao ya mifugo kipo Musoma. Kenya wana viwanda zaidi ya vinne vya mazao ya mifugo. Naiomba Wizara ihamasishe wawekezaji ili nasi tuwe na viwanda vingi ukilinganisha na idadi ya mifugo tuliyonayo.

Kwanza, naipongeza Wizara kwa kupiga marufuku uvuvi wa kamba na samaki wadogo, hatua ambayo itafanya samaki kuongezeka baada ya mwaka mmoja huu; lakini bado kuna meli baharini *(high seas)*, ambazo zinaendelea na uvuvi kwa kasi sana. Naiomba wizara iliangalie suala hili, isiwe waliopigwa marufuku ni wazalendo tu.

Sasa hivi kuna migongano mingi kati ya wakulima na wafugaji kwa sababu wafugaji wanafuata maji karibu na wakulima. Wakati mwingine hata umwagaji damu hutokea. Naiomba Wizara ifanye mpango mkakati wa kujenga mabwawa na malambo kwenye maeneo maalum ya wafugaji ili kuepusha migongano hii.

**MHE. SIGIFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Pili, najua Mheshimiwa Waziri anaipenda sana Ruangwa. Mheshimiwa Waziri akumbuke sana alivyonijengea nyumba alipokuwa Ardhi. Naomba aendelee kutupenda kwa vile hatuna kitoweo kule, yaani mifugo *zero* na samaki *zero*.

Tatu, namba nizungumzie ombi la bwawa kubwa la samaki. Pale Ruangwa Mjini au Nkowe, Tarafa ya Mnacho au Mandawa, naogopa sana wapiga kura kuwa watakamatwa na askari wanaolinda *Selous Game Reserve.* Nadhani wapo karibu sasa kushindwa kulinda wanyama pori. Tafadhali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na pia kutoa ushauri ufuatao:-

Kutokana na kuanzisha Kiwanda cha Nyama Shinyanga, naishauri serikali ianze maandalizi kwa wilaya zilizo karibu na kiwanda hicho, ziweze kufuga kitaalamu na ziweze kunufaika na ufugaji na pia kunufaika na kiwanda hicho.

Serikali itilie mkazo uhamasishaji na kuelimisha wafugaji, wawe na utaratibu wa uvunaji wa mifugo ili waweze kufuga kwa tija.

Wananchi waelimishwe ili waweze kutafsiri utoaji wa mifugo waliyonayo uweze kuonekana kwa maisha bora wanayotakiwa kuishi; kwa sasa wafugaji wengi wanaishi maisha duni sana wakati wanao utajiri mkubwa.

Tanzania inayo mifugo mingi sana inayochungwa, haifugwi kisasa, ndiyo maana mchango wa Sekta ya Mifugo katika Pato la Taifa ni mdogo sana.

Serikali iendelee kuimarisha upelekaji wa huduma za utafiti na ugani kwa wafugaji, sambamba na hili iimarishe vyuo vya utafiti.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza hotuba hii na naunga mkono hoja.

Naomba kuwe na uendelezaji thabiti wa Sekta ya Mifugo kwa kuelimisha zaidi wafugaji wenyewe ili wafuge ufugaji bora na hatimaye kuwa na mifugo mingi na bora. Kuwaelimisha wasindikaji wa mazao ya nyama na ngozi na kutoa bidhaa bora ambazo tutauza nje na ndani kwa bei kubwa.

Msisitizo wangu upo katika ubora wa ngozi na bidhaa zake, kwani kidunia ngozi na vifaa vya ngozi ni muhimu sana.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naipongeza Wizara kwa utendaji wake mzuri chini ya usimamizi wa Mheshimiwa John P. Magufuli na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo kwa upande wa nchi yetu bado ni duni. Kwa hiyo, kupitia bajeti hii, naiomba serikali itoe elimu na mikakati ya kisasa, majosho, dawa na kadhalika. Serikali pia iwawezeshe kifedha kwa kutumia mabenki ya ndani na za nje ili Sekta ya Mifugo na Uvuvi zote ziende sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania katika bahari yetu tunao samaki au (kitoweo) kingi na kujipatia mahitaji ya lazima ya kujikimu maisha kwa serikali na wananchi wenyewe. Naiomba serikali kusimamia, kutoa nguvu zote za elimu na vifaa au zana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa uvuvi na ufugaji unatoa ajira kwa wananchi pia kuwa na pato nchini mwetu, serikali iwe na mpango wa kujitosheleza na kutumia wataalam kwa faida ya taifa letu. Juu ya yote, tujiulize kwa nini Tanzania hatupati maendeleo kwa haraka na umakini?

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalendo, uaminifu, akili, ukiaminiwa ujiamini pia mletemaendeleo Tanzania ni Mtanzania. Basi tubadilike kuleta maendeleo nchini mwetu na chini ya usimamizi wake Mheshimiwa Waziri, sina shaka tutaendelea.

Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni na mimi naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa ulinzi wake kutupa uzima kama jinsi apendavyo. Nitumie fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa ujumla. Natoa pongezi hizi kwa dhati kwa umahili wao katika kuiongoza Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu, nielekeze mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) 2005, imeeleza suala la kutenga maeneo ya malisho ili kuondoa migogoro baina ya wafugaji na wakulima. Naishauri Serikali Kuu iingilie kati suala hili ili kuzitaka Halmashauri za Wilaya zitenge maeneo. Nasema hivyo kwa sababu serikali imekuwa ikitupiana mzigo mfano katika Wilaya ya Bukombe, Halmashauri imepeleka suala kwenye Kata; na Kata imezitaka Serikali za Vijiji zitenge maeneo. Kwa mfumo huu hatutatekeleza ahadi hii, kwani maeneo ya vijiji ni madogo. Halmashauri zinaweza kabisa kutenga maeneo ndani ya maeneo yake ya utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tatizo la maji (malambo na majosho), linasababisha uharibifu wa mazingira. Naiomba serikali ihakikishe inawapatia maji ili wasiendelee kuhamahama. *DADPs* tusipoangalia haitasaidia wafugaji, kwani haitumiki ipasavyo. Naomba Serikali Kuu muunde timu ya wataalamu itakayofuatilia utekelezaji wa Miradi hii.

Naomba Wizara msaidie Jimbo/Wilaya ya Bukombe kutupatia bwawa kubwa litakalosaidia wafugaji.

Nashauri serikali iangalie uwezekano wa kujengwa mnada katika Wilaya ya Bukombe. Naamini tukifanya hivyo, wananchi wafugaji watapata sehemu nzuri itakayoshawishi wafanyabiashara wakubwa kuja kununua mifugo hiyo. Naipongeza

serikali kwa uamuzi wa kuwahamisha wafugaji katika Bonde la Ihefu. Tatizo kubwa ni usimamizi wa utekelezaji wa zoezi hili la kuwahamisha. Zoezi hili limesababisha umaskini kwa wafugaji hawa, kwani ilifika hatua ng'ombe waliuzwa kwa bei ndogo sana. Bado watendaji walifanya zoezi kwa nguvu nyingi mno. Nashauri serikali iwe makini katika kulinda maeneo yake muhimu, kwani serikali inawaacha wafugaji wanaingia hadi inaleta madhara, kumbe wangeweza kuzuia suala hili kwa kutoruhusu waishi maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri serikali ijue kuwa, Sekta ya Wafugaji inahusisha jamii nyingi sana. Bado uvuvi inajumuisha kundi kubwa la Watanzania. Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2009/10 iongezwe ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake vizuri. Bajeti inayopangwa ni ndogo sana, inasababisha kutoingiza mapato mengi, kama bajeti itaongezeka; Viongozi wa Wizara hii ni wajasiri, chini ya Mheshimiwa John P. Magufuli, watafanya mambo mazuri sana, lakini kama bajeti ni ndogo tutawalaumu sana Viongozi na Watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, orodha tuliyokuwa nayo imekwisha, sina wachangiaji wengine katika orodha hii, lakini ili kuweza kumpa nafasi nzuri Mheshimiwa Waziri ya kuweza kupitia hizi hoja ambazo zimetolewa nanyi Waheshimiwa Wabunge, basi tutarudi saa kumi na moja, Mheshimiwa Waziri atapewa dakika zake na Naibu wake watajibu halafu tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, sina matangazo mengine, isipokuwa Kamati ya Uongozi na Tume tuna kikao sasa hivi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka jioni saa kumi na moja.

*(Saa 6.45 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati nasitisha Shughuli za Bunge mchana nilikuwa nimesema tutaanza na watoa hoja kuanza kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbalimbali mlizozitoa. Kwa hiyo, nitamwita Naibu Waziri dakika 15 Mheshimiwa Waziri saa moja.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa nilipo nikiwa na afya njema, nguvu na uwezo wa kuendelea kuwatumikia wananchi. Nianze mchango wangu kwa kutamka kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, naomba kwanza nitoe pongezi zangu nyingi kwa Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Aidha, nampongeza kwa kazi kubwa na ngumu anayoendelea kufanya ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda - Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuwa Waziri Mkuu. Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Vile vile nawapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri wote walioteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais, nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge, walioteuliwa ama kuchaguliwa kuwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukue nafasi hii pia kwa namna ya pekee kumshukuru sana Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani aliyonipa kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo. Uteuzi niliupokea kwa unyenyekevu mkubwa sana namuahidi kuwa nitakuwa mwaminifu kwake na kwa Taifa langu katika utumishi wangu. Pia, namuahidi kuwa nitafanya kazi kwa nidhamu, uadilifu na nguvu zangu kadri mwenyezi Mungu atakavyoniongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichukue nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Chacha Wangwe, aliyekuwa Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Salome Mbatia, aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Benedict Losurutia alieyekuwa Mbunge wa Kiteto. Aidha, kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliofiwa na ndugu zao. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kunishirikisha kwa karibu sana katika majukumu ya kuongoza Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wanaonipa katika utendaji wangu wa kazi ndani na nje ya Bunge. Nawaahidi ushirikiano na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu - Dr. Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu Jonas Mlewansi, Wakuu wa Idara na Taasisi chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara. Napenda kushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana wapiga wangu wa Jimbo la Serengeti ambao walinipa kura na kunichagua kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Bila wao kuniamini na kunipa kura, naamini leo isingewezekana nikawa nimesimama hapa. Pia nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Serengeti kwa ushirikiano wanaonipa japo muda mwingi, siko karibu nao jimboni kwa sababu ya shughuli nyingi muhimu za kitaifa. Lakini nawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa moyo na uwezo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru kwa dhati mke wangu Mama Neema, watoto wangu wapendwa Neema, Winfrida, Mwita na Marwa kwa uvumilivu wao wa kutokuwa nao mara kwa mara na kwa msaada mkubwa kwangu kwa kunitunza na kuwa karibu sana siku zote katika mambo yote magumu na mepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa nianze kuchangia hoja kwa kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia kwa kusema hapa Bungeni au maandishi. Lakini natangulia kusema kwamba mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atawatambua rasmi kwa kuwataja mmoja mmoja kama ilivyo desturi yetu. Lakini kwa ujumla wao, wote tunawashukuru sana kwa kuchangia kwa michango yao. Tunathamini michango hiyo na tutaendelea kuifanyia kazi. Niseme tu kwamba, michango ni mingi sana na yote tumeitolea majibu ila kutokana na muda hatutaweza kuisoma yote kwa kina katika kipindi hiki. Hivyo tumeiweka kwa maandishi ambayo Waheshimiwa Wabunge watapatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuziona sekta ya mifugo na uvuvi kama muhimu kwa Taifa letu na kwamba bajeti ni ndogo, lakini hii yote ni kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia na kufafanua hoja chache na kumwachia Mheshimiwa Waziri kuhitimisha kuwajibu hoja nyingine ambazo nitakuwa sikutolea maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingi zimetolewa na mojawapo ya kwanza ambayo nitaanzia ambayo ilitolewa ni kwamba tuwawezeshe wafugaji na wavuvi kuongeza uzalishaji. Wizara yangu imeweka mikakati. Ili kuwezesha hilo kwanza Serikali itaendelea kuhamasisha wafugaji na wavuvi kuanzisha Vyama vya Akiba na Mikopo ambavyo ni *SACCOS*.

Pili, Serikali itahamasisha taasisi za fedha kutoa mikopo kwa wafugaji na wavuvi kwa ajili ya kununua pembejeo, zana bora za uvuvi, kujenga miundombinu muhimu na kuwapatia wafugaji mbegu bora za mifugo. Tatu, tutaendelea kutoa mafunzo na elimu kwa wafugaji na wavuvi kuhusu ufugaji na uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine lililotolewa ambalo hoja ilitolewa ni kwamba maeneo ya wafugaji na wakulima yatengwe ili kuzuia migogoro. Tumeona kwamba kuna migogoro mingi na hivyo basi Wizara yangu imeanza kuchukua hatua. Hadi sasa jumla ya hekta 930,276 katika vijiji 155 vya Halmashauri 24 zimetengwa na kupimwa kwa ajili ya ufugaji.

Pili, zoezi hilo litaendelezwa mwaka 2008/2009 kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Halmashauri ili kuhakikisha maeneo mengi yanatengwa na wafugaji wanapokwenda huko hawapati matatizo kama ilivyo sasa.

Tatu, Wizara isaidie Halmashauri kuwa na mipango mizuri ya ardhi. Hili nalo tumelichukulia na kwa kushirikiana na Halmashauri zitahamasishwa kutenga maeneo kwa ajili ya ufugaji na kutoa mafunzo kwa wafugaji bora kwa kuzingatia sheria ya matumizi ya ardhi Na. 6 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni kwamba kuwepo vituo maalum vya mafunzo ya ufugaji bora wa mifugo na samaki. Mafunzo ya ufugaji bora kwa mifugo katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yatatolewa kupitia vyuo vya Uyole na Madaba. Mafunzo ya Uvuvi yatolewe kupitia huko nyanda za Kusini, yatatolewa na *TAFIRI* iliyoko Kyela.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni kwamba wakati wa ukame wafugaji waruhusiwe kuchungia katika maeneo ya hifadhi. Hilo halitawezekana kwa sababu inatokana na maeneo ya hifadhi yametengwa kisheria, wafugaji hivyo hivyo wanaombwa wasiingie humo ila tunawahamasisha kufuga ng'ombe kulingana na uwezo wa ardhi na kuboresha maeneo yao ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni kwamba shamba la kuzalisha mitamba na mafuke litumike kujenga uwanja wa ndege. Ukweli ni kwamba shamba hilo ni muhimu sana, lina mambo matatu ambayo yanafanyika pale. Shamba la Mifugo la Mabuke ni chanzo kikubwa cha mifugo bora katika miaka mitano iliyopita kituo hicho kimesambaza jumla ya mitambo 285 katika Wilaya za Mkoa wa Mwanza.

Pili, katika shamba hilo kuna kituo cha kutoa mafunzo kwa wafugaji ambapo wafugaji 385, wamepatiwa mafunzo ya ufugaji bora katika kipindi cha kuanzia mwaka 2006,2007 na 2008. Aidha, kuna kituo cha utafiti wa mifugo na shamba la mbegu bora hapo. Kwa hiyo, tunaomba kwamba kwa kweli tuache hicho kituo kiendelee kuwa mahali pa kufugia mifugo badala ya kujenga uwanja na nahisi kwamba Mheshimiwa Mbunge aliyetoa hii hoja atatafuta sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lilitolewa ni kwamba, kuimarisha utafiti wa mifugo na uvuvi na hoja zilizotolewa ni kwamba *TAFIRI* ipewe fedha na ijengewe maabara ya kufanyia utafiti kituo cha Dar es Salaam, kituo cha Utafiti Mabuki, kupatiwa ofisi na vitendea kazi, *sample* zipelekwe nje ya nchi.

Hizi ni hoja ambazo zilitolewa katika Wizara yetu. Wizara imeendelea kuimairisha taasisi ya vituo sita vya utafiti vya mifugo na *TAFIRI* kwa upande wa uvuvi. Vile vile maabara kuu ya mifugo imeimarishwa ili iweze kufanya tafiti mbalimbali pamoja na kutengeneza chanjo za magonjwa ya mifugo ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa miguu na midomo.

Tatu, Idara itendelea kuimarisha vituo vya utafiti wa mifugo na vituo vya kuchunguza magonjwa ya mifugo, *VIC* pamoja na kutoa kituo cha Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni kwamba tuimarishe vyuo vya mafunzo vya mifugo na uvuvi. Tayari Wizara inaendelea kuvikarabati hivyo vyuo na kuvipatia vitendea kazi vyuo vya mafunzo ya mifugo na uvuvi ili kuweka mazingira bora katika vituo hivyo. Chuo cha Mafunzo ya Mifugo Temeke kimeanza tena kutoa mafunzo. Vyuo vitaendelea kupatiwa fedha kulingana na uwezo wa Serikali na hatua za kuwatenganisha watumishi katika ngazi ya Wilaya imechukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lilitolewa ni kwamba mazalia ya Samaki kuweko na mpango wa kulinda mazalia ya samaki katika Ziwa *Victoria.* Hatua zimeshachukuliwa na kwa sasa hivi kuanzia tarehe 1 Januari hadi Juni, hakuna uvuvi wowote unaofanyika katika sehemu hiyo ili kuhakikisha kwamba samaki wanapata maeneo mazuri ya kuzalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni kuwa, mkakati wa kudhibiti magonjwa ya mifugo Wizara imeshaweka mikakati mfano Wizara imeandaa mikakati mbalimbali ya kudhibiti magonjwa ya mifugo ikiwa ni pamoja na magonjwa ya milipuko, magonjwa yanayoenezwa na wadudu na ya mifugo yanayoambukiza binadamu.

Pia, katika mwaka 2008/2009 Serikali imeongeza ruzuku ya madawa ya kuogesha mifugo kutoka shilingi bilioni 1.2 mpaka bilioni 1.4. Wizara imepeleka dozi 1,500 kwa kudhibiti ugonjwa wa kichaa cha mbwa katika Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge, wameomba ni kwamba kuwepo na mbegu bora za mifugo. Nataka kuhakikishia Bunge lako tukufu kwamba kwa sasa hivi Kituo cha *NAIC* kilichoko Arusha kimeimarishwa na kitazalisha mbegu za kutosha kwa yeyote atakayekuwa anahitaji. Tunategemea kitakuwa kinatoa mbegu 100,000 kwa mwaka. Kwa hiyo, anayezitaka atapatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa mbegu bora, tunayo mashamba na wale ambao watakaokuwa wanahitaji madume/mitamba, wataipa. Hoja kuhusu ushuru wa madawa, kuingizwa madawa utatolewa; hii ni kweli na sasa hivi tunashirikiana na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba ushuru wa madawa ya mifugo na pembejeo unatolewa na nafikiri tutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kurejesha kituo cha *Tanganyika Parkers* cha Mbeya, hicho kituo tuko katika harakati *actually* ya kukikamilisha na baadaye tukipata mwekezaji ili kiweze kufanya kazi yake iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulitokea na hoja kwamba Maofisa wa Ugani ni wachache na tuongeze bidii ya kuwaongeza. Nashukuru kwamba mwaka 2007/2008 tulipeleka wanafunzi 1006 katika vyuo vya mafunzo na mwaka huu tunatarajia tena kupeleka wanafunzi 1,185. Kwa hiyo, hii Serikali ya awamu ya nne imelivalia njuga na tutahakikisha kwamba muda sio mrefu tutakuwa na Maafisa Wagani wa ugani wa kutosha ili tuweze kuwasaidia wafugaji huko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia malisho ya vyakula vya mifugo, Serikali iongeze mashamba ya malisho. Nashukuru kutamka kwamba katika mwaka 2007/2008 Wizara imeimarisha mashamba yake ya kuzalisha mbegu bora za mifugo na vile vile kwa kushirikiana na watu binafsi na wenyewe wameanza kuzalisha. Yapo mashamba 16.

Mheshimiwa Naibu Spika, sensa ya mifugo, napenda kutamka kwamba katika mwaka 2008/2009 shilingi milioni 400 zimetengwa kwa ajili ya Wizara kuendesha sensa ya mifugo kwa njia ya *sampling*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumetokea hoja hapa kwamba kuna wafanyakazi ambao walikuwa Talilo na hawalipwi mafao yao. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo hoja tumeitazama na ni kwamba hawa wafanyakazi wanalipwa na ambao hawajalipwa mpaka sasa ni wale tu ambao wapo, bado hawajastaafu, lakini kukitokea matatizo tutahakikishia kwamba Wizara yangu inashirikiana na wafanyakazi ili walipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine kuhusu ufugaji wa samaki kwamba kuwepo uzalishaji wa samaki na mbegu bora za samaki, napenda kusema kwamba vifaranga vya samaki vinapatikana katika vituo vya ufugaji wa samaki vya Taranga Moshi na Kingorwila Morogoro na anayehitaji tutampatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuliwepo na ombi la mabwawa ya samaki. Kwa heshima na taadhima nao Waheshimiwa Wabunge, naomba tuhamasishe wananchi wapitishie miradi hii katika miradi ya *DADPs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja imetolewa kuwa kilimo cha mwani kwamba kiendelezwe, Wizara itaendelea kuhamasisha vikundi ili viongeze uzalishaji wa mwani na thamani yake katika Wilaya zote za ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja imetolewa kuwa kuwepo na utambulizi wa mifugo, alama kwa mifugo. Mfumo wa kutambulisha usajili wa mifugo na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake unaendelea kuimarishwa kama ilivyoelekezwa katika hotuba ukurasa 69.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya mifugo na uvuvi, sheria ya nyama ifanye kazi yake vizuri: hoja hii ilielezwa kwamba sheria ya nyama ifanye kazi yake vizuri pamoja na *meat council.* Katika mwaka 2008/2009 Wizara itaunda Bodi ya Nyama ambayo itasimamia sheria ya nyama Na.10 ya mwaka 2006 na kuandaa kanuni za kutekeleza sheria hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwa kiasi fulani na kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge zinazohusu Bajeti ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utakavyoona hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge sana, wapo 130.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama unavyojua, katika Wizara nyingine zikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, walichangia Waheshimiwa Wabunge zaidi ya 35. Katika hoja ambayo tuliiwasilisha hapa, wamechangia kwa maandishi Waheshimiwa Wabunge 65 na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kuona kwa muda huu ulionipa ambao sasa hivi umekwishapungua, hazifiki hata dakika 60 kujibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge hawa kwa muda wa dakika 60 ambao wao wamechangia kwa wiki kadhaa. Naona muda hautoshi. Lakini nitazungumza tu ya jumla, lakini yale mengine yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia, majibu yake tunayo hapa na tumekwishaandaa yote na tutawagawia na tumeyajibu kwa umakini ili kila Mheshimiwa Mbunge maswali aliyeuliza katika Waheshimiwa Wabunge wote 130 wapate majibu yao kwa ajili ya *document* ambazo zitawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika Wizara nyingine, kwa sababu wamekwishatambuliwa ni 35. Sitapenda niwataje hapa, lakini wale waliochangia kwa maandishi ningependa basi niwataje hapa. Wa kwanza, ni Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Danile Nsanzugwanko, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Zuberi Ali Maulid, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Prof. Phillemon Sarungi, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Rajab Mohammed Juma, Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Fred Tungu, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa

Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, Mheshimiwa Benedict Ole - Nangoro, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji na Mheshimiwa Hawa Ghasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni wapo 30 ambao ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha - Mbunge wa Wete na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Benedict Ole - Nangoro, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa Felister Bura. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Salum Hemed, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Vedastusi Mathayo, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. James Wanyancha pamoja na Mheshimiwa William Ngeleja ambaye alichangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyowataja hawa wachangiaji na kama nilivyoahidi kwamba wote ambao wamechangia hoja zao kwa maandishi na kwa kuzungumza hapa Bungeni wote tutawajibu kwa maandishi na tayari majibu tumekwishayatayarisha. Lakini utaona kwamba Wizara hii kwanza kwa kuchangiwa na Waheshimiwa Wabunge inaonyesha ni kwa namna gani ilivyo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda niseme kwa uwazi kabisa kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge wa pande zote ya CCM na Upinzani wamechangia vizuri sana na mimi ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwa dhati kabisa kwamba ushauri wao wote tumechukua na hasa ikizingatiwa kwamba Wizara yetu sisi ina miezi kama mitatu, minne tu, kwa hiyo, kama ni mtoto alikuwa hata hajaanza kutambaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, michango hii ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge ambayo kwa kweli ni michango mizuri sana imetusaidia sana sisi na ninaamini tutaifanyia kazi katika kuhakikisha kwamba tunaboresha Sekta hii inayohusu Mifugo pamoja na Uvuvi. Kwa hiyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kama michango ilivyojitokeza utaona wazi suala lililokuwa linazungumziwa ni kuhusu mifugo, uvuvi pamoja na wakulima. Mimi wakati nateuliwa kuja kwenye Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, nilisema kwamba sasa nakwenda kupumzika, kumbe nilikuwa najidanganya. Kwa sababu huku nako tumekuta migogoro mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia mifugo na mifugo yenyewe ni zaidi ya milioni 18.8 ng'ombe, mbuzi zaidi ya milioni 13.5, unazungumzia juu ya kondoo zaidi milioni 3.6, unazungumzia juu ya nguruwe milioni 1.4, unazungumzia juu ya kuku wa kienyeji tu ambao wamefugwa Tanzania nzima ndani ya kilomita 949,000 zaidi ya milioni 33, unazungumzia kuku hao wa kisasa zaidi ya milioni 20 na bado hujazungumzia bata mzinga, mbwa ambao wanafuga wengi sana na watani zangu Wahehe, hujazungumzia Kanga, halafu hujazungumzia idadi ya wananchi wenyewe ambao ni zaidi ya milioni 37 na bado hujazungumzia tani za samaki zilizopo katika Maziwa yetu kwa sababu tuna maziwa zaidi ya 21, tuna mito mingi, mbali na Bahari ya Hindi ambayo ukianzia kule Moa hadi Msimbati zaidi ya kilomita 1,422, bado hujahesabu *territorial water* ambazo ni kilomita 54,000 ambazo zinavuliwa na wavuvi wadogo wadogo na kilomita za mraba nyingine 223,000 ndani ya *EEZ*.

Kwa hiyo, unaweza ukaona haya yote ni chimbuko la matatizo yaliyo mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sisi tumeona na nimeona pamoja na mwenzangu Mheshimiwa Naibu Waziri na viongozi wote chini ya Wizara tunaona kwa kweli ni Wizara iliyo na mambo mengi sana. Kwa sababu utakapogusa tu mfugaji, ukishagusa mfugo maana yake wapo wafugaji ambao vilevile ni wakulima. Kwa hiyo, umekwishagusa Watanzania wote, ukishagusa mvuvi, wavuvi wanaoshiriki katika uvuvi katika nchi hii ni zaidi ya watu milioni 4, sasa bado hujahesabu wake zao, watoto wao, jamaa zao. Kwa hiyo, ni kama unagusa *population* ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunajua tuna *challenge* kubwa, lakini pia unazingatia hasa kwa kuangalia pamoja na matatizo haya yote ambayo yanagusa karibu Watanzania wote, bajeti ni ndogo na ndiyo maana tunasema tutaifanyia kazi kwa imani kwa sababu Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa amesema na wanazungumza mara nyingi hata kwenye vitabu vya dini: "imani yako imekuokoa." Ninaamini katika imani mliyotuonyesha Waheshimiwa Wabunge, itatuokoa katika kutekeleza Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nazungumzia kuhusu hizo *challenges* tulizonazo, bajeti ya mwaka huu ambayo imetolewa kwa ajili ya kushughulikia chanjo tu za ng'ombe pamoja na mifugo mingine zinatosha kuchanja ng'ombe milioni 2.5.

Kwa hiyo, katika idadi yote ya ng'ombe hao tutachanja asilimia 12 kwa sababu tumepewa bilioni 1.4, hiyo ni *challenge* kwetu, unafanyaje? Lakini wakati tunashughulikia hilo tunajikuta tuna Shirika la *NARCO* ambalo limeanza na ambalo linashughulikia hekta zaidi ya 230,000 katika nchi hii na ambalo lina *ranch* zaidi ya 10. Lakini tangu libinafsishwe baada ya *PSRC* mwaka 2006 ng'ombe wao ambao ni *constant* tu, kila mwaka ni ng'ombe 41,000, unaweza ukajiuliza hawa ng'ombe huwa hawazaliwi? Je, hawa ng'ombe huwa wanakufa tu? Wako *constant*. Kwa hiyo, hizi ndizo *challenges* tulizonazo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilijaribu kutembelea ranchi moja ya Ruvu tangu mwaka 2003 na mimi nataka nizungumze tu ukweli kwa sababu hizi ni *challenges* zetu wote. Mwaka 2006 wakati imetoka kwenye *PSRC* ilikuwa na ng'ombe 3,024, siku nilipokuwa nikiitembelea miezi miwili iliyopita ilikuwa bado na ng'ombe 3,024. Nilipojaribu kuhesabu wale ng'ombe waliokuwa na mimba walikuwa zaidi ya ng'ombe 750. Nilipouliza pale nikaambiwa kwa mwaka huu Watazaliwa ndama zaidi ya 1,200 hadi 1,500.

Kwa hiyo, ukishachukua *ratio* hiyo kwamba ikiwa katika kila ng'ombe 3,000 wanaozaliwa kwa kila mwaka ni ng'ombe 1,200 hadi 1,500 ukihesabu kwa mwaka tangu 2006 mpaka sasa 2008 unaweza ukajua ng'ombe walizaliwa wangapi. Ukizidisha kwa ng'ombe wote walioko kwenye ranchi ambao 41,000 kila siku tangu miaka hiyo, unaweza ukajua walizalishwa ng'ombe maelfu mangapi na ndiyo maana katika mwaka huu tutachukua hatua ya kuhesabu ng'ombe wote walioko katika ranchi zote ili tuweze kuwahakiki kusudi hawa ng'ombe wasiwe wanafanyishwa kazi na watu wengine na kujitajirisha kwa ajili ya ng'ombe za ranchi za Taifa. Lakini hizi ndizo *challenges* tulizonazo.

Lakini *challenge* nyingine unakuta palikuwa na ranchi zilizokamilishwa zaidi ya 124 pamoja na viwanda vinavyohusu mifugo. Katika ranchi hizi zote 124 ambazo zilipewa na wawekezaji mbalimbali kwa ajili ya kushughulikia masuala ya mifugo ni chache sana ambazo zimeendelezwa. Zipo nyingine zaidi ya 38 ambazo hata ng'ombe mmoja hazina na wamepewa. Lakini zipo nyingine hasa kwa upande wa sehemu za Kagera, hizo ranchi walizopewa, hizo *sublease* wanazitumia kukodisha watu wengine wakiwepo hata watu wa nchi za nje kwa kulipa ng'ombe mmoja Sh. 50,000/= kwa malisho kwenye haya maeneo yetu na ndiyo maana tumejikuta nchi yetu ni kama shamba la bibi, kila siku ukienda kusini kuna bibi, ukienda kushoto kuna bibi, nyuma ni bibi ni mabibi tu wamejaa katika kila sekta.

Kwa hiyo, hii ndiyo *challenge* tuliyonayo katika Wizara yetu na ndiyo maana nasema michango ya Waheshimiwa Wabunge imetusaidia sana.

Lakini mbali ya hiyo unakuta mifugo mingi iliyouzwa nje katika mwaka mzima iliingiza shilingi bilioni 1.8 tu pamoja na ng'ombe hawa wote, mbuzi hawa wote na tani za minofu ya nyama iliyouzwa nje ni tani 195 tu ambayo iliingiza milioni 500 tu, sasa unaweza ukajiuliza hii ndiyo Wizara umekabidhiwa, bajeti yenyewe ndogo, changamoto

ni hizi zote na ndiyo maana tunasema tutafanya, kwa sababu nilisema kwamba unaweza ukapewa hata paja, lakini ukashindwa kulitumia vizuri likakuozea lakini ukapewa hata kakidole ukakitumia vizuri watu wakafanya kazi.

Mimi nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Naibu Spika Wizara itafanya kazi na watu watafanya. Wale watakaoshindwa kufanya wataondoka na tutachukua hatua za kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata ukiangalia katika mazao ya samaki, nimetaja kwamba tuna maziwa zaidi ya 21, tuna mito, tuna bahari, lakini unaweza ukakuta katika tani nzima katika mwaka mzima zinazozalishwa ni tani 328 zenye thamani ya shilingi bilioni 327, hii inasikitisha na hizo ni zile zilizozalishwa, zile zilizouzwa nje ni tani 57,000 tu ambazo ziliingizia nchi bilioni 7.6. Pamoja na mito hii yote, pamoja na maziwa haya yote pamoja na bahari hii yote, lakini wananchi wanaovua kwenye maziwa yetu na kwenye maji yetu ni zaidi ya 163,000 na wana vyombo zaidi ya 51,000 na maboti kibao lakini unakuta katika sekta hii fedha zinazoingia ni kutoka Ziwa *Victoria* ambapo zaidi ya shilingi bilioni 224 ndiko zimepatikana. Pamoja na kwamba ukubwa wa Ziwa *Victoria* ni kilomita za mraba 33,088 wakati bahari ina kilomita za mraba kwenye *EEC* zaidi ya 223,000 *square kilometre* na wamezalisha shilingi milioni 981 kwa mwaka mzima.

Kwa hiyo, unaweza ukaona hii ni *challenge*, lakini wavuvi wamo na wa nje wamo na ndiyo maana nimetoa wito kuanzia mwaka huu, tunafuta leseni zote za meli 69 na wale waliokuwa wanaiba kwenye bahari yetu ili kwanza tuanze kujipanga upya ili sekta ya uvuvi katika bahari yetu iweze kuchangia kwa sababu tumechoka.

Sehemu nyingine kwa mfano kama Namibia asilimia 23 ya uchumi wake unatokana na uvuvi na inafuata baada ya madini, lakini sisi sekta ya uvuvi inachangia kwa asilimia 4.8 na inachangia kwenye ukuaji wa pato la Taifa kwa asilimia 1.6, wakati sekta ya mifugo inachangia kwa asilimia 2.4 na inachangia kwenye ukuaji wa pato la Taifa kwa asilimia 4.7 wakati ni wa tatu katika Afrika kwa kuwa na mifugo mingi, tuna maziwa karibu kila mahali kuliko nchi ya Uganda, Kenya na kadhalika. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema *challenge* tulizopewa na Waheshimiwa Wabunge nimezipokea kwa mikono yote, tutazifanyia kazi ili kuhakikisha sasa sekta hii ya uvuvi na mifugo inabadilika ili iweze kuchangia kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati unakutana na *challenge*, kama hivi unakuta Wizara hii ina upungufu wa Maafisa Ugani, ina Maafisa Ugani 2,500 tu katika nchi nzima, wakati wanaotakiwa ni zaidi ya 13,500, unafanyaje kazi? Unawahamasishaje wananchi? Ndiyo maana katika mwaka huu na mwaka uliopita tumeanza kujipanga, sasa kwa kutumia Vyuo vya Mifugo na Uvuvi kuanza ku-*train* Maafisa Ugani.

Katika bajeti ya mwaka huu kuna zaidi ya shilingi milioni 720 ambapo tutaanza ku-*train* Maafisa Ugani wanaohusika na mifugo zaidi ya 1,185 na wanaohusika na uvuvi zaidi ya 120 na mwaka jana tuli-*train* watu 1,006 ambao sasa watamaliza katika mwaka huu. Ninajua katika kupanga hizi taratibu itaweza kutusaidia kuanza kupunguza Maafisa

Ugani ambao tunaweza tukawagawanya katika kila Mkoa na kusaidia na kufanya kazi kwa pamoja.

Lakini tatizo lingine unakuta Wizara hiyo hiyo unayo-*deal* nayo hata una mifugo mingi lakini hamna viwanda na ndiyo maana wafugaji wengi wamekuwa wakitoka mahali fulani kwenda mahali fulani. Tumeanza sasa kulaumiana sisi wenyewe ni kama senene ukiwashika kwenye kibuyu huwa hata wanaanza kujiuma wenyewe wakati kumbe wangeanza kutafuta sababu za kuweza kujiokoa na ndiyo maana uliona katika michango hii mkulima anamlaumu mfugaji, mfugaji anamlaumu mkulima, mvuvi anamlaumu na kadhalika. Ni kwa sababu hatujapanga mikakati mizuri ya kuweza kutusaidia. Lakini unajikuta katika Wizara hiyo hiyo hata ulaji wa mazao yanayotokana na mifugo, yako chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulaji wa nyama wa Watanzania ni kilo 11 kwa kila mtu kwa mwaka wakati *FAO* wanasema tule kilo 50 za nyama, unawasaidiaje hawa Watanzania? Hata nyama wanaogopa kula! Hiyo ni *challenge* katika Wizara hii. Lakini unajikuta hata unywaji wa maziwa mwaka huu tumezalisha lita bilioni 1.5 lakini unywaji wa maziwa katika nchi hii ni lita 41 kwa kila mtu kwa mwaka, ukilinganisha na ule unaotakiwa wa lita 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya tunawazidi ng'ombe, lakini wanatuzidi unywaji wa maziwa. Malawi tunawazidi ng'ombe lakini wanatuzidi unywaji wa maziwa. *Egypt* wana ng'ombe wachache tu, lakini wanakunywa lita 99 kwa kila mtu kwa mwaka. Sisi lita 41 kwa kila mmoja. Ukienda kule kwao alikotoka Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Pinda tulipokuwa kule, Wafipa wanakunywa lita 8.1 kwa kila mmoja kwa mwaka, kwa maana nyingine ni kama kila Mfipa anakunywa kijiko kimoja kimoja cha maziwa kwa mwaka pamoja na kuwa na ng'ombe wengi. Hii ndiyo *challenge* ya Wizara, lakini tuna maziwa mengi, tuna bahari na mito na ulaji wa samaki ukoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ulaji wa samaki ni kilo 6.9 kwa kila mtu kwa mwaka wakati tunatakiwa tule kilo 10.96 kwa kila mmoja. Mwaka jana tulipata mayai bilioni 2.96, lakini ulaji wa mayai nao uko chini. Kila mtu anakula mayai 64 kwa mwaka wakati tunatakiwa tule mayai 300 kila mmoja kwa mwaka.

Kwa hiyo, nafikiri siku moja ije itokee tupange mayai pale nje kila Mbunge anatoka pale analazimishwa kula yai ili kusudi iwe changamoto kwa Watanzania wote kwamba mayai yanahitajika, maziwa yanahitajika, nyama zinahitajika ili kusudi tuweze kutengeneza soko la mazao ambayo ni muhimu sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati unakutana na changamoto hizi, unakuta mazao yaliyoko baharini nayo yanapungua. Kwa sasa hivi kwa utafiti uliofanywa na *TAFIRI* ambapo *TAFIRI* ni chombo cha Taifa chenye wataalamu wengi sana wamegundua kwamba sangara kwa sababu ya *overfishing* kwa sasa hivi wamepungua, wametoka kwenye tani 750,000 hadi kwenye mwezi Februari, 2008 palikuwa na tani 375 tu katika Ziwa Victoria. Kwa maana nyingine, tukiendelea hivyo tutajikuta sangara watakuwa hawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi *prawns* ambazo wanaitwa kambamiti kwa wenzetu wa ukanda wa bahari wamepungua kutoka tani 1,300 hadi tani 202 na ndiyo maana palikuwepo na meli za kigeni 10 ambazo zilikuwa zinavua, nazo tumezipiga marufuku, hakuna kuvua. Tunawaachia wananchi tu wa kawaida wao ndio wataendelea kuvua ili kusudi waendelee kuzalisha hii mali na kuuza, lakini meli za kigeni na za wapi zote tunazifutilia mbali. *(Makofi)*

Lakini kutokana na utafiti huo, tumejikuta kidogo dagaa wameanza kuongezeka kwa mfano katika Ziwa Victoria kutoka tani milioni 1.1 hadi milioni 1.3 na furu ambao walikuwa wanazungumzwa na Mheshimiwa Ernest Mabina nao wameongezeka na samaki wengine gogogo na kadhalika wameanza kuongezeka hadi kufikia tani 775. Hii ni kutokana na hatua ambazo tumekuwa tukizichukua ikiwa ni pamoja na kuharibu zana haramu ambazo zinatumika kwa ajili ya uvuvi.

Katika mwaka uliopita tumeharibu zaidi ya mitego 150,000 ambayo ilikuwa inatumika kwa ajili ya uvuvi haramu na kupeleka watu Mahakamani zaidi ya 614 na wengine wamefungwa akiwemo Mwenyekiti wa CCM kule Musoma pamoja na mtu mwingine kutoka nje alifungwa miaka nane kwa sababu uharibifu hauna chama, uwe *CUF*, CCM, CHADEMA utashtakiwa tu kwa mujibu wa Sheria Na. 22 ya mwaka 2003.

Kwa taratibu tunazozifanya sasa hivi tunapokwenda kusaka, tunakwenda moja kwa moja na Hakimu anayeshikwa pale anasomewa mashtaka hapo hapo, kama ni kufungwa anapakiwa hapo hapo na kwenda kufungwa ili kusudi tuweze kulinda rasilimali hii ya uvuvi katika nchi yetu. Bila hivyo itafika siku moja tutajikuta hatuna hii rasilimali. Kwa hiyo, ningewaomba sana Waheshimiwa Wabunge mtusaidie katika hili, tuwaendeleze wananchi wetu kwa kutumia zana ambazo zinakubalika lakini kwa kuzingatia pia sheria ambazo tumezipitisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilijaribu kuangalia katika *arguments* ambazo zilikuwa zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, wengine wanasema wapunguze ng’ombe, wengine wapunguze nini na kadhalika. Lakini kama nilivyosema, kwa ujumla michango yote ilikuwa mizuri.

Lakini nilijaribu kupiga hesabu ya haraka haraka, mwaka jana palizalishwa tani 410,000 za nyama ikiwa ni pamoja na nyama ya ng’ombe, mbuzi, kondoo na kuku ambayo ilikuwa tani zaidi ya 77,000. Sasa tu-*assume* kwamba hizo tani 410,000 ambazo zilizozalishwa mwaka jana tusingekuwa na hayo mazao. Kwa maana nyingine tukaangalia kwenye *Supermarket* Dar es Salaam kilo moja ya nyama inauzwa shilingi ngapi? Tukajikuta ni kama Sh. 10,000/= ukizidisha tani 410,000 mara 1,000 ili upate kilo na uzidishe mara 10,000 maana yake ni trilioni 4.1. Kwa hiyo, tusingekuwa na mazao haya ya mifugo. Mwaka jana ilibidi Serikali iagize mazao ya nyama pamoja na kwamba sisi sio walaji sana wa nyama lakini tungetumia trilioni 4.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikapiga hesabu ya mayai yaliyozalishwa bilioni 2.69 na mwaka huu tutazalisha mayai bilioni tatu, uzidishe kila yai linavyouzwa labda

Sh. 200/= ukajikuta ni karibu trilioni 0.5 zinahitajika. Bado hujahesabu minofu ya samaki ambao ilizalishwa zaidi ya tani 328,000 nazo uzidishe kwamba angalau kilo moja ya mnofu wa samaki unaiuza kwa shillingi 1,000 tu.

Lakini katika mwaka huo huo 2007, mazao ya ngozi, zilizalishwa zaidi ya ngozi karibu milioni sita. Ngozi milioni 2.5 zilikuwa za ng'ombe, ngozi milioni 1.9 zilikuwa za mbuzi, ngozi milioni 1.5 zilikuwa za kondoo na zile zote zilipokusanywa zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 13.5. Lakini zilipouzwa nje zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 41.5. Sasa uzijumlishe hizi kama ungekuwa unanunua kila ngozi Sh. 5,000/= tu ungejikuta unatumia trilioni tatu.

Sasa ukijumlisha haya mazao kama ingebidi tuyanunue nje ikiwa ni pamoja na maziwa, nyama, mayai, samaki maana yake tungetumia zaidi ya trilioni 10. Bado hujaweka wanyamakazi ambao wanatumika kule Kalambo, bado hujaweka punda na sungura wengine, bado hujaweka *employment opportunities* ambayo uvuvi kwa mfano imeajiri watu zaidi ya milioni nne, bado hujaweka samadi ambayo unaweka kwenye mashamba wala hawahitaji *phosphate of ammonia* na kadhalika. Ukijumlisha gharama hii yote unaweza ukajikuta Serikali labda ingekuwa inatumia karibu trilioni 20 kwa kila mwaka. Nikaangalia bajeti ya Wizara zetu hapa ni trilioni saba tu, tungeweza kama tungekuwa hatuna mifugo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawapongeza hata waliosema kwamba wafugaji nao ni wawekezaji kama wawekezaji wa migodi. Wavuvi nao ni wawekezaji, hawa wote wawekezaji tunatakiwa tuwalinde katika kulinda rasilimali yetu. Kitu kinachotakiwa ni kuweka *infrastructure* nzuri zitakazowasaidia hawa wawekezaji wa uvuvi na kuchunga ng'ombe. Tukijenga viwanda vingi, kwa vyote, wananchi hawa watashindwa kuzurura kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine. Kwa hiyo, watatumia mifugo yao katika kuuza na kujitajirisha. Ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu tutajenga viwanda vitatu vya nyama Ruvu, Arusha na sehemu ya Kyaka kule Kagera.

Lakini pia kuna viwanda vingine vya watu binafsi ambavyo viko Sumbawanga na kingine kiko Shinyanga SSS na kingine kiko Morogoro. Lakini pia tutatangaza viwanda vingine vya nyama kule Mwanza pamoja na Mbeya. Tutaendelea katika njia hii na njia ya kuhamasisha hata watu binafsi wajenge viwanda vingi, wajenge machinjio ya kisasa kama haya ya Dodoma ili watu wale nyama hata wale ambao wanapata *allegic* na nyama wale, wale mpaka ile *allegy* ipotee ili kusudi zao la nyama liweze kuleta faida na wale hata walio *allegic* na samaki nao waendelee kula.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya muda ni mdogo sana. Lakini kwa ujumla tu sekta hii ina changamoto nyingi na sisi tumezipokea na ndiyo maana katika ujumla wake.

**NAIBU SPIKA:** Muda uliosoma majina hatuuhesabu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Aah! Muda niliosoma majina hauhesabiwi, basi ni vizuri sana Mheshimiwa Naibu Spika. Yes! Baada ya kuniongezea muda huo, sasa niendelee kutoa uchambuzi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Wizara hii ina changamoto kubwa. Nilipokuwa nikizungumza kuhusu bajeti iliyokuwa Wizara ya Mifugo mwaka jana ilitengewa shilingi bilioni 22.3 hivi na iliyokuwa sekta ya uvuvi mwaka jana ilitengewa shilingi bilioni 25.8 hivi ukizijumlisha zote ni karibu shilingi bilioni 47. Mwaka huu tuna shilingi bilioni 41.

Kwa hiyo, kwa maana nyingine Wizara yetu sisi bajeti imeshuka. Lakini kwa sababu ni mtoto mdogo anayeanza ndiyo maana napenda kuahidi kabisa Waheshimiwa Wabunge tutaitumia hii *resources* ndogo tuliyonayo, tutaleta *changes* mpaka mtashangaa, mwaka kesho ndipo mtuulize. Lakini ninajua wakati tutakapokuwa tunatekeleza haya, wako wengine watakuja kuwalalamikia. Wako wengine watalia na kwa kweli unapotaka kutoboa jipu litoboe tu hata kama watalia lakini mtu apone. Lakini wapo wengine watakuja ku-*complain* hata kwenu Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, ninachowaomba, mtu-*support*, mtupe nguvu, sisi tuko hapa kwa ajili ya kufanya kazi na nataka kuwaahidi kwamba tutatumia sheria zote zilizoko. Kwanza tutatumia Sera ya Mifugo ya mwaka 2006, tutatumia Sera ya Uvuvi ya mwaka 1997, tutatumia Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 pamoja na *regulations* zake za mwaka 2005, tutatumia Sheria ya *Veterinary* Na.16 ya mwaka 2003, tutatumia Sheria Na. 17 ya Magonjwa ya Mifugo ya mwaka 2003, tutatumia Sheria Na. 8 ya mwaka 2004 ya Maziwa, tutatumia Sheria Na.10 ya mwaka 2006 ya Nyama, tutatumia hata sheria ambayo imeanzishwa hivi karibuni ya mwaka 2007 iliyoanzisha *Deep Sea Authority* ili kusudi tuweze kuvuna kwa pamoja kati ya Serikali ya Zanzibar na Tanzania Bara hii mali inayopatikana katika bahari ya Hindi na imeanzishwa na *government notice*, imeshatangazwa na Mheshimiwa Rais ameshasaini.

Kwa hiyo, tutaanzisha kwa pamoja ushirikiano huu na hii itatusaidia katika kuzuia hata wizi unaofanyika kwenye Bahari ya Hindi. Pamoja na sheria nyingine, lakini pia tutaendelea kuzitumia hizi sheria kwa mfano *Land Planning Act* No. 6 ya mwaka 2007 ambao tuliileta hapa wakati nikiwa Wizara ya Ardhi kwa kupanga matumizi bora ya ardhi na hii inasaidia ku-*harmonise* uadui na ugomvi unaotokea kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sheria nyingine Sheria Na.4 ya mwaka 1999 na Sheria Na.5 ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999. Pamoja na sheria nyingine ambazo tutazileta, kwa mfano ya Ustawi wa Wanyama ambao nina uhakika inaweza ikaletwa katika bajeti ya mwaka huu na kadhalika, lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba sekta hii ya uvuvi angalau kama haitaweza kushindana na sekta ya madini, basi ishindane na sekta nyingine hata iwe ya kwanza. Kwa sababu ninafahamu tukitumia vizuri mifugo yetu tukatumia vizuri rasilimali yetu ya uvuvi, samaki tulionao tukatumia mwani, kwa mfano mwaka jana wamezalisha tani 411 tu wakati mwani inaweza ikatumika na inaajiri akinamama wengi wa ukanda wa Pwani na kadhalika. Ninaamini tunaweza tukaleta mabadiliko katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa ufupi nianze tu kujibu haraka haraka baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati kwanza amepongeza na wametoa changamoto nyingi tu ikiwa ni pamoja na kodi, *TAFICO* ifufuliwe na mimi napenda kumuahidi kwamba kwa sasa hivi tutaitumia kwa mfano ile *Landing Site* ya *TAFICO* kwa ajili ya wavuvi wadogo wadogo katika maeneo ya Pwani. Kwa sababu chini ya *PSRC* imesharudishwa kwetu, kwa sasa hivi tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili kusudi ile *TAFICO* iwe ndiyo *Landing Site.* Meli zote zinazotoka kule kuja kuvua hapa ziwe zina-*declare* samaki zimevua kiasi gani, zinapimwa na watu wetu wawe wanatumwa, wakiwa wanakwenda kuvua kule kama *observers* na hii itatusaidia inawezekana kutokuibiwa sana rasimali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tutaangalia suala la kodi ambayo tunaitoza kwa sababu sisi hapa tunatoza kwa dola 18,000 wakati wenzetu Sheli Sheli wanatoza zaidi ya 20,000 na hii ni kutokana na kwamba wao wamejiunga na *European Union* katika uvuvi. Lakini nchi nyingine kwa mfano kama Kenya ni 15,000, *Mozambique* ni 15,000 na kadhalika. Lakini hili lote tutaliangalia katika kuhakikisha pato la samaki na uvuvi kwa ujumla linaleta mchango mkubwa. Kwa hiyo, kwa ujumla tu changamoto zilizotolewa na Kamati inayohusika na sekta hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ninazikubali zote na tutazifanyia kazi na tunawashukuru sana kwa ushauri wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jecha ambaye amezungumza kuhusu Kambi ya Upinzani, ni Waziri Kivuli wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza, ametoa pongezi na mimi nimeshukuru kwa sababu kama Upinzani unaweza ukatoa pongezi hii inaonyesha kwamba ni kwa namna gani sera na Ilani za Chama cha Mapinduzi zinatekelezwa. Kwa hiyo, ni matumaini yangu Mheshimiwa Jecha siku nyingine anaweza akatuunga huku katika kutekeleza na kulisukuma hili gurudumu la maendeleo. Lakini nashukuru kwa changamoto zake. Mheshimiwa Jecha bahati nzuri ni Mjumbe katika Kamati na huwa anatoa michango yake mizuri sana kwa niaba ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru na karibu yote tu amepongeza na ndiyo maana nasema leo sina chochote cha kumweleza, ninawashukuru na waendelee kupongeza hivi hivi kwa sababu mwendo huu ni mzuri. Hii itafika wakati fulani tuwe na Chama kimoja tu cha CCM humu, kwa sababu tunatekeleza yale yale ambayo tunatakiwa kuyatekeleza. Kwa hiyo, nampongeza sana aendelee hivyo hivyo na mwaka kesho apongeze na changamoto hizi ni nzuri na kwa sababu ukweli wananchi wana *interest* ya kutaka kupatikana mabadiliko ya kweli, hivi vyama tu ndiyo ni vizuri, lakini wananchi wanataka mabadiliko ya kweli. Kwa hiyo, kama mabadiliko ya kweli yanaweza yakaletwa na chama kimoja kama CCM hivi na Mheshimiwa Jecha wa *CUF* akatupongeza, mimi namshukuru sana Mheshimiwa Jecha. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Selelii naye ametoa changamoto kubwa na hasa katika suala la kusema ukweli. Mimi Mheshimiwa Selelii naku-*support* kwa kweli kwa sababu hata watu wanasema msemakweli ni mpenzi wa Mungu. Siku zote tukizungumza ukweli mambo yetu yatakwenda na ukificha ukweli saa nyingine yanakuwa mabaya. Kwa hiyo, nakupongeza Mheshimiwa Selelii, endelea kusema ukweli

na sisi tunakuombea na wapiga kura wako nafikiri wanakusikia, mwendelee kusema ukweli. Ukweli hata ukienda Mbinguni wewe sema ukweli, ukienda motoni utasema nilifanya dhambi, unasema ukweli; ukienda kwa Malaika kule unasema ukweli. Kwa hiyo, ukweli ni kitu kizuri.

Lakini Mheshimiwa Selelii amezungumzia kuhusu changamoto ya mifugo kwamba mifugo haina Benki. Ni kweli hakuna Benki, lakini mfugaji hakuzuiwa kutumia Benki zilizopo katika kukopa, hata fedha za JK hawakuzuiwa wafugaji kukopa. Wapo waliokopa kwenye fedha hizi na bado wakaenda kununua ng'ombe. Lakini ni kweli katika siku zinazokuja nafikiri ni vizuri pakawepo na Benki itakayohusu wafugaji tu au wavuvi tu na kadhalika. Kwa hiyo, hizi nazo ni changamoto. Lakini pia amezungumzia juu ya matatizo ya miundombinu, malambo, majosho na madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya majosho na malambo kupitia mradi wa *DADP's* ambao unasimamiwa na TAMISEMI na Wizara ya Kilimo, katika bajeti ya mwaka huu kuna shilingi bilioni zaidi ya 53 ambazo zimetengwa na katika fedha hizo zaidi ya bilioni 15 zitahusika na masuala ya malambo, chanjo pamoja na madawa.

Kwa hiyo, fedha hizi nisingeweza kuziweka huku kwa sababu sasa hivi tunarudisha madaraka kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, wito wangu ni kutoka kwenu Wabunge kwamba wakati tunapopanga mikakati na miradi mbalimbali katika Halmashauri zetu, basi tuhakikishe kwamba katika Halmashauri zetu hii miradi ambayo imepangwa kwa ajili ya malambo na majosho na kadhalika basi itumike kikamilifu katika kuhakikisha kwamba huduma hii muhimu inapatikana.

Mheshimiwa Selelii amezungumzia pia Viwanda vya Nyama na Ngozi kwamba havipo na kadhalika. Amezungumzia sensa, wafugaji wanafukuzwa ovyo ovyo. Ripoti ya Tume haijaletwa, kuna nini na kadhalika? Mimi nafikiri katika suala la Tume kwa sababu ile ilikuwa ni Tume ya Mheshimiwa Rais na bahati nzuri Mheshimiwa Rais alipokuwa akiunda hii Tume hakuombwa na mtu yeyote, ni yeye mwenyewe aliamua kuunda Tume na Rais wetu ni msikivu na ni mchapakazi na anawapenda wananchi wake wakiwemo wafugaji.

Ningewaomba Waheshimiwa Wabunge tumpe nafasi Mheshimiwa Rais, yeye anajua anachofanya na hiyo Tume aliyoiunda. Kwa sababu ile Tume iliundwa, kwanza haikuundwa na Waziri, ni Tume ya Rais. Sasa tumwaache Rais na hiyo Tume, inawezekana katika ushauri uliotolewa kule ndiyo maana hata sasa hivi kuna Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na kadhalika.

Kwa hiyo, tumuache Mheshimiwa Rais afanyie kazi maoni yaliyoko kwenye Tume kwa sababu hakushinikizwa na mtu yoyote kuunda Tume na Mheshimiwa Rais ana busara zake, anafahamu na anawapenda sana wafugaji na ndiyo maana hata katika bajeti ya hii kuna zaidi ya shilingi bilioni 1.4 ambazo zitahusika kwa ajili ya ruzuku ya madawa kwa ajili ya wafugaji. Ninaamini kwa njia moja au nyingine, wafugaji na wengine watazingatiwa kikamilifu. Lakini tuiache hii Tume Rais atatoa matokeo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri Mheshimiwa Selelii na wengine wote wa Kambi ya Upinzani hawanitakii mema. Kwanza Tume ilipokuwa ikiundwa mimi sikuwepo Wizara ya Mifugo, halafu niende nikamwulize Mheshimiwa Rais: "Mheshimiwa Rais leta ile ripoti ya Tume." Mnataka nifanyeje? Nifukuzwe! Nenda wewe mwenyewe ukamwulize kama unataka! Lakini naamini Mheshimiwa Rais atatumia nafasi yake katika kutatua matatizo haya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Lubeleje ametoa pongezi nyingi sana kwa sekta ya mifugo, lakini pia amezungumzia juu ya Taasisi ya Mifugo Mpwapwa. Mheshimiwa Lubeleje nataka kukuhakikishia kwamba Taasisi ya Mifugo Mpwapwa, najua unaitetea sana. Mwaka huu tumewaongezea fedha nyingi sana ikiwa ni pamoja na za kununulia magari kusudi wafanye utafiti wa kweli na Taasisi hii imefanya kazi nzuri sana katika nchi hii, imetafiti juu ya kuku, mbuzi, mifugo mbalimbali. Kwa hiyo, kwa mwaka huu tumewaongezea hela pamoja na tafiti na Taasisi ya Utafiti ya *TAFIRI* pamoja na ya Temeke pamoja na *branches* zake zote zilizoko katika nchi hii.

Amezungumzia pia juu ya uhamisho wa kituo kwamba, kinahamishiwa Dodoma. Nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Lubeleje kwamba, hiki kituo hakihamishwi Mpwapwa. Dodoma ipo kwa wagogo na Mpwapwa ipo kwa wagogo, kwa hiyo, kinabaki pale pale Mpwapwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichofanyika pale ilitafutwa *plot* moja kwa ajili ya kuweka kituo kidogo kwa ajili ya kuangalia na kudhibiti hasa baada ya kujengwa machinjio ya kisasa hapa Dodoma, lakini haihusiki zaidi na kuhamisha kituo au vituo vya utafiti vilivyoko Mpwapwa. Vituo vya Utafiti Mpwapwa vitaendelea kuwepo. Mimi nakupongeza sana Mheshimiwa Lubeleje kwa kufuatilia, endelea hivyo na nina uhakika nitawashangaa sana watu wa kituo hiki, wakikunyima kura tena katika miaka mingine inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Benedicto Ole Nangoro, ametoa pongezi kwa Wizara, ameelezea mambo mengi, pamoja na kero zinazowahusu wafugaji na kwamba, Wizara ishirikiane na Wizara ya Ardhi kwa kuwapatia wafugaji, ardhi ya kutosha na hili tumelifanya. Mheshimiwa Naibu Waziri, ameeleza hapa kwamba, mwaka 2007 tumepima zaidi ya hekta 930,000 katika Mikoa kumi, Wilaya 24 na Vijiji 155 katika nchi hii. Kazi hii itaendelea katika kuhakikisha kwamba, wananchi hawa wafugaji wanapatiwa maeneo na wao waishi kwa amani lakini kwa kushirikiana pia na wafugaji na kuendelea na wengine.

Suala la magonjwa amelizungumzia pia lakini nimelieleza. Tutaendelea kulidhibiti na utaona katika mwaka huu tumeongeza dozi. Hata katika dozi za magonjwa ya kuku, mwaka huu tutatengeneza zaidi ya dozi milioni 30, ukilinganisha na dozi milioni 24 zilizotayarishwa mwaka 2007 na kadhalika. Kuhusu Maafisa Ugani, umelizungumza nalo nimelieleza katika masuala ya ujumla. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ole-Nangoro tunakubaliana na ushauri wako, lakini pia tunachukua kama changamoto katika Bajeti zinazokuja; ni kwa namna gani tunaweza kuiboresha Sekta hii ya Mifugo na Sekta ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa ujumla.

Mheshimiwa Bujiku Sakila, ametoa pongezi nyingi, amezungumzia juu ya Ranchi ya Mwabuki. Nataka kumhakikishia kwamba, Ranchi ya Mwabuki inatoa pia mafunzo kwa wafugaji wadogo wadogo katika maeneo hayo na katika Bejeti ya Mwaka huu tumeiongezea fedha. Mwaka 2007, ilitoa mafunzo kwa wanavijiji zaidi ya 385. Kwa hiyo, ninaamini hizi Ranchi ambazo zimeachwa kwa ajili ya mfano, lengo lake kubwa pia ni katika kuwaelimisha wananchi na kutoa elimu kwa wafugaji wanaozunguka maeneo hayo, ikiwa ni pamoja na kutoa mazao bora ya mifugo. Yeye amezungumzia pia Operesheni ya Sengasenga ya Ufyekaji wa Miti na mimi nimeshukuru sana kwa elimu hiyo. Amenisaidia kujua kwamba, kumbe Wasukuma hawana tabia ya kukata miti, bali aliyesababisha kuanza kukata miti ni Malkia alipoleta ng'ombe kwenye mwaka 1931 na wakaambiwa wafyeke miti kwa ajili ya kuwafukuza mbung'o. Baada ya hapo sasa, *by induction* wakawa wanakata miti kila mahali wakifikiri kwamba kuna mbung'o. Kwa hiyo, nashukuru kwa mchango huo na amenielimisha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaoishi katika maeneo jirani hawana faida sana na Ranchi hiyo. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Bujiku Sakila kwamba, wananchi watapata faida sana kutokana na Ranchi hizi zitakazoanza. Ranchi ya Malya iligawanywa lakini watu waliopewa sasa hivi wanaikodisha. Tutalifuatilia suala hili katika kuhakikisha kwamba, Ranchi ya Malya pamoja na Ranchi nyingine 38, zinazingatia masharti ya kuuziwa, *otherwise* kama watakuwa wameshindwa kuitekeleza kama inavyotakiwa, tutawanyang'anya na tutawapa watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mauzo mazuri kwa kilo, nami nakubaliana na mazao ya mifugo; Kiwanda cha Ngozi Mwanza kimefikia wapi? Hizi zote ni changamoto na katika mwaka huu tutaleta Sheria ya Ngozi ili kuhakikisha kwamba ni kwa namna gani tunaweza tukazingatia baadhi ya masuala mengine yanayohusu ngozi. Amezungumzia juu ya ufugaji wa samaki kwamba, angependa katika bwawa lake litakalochimbwa hivi karibuni, pawepo na ufugaji wa samaki. Napenda kukubaliana na yeye kwamba, mara bwawa hili litakapokamilika kuchimbwa kwa maeneo uliyoyataja, basi wataalam wangu na mimi mwenyewe, tutakusaidia namna ya kupandikiza samaki mle. Bahati nzuri, mifugo hainywi samaki ingawa bahati mbaya mayai yakikimbilia kwenye mdomo, yanaweza yakamezeka.

Tunataka tufanye mabwawa yote yanayochimbwa kwa ajili ya mifugo pia yahusike katika kufuga samaki, kwa sababu tukiendelea kufuga samaki ndiyo pato la wavuvi nalo litandelea. Kwa mfano, nchi kama Vietnam, kwa sasa duniani ndiyo inasafirisha samaki wengi kwa kutumia mabwawa. Nchi ya China, sasa hivi imechimba mabwawa mengi sana ya samaki aina Tillapia (Sato). Kwa hiyo, nafikiri na sisi ni wajibu wetu sasa kuanza kujipanga, badala ya kuendelea kuvua tu, tutumie *opportunity* za mabwawa ambayo tunayapata katika kupandikiza samaki na tuna vituo vyetu vya kupandikiza vifaranga vya samaki kikiwepo cha Kingorwila kule Morogoro na sehemu nyingine. Tutavitumia vizuri katika kuzalisha vifaranga. Mwaka 2007, tulizalisha vifaranga zaidi ya 603,000. Kwa hiyo, katika mwaka huu tutazalisha vingi zaidi ili tuweze kuwagawia wale wananchi na Wilaya mbalimbali ambazo zitapenda kuanzisha mifano ya kufuga samaki.

Mheshimiwa Ernest Mabina, amezungumzia kuhusu zana zilizopigwa marufuku, kwa nini zisizuwiwe madukani? Hili nakubaliana naye na katika *operations* zetu ambazo tumezianza sasa hivi, tunapofanya *operation* kwa zana haramu katika Maziwa na katika Bahari, pia tunafanya *operation* katika maduka. Muuzaji anaposhikwa akiuza zana ambazo ni haramu katika maduka, anapelekwa mahakamani kwa mujibu wa sheria. Kuna zana fulani zinaitwa *monofilaments;* hizi zimepigwa marufuku duniani kote. Ukimtega samaki hata kama kwa bahati mbaya, ikazama hiyo nyavu ziwani au baharini, samaki wataendelea kutegwa tu na kuuwawa miaka yote dunia nzima na haziozi. Zimekuwa zikiingizwa kwa magendo na nyingine zimekuwa zikitengenezwa nafikiri China na sehemu mbalimbali.

Kwa hiyo, udhibiti utaendelea na hasa kwa kuzingatia kwamba, Sheria hii sasa tunashirikiana na vyombo vya dola, ikiwa ni pamoja na Polisi katika kuhakikisha Sheria zinazingatiwa katika kulinda rasilimali zetu. Ameuliza furu watavuliwaje? Kwa Kisukuma wanaitwa *nchimamuyu.* Uvuvi wa furu haukatazwi lakini kuna taratibu zake za kuvua na ndiyo maana sasa hivi aina ya furu wameendelea kuongezeka. Kwa hiyo, utaendelea kuwavuna hao *nchimamuyu.*

Sangara wadogo wadogo wanaitwa *joa*; sasa kwa nini uvue sangara mdogo halafu umtupe? Katika Sheria za Zanzibar, kwa mfano, Sheria ya mwaka 1988 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 1998, ukimvua samaki ambaye ni mchanga, unatakiwa umrudishe majini. Hivyo ndiyo Sheria inavyosema. Sasa wewe umevua samaki mchanga, bado unambeba unampeleka kumuuza. Kwa hiyo, Kisheria utakapokamatwa ni lazima ushitakiwe kwa mujibu wa Sheria Namba 22 ya mwaka 2003.

Kwa hivi sasa, kwa sababu pamekuwepo na uvuvi pia wa kutumia mabomu na baruti, kila mahali au kila Kata tutakapokuwa tunakamata zana haramu, Maafisa Uvuvi nao watahusishwa kwenye kesi hiyo ili waweze kufungwa. Hii ni kwa sababu tumegundua kwamba, baadhi ya Maafisa Uvuvi wanahusika katika kuchangia uvuvi haramu katika nchi yetu. Ninajua kwa njia hii, pakipatikana Maafisa Uvuvi 60 au 70 na wakafungwa, wataanza kujifunza na kutoa elimu nzuri kwa wananchi, badala ya kuendelea kuwasakama wananchi na kuwaacha Maafisa Uvuvi. Kwa hiyo, tutaanza kuchukua hatua, ikiwa ni pamoja na kupelekwa mahakamani Maafisa Uvuvi kwenye maeneo unapotokea huo uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mikopo itapatikanaje kwa wavuvi wadogo wadogo, wanaomaliza samaki ni viwanda vikubwa na kadhalika. Ni kweli katika viwanda vilivyoko kwa mfano, Ukanda wa Ziwa Victoria, kuna viwanda zaidi ya 12. Tumegundua kwamba, baada ya kupitisha Sheria kwamba, Sangara wanaotakiwa kuvuliwa wasiwe *under slot* zaidi ya sentimita 45; wapo baadhi ya watu ambao si waaminifu, wamekuwa wakisafirisha samaki kwenye maeneo ya nchi nyingine. Katika mwaka huu, tutafanya mkutano chini ya *Lake Victoria Fisheries Organization* na bahati nzuri tumeshapata *Chief Executive* na Mwenyekiti kwa mwaka huu ni mimi mwenyewe. Kwa hiyo, tutawaeleza Mawaziri wenzangu wa Uganda na Kenya katika kuhakikisha kwamba, wanazingatia Sheria. Bahati nzuri kwa hili, katika ziara niliyoifanya Kenya Kisumu, niliwaeleza kuhusu masuala ya kuacha kuvua samaki ambao wapo *under slot.* Nina uhakika katika kikao chetu tutakachokifanya mwezi wa

tisa, tutaiweka hii na tutawahusisha viongozi wetu ili sheria ziweze kutumika katika nchi zote ili samaki hawa (sangara), waweze kulindwa katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia kuhusu masuala ya malambo katika Wilaya ya Geita na bahati nzuri akanisemea na mimi katika Jimbo la Chato, ambako sijawahi kuona lambo katika Wilaya yangu, lakini ndiyo hivyo tunamshukuru Mungu. Mheshimiwa Laizer, yeye ameipongeza Wizara kwamba, hakuna awamu yoyote iliyothamini mifugo, ameanzia Wizara ya Kilimo na Mifugo, akaja Wizara ya Mifugo na Maji, amekuja sasa hivi Wizara ya Mifugo na Uvuvi anasema, bado tunaelekea tu kwenye samaki na hatuthamini mifugo. Mheshimiwa Laizer, ndugu yangu, nataka kukuthibitishia kwamba, Wizara hii itathamini samaki na mifugo. Kwa sababu bahati nzuri hata *combination* ya Wizara tuliyonayo, wapo wafugaji. Naibu Katibu Mkuu ni Mmasai mwenzio, nina uhakika hataweza kuwasahau ng’ombe.  Katibu Mkuu ni mtu wa Musoma, kwa hiyo ni mfugaji na pia ni mvuvi.

Mimi ni mvuvi pia ni mfugaji na nina ng’ombe na wanatoa maziwa kweli, hata ukija kwangu utakunywa maziwa. Kwa hiyo, nataka kukuthibitishia Mheshimiwa Wanyancha, ndiyo mwenyewe sasa pamoja na kwamba, unaweza uka-*cross* kwenda kufanya kazi nyingine ya ng’ombe. Nataka kukuhakikishia kwamba, thamani ya mifugo na uvuvi yote tutaizingatia kwa pamoja na ndiyo maana tumepokea michango yote na hasa kwa sababu hii ni Bajeti ya kwanza ya Wizara mpya na Wizara ina miezi mitatu tu.

Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote wafugaji na wavuvi, sekta hizi zote ziko pamoja. Tutahakikisha tunazijenga kwa pamoja katika kuleta matunda ya kweli na kuleta maendeleo ya kweli katika nchi yetu.  Ndiyo maana mimi sikubaliani na wale wanaosema wapunguze, kwa nini wapunguze?  Wewe una mkono wako halafu uupunguze ubaki na mkono mmoja; kwa nini usiwe na mikono yote!  Kwa hiyo, samaki waongezeke, ng’ombe waongezeke na uchumi upande, hicho ndicho tunachokitaka. Katika ku-*harmonize* watu wote; wakulima, wafugaji na wavuvi ili tuweze kuchangia katika Pato la Taifa kwa kiasi kikubwa sana.  Ndiyo maana nilitoa wito hata wanaoweza kufuga *samaki nchanga* wafuge, wanaoweza kufuga mbwa wafuge, tuwasafirishe nje kwa sababu vyote hivi ni vitoweo.  Kwa hiyo, kila mmoja ajenge mbinu yake ni namna gani tunaweza kuimarisha vitoweo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya watu waliowanyanyasa wafugaji wachukuliwe hatua.  Bajeti ya Wizara hii kweli ni ndogo, dawa za mifugo ni kweli kabisa zinatosha kwa asilimia 12 tu.  Bahati nzuri nimeshamwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu na nimeshalielezea hili suala ni kwa namna gani liweze kutatuliwa na Serikali. Nina uhakika baadae tunaweza kuongezewa fedha ili dawa za mifugo ziweze kufikia asilimia 80 ya kuchanja.  Kwa sababu asilimia 72 ya vifo vinavyotokana na mifugo vinatokana na kupe. Kwa hiyo, tukiweza kuogesha mifugo tutaweza ku-*save* mifugo mingi sana. Kwa hiyo, nakubaliana naye, lakini amechangia mengi kuhusu dawa na kadhalika.

Mheshimiwa Shah, ametoa pongezi nyingi kwa Wizara; ametoa wimbo wa Msondo Ngoma kwamba, *ukiona mtu mzima analia ujue kuna jambo*. Bahati nzuri Mheshimiwa Shah hakulia, kwa hiyo, naona hakuna jambo. Ninakubaliana na changamoto yake na bahati nzuri Mheshimiwa Shah ni Mjumbe wa Bodi ya Maeneo Tengefu katika Wizara yangu na amekuwa akichangia kwa kiasi kikubwa sana katika kutoa ushauri. Mimi nimeshakutana naye na siku moja pia alitoa malalamiko haya mbele ya Rais kwamba, kuna uvuvi mbaya unafanyika kule Mafia. Kwa hiyo ni mdau mzuri, lakini ninachotaka kumweleza yeye na wapigakura wake walioko kule Mafia ni kwamba, lazima tufuate Sheria. Kwenye Jimbo langu nimechoma nyavu. Mimi Kata zangu karibu tano/sita, zipo kandokando ya Ziwa Victoria; Kata za Chato, Mganza Buzilayombo na kadhalika zote zipo Kanda ya Ziwa.

Kwa hiyo na mimi naweza nikanyimwa kura kwa sababu ya kuchoma, lakini wameniambia nitachoma nyavu na kura watanipa kwa sababu ninasimamia Sheria. Sheria Namba 22 ya mwaka 2003; naomba ndugu zangu kama tunataka kulinda rasilimali ya taifa hili, lazima tusimamie Sheria. Bahati nzuri Waraka wa Mkurugenzi, upo chini ya kifungu namba 4(3) cha Sheria Namba 22 ya mwaka 2003. Kifungu hiki kinamruhusu Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi kutoa nyaraka ambazo zitasaidia kuimarisha utekelezaji wa Sheria hii ili kuhakikisha kuwa, rasilimali ya uvuvi inakuwa endelevu. Pia Kanuni ya 14 na 15 (c) zinampa mamlaka ya kuzuia utoaji au kufuta leseni yoyote ya uvuvi. Aidha, Kanuni Namba 17(2)(a), inatoa mamlaka kwa Mkurugenzi wa Uvuvi kuweka masharti juu ya zana na mbinu zinazotumika kwenye uvuvi. Hii Sheria tumeipitisha sisi wenyewe hapa Bungeni; kama mnaona haifai tuitengue, watu wavulie hata mayai na kadhalika; samaki waishe.

Mimi nafikiri ni vizuri tukatekeleza Sheria katika kulinda rasilimali zetu. Kama wapo watu ambao wanapenda kuvua samaki hata wachanga, wakachimbe mabwawa yao, wavue samaki wao hata wakitaka wavue mayai; lakini hii rasilimali ambayo tunaitegemea sote, ambayo tunatakiwa kuiendeleza kwa pamoja; ni vizuri ndugu zangu tulinde Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana mimi nampongeza sana Mheshimiwa Shah, amekuwa akilinda Sheria na ni mtekelezaji mzuri katika mikutano yote tuliyonayo. Yale mengine ambayo ameyazungumza, tutayafanyia kazi na tuone ni kwa namna gani kama kuna uonevu ambao unafanywa kwa makusudi kwa wananchi. Bahati mbaya, wanaotoa leseni hizi ni Halmashauri hazitolewi na Serikali Kuu. Sisi ni wasimamizi wa sera, kwa hiyo, tutaangalia ni kwa namna gani Wavuvi wa Mafia na maeneo mengine, kama kwa njia moja au nyingine, wananyanyasika kutokana na hii. Tutaangalia ni namna gani tunaweza tukaifanyia kazi. Lengo letu ni kuhakikisha wavuvi wadogo wadogo wanavua na wanapata chakula, kwa sababu ime-*emplo*y zaidi ya watu milioni nne.

Ndiyo maana katika Ukanda wa Pwani wote, kuna Mradi ambao tumeuanzisha wa *MACEMP*, ambao una karibu shilingi bilioni 51, inagawa fedha nyingine zitakuwa kwa upande wa Zanzabar na nyingine upande wa Tanzania Bara. Katika mwaka huu; mwezi huu tumesaini mkataba na Halmashauri 16 kutoka Mtwara hadi Tanga, ambazo zipo kando kando mwa bahari ili kuangalia ni kwa namna gani Mradi huu wa *MACEMP*

unaweza kuwasaidia katika kupata zana bora na nzuri za kuvulia na pia tunazingatia Sheria. Wavuvi wa Tanzania hawana Mfuko wowote wa kuwaendeleza. Hili nakubaliana nalo, nafikiri ni changamoto na nafikiri tuangalie ni namna gani tunaweza tukaanzisha Mfuko wa kuweza kuwasaidia wavuvi wetu wakiwepo Wavuvi wa Mafia.

Mengi yaliyozungumzwa hapa ni ya kumbana mwananchi, hapana si ya kumbana mwananchi; lengo letu ni kumwendeleza mwananchi kwa kuzingatia Sheria na ndiyo maana tuliowabana zaidi ni wavuvi wakubwa wanaovua kwenye *EEZ* na wale waliokuwa wanavua *prawns*, wenye meli kubwa wale tumewapiga marufuku, lakini wavuvi wadogo wadogo wataendelea kuvua samaki kwa kuzingatia Sheria zetu.

Hali ya Ukanda wa Pwani inaendelea kuwa na matatizo hasa katika masuala ya nyavu, kufunga meli zote za uvuvi na kadhalika. Ushauri wao tumeuzingatia lakini uvuvi haramu unaanzia Dar es Salaam, hakuna mtu aliyezuwiwa kuvua. Tumeanza kuchukua hatua Tanga na Dar es Salaam. Kweli kuna uvuvi wa kutumia hata baruti, wengine wapo wanachanganya *Sulphate of Ammonia* ili ilipuke zaidi. Ndiyo maana nilitangaza kwamba, tutatumia Jeshi la Wananchi, Jeshi la Polisi, Wananchi, pamoja na *Beach Management Unit* katika kuhakikisha kwamba, tunazuia uvuvi haramu. Kwa mfano, sasa hivi majongoo yamepungua sana na ndiyo maana Sheria hiyo imepiga marufuku. Kamba miti pia wamepungua kutoka tani 1300 hadi tani 202. Kwa hiyo, lazima tuwe na uvuvi endelevu, utakaosaidia wananchi wote.

Mheshimiwa Mudhihir, naye amezungumza mengi kuhusu uvuvi na amenipa elimu nyingi tu ya masuala ya uvuvi. Ninachosema ni kwamba; ni vyema tukazingatia Sheria na katika ufafanuzi ambao nafikiri ninaweza nikautoa kwa Waheshimiwa Wabunge baadae, kwa wanaotoka katika maeneo ya Ukanda wa Pwani nitaelezea *beach sign* zinatakiwaje, kwa mfano *sign net* zinatakiwaje, neti za mtando zinatakiwaje, *ring net* zinatakiwaje na kadhalika. Tatizo linalojitokeza kwa mfano, *ring net* hazizuiliwi, lakini wavuvi hawa wanafanya *modification.* Ikitakiwa kuvua juu ya maji kule, inafungwa nyingine na nyingine mpaka inafika chini ya ardhi. Kwa hiyo, samaki anayetoka kule kwenda kutaga mayai lazima ashikwe na mdogo anayetoka kule lazima ashikwe. Kwa hiyo, mitego au nyavu hizi zinazuiliwa kutokana na mahali unapovulia. Ukiwa na nyavu za dagaa ambazo zinatakiwa kuvulia kwenye maji marefu kwa kutumia karabai, wewe ukachukua nyavu hizo za dagaa ukaenda kuvulia sangara kando kando ya Ziwa, ukishikwa nazo unapelekwa mahakamani.

Ukishikwa baharini unavua na karabai yako wewe ni mvuvi halali. Kwa hiyo, uvuvi wa nyavu hizi unategemea unavulia wapi. Unapovaa *oxygen mask* kule inakusaidia kumfukuza na kumfuata huyu samaki, wewe ukiwa unapumua vizuri na kwenda kumchoma mahali hata akiwa ametaga mayai; nenda hivyo hivyo bila *mask* maji yakuingie puani kusudi ukahangaike kule namna ya kumtafuta. Hilo ndilo tunalotaka, tusipofanya hivi samaki watatoweka na itakuwa ni historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakumbuka Ukanda wa Ziwa kule kweli Chato, kwenye miaka ya 1961 akina mama walikuwa wanakwenda kuchota maji Ziwani, waliweza kuchota na samaki. Siku hizi hata yai la samaki huwezi kulipata, kwa sababu

samaki wamepungua. Kwa hiyo, lazima tuanze kuiendeleza hii Sekta ya Uvuvi katika maeneo yetu na ndiyo maana tumetoa wito mkubwa wa kuanza kufuga samaki. Tutafufua maeneo yote ya kuzalisha vifaranga na nampongeza sana Mheshimiwa Shah, kwa kumhamasisha mtu mmoja ambaye amefuga zaidi ya hekta 1.5 za samaki ambazo zitazalisha zaidi ya dola milioni 8.5. Kuna kiwanda kimeanzishwa huko Mafia na bahati nzuri Mheshimiwa Shah, amefuatilia sana katika kupata kibali cha huyu mfanyabiashara kuanza kuuza *prawns* nje na tumekubaliwa tarehe 1 Agosti, 2008 kwamba, sasa ameruhusiwa kuuza *prawns* wake wa kufuga na kusafirisha *European Union.* Sasa mfano wa Mheshimiwa Shah na Wabunge wengine tunatakiwa tuundeleze hivyo. Hata sisi Wabunge, tuanze kujifunza kufuga samaki, kutengeneza mwani, kufuga ng'ombe, mbuzi, nguruwe, kuku na kadhalika ili tuwe mfano wa kweli katika maeneo yetu.

Kwa hiyo, hili suala la ufafanuzi kuhusu *net* zinazohusika kwa sababu ya muda; Mheshimiwa Shah na Mheshimiwa Mudhihir nitalifafanua. Nashukuru sana Mheshimiwa Mudhihir kwa mchango wako na hasa wafugaji ambao wapo katika sehemu zako. Kwa hiyo, tutayafuatilia na miradi ya majosho na kadhalika itakuwa chini ya *DADPs,* ambapo kuna zaidi ya shilingi bilioni 15 zimetengwa kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, ameelezea masuala yake mengi, napenda kupokea ushauri wake kwa dhati kabisa. Mheshimiwa Bura, amezungumzia masuala mengi na muda umeniishia lakini tunakubaliana nayo. Mheshimiwa Mtulia, amezungumzia uvuvi katika masuala ya Hifadhi ya Taifa, amezungumzia juu ya watu waliouawa na kuhusu malambo. Yote hayo nimeyazingatia. Mheshimiwa Telele, naye ametoa michango mizuri sana inayohusu ufugaji na maeneo; amesema kuna maeneo fulani ambako palikuwa na nyati zaidi ya 200 sasa wamekwisha kwa sababu wafugaji waliwatoa. Mimi nafikiri haya mambo yanatakiwa ku-*harmonise* kati ya wafugaji na Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Msemaji wa Upinzani naye amezungumzia mengi na ameunga mkono na mimi nimempongeza. Mchango wake na changamoto zake tumezikubali. Bahati nzuri mwaka huu katika bajeti hii, Upinzani wote wame-*support,* kwa hiyo, namshukuru sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mlingwa, nakubaliana naye kwa ushauri wake mzuri ambao ameutoa na bahati nzuri Dr. Mlingwa ana uzoefu mkubwa sana na Wizara hii; tunapokea kwa dhati changamoto na ushauri uliotupa. Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, naye ameelezea mengi na changamoto kubwa na lengo la kuanzisha mabwawa na maeneo ya majosho. Tutaendelea kuzungumza na kutumia Miradi hii ya *DADPs* kuhakikisha kwamba, nini kifanyika. Mheshimiwa Manyanya amesema, niende naye huko lakini amesema nitakapokwenda kwenye Ziwa Nyasa ataniacha huko huko. Sasa hicho ndicho nilichoanza kuogopa na hasa aliposema anataka kuanza kuingia kwenye miguu yangu, nikamwambia aingie kwenye koti kabisa lakini changamoto yake naishukuru na katika Ziwa Nyasa tumetoa boti mbili kwa mwaka huu, ambazo nina uhakika zitaweza kuimarisha uvuvi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kitengo cha *TAFIRI* kitafanya kazi katika kutafiti kwenye Ziwa Nyasa ili kuhakikisha kwamba, uvuvi katika Ziwa Nyasa nao unaendelezwa kikamilifu. Mheshimiwa Kingunge Ngombele-Mwiru, naye ametoa pongezi nyingi na ametoa changamoto ni namna gani tunaweza kufanya kazi nzuri katika sekta hii. Mheshimiwa Hewa, naye ameelezea mengi sana na elimu muhimu kwa wafugaji inatakiwa itolewe. Wavuvi nao wanahitaji kuelemishwa na kadhalika. Michango ya Mheshimiwa Hewa, ninaikubali kabisa na tudhibiti mazalio ya samaki hawa wakubwa na tuwabane hasa wanaojenga kando kando ya pwani za bahari na maziwa. Mheshimiwa Lucy Msafiri, amezungumzia kuhusu Muleba na amezungumzia sana kilio chake kuhusu Ranchi yake ya Kagoma. Ninakubaliana na Mheshimiwa Msafiri, lakini katika kujaribu kufuatilia takwimu, tumekuta suala hili limeshaanza kushughulikiwa kikamilifu sana, ikiwa ni pamoja na kugawa baadhi ya maeneo kwa ajili ya wananchi. Kilichojitokeza ni kwamba, tumegundua kuna kesi ambayo imefunguliwa na wananchi wake, wakiishtaki *NARCO.* Sasa baada ya kesi hii kufunguliwa, imekuwa vigumu na imeniwia vigumu ni kwa namna gani naweza nikalishughulikia hili kwa sababu nitakuwa ninaiingilia Mahakama. Kwa hiyo, ningemwomba dada yangu, Mheshimiwa Msafiri, awaombe hawa waliotufungulia kesi katika Mahakama Kuu ya Ardhi, Kitengo cha Ardhi Mahakama Kuu na nimeambiwa ni Ndugu Rutatiza Jonas sijui na nani; kama unaweza ukawashawishi angalau hata wakaifuta hii kesi basi itatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana wote na ninaamini kwamba, kwa maelezo haya mafupi mpaka na muda wangu umeisha, Waheshimiwa Wabunge wote hawatasimama. Wataiunga mkono hoja, hasa kwa kuzingatia kwamba, hata Bajeti yenyewe ni ndogo. Kwa hiyo, mtoto mwenyewe bado hajaanza kutembea unamkata mguu. Watuunge mkono ili tukafanye kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 99 - Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... Sh. 2,254,486,500

**NAIBU SPIKA:** Subirini muandikwe; Mheshimiwa Msafiri, Mheshimiwa Mabina, Mheshimiwa Mhagama, Mheshimiwa Msindai, Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Killimbah, Mheshimiwa Kirigini, Mheshimiwa Mwananzila, Mheshimiwa Dr. Slaa, Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Mwinchoum, Mheshimiwa Jecha, Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, Mheshimiwa Shah, Mheshimiwa Dr. Sigonda na Mheshimiwa Masoud.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote* 99, *Pragramme* ya 10, *Subvote* 101 na kifungu 250100. Kwanza nashukuru kwamba, wakati Mheshimiwa Waziri anaishiwa muda, alikuwa anaielezea hoja yangu ambayo ni ya msingi ya kuweza kumalizia majibu na ndiyo hoja hiyo ambayo inanifanya nisimame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika Ranchi ya Kagoma wapo baadhi ya wananchi waliojitolea kwenda Mahakamani. Pamoja na hao wananchi waliokwenda Mahakamani, wananchi walio wengi pamoja na uongozi wao, wakiongozwa na mimi mwenyewe na Mheshimiwa Diwani na Uongozi wa Serikali za Vijiji na Vitongoji, hatukuwa tunakubaliana kwenda Mahakamani. Tulikuwa tunaendelea kufuatilia katika utaratibu wa kawaida wa Serikali, ambao mpaka sasa hivi wananchi walikuwa wanaendelea kufuatilia kusikiliza Serikali itawajibu nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kukubaliana kwamba, mimi nitajaribu kuwashawishi hawa waweze kuondoa kesi yao Mahakamani, maana si kwa *interest* ya wananchi; wananchi hawapo tayari kuungana nao katika hili kwa sababu wanawachangisha na wapo tayari kuchangia. Vilevile wanashindwa kujua wasikilize waliokwenda Mahakamani ama wamsikilize Mbunge wao. Mimi wananisikiliza na wapo tayari kusikiliza ambacho Serikali itajibu. Ninaomba Serikali iwasikilize hawa wananchi na hii kesi ninaamini itatoka Mahakamani baada ya jibu lako Mheshimiwa Waziri kwamba, wakitoa kesi Mahakamani nini ambalo unaweza ukatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua; Mahakama huwa haingiliwi na ndio maana nimesema kwamba, baada ya kufunguliwa hiyo kesi, imetuwia vigumu ni namna gani tunaweza kulitatua hili tatizo. Sisi katika Wizara, baada ya Mheshimiwa Msafiri kuleta matatizo yake hapa na baada ya kupata ripoti nzuri kutoka kwa Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, ambaye namshukuru sana kwa kazi nzuri ambayo aliianza; tulianza kulifanyia kazi kwamba katika Block Na. 291/1 zilikuwepo jumla ya hekta 30 kwa ajili ya wanavijiji, palikuwa na Block 261/P eneo lote la hekta 2449 lilitolewa kwa wanavijiji, Block Na. 291/7 familia 50 zenye makazi ya kudumu zilitengewa eneo hilo, Block Na. 291/8 zilitengwa hekta 20 kwa wanavijiji na kadhalika. Sasa utekelezaji wake umekwama baada ya kugundua kwamba, kuna kesi Mahakamani. Hatuwezi tukasikiliza kesi, tuwaache waendelee Mahakamani au wakifuta kesi sisi ndio tutafanya kazi hii kwa ajili ya *administration*. Kwa hiyo, ndio maana nilisema, Mheshimiwa Mbunge kama anaweza akawashawishi wakafute kesi Mahakamani, hakuna tatizo. Hatuogopi kupelekwa Mahakamani na inawezekana tukipelekwa Mahakamani, hata hizi Blocks hatutazitoa kwa wanakijiji kwa sababu kule itakuwa ni kupambana sasa mbinu za Mahakamani na sisi tutaangalia. Kwa hiyo, ni chaguo lake Mheshimiwa Msafiri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msafiri unasemaje?

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nirudie yale niliyoyasema kwamba, mimi nikiwa Kiongozi wa Wananchi wale, Mheshimiwa Diwani na Viongozi wao wengine mpaka kwenye Kitongoji, tunakubaliana na maamuzi ya Serikiali na ndio maana nimeendelea kuifuatilia Serikali; ningeshanyamaza nikasema si wamekwenda Mahakamani, ngoja waende Mahakamani. Nilipofanya nao mkutano tarehe 3 Mei, 2008, waliniuliza swali hili hili, nikasema waliokwenda Mahakamani mimi nashindwa kuwazuia, lakini sisi tuendelee kuiambia Serikali tunaiomba ituongezee eneo. Kwa hiyo, tupo pamoja, sisi tunaomba eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kutumia pengine nafasi hii kwamba, waliopeleka kesi Mahakamani waifute, sisi hatupendi kesi, tunataka eneo. Hatuna haja na kesi, tunataka tu kuongezewa eneo.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Wakati nachangia, programu….

**MWENYEKITI:** Endelea tu kwa sababu tunajua ni kamshahara ka Waziri. *(Kicheko)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Wakati nachangia nilikuwa nazungumzia kuhusu malambo na nilimwambia Waziri kwamba, malambo yaliyokuwepo Geita, yamechimbwa miaka mingi ya ukoloni na yalikuwa yanasaidia sana wakulima na wafugaji katika maeneo yale. Baada ya kupata uhuru mwaka 1961, kulikuwa na mvua kubwa sana, ambayo ilisababisha malambo yale yakabomoka, lakini yamekuja kumaliziwa na mvua ya *El-Nino*. Sasa nikamwomba kwamba, angalau atusaidie katika malambo yale kuweza kuyakarabati yarudi katika hali ya kawaida na nilimtajia malambo kama ifuatavyo; kuna Lambo la Isotundwe, Bulela, Kasamwa, Bulegezi, Mbabani, Ndoselo, Nyalugusu, Nyang'hwale na Malambo ya Buzilasoga na Bitoto ambayo yako Sengerema, Lambo la Bwanga na Katende ambayo yapo Chato na ndio maana nikataja kwamba na yeye yanamhusu. Amesema kwamba, pesa hizi zipo katika Mradi wa *DADPS*, lakini ule mradi unachagua na unaweza ukatengeneza malambo mapya.

Mimi nilikuwa nasema kwamba ni ukarabati tu na katika kukarabati yale malambo, kwa sababu ni madogo madogo siyo makubwa sana shilingi milioni 20 zinaweza kutosha malambo hayo 13. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kusaidia malambo haya?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kupitia Sheria Na. 7 iliyopeleka madaraka kwenye Halmashauri zetu, ndio kupitia Mradi wa *DADPS* ambapo nilisema kuna zaidi ya shilingi bilioni 53 zimepelekwa kule kwa ajili ya kushughulikia miradi itakayotekelezwa katika maeneo ya Halmashauri zetu. Kwa hiyo, kitu ambacho ningeweza kutoa wito kwa Mheshimiwa Ernest Mabina, ambaye pia ametaja malambo yaliyoko kwenye Jimbo langu ya Katende, Bwanga na sehemu nyingine, fedha zilizoko ni kupitia Tawala wa Mikoa na Serikali za

Mitaa ambapo katika bajeti ya mwaka huu zimetengwa Sh. 15,131,555,000 katika nchi nzima kwa Wilaya zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni jukumu la Halmashauri kupanga mikakati na kukaa katika Kamati zao za Madiwani na kadhalika, kuona ni namna gani wataweza kuzipata hizi fedha kupitia Tawala wa Mikoa na Serikali za Mitaa. Kupitia Wizara yangu, hakuna hela yoyote iliyotengwa kwa ajili ya malambo, lakini kama panaweza pakabadilishwa Sheria, hizi shilingi bilioni 55 zikarudi tena huku kwetu, mimi nitashangilia sana, tutapanga namna gani tunaweza tukampatia. Zipo kule kwenye Halmashauri, kwa hiyo, zikatumike katika kutengeneza hayo malambo yakiwemo malambo ya Mheshimiwa Ernest Mabina kama alivyoomba. Natoa wito kwa Halmashauri ya Geita, imtengenezee haya malambo kwa sababu Mheshimiwa Mabina, ana ng'ombe wengi katika Wilaya yake ya Geita.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nipo kwenye hiyo *vote* kama inavyosemwa na nisitumie muda zaidi kutaja hayo. Kwanza kabisa, ninaishukuru sana Wizara kwa kutoa kipaumbele katika kile Chuo changu cha LITI Madaba, ambacho kinatoa mafunzo ya Mifugo. Lipo tatizo la msingi ambalo nilishaliwasilisha kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, labda ningependa nipatiwe ufumbuzi; pale Luhila - Songea, Halmashauri ya Wilaya ya Songea ilikuwa inamiliki mabwawa makubwa sana kwa ajili ya kuzalisha vifaranga vya samaki ili kusambaza kwa wafugaji wadogo wadogo wa samaki katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea na Mikoa yote ya Lindi, Mtwara na Mkoa mzima wa Ruvuma. Mabwawa yale sasa Wizara imeyabinafsisha; kuna mtu amepewa ili aweze kuyaendeleza kwa sababu Wizara inadai haina uwezo tena wa kuyaendeleza. Katika Jimbo la Peramiho, tuna mabwawa tena mengine makubwa katika Kijiji cha Lundusi, sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri, kufungwa kwa mabwawa yale ama kupewa yule mtu mabwawa yale ni kuua nguvu za ufugaji wa samaki katika maeneo hayo niliyoyataja.

Sasa kama hivyo ndivyo, basi Wizara itoe fedha kwenye mabwawa yale ya Lundusi, hayo mabwawa mengine yaweze kuendeleza kazi hiyo hiyo ambayo ilikuwa inafanywa na mabwawa ya Luhila, vinginevyo mimi sioni mantiki ya Wizara kuacha kuendelea kutoa fedha ili mabwawa ya Luhila yaendelee kufanya kazi iliyokusudiwa na Serikali. Kwa hiyo, ninaomba mwongozo na ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri; j e, tutashirikiana katika kufanya hilo, ama sasa ndio tunaua ufugaji wa samaki katika Mkoa wa Ruvuma, Jimbo la Peramiho na Halmashauri ya Wilaya ya Songea?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Mhagama, kwa kuonyesha nia nzuri sana ya kuanza ufugaji wa samaki katika eneo lake. Katika *instrument* tuliyopewa na Mheshimiwa Rais, wakati tunakabidhiwa hii Wizara ni pamoja na kuhamasisha ufugaji wa samaki. Kwa sababu suala hili alituandikia, lakini kwa bahati mbaya nisingeweza kujibu yote yaliyoko hapa; Wizara yangu itafuatilia hayo mabwawa, tutaonana na huyo mtu na sheria alizopewa kwa sababu ni yale mambo tuliyoyakuta. Ukweli lengo kubwa ni kuhamasisha ufugaji wa samaki na mabwawa yote yaliyokuwa yanatumika kwa ajili ya ufugaji wa samaki; tutahakikisha tunayafufua na tunayarudisha Serikalini katika kuhakikisha kwamba, vifaranga wa samaki sasa wanapatikana ili

wasaidiwe wafugaji wanaoweza kupandikiza samaki katika mabwawa yao. Kwa hiyo, nakubaliana naye, tutalifuatilia hili. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilipokuwa nachangia nilizungumzia sana juu ya Mkoa wetu wa Singida kuhusu ufugaji wa kuku wa kienyeji. Toka nitoke nimepigiwa simu zaidi ya kumi, wananachi wakitaka wapate majibu ya Serikali jinsi ya kuwasaidia waanze kufuga kisasa kuku hawa hawa wa kienyeji, wapate na dawa ili tuongeze idadi ya kuku na ninyi mnaokaa Mikoa mingine mfaidike kupata kuku wengi zaidi kutoka Singida. Naomba Waziri aniambie, atasaidia nini juu ya ufugaji wa hao kuku?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Hata sisi umetuambia tufuge kuku.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni muda. Waliochangia ni watu 130.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, wewe jibu tu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Ninachotaka kumweleza ni mikakati ya kufuga kuku na ndio maana nimetaja idadi ya kuku wa kienyeji katika nchi hii kwamba, wapo milioni 33 wakiwemo wa Singida. **Ranchi ya Mpapwa** inafanya utafiti mkubwa wa kuendeleza kuku wa kienyeji, ikiwa ni pamoja na kuongezea uzito na kuongeza idadi ya kutaga mayai. Kwa sasa hivi lengo ni kwamba, kuku wa kienyeji wawe wanataga mayai kutoka 45 hadi 145. Kwa hiyo, eneo lake pia litahusishwa katika kufanya hayo yote katika kuendeleza ufugaji wa kuku, lakini pia hata ufugaji wa ng'ombe katika maeneo ya Iramba kwa Mheshimiwa Msindai.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Namwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na majibu yake mazuri, watumishi waliokuwa *TARILO* watalipwa mafao yao wakati watakapokuwa wanastaafu. Sasa kwa kuwa watumishi wengine bado wapo kazini na wengine wamestaafu na ili waweze kufahamu kwamba, mafao yao yatalipwa; je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba, ipo haja sasa ya kuandika Waraka kwa watumishi wote waliokuwa *TARILO* wale waliostaafu na ambao wapo ili waweze kuwa na kumbukumbu kwamba mafao yao yatalipwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kuhusu swali la Mheshimiwa Lubeleje ni kwamba, kuna swali ambalo wameshauliza hapa Bungeni na hilo lilifanya sisi tufuatilie na kujua watu waliokuwepo wangapi wamelipwa na ambao hawajalipwa. Tunayo majina ya ambao hawajalipwa na ambao wamelipwa. Watu ambao hawajalipwa ni ambao bado wapo kazini. Kwa hiyo, kama nilivyosema nilipokuwa naelezea hapa ni kwamba, Wizara yangu inalifahamu hilo na tutafuatilia na mfanyakazi yeyote yule ambaye atapata matatizo, tutamsaidia kwa sababu majina tunayo. Sikuja nayo hapa, lakini siku ya kujibu swali naweza kukupatia. Wale ambao hawajalipwa tunawafahamu, tunaomba uvute tu subira, hilo tunalishughulikia kikamilifu.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimechangia kwa maandishi lakini pia nimechangia kwa kuzungumza. Wakati nimeandika, nilikuwa nimezungumzia kuhusu Ziwa Kitangili. Ziwa Kitangili ni maarufu kwa kuzalisha samaki aina ya Perege, Kamongo na Kambare. Pamoja na kwamba wavuvi wana hali mbaya hasa kiuchumi, namna ya kuweza kukabiliana na shughuli za uvuvi kutokana na kuwa na zana duni na matatizo hasa ya kuvamiwa na wavuvi haramu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004 aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zakia Meghji, aliwahi kufika Kitangili na akajionea hiyo hali. Kwa kuwa Wizara siyo mtu ni taasisi ambayo ipo siku zote na nashukuru sasa imehamishwa ambayo ilikuwa Maliasili imeshaingia kwenye Wizara mpya ya Mifugo na Uvuvi na ninaamini Mkurugenzi wa Uvuvi bado yupo yule yule na wakati ahadi ilikwenda kutolewa na Mheshimiwa Meghji, kuhusiana na kutoa boti, Serikali ilikuwa imeahidi kutoa boti kwa Wavuvi wa Kitangili kwa ajili ya doria. Sasa nataka tu nimuulize Mheshimiwa Waziri, kutokana na jinsi anavyoweza kufuatilia na jinsi anavyoweza kuchapa kazi; je, ile ahadi itatekelezwa ili wananchi wa pale Kitangili waondokane na ile hali ya kuzingirwa na wavuvi haramu?

**MWENYEKITI:** Hiyo ni boti? Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafuatilia nione zile ahadi ambazo zilifanywa na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii ili tuone ni kwa namna gani zinaweza zikatekelezwa na Serikali.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nianze kwa kumpongeza Waziri na Wizara kwa ujumla, kwa mipango mizuri sana ambayo wameipanga katika kuiendeleza Sekta hii ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wasi wasi ni kidogo sana; kuhusu suala zima la sensa. Naona katika mikakati yote iliyopangwa na Wizara katika sekta nzima ya mifugo, inategemea sensa ya mwaka 1984 mpaka sasa miaka kama 24 imepita. Sasa sina hakika kama sensa ile au idadi ile ya mifugo, bado inaendana na hali halisi ya sasa. Kwa mfano, kuna Mikoa ambayo ili-*locate* mifugo mingi zaidi. Sasa sina hakika kama ni Mikoa ile ile bado ina mifugo mingi zaidi mpaka leo hii. Ningependa tu kujua ni kwa nini Wizara haijaona kama suala hili la sensa ni muhimu sana katika kuendeleza sekta nzima ya maendeleo ya mifugo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Kirigini kwamba, suala la sensa ni muhimu. Kama unavyojua, kupanga ni kuchagua; unaweza ukapanga shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kuogesha ng'ombe au ukaamua kuwahesabu halafu usiwahesabu halafu usiwaogeshe wafe wote! Kwa hiyo, sisi tulifikiri kutokana na bajeti hii tuliyokuwa tumepewa ambayo ni ndogo, tukafikiri labda hii shilingi bilioni 1.4 tuliyopewa tuitumie angalau kuogesha ng'ombe, lakini tuitumie pia katika utafiti, katika kusomesha maofisa ugani zaidi ya 1105 na vitu vingine.

Katika bajeti ya mwaka huu pia tutakachokuwa tunafanya kwa sababu sensa kamili ya ng'ombe tunategemea kuifanya kwenye mwaka 2010, hii ni kutokana na hali halisi ya masuala ya sensa yanavyoendana. Kwa sasa hivi tunachokifanya ni ile *sampling* ya sensa kutoka mahali fulani na fulani na hii ni kutokana na kwamba, katika Mikoa yote 21 sasa hivi kuna ng'ombe na tunafahamu kwamba, kuna baadhi ya Wilaya ambazo zina ng'ombe wengi sana; kwa mfano, Maswa ndiyo inaongoza; hapa kwa Mheshimiwa aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Malecela ndio wanafuata katika Tanzania na kadhalika. Kwa hiyo, tunajaribu kuangalia ni kwa namna gani, lakini lengo kubwa ni kutokana na bajeti ndogo, tungepewa hela kwa ajili ya kuhesabu ng'ombe wote, tungeshukuru sana, lakini hiki ni kidogo, kwa hiyo, tunaamua kwanza uanze kula sikio, mkia au pua. Kwa hiyo, hicho ndicho tulichokifanya.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia kuhusu uvuvi unaoendeshwa katika Ziwa Tanganyika. Mheshimiwa Waziri, amezungumzia jinsi samaki wanavyoweza kuiingizia nchi hii fedha nyingi sana. Samaki wanaotoka katika Ziwa Victoria, kwa sababu ya viwanda vilivyopo, wanaingiza fedha za kutosha ingawa bado kuna ujanja unaotumika. Uvuvi unaofanywa katika Ziwa Tanganyika, samaki wengi wanaopatikana katika Ziwa lile kutoka katika upande wetu wa Tanzania, wanauzwa katika nchi ya Zambia, Kongo na Burundi, lakini hakuna takwimu za dagaa na samaki wa aina nyingine wanaokwenda kuuzwa kule na hakuna ushuru wowote unaolipwa pale. Je, Waziri haoni kwamba, sisi tunaendelea kupoteza fedha nyingi zinazopelekwa katika nchi hizi? Nilitaka maelezo hayo.

Pamoja na kwamba, Mheshimiwa Waziri hajazungumzia lolote kuhusu viwanda vinavyoanza kushamiri katika Miji ya Kigoma na Kasanga, wapo wawekezaji ambao wameshajitokeza na wameshaanza ku-*process* samaki kiasi kidogo katika maeneo hayo. Je, Serikali inasema nini ili nchi yetu ipate kutokana na samaki wanaouzwa kwa wingi katika nchi ya Zambia, Kongo na Burundi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Tanganyika lina zaidi ya kilomita 13,000 katika upande wa Tanzania na lina wavuvi zaidi ya 7214 hivi. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mwananzila, mimi mwenyewe kama mwezi mmoja uliopita, nimefika mpaka Kasanga na nimekuta wapo watu wengi na samaki wengi wanaovuliwa pale *especially* Migebuka, wanauzwa upande wa Zambia ambako kuna viwanda zaidi ya vitano, ambavyo vina-*process* samaki. Upande wa Tanzania hasa sehemu ya Kasanga hakuna; kuna mmoja ambaye anajaribu kuanzisha kiwanda pale. Kwa hiyo, wito wangu ambao ningependa kuutoa kwa Halmashauri ile ni kwamba, basi waanzishe utaratibu hata wa kuwa na soko pale la Kimataifa ambalo litawasaidia Halmashauri ya eneo hilo kuweza ku-*collect* fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, palikuwa na matatizo ya Maofisa Ugani na bahati nzuri sasa hivi tumeshapeleka Maofisa Ugani wanaohusika na masuala ya uvuvi katika sehemu ya Kasanga na maeneo mengine ya mwambao. Napenda kukubaliana na yeye, kama wapo hawa wawekezaji, basi tutashirikiana na Wizara yangu katika

kuhakikisha kwamba, wanaanzisha viwanda katika upande huo ili hizo *resources* za samaki zisiendelee kupelekwa *DRC*, pamoja na Zambia.

Kwa hiyo, nakubaliana naye kabisa, kama wapo hao wawekezaji, Wizara yangu itawapa *support*. Mwisho kabisa, chini ya Mradi wa *Lake Tanganyika,* mwaka huu kuna zaidi ya shilingi bilioni 26 ambazo zimewekwa kwa ajili ya kuendeleza Bonde la Ziwa Tanganyika. Nina uhakika fedha hizi zikitumika vizuri katika upande wa Rukwa, pamoja na Kigoma, zinaweza kusaidia kwa kuongeza rasilimali na kuongeza zana nzuri kwa wavuvi katika maeneo hayo.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake kuhusu taarifa ya Jaji Chande, iliyohusu wananchi walioondolewa kule Ihefu, alieleza kwamba, wanaohoji hawamtakii mema kwa sababu anaweza kupoteza kazi yake akimuuliza Rais. Nina hakika amesema hivyo kwa utani, lakini nataka niseme tu pia kwamba, nina hakika Waziri anajua kwamba na sisi Wabunge pia tuna mabosi wetu ambapo tusipohoji suala hili, tunaweza kupoteza kura.

Mimi sina hakika kama Waziri anajua nina kaya zangu zaidi ya 30 za Wadatoga ziliathirika na wananihoji kupitia familia zao na hata wao wenyewe wameshatuhoji. Sasa ninachotaka kujua hapa ni kwamba, taarifa ile inawezekana Waziri kwa ajili ya upya hakuzipitia, inahusu masuala mengi sana yakiwemo ya haki za binadamu, wale wananchi kupoteza au kutengana na familia zao, watoto wengine mpaka leo hawajulikani walipo, kuna upotevu wa fedha za wale watu zimechukuliwa kinyume cha utaratibu na bila risiti, ng’ombe wamekufa kwa utaratibu uliohamishwa. Waziri aliyetangulia ninakumbuka ndani ya Bunge hili, aliwahi kutamka kwamba, taarifa ya Jaji Chande sasa imekwishafika kwenye ofisi yake na mimi ninachojua ni kwamba, Rais ndiye aliyeunda; ni kweli, lakini aliunda baada ya kelele za watu tukiwemo sisi Wabunge.

Baada ya kuunda ile Tume, tulitegemea kwamba, taarifa ile italetwa itawekwa hadharani wananchi tuione au taarifa itatolewa kuhusu mapendekezo ya Tume kutekelezwa. Baada ya kuona kimya na kwa majibu ya Waziri leo, naanza kushituka kidogo, Rais haingii ndani ya Bunge, tunamhoji nani wakati Waziri ndiye mwakilishi na Serikali iliyopo hapa ndiyo mwakilishi wa Rais aliyepo kule nje na haji kuhojiwa hapa. Mimi ningependa kujua ni lini sasa taarifa ile itawekwa hadharani au ni lini tutajulishwa nini kimetekelezwa katika mapendekezo yale na wananchi wale ambao wanatuhoji tuwajibu nini? Hakuna mwingine wa kutujibu isipokuwa Serikali.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Slaa kama ifuatavyo:-

Kwanza, nashukuru alizungumza kwamba, nilikuwa natoa utani, lakini katika utani ule yale maneno kwamba naweza kupoteza kazi sikuyasema, nafikiri *Hansard* zinaeleza. Ninachotaka kumweleza ni kwamba, hiyo Tume ni Tume ya Rais, huwa kuna Tume ya Rais…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ulisema utapoteza kazi! Umesahau?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Ninachotaka kumweleza ndugu yangu, Mheshimiwa Dr. Slaa ni kwamba, Ripoti ya Tume bado sijaipata. Kwa hiyo, ndiyo maana nasubiri kama italetwa au itatolewa na aliyeiunda, tutapata taarifa. Kwa hiyo, siwezi kuzungumzia kitu ambacho sijakiona, wala sijapata taarifa zake na hata aliyekuwa amenitangulia kwenye Wizara inayohusika na Mifugo, sikupewa hiyo Ripoti ya Tume ya Ihefu.

Kwa hiyo, nashindwa kujibu kitu ambacho sijawahi kukiona na *point of reference* sizijui na waliokuwa wajumbe siwajui na hasa hiyo Tume iliundwa na Mheshimiwa Rais. Bahati nzuri hata katika kuunda, hakuna mtu aliyemlazimisha kuunda, aliunda kwa misingi ya kutaka kujua. Kwa hiyo, Mheshimiwa atakapoona umuhimu wa kuitoa hadharani au kuileta Wizarani, sisi tutakuja kutoa taarifa. Kwa sasa hivi hiyo Tume sijaiona na matokeo yake sijayaona.

**MWENYEKITI:** Lakini ukamwambie unadaiwa huko! *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Sisi kama Waziri alivyoeleza kwamba, Kambi ya Upinzani imepongeza sana ni vyema nazidi na mimi kumpongeza Waziri na Timu yake kwa sababu tumepongeza kwa historia aliyoifanya katika sekta hii na kuweza kufuata sehemu kubwa au malalamiko yetu yote ya Kambi ya Upinzani, hasa kuhusu meli zile, kufuta leseni na *at least* wavuvi wetu sasa wanaweza kupata samaki. Meli zile zilikuwa zinatupunguzia samaki kwa wingi, kwa hiyo, tunapongeza kwa sababu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka Mheshimiwa Waziri, atufafanulie kutokana na hii barua ya Mkurugenzi na vitu vyote vilivyopigwa marufuku; hizo nyavu za *ringnet*, viatu vile vya kuogelea, uvuvi wa kutumia *oxygen*, *alternative* yake itakuwa ni kitu gani kwa sababu katika bahari kuna aina nyingi, sisi ndio wavuvi; kuna mitego ya madema, kuna mitego ya mishipi, kuna mitego hiyo ya kutumia *oxygen?* Kwa taarifa yake, wale wanaotumia *oxygen* ndio ambao hawaharibu matumbawe au hawaharibu samaki wadogo wadogo kwa sababu wanapiga samaki kwa kumwona, amevaa kioo, amevaa vile viatu, anakwenda *deep sea*, anachagua ni samaki gani mkubwa. Sasa ikiwa leo vitu vyote hivyo vimezuiliwa, hawa tunaotaka kuwanyanyua wavuvi wadogo wadogo, tunawanyanyua au tunazidi kuwadhalilisha na *alternative* gani ya Wizara tutaitumia? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, muda upo leo?

**MWENYEKITI:** Wenzako hatujawapa nafasi, ngoja ajibu hilo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Wakati nikitoa ufafanuzi, kwanza, Mkurugenzi wa Uvuvi analindwa kwa mujibu wa Sheria Na. 22 ya Mwaka 2003, pamoja na *regulations* zake za mwaka 2005; nilieleza kwamba, kuna maelezo mengi ya nyavu zinazokubalika kwa mahali gani na mahali gani. Kwa mfano,

*ringnet* alizozizungumza zikivuliwa mahali zinapotakiwa hazizuiliwi, lakini zinapofungwa mawe na kuzuia mpaka chini na kuzuia hata samaki wengine wanaokwenda kuzaa wasiende kuzaa na kadhalika, inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, suala hili la nyavu haramu ni *complicated* kidogo, kwa sababu nyavu inakuwa haramu mahali inapokutwa ambapo ni haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa mfano, nyavu za dagaa zinapovuliwa kwenye maji marefu haziwi haramu, lakini zinapopelekwa kandokando ya mazalia ya samaki zinakuwa haramu. Ndiyo maana nilipokuwa nikimjibu Mheshimiwa Shah, nilisema nitatoa maelezo baadaye ya kufafanua ni nyavu zipi kwa kila mmoja na niweze kuwagawia Waheshimiwa Wabunge. Maelezo hayo yapo mengi hapa ili waweze kuyachambua na waweze kutoa maelezo vizuri kwa wapiga kura wao na wavuvi katika kuwasaidia, kwa sababu lengo kubwa ni kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ametoa ufafanuzi wa nyavu sasa kwa nini vile viatu ambavyo wanatumia hajatoa ufafanuzi na wanaotumia bunduki kwa kuchagua samaki wakubwa au wanaotumia mishale wakati wanakwenda chini baharini? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kitu kina-*depend* kipo wapi; *oxygen* ukiitumia kwa ajili ya kufanya mazoezi umevaa haina tatizo, lakini ukiitumia kwa ajili ya kumfuata samaki aliyeko kule kwenye pango na kwenda kumchoma inakuwa ni tatizo, kwa sababu mara nyingi wamekuwa wakiua samaki ambao wanataga mayai. Haya masuala ya kuogelea, kuvaa unapoweza kuogelea kwa ajili ya kuokoa watu au unapokuwa nayo baharini kule katikati hayana matatizo. Unapoenda kuogelea na kumchokonoa samaki aliyeko kule na kwenda kutega mabomu ili alipuke inakuwa ni matatizo.

Kwa hiyo, ndiyo maana nimesema ufafanuzi huu nitawatolea Waheshimiwa Wabunge ili kusudi waweze kuchambua mahali gani panatumika nini na mahali gani hapatakiwi kutumika nini. Ndicho nilichoweza kuzungumza, kwa hiyo ni hayo tu maelezo ambayo ninaweza nikayatoa.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilielezea suala la ukiritimba wa leseni kwa wavuvi, kwa maana ya kwamba, mvuvi mmoja anatakiwa awe na leseni zaidi ya tatu; leseni ya chombo, leseni ya uvuvi wa pweza, leseni ya uvuvi wa kamba na leseni ya uvuvi wa samaki. Nikatoa mfano kwamba, wenzetu wawindaji wanakuwa na leseni moja tu hawaambiwi ukiwinda swala uwe na leseni ya kuua swala, ukiwinda nyati uwe na leseni ya kuua nyati, sasa mambo haya kwa nini yawe kwa mvuvi awe na leseni zaidi ya tatu au nne?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba, masuala ya leseni ni ya Halmashauri; je, kama Serikali Kuu ambayo inasimamia Sera inatoa tamko gani juu ya leseni hizi ambazo kwa kweli baada ya wananchi kuwaondoshea umaskini inazidi kuwazidishia umaskini; je, Serikali ipo tayari kutamka kwamba mvuvi awe angalau na leseni moja ya chombo na ya pili ya uvuvi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi leseni za uvuvi zinatolewa na Halmashauri na Halmashauri wana sheria zao. Sisi ni wasimamizi wa Sera kwa mujibu wa Sheria Namba 22 ya mwaka 2003, pamoja na *regulations* zake za mwaka 2005. Kwa hiyo, ninaogopa kutoa tamko wakati sijui Sheria hizo za Halmashauri zinazungumza nini, sijui hizo *regulations* zilizopo katika Sheria Namba 22 ya Mwaka 2003 zinazungumza nini. Naogopa kuvunja Sheria na Sheria hiyo imepitishwa na Wabunge akiwemo Mheshimiwa Mwinchoum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri suala hili linaweza likajadiliwa vizuri katika Halmashauri zake, kama leseni zipi ziweze kutolewa kama ilivyo kwa wawindaji kwamba, wana leseni ya kuwinda swala lakini pia ni lazima wawe na leseni ya bunduki.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri, pamoja na Wizara kwa ujumla, kwa kukubali na kuitambua michango yangu, lakini pia kwa kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mambo ambayo tumechangia mengi ilikuwa suala zima la uzalishaji wa nyama kwa ajili ya soko la nje na la ndani ya nchi. Hii ni dhahiri kwamba, katika kutekeleza azma hii inatakiwa kuwe na chombo madhubuti ambacho kitakuwa kinasimamia na kuratibu taratibu mbalimbali ambazo zitaundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuipa nguvu sekta hii, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Nyama Namba Kumi ya Mwaka 2006, baadaye Wizara iliunda na kuzindua Baraza la Wadau wa Nyama nafikiri mwaka jana. Najua kwamba, ipo *NARCO* lakini Wizara hii inasimamiwa na Bodi kadhaa ikiwa ni Maziwa lakini hadi leo hakuna Bodi ya Nyama iliyoundwa.

Ningependa kupata ufafanuzi iwapo Wizara hii inaona upo umuhimu wa kuunda Bodi ya Nyama na kama imeridhika tu na kuwepo na Baraza la Wadau wa Nyama na kama wanaona umuhimu wa kuunda Bodi ya Nyama upo, basi waniambie ni lini Bodi hii itaundwa? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Jecha, kwa mchango wake. Michango yake ilifuata michango ambayo imeshatolewa na Waheshimiwa Wabunge wa CCM, Sera za CCM na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na vitu vingine. Kwa hiyo, ninamshukuru kwamba, ameisoma vizuri Ilani ya Uchaguzi katika kulitekeleza hili.

Kuhusu Bodi ya Nyama, Serikali ilipitisha Sera ya Nyama ya Mwaka 2006 ikapitisha Sheria Namba Kumi ya Mwaka 2006, ndiyo tumezindua Baraza la Wadau wa Nyama, kinachofuata *actually* mwaka huu ndiyo Bodi kwa sababu hivi vyote vinategemeana. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Jecha, hiyo Bodi itaundwa na itaundwa katika bajeti ya mwaka huu; asiwe na wasiwasi ili uuzwaji wa nyama uongozeke kwa sababu sasa hivi katika mwaka uliopita, tumeuza nyama zenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 na minofu tani 149, yenye thamani ya shilingi milion 500

tu. Kwa hiyo, tunaamini kukianzishwa Bodi ya Nyama kwa kusimamia hizi Sheria, uuzwaji wa nyama unaweza ukaongezeka katika nchi yetu.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba, Mheshimiwa Waziri ana majibu tayari ya maswali yangu mengi ambayo niliuliza lakini hakupata muda wa kuyajibu. Naomba ufafanuzi kwenye masuala mawili ambayo yatashabihiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali langu ambalo niliuliza wiki iliyopita la uvuvi katika Ziwa Nyasa, Mheshimiwa Naibu Waziri alinieleza kwamba, sisi watu wa Ludewa tulikuwa tumeahidiwa kupata boti kwa ajili ya mafunzo ya *sustainable fishing* na akaniahidi kwamba, boti hizo zipo lakini ni ngapi; atatoa majibu wakati wa bajeti; naomba kujua boti hizo ziko wapi au ni hizi mbili zilizotajwa humu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili linalofanana na hilo ni kwamba, kuna kituo kimoja tu kinachosimamia au kufanya doria katika Ziwa Nyasa na kipo *based* Kyela, lakini Kyela ipo mbali sana na mwisho wa Ziwa ambalo ni eneo la Tanzania, maeneo ya Mbambabay na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziwa kama lile la Nyasa wale watu wa Kyela hawawezi hata siku moja kufika Kusini kabisa mwa Ziwa; kwa hiyo, hakuna usimamizi wowote unaofanywa hasa wakati wa dhoruba kali; je, kwa nini Wizara isiweke kituo kingine labda sehemu za Manda au Mbambabay?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na *concern* ya Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, lakini kama nilivyokuwa nikieleza; matatizo yanayotukabili katika Wizara yetu ni bajeti. Hata hivyo, katika kujibana kote na kwa barua nyingi ambazo amekuwa akituandikia Mheshimiwa Profesa Mwalyosi na ahadi ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Maghembe siku za nyuma, ndiyo maana tumejitahidi katika bajeti ya mwaka huu tutanunua boti mbili, ambazo zitatumika katika Ziwa Nyasa. Ninaamini hiki kinaweza kikawa kianzio kizuri na kinaweza kikawa kinazungukia katika maeneo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haya masuala ya usimamizi na mengine, tumepanga katika bajeti ya mwaka huu; Kitengo chetu cha Tafiti kitakwenda kufanya utafiti mzuri katika Ziwa Nyasa ili tuainishe maeneo mbalimbali, namna gani tunaweza kusaidia wavuvi katika maeneo hayo ambapo kuna zaidi ya wavuvi 12,574 na ambao wanatumia vyombo zaidi ya 7,124.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi namshukuru Mheshimiwa Waziri ameeleza na ni kweli mimi ni mwanamazingira mzuri na ninapigana kufa na kupona katika kuhakikisha mazalia yetu ya samaki yanalindwa na tunayalinda kwa faida ya nchi na ulimwengu. Ninachotaka kusema, nataka ufafanuzi kuhusu huu Waraka, haya unayoyasema hayamo ndani ya Waraka huu. Huyu aliyeandika ametumia kama *force*, utafikiri huyu Afisa wa Uvuvi ni *IGP* au Mkuu wa Majeshi.

Tunachosema nia ni kulinda mazingira na kutumia nyavu halali ambazo haziharibu mazingira na zile ambazo tutaona zinafaa kwa maji mengi, ndiyo ziruhusiwe. Mimi ni mvuvi kwa fani yangu, ninachoomba hayo yote tuliyoyazungumza na waliyoyazungumza akina Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Jecha na wengine, kuhusu suala hili, Waraka huu kwa hivi sasa kwa njaa iliyopo Mafia, naomba Mheshimiwa Waziri kwa heshima zote ama usimamishe au utoe kauli ya kusema wale waliokuwa sasa hivi basi tupo tayari. Nafikiri hawezi kufa mtu kwa siku moja au mbili, lakini ufanye haraka na ufafanuzi wote wa nyavu, mitungi ya gesi, bunduki za kuulia samaki, siungi mkono kabisa.

Naomba ufafanuzi huu ukautoe Mafia haraka iwezekanavyo ili wavuvi wa Mafia, kwa sababu unapozungumza Mafia unazungumza kwa niaba ya Watanzania; basi wote waweze kuelewa na wewe mwenyewe uweze kuona. Inaelekea hawa waliokwambia yote ni tofauti na fikira zako; ni vitu tofauti, inawezekana wamekujaza, wamekupiga pampu, umeingia umajaa sasa unashindwa lakini kwa hekima uliyotumia hapa, nafikiri kauli yako ni nzuri na leo wavuvi wa Mafia wamefarijika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mambo mawili, unikubalie haraka iwezekanavyo twende mafia tukafanye mkutano uongee na wavuvi lakini la pili huu waraka kidogo uupige *pulse* usimame ili wananchi waweze kujua nini cha kufanya bila kuathiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa samaki kwa maji chumvi hakuna, huyu anayefugwa Msusa ni sehemu tu ya vibwawa lakini leo ukisema samaki asivuliwe Mafia uwe unamlinda; hawi kama perege akitoka chato anakwenda Sengerema, Changu akitoka pale Seychelles, Mozambique, Mombasa na nchi nyingine katika Bahari ya Hindi. Kwa hiyo, huwezi ukamdhibiti, bora tuwaruhusu hawa wavuvi wawavue kwa zana hizi na hii mitando, kwani kinachotafutwa ni karabai ndiyo inatoa uhalali wa kuvua nyavu ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokuomba kwa kuwa haujalifahamu zaidi kutokana na ugeni, Mheshimiwa Waziri nikubalie haraka iwezekanavyo, twende Mafia ukatoe ufafanuzi kwa Wananchi wa Mafia na Watanzania ili waweze kulewa uhalali na uharamu wa vifaa hivi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka wa Mkurugenzi wa *Fisheries* haukutolewa Mafia peke yake, Waraka huu ni wa Tanzania nzima; unawahusu watu wa Chato kwenye Jimbo langu, unawahusu watu wa Musoma, Muleba, Tanga, unawahusu watu wote wa Maziwa yote mpaka Tanganyika na ndiyo maana umeanza kutekelezwa. Mimi mwenyewe nimeenda Musoma, nimehusika kuchoma makokoro zaidi ya 700, nimechoma mitego haramu Mwanza zaidi ya 350. Sheria ni Sheria na sheria ni msumeno, kwa hiyo, huu Waraka siubadilishi, ninausimamia ili watu wajifunze kufuata Sheria na hizi ndizo Sheria za nchi.

**MWENYEKITI:** Mafia huendi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwenda Mafia; nitakwenda kushika nyavu kule zilizoharibika nizichome. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa umahiri wake ambao amekuwa akiutumia wakati wa kujibu maswali. Vilevile nina imani kwamba, ile ahadi aliyoisema kwamba ataitekeleza atatekeleza. Kitu kilichonisimamisha ni kupata ufafanuzi katika masuala ambayo Waziri ameyazungumza na hasa nikianzia na hotuba yake. Wakati wa kujibu masuala mbalimbali amejibu vizuri sana, lakini hata sehemu moja hakuzungumzia Ziwa la Rukwa. Ziwa hili ni baadhi ya Maziwa ambayo yana rasilimali zote ambazo zipo chini ya Wizara yake, kuna mifugo. Bahati nzuri au mbaya, baadhi ya mifugo iliyotoka Ihefu imekimbilia Ziwa Rukwa; tunao wavuvi, ziwa lile linatoa rasilimali nyingi sana, lakini hakuzungumzia hata kidogo. Haya mambo mazuri ambayo ameyazungumza ya kuweza kusaidia kuboresha, mimi nataka nipate ufafanuzi; je, katika uboreshaji wa yale yote ambayo ameyazungumzia katika Maziwa mengine; Ziwa Rukwa nalo limo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika yote mazuri niliyoyazungumza, yamo pia katika Ziwa Rukwa. Tunafahamu kazi nzuri zinazofanyika katika Ziwa Rukwa, kwa sababu kuna wavuvi zaidi ya 1,676 na Ziwa hili lina ukubwa wa zaidi ya kilomita za mraba 3,000 na kuna vyombo zaidi ya 2,013 ambavyo vinatumika.

Katika bajeti ya mwaka huu, tumeshaelekeza katika kitengo chetu cha tafiti kwamba ni lazima kwanza tutakwenda kufanya utafiti kwa nini Ziwa Rukwa linakauka na kupungua maji yake kila mwaka. Huo pia ulikuwa ni mchango uliochangiwa na Wabunge wengi wa Mkoa wa Rukwa, akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, katika bajeti ya mwaka huu, tutaenda kuangalia ni kwa namna gani Ziwa Rukwa linaweza kutumika katika uvuvi lakini na kuangalia idadi ya uharibifu wa mazingira unaosababishwa na mifugo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia mtani wangu, Mheshimiwa Sigonda kwamba, Ziwa la Rukwa limo na tutahakikisha kwamba ni kwa namna gani tunaweza kuliboresha katika kuhakikisha kwamba, wananchi wa kule watani zangu Wafipa wanashiriki kikamilifu katika kuvua samaki.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia jinsi gani ambavyo vifo vinawapata wavuvi wetu wanapokuwa Baharini na kwenye Maziwa hasa wakati wa dhoruba kali na wale ambao wananusurika na vifo hivyo, wanaposimulia kwa kweli wanasikitika sana; wanakwambia kwamba mimi nilinusurika kwa kukamata ubao au mlingoti! Nataka kufahamu; je, Serikali ipo tayari kuwakopesha boti za kuokolea maisha ya wavuvi wetu wadogo wadogo ili kunusuru maisha yao wakiwa baharini na wawe wanavua samaki kwa ujasiri mkubwa wakiwa baharini bila wasiwasi wowote?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kueleza kwa ufupi tu, wavuvi wa upande wa ukanda wa bahari wanaweza kutumia Mradi wao wa *MANCEP* katika kuhakikisha kwamba, wanajipanga vizuri na kuweza kupata boti ambazo zinaweza kuwasaidia katika kuokolea, Mradi ule unagharimu zaidi ya shilingi bilioni 51. Kwa upande wa *Lake Victoria*, kuna Mradi ambao upo chini ya *Lake Victoria Environmental* ambao una zaidi ya *Euro* 29.9. Kwa upande wa *Lake Tanganyika* kuna zaidi ya shilingi bilioni 26 ambazo zinatolewa. Kwa hiyo, wanaweza kuitumia hii Miradi, pamoja na B*each Management Unit Organisation* na mambo mengine katika kujipanga vizuri ni namna gani wanaweza kujiokoa wanapokuwa wanavua samaki.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Wakati natoa mchango wangu kwa njia ya maandishi, nilikuwa nimezungumzia kuhusu Ziwa Kitangiri ambalo ni mkombozi katika Mkoa wa Singida kwamba, lina samaki wachache na vilevile wavuvi hawana taaluma. Nikamwomba Mheshimiwa Waziri, atupatie Maafisa Uvuvi watakaotusaidia kutoa elimu kwa wavuvi na watakaosaidia hata kutupandikizia samaki wengine; kwa mfano, Mheshimiwa Killimbah ameeleza kwamba, Ziwa lina samaki aina tatu tu na lina uwezo wa kubeba samaki wa kutosha.

Naamini tukipatiwa Maafisa Uvuvi, Ziwa hilo litapandikizwa samaki wa kutosha na wavuvi watapewa elimu kiasi kwamba, Ziwa lile litatuletea manufaa sana Wanasingida kupata samaki ambao wanawapatia wanadamu *calcium*. Tuliambiwa hapa juzi kwamba, watu wanaokula samaki wana akili nyingi na sisi tupate na akili nyingi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea mchango wa Mheshimiwa Diana Chilolo, ulikuwa mzuri sana. Nataka kumhakikishia kwamba, hao Maafisa Uvuvi watapatikana mara baada ya wale wanaohitimu mwaka huu kuwatuma katika Ziwa Kitangiri ili waweze kwenda kutoa elimu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* …. ….. …. . .. .... Sh.402,300,700
Kif. 1003 - *Policy and Planning…. ….. …. ...* .... .... ... ... Sh.620397600
Kif. 1004 - *Livestock Reseach and training*
*Institute…. …..* ... .... . .... .... ..... .... .... Sh.2,970,175,000
Kif. 1005 - *Information, Communication and Edu.*
*Techn* ….. …. ... .... .... .... ..... ..... ..... .... Sh.87,153,700
Kif. 1006 - *National Livestock Inst. Mpwapwa.* …... ….Sh. 761,625,000
Kif. 1007 - *Internal Audit Unit* …. ….. …. .... ..... ..... ..... Sh. 68,4932,500
Kif. 1008 - *Procurement Unit* …. ….. …. .... .... .... .... .... Sh.91,515,500
Kif. 1009 - *Legal Unit* …. ….. …. .... ..... ..... ..... .... ..... Sh. 37,672,100
Kif. 7001 - *Veterinary Services* …. ….. …. ... .... .... ... Sh. 2682322200
Kif. 7002 - *Livestock Identif. Regist. Traceab.*

*Unit…. ….. …. .... .... .... .... .... ..... ..... ....* Sh. 274,474,200
Kif. 7003 - *Pastoral System Development …. ….. ….* Sh.437,583,300
Kif. 7004 - *Central Veterinary Laboratories. ….. ….*Sh. 14947,520,300
Kif. 8001 - A*nimal Production …. ….. …. ... .... ..... ..* Sh. 1450,895,600
Kif. 9001 - *Fisheries.… ….. …. ... ..... ..... ..... .... ......* Sh.7,413,451800

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 99 - Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi**

Kif. 1001 - *Administration and General …. …. …. ... ... Sh.* 82, 500,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning*…. …. …. ... .... .... .... Sh.1,992,662,000

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* 99, *Sub-vote* 1003, kifungu cha 4486 - *Agriculture Sector Development Program - Livestock*, nilikuwa nataka ufafanuzi fulani kuhusu mipango ya Wizara hii hasa kwa mfumuko mkubwa duniani hivi sasa wa mahitaji ya *organic meat* na hapa kwetu mpaka sasa hivi masoko ya ndani pia hasa katika ukuaji wa hoteli, watu wanapendelea hiyo *organic meat* kwa wingi wa sifa zake na faida zake.

Hata Mheshimiwa Naibu Waziri, nategemea hivi karibuni katika ziara yake alikumbana na masuala kama hayo na sisi tunatumia chanjo kwa wingi na dawa ya kuogeshea ambayo ni tofauti na uzalishaji wa nyama hiyo ambayo inahitajika. Nataka kujua mipango ya Wizara; imejiweka tayari vipi kwa soko hilo ambalo limekua nje na ndani ya nchi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu aliyoitaja inahusu kuanzisha na kuiimarisha benki ya takwimu za mifugo, inahusu kufuatilia Programu ya *SDP*, inahusu mkakati wa kutekeleza Sera ya Programu ya Maandalizi ya Sensa ya Mifugo na sensa ya sampuli, lakini kwa kumpa taarifa Mheshimiwa Mnyaa ni kwamba, tuna Ranchi ya Taifa ambayo ina hekta zaidi ya 230,000 na ng'ombe zaidi ya 41,000. Kwa hiyo, wamejipanga katika Ranchi za Taifa ambazo ni karibu kumi; namna gani wanaweza wakawa wana-*produce organic meat* ambayo inaweza ikawa inasafirishwa nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kifungu alichokitaja hakihusiani na mambo ya *organic meat*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Livestock Research and Training Institute*….. ….. ….. .. ... .... .... .... ..... .... Sh.2,125,754,700
Kif. 1005 - *Information, Communication and Education*….. ….. ….. .. .... ..... ..... ...... ..... Sh. 52,500,000
Kif. 1006 - *National Livestock Institute Mpwapwa*….. ….. ….. ... .... ..... ..... ....... ... Sh.541,606,300
Kif. 7001 - *Veterinary Services*….. ….. ….. ... .... ..... ..... Sh.886,294,800
Kif. 7002 - *Livestock Identif. Regist. Traceab. Unit*….. ….. ….. ... .... .... .... .... ... .... .... ..... Sh.194,468,700
Kif. 7003 - *Pastoral Sytem Development*….. ….. ….. ..Sh.177260,900
Kif. 7004 - *Central Veterinary Laboratories*….. ….. ..Sh. 1,392,538,900
Kif. 8001 - *Animal Production*….. ….. ….. ... .... .... .... Sh.4,633,095,700

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 9001- *Fisheries* ….. …. ….. ... .... .... .... .... .... .... Sh.7,993,825,000

**MHE. SALIM HEMED HAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita Benki ya Dunia ...

**MWENYEKITI:** Anza na kifungu chenyewe.

**MHE. SALIM HEMED HAMIS:** Nirudie, *Vote* 99, *Sub-vote* 9001, *item* 6501; katika bajeti iliyopita, Mradi huu ulipokea shilingi bilioni 19.6 na katika mgao Zanzibar walipata shilingi bilioni 10.4 na Tanzania Bara shilingi bilioni 9.2. Nilimpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuunga mkono Muungano kwa vitendo bila kujali ukubwa; Zanzibar walipata fungu kubwa zaidi.

Katika bajeti ya mwaka huu, amesema kuna shilingi bilioni 51, nilitaka kujua katika fedha hizi Zanzibar inapata ngapi na kama ule moyo wake wa kuuenzi Muungano kwa vitendo bado upo, Zanzibar inapata fungu gani ambalo nafikiri litakuwa ni kubwa zaidi?

**MWENYEKITI:** Unamaanisha hizi shilingi bilioni saba au zipo nyingine mahali pengine?

**MHE. SALIM HEMED HAMIS:** Tuangalie hizi hizi kwa sababu yeye alisema kuna shilingi bilioni 51 lakini sizioni hapa.

**MWENYEKITI:** Sasa hilo ndio swali.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi mzima una shilingi bilioni 51, lakini una fedha nyingine *extra* kama shilingi bilioni kumi. Kwa hiyo, Mradi mzima una kama shilingi bilioni 61 na katika fedha hizo karibu katika ule Mradi wa shilingi bilioni 51; asilimia karibu nusu kwa nusu ipo Tanzania Bara na nyingine Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya mwaka jana, fedha zilizokuwa za Tanzania Visiwani na Tanzania Bara katika Mradi wa *MANCEP* zote ziliwekwa pamoja. Mwaka huu zilizo kwenye *MANCEP* kwa upande wa Tanzania Visiwani tumewaachia wapange wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizo hakuna hata senti tano ya Tanzania Visiwani; za Tazania Visiwani zitatangazwa na Waziri anayehusika na mambo yanayohusika Tanzania Visiwani. Mradi mzima kwa pamoja ni nusu kwa nusu, kwa hiyo, nusu zinabaki huku na nusu zinakuwa kule, ambazo ni karibu shilingi bilioni 61. Shilingi bilioni 51 na shilingi bilioni kumi nyingine ni mfadhili mwingine. Kwa hiyo, ndiyo ufafanuzi lakini kwa ufafanuzi zaidi; kwa mwaka huu tumeingia pamoja na wenzetu wa Zanzibar chini ya *Deep Sea Fishing Authority*, ambayo imeanza mwezi uliopita katika kuhakikisha kwamba, haya mambo yote tunayafanya pamoja tusiendelee kuibiwa zaidi, tufanye *operation* kwa pamoja katika kulinda rasilimali zetu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

## T A A R I F A

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha 2008/2009, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe makadirio hayo ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, nakutakia kazi njema na ulivyopongezwa na Wabunge ni dalili njema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kesho tuna Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; ni ya siku moja kama mnavyofahamu. Mimi sina matangazo mengine zaidi ya kwamba, nawashukuru kwa siku ya leo, tumeendesha vizuri, kwa amani na utulivu na niombe mkapumzike mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.34 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 05 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*